

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 3 Mei, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja, Kikao cha leo ni cha Ishirini na Moja, Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima nchini kwa kipindi cha Mwaka ulioishia 31 Desemba, 2016 (*The Annual Insurance Market Performance Report for the year ended 31st December, 2016*).

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

MHE. SALUM MWINYI REHANI (K.n.y. MHE. MUSSA A. ZUNGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana umesoma kwa niaba ya Mwenyeikit wa Kamati ya Mambo ya Nje; Waziri Kivuli hana cha kuweka mezani, Katibu tunaendelea.

NDG. NENELWA WANKANGA - KATIBU MEZANI:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni hayupo, kwa hiyo tunaanza na Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Waislam wenyewe imani ya Kiislam, mwezi huu ni mwezi unaokaribia kuingia kwenye Ramadhan bado kama siku saba au 10 hivi, lakini huko nje bidhaa adimu ambayo inatumika na Waislam wote sukari imepanda sana, inauzwa Sh.2,800, Sh.3,000, Sh.3,200.

Mheshimiwa Spika, Serikali yangu inatoa tamko gani na msimamo gani kuweza kuwasaidia hawa watu ambao wanaingia kwenye mfungo wa Ramadhani waweze kupata bidhaa hii kwa unafuu?

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba jibu. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la sukari tumelitafutia ufumbuzi tukiwa tunalenga kwanza upatikanaji wa bidhaa yenyewe iwe ya kutosha na kila mwenye mahitaji ya matumizi aweze kuipata sukari kwa urahisi na kwa ukaribu ikiwemo na Waislam ambao wataanza mfungo wa Ramadhan siku chache zijazo.

Mheshimiwa Spika, tunajua kila mwaka tunakuwa na upungufu wa sukari. Utaratibu tunaoutumia ni kutoa vibali vya kuingiza sukari ile ambayo tunaita *gap sugar* ili kuweza kufanya soko la sukari kuendelea kuwepo na kwa kufanya hilo tunapoagiza sukari ya njie inasaidia pia hata kupunguza bei ya sukari ya ndani. Kwa hiyo vibali tumeshaviagiza na tayari sukari imeshaanza kuingia na Bodi ya Sukari kuititia Wizara ya Kilimo inaendelea kufuutilia mwenendo wa uingiaji wa sukari nchini ili sukari iweze kusambazwa mpaka kwenye ngazi za vijiji na huduma hii iweze kupatikana maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niwaondolee mashaka Watanzania na hasa Waislam kama ambavyo Mheshimiwa Bulembo amesema, kwamba sukari itapatikana katika kipindi chote cha Ramadhan na maeneo yote ambayo yanahitaji sukari kuititia vibali ambavyo tumevitoa na tutaendelea kufuutilia pia na mwenendo wa bei ili watu wasiweze kupandisha bei ya sukari kwa maksudi tu, kwa sababu watu wanajua mahitaji ya sukari yatakuwa makubwa kwa sababu ya mfungo wa Ramadhan.

Mheshimiwa Spika, hili pia nalo tutalifanyia ufuutilaji kwenye maduka kwa sababu tumeweka utaratibu kusiwe na mtu ye yeyote anayeweza kupandisha bidhaa ya aina yoyote ile wakati wa Ramadhan, kwani kwa kufanya hivyo atakuwa anawaadhibu Waislam wanaofunga Ramadhan kwa sababu tu mahitaji yanakuwa makubwa. Kwa hiyo, Serikali inataka kumhakikishia kwamba utaratibu upo na tutaendelea kusimamia kikamilifu. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Bulembo bado una swal?

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, nina swal dogo. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Waziri Mkuu na Watanzania wamesikia, lakini nina ushauri kidogo, kwa sababu huko mikoani tuna Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, naomba Serikali yangu ingewapa agizo kuliangalia kwa sababu nchi hii ni kubwa. Tunaweza tukaangalia mjini lakini kumbe vijijini sukari ikafika Sh.5,000 kama atawapa agizo wakalisimamia amani inaweza kupatikana kwenye mwezi wa Ramadhan. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Wakuu kwa kifupi sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kufuatia maelezo haya naamini Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Blashara hata walioko kwenye Halmashauri za Wilaya wamenisikia. Kwa hiyo ni wajibu wao kusimamia kuhakikisha kwamba sukari na bidhaa nyingine zote hazipandi bei kwa sababu tu ya kutaka kuwakomoa Watanzania. Malengo ya Serikali ni mazuri, tunataka huduma zote zipatikane na tutaendelea kusimamia hilo kwamba bidhaa hizi muhimu zinapatikana kwa wakati. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Godbless Lema, swal.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Natambua kwa dhati kabisa nia ya Serikali ya kulinda viwanda vyta ndani kwa ajili ya *ku-raise* kazi za mashambani. Hata hivyo, hivi sasa kumekuwepo na tatizo kubwa ambapo mafuta ya chakula yamepanda bei kwa asilimia 15 mpaka asilimia 30. Wakati huo kuna meli mbili ziko bandarini zimezuiwa kushusha mafuta kwa sababu ya *confusion* ya kodi, ambapo *TRA* wana-demand asilimia 25 ya kodi kutoka kwenye *crude oil* wakati Bunge hili Tukufu lilipitisha asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia hiyo njema ya dhati kabisa ya kulinda viwanda vyta ndani, ni kwa nini sasa Serikali isiweke mkakati ambao utakuwa ni *procedures*

kwamba sasa hatuwezi kuwa na mahitaji ya kutosha ya mafuta kwa *local industry* zilizopo. Kwa nini Serikali sasa isiendelee kuona kwamba *importation* ya mafuta sasa ni muhimu sana *especially*sasa ambapo mafuta yanaonekana kuleta mfumuko mkubwa wa bei?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kwamba liko tatizo la uingiaji wa mafuta na mfumo wa ulipaji kodi linalopelekea hata hizo meli mbili ulizosema kubaki huko bandarini. Hili lilikuwa na utaratibu wa kufuatilia mwenendo wa uingizaji wa mafuta ya kula nchini, kwa sababu ili kulinda viwanda vya ndani tulikubaliana mafuta yanayoingia hapa nchini tuweze kuyatoza kodi kwa kiwango ambacho Bunge pia lilishawahi kuridhia.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea baada ya wafanyabiashara wachache sana ambao siyo waaminifu wamekuwa wakileta mafuta na kuzungumza kwamba kuna mafuta ghafi na mafuta safi. Sasa mafuta ghafi na safi kila aina ya mafuta ina gharama yake ya kulipia kodi. Mafuta ghafi ndio asilimia 10, safi ni yale asilimia 25 au kinyume chake. Kwa hiyo, tumeunda timu inafanya ufuatiliaji wa karibu, lakini kwa sababu ya kodi na Waziri wa Fedha naye keshokutwa Jumamosi wanakutana Arusha na Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kodi zetu ziwe za pamoja zaidi tunapoweza kutoza bidhaa hizi ziwe za pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina matumaini jambo hili litakwisha katika kipindi kifupi kijacho. Baada ya hapa sasa nitawasiliana na mamlaka hizo kujuwa mwenendo uliofikiwa kufikia leo hii mchana ili tuweze kutanzua tatizo hili ili tusije tukapandisha mafuta ya ndani ya kula kwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

gharama ya juu kwa sababu pia tunaamini kwamba pia bado uzalishaji wa mbegu nchini sasa ndiyo tumeanza kuwekeea nguvu lakini hatujafikia kiwango, kwa hiyo lazima tupate pia mafuta ya nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutafanya *harmonization* ya viwango hivi lakini na kutambua ni aina gani ya mafuta yanaingia na kodi stahiki lazima ilipwe. Kwa hiyo hilo Mheshimiwa bado tutaendelea kufuatilia baada ya kipindi cha Bunge asubuhi hii ili tujuje *position* ikoje na nitampa mrejesho wa hatua sahihi tuliofikia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Nashukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Felister Aloyce Bura

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi hiki kifupi ni pamoja na Serikali kuhamia Mkoani Dodoma na sherehe za Kitaifa zinafanyika Mkoani Dodoma kwa sasa, mambo mengi ya Serikali yanafanyika Mkoani Dodoma kwa sasa ikiwa ni Makao Makuu ambayo yametangazwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Aprili, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alipandisha hadhi ya Manispaa ya Dodoma kuwa Jiji. Uamuzi huu haukuja bure kwa sababu vikao vyote vilikaa na tunaamini kwamba ili Mji huu upanuke haraka na ujengwe kwa haraka lazima upewe hadhi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wameamua kubeza maamuzi haya mazito yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Najua Mheshimiwa Waziri Mkuu ana jibu sahihi kwa wale wanaobeza maamuzi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awaambie wananchi juu ya uamuzi huu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu endapo umelielewa swali, majibu tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sasa hili sijui ni swali au nitoe tu maelezo na kama naruhusiwa kutoa maelezo niyatoe. Kwamba kwanza maamuzi ya Mheshimiwa Rais ni sahihi na yamefika kwa wakati muafaka na naamini sana wananchi wa Dodoma na Watanzania wote wamepokea maelekezo haya vizuri na kwa mikono miwili kwa sababu kwanza hata kisheria Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya kupandisha mji wowote ule hadhi kadri ya mahitaji na hasa kama vigezo vinatosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi peke yake inaipa sifa Dodoma kuwa Jiji vilevile. Pia unapopandisha hadhi eneo lolote lile lazima ujiridhishe kwamba huduma zile muhimu zinapatikana na Dodoma hatuna shida ya huduma muhimu. Tuna maji ya kutosha kutoka Mzakwe na huduma hizi zinaendelea pia tunatengeneza bwawa letu la Farkwa, liko bwawa ambalo pia linaleta maji hapa.

Mheshimiwa Spika, pia suala la huduma ya afya, wote mnajua tuna hospitali kubwa tu ya Benjamini William Mkapa na Hospitali ya Mkoa imeimarishwa na tunaendelea kuiimarisha ili iweze kuendelea kukidhi zaidi mahitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara, viwanja wa ndege na tunajenga tena Msalato kiwanja kikubwa tu. Barabara za ndani tunaendelea kuzisafisha kwa hiyo Jiji la Dodoma litaendelea kuwa na huduma ya miundombinu mingei ya kutosha. Hatuna shida sana na mapato ya Manispaa yetu ya zamani ambayo sasa ni Jiji kwamba mapato yake yanaendelea kuongezeka na yataendelea kukua kwa kipindi kifupi kwa sababu tumeanza kuona pia hata ujaji wa wanaoomba kuwekeza hapa Dodoma. Kwa hiyo, tunaamini tunaendelea kuboresha tu na kupata sifa ya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa Taasisi muhimu, Bunge liko Dodoma taasisi kubwa sana, vyuo vikuu viko Dodoma zaidi ya vitano, pia taasisi binafsi nazo zimeshaanza kuja hapa pia hata ile Taasisi ya Umoja wa Mataifa iko pia Dodoma. Kwa hiyo, Dodoma panajitosheleza kwa mahitaji mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alifanya maamuzi sahihi na naamini Watanzania wamepokea vizuri. Nami nitumie nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi yake kwa sababu maamuzi yake haya yanaleta tija kwa Watanzania wote na hasa wananchi wa Dodoma kutumia fursa za mabadiliko haya ili kuweza kujiongezea uwezo wa kiuchumi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwaomba sasa wananchi wa Dodoma na Mheshimiwa Felister Bura ni Mbunge aendelee kuwahamasisha wananchi wa Dodoma kutumia fursa ya maamuzi ya Mheshimiwa Rais ambayo ni sahihi na wala hakukosea ambayo pia nasi kama Wabunge hapa tunaendelea kuona maamuzi yake kuwa ni maamuzi sahihi ambayo yanaweza kufanya Dodoma kuwa ni eneo la kivutio na eneo kimbilio.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Waziri Mkuu kwa jibu hilo zuri, lakini niongeze tu swalii moja kwamba ni lini sasa wataleta Muswada wa Sheria wa kuitambua Dodoma kama Makao Makuu?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, pale ambapo Mheshimiwa Rais huwa anatoa maelekezo ya kuanzishwa kwa Mji Mdogo au aidha Mji kama hapa Dodoma imekuwa Jiji, baada ya maagizo yale sasa maana yake Serikali kuititia vyombo vyake sasa wataanza kufuata taratibu za

kuhakikisha kwamba maagizo yale sasa yanaingia kisheria. Kwa hiyo baada ya maagizo yake Serikali kila idara, TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wanasheria maana yake sasa wameshaingia kazini kuhakikisha kwamba jambo hili linaletwa kwa wakati mfupi ili liweze kufanyiwa maamuzi ya kisheria liweze kwenda sambamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Bura, Wanadodoma na Watanzania wote kwamba jambo hili sasa baada ya maagizo yale tunaendelea na taratibu za kuhakikisha kwamba tutaiweka kwenye sheria zaidi ili kila kitu kiweze kwenda kama ambavyo tulifanya maamuzi ya Dodoma kutoka CDA kuwa Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza tamko lilitoka halafu baadaye tukaanza taratibu za kisheria ili kudhibitisha na kufanya jambo hili kuwa rasmi. Kwa hiyo, taratibu zitaanza mara moja na wahusika wamesikia kwamba lazima waharakishe sasa utaratibu huu ili uweze kuwa rasmi zaidi na kisheria.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu hayo. Natumaini Mwanasheria Mkuu wa Serikali unasikiliza hayo maneno, safari hii isomwe mara ya kwanza mwishoni mwa kikao hiki kwa ajili ya Oktoba. Nilishamwambia Mheshimiwa Jenista tusipofanya hivyo itakuwa hatari patawaka moto hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshapigia mstari hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na upande wa *CUF*, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kutokana na mvua ambazo zimeendelea kunyesha hapa nchini, baadhi ya maeneo mbalimbali ya nchi yetu yamepata matatizo makubwa ikiwepo mafuriko, lakini pia miundombinu kuharibika, shule kuanguka, nyumba za watu kuharibika.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ya Kaliua katika Kata moja ya Usinge wananchi 500 hivi sasa hawana nyumba za kukaa, zimebomoka kabisa, lakini pia nyumba 167 zimepata nyufa kubwa kiasi kwamba, tumewahamisha watu hawana makazi. Kwa hiyo, watu wameishi kwa kujibanza kwenye nyumba za watu.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua, je, Serikali Kuu ina mpango gani wa haraka wa kusaidia kuweza kutoa fedha kwenye Mfuko wa Maafa wa Taifa ili wananchi wale waweze kuokolewa maisha yao kwa sababu, kwa madhara yaliyotokea hata Halmashauri haina uwezo wa kuweza kuwasaidia?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wake/wetu kule Usinge na kwa bahati nzuri eneo lile nalifahamu sana kwa matatizo haya makubwa yaliyowakuta kutokana na mvua kubwa. Hii ni nchi nzima maeneo mengi yamepata athari kubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu tunayo maelekezo ya kila eneo kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya, ngazi ya Mikoa, ambako tumeunda Kamati za Maafa kwa kila ngazi. Kwa hiyo, wajibu wa kufanya tathmini ya matatizo yaliyojitokeza tunaanza kule chini. Ni kweli, ametaka kauli ya Serikali Kuu, lakini bado Serikali Kuu itahitaji kupata taarifa kutoka kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwanza Wilaya ya Kaliua inatakiwa iwe imeshakwenda kufanya tathmini ya athari iliyojitokeza pale matukio haya yalipojitekeza. Baada ya kuona kwamba, Kaliua haina uwezo, kama alivyoeleza, wanatakiwa wapeleke pia Mkoani. Mko nao utakwenda kujiridhisha na tathmini iliyofanywa na Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mkoa nao ukiona kwamba hauna uwezo wa kuhudumia tatizo hilo, lakini huwa mara nyingi tunawataka wao waanze kutoa huduma ya kwanza, ili sasa taarifa za mahitaji makubwa zije Taifa, Ofisi yangu ya Waziri Mkuu, tuna Kitengo cha Maafa ambacho kinaratibu matukio kama haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pindi tutakapopata taarifa hizo kutoka Kamati ya Maafa ya Mkoa, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Waziri wa Nchi atashughulikia, atakuja kuona na yeye na atapeleka kitengo kile kuona mahitaji ni nini kwa haraka sana tutaweza kushirikiana nao ili kuwafanya waweze kuendelea na shughuli zao kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukishapata taarifa kutoka mkoani, inawezekana pia Waziri wa Nchi ana taarifa au hana taarifa. Nadhani baada ya hapa hebu awasiliane na Waziri wa Nchi, ili kuona jambo hili kama limeshafika ofisini aweze kujiridhisha pia na aweze kuwaunganisha na mkoa wake na Wilaya na hili eneo kuona namna ambavyo Ofisi ya Waziri Mkuu itakavyofanya kazi yake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Nyongeza Mheshimiwa Magdalena.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri. Kamati ya Ulinzi na Usalama imefika Usinge, lakini sasa hivi ni wiki *almost* ya pili wananchi wanazidi kuteseka na kiukweli hakuna hatua za uhakika na za haraka zinazochukuliwa. Kwa hiyo, kama Mbunge naumia kuona kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama imekwenda pale, hii ni karibu wiki ya pili na hii ni wiki ya tatu tangu haya yametokea na kila siku mvua zikinyesha zinaendelea kubomoka nyumba.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe maagizo ya haraka kwa hiyo Kamati ya Mkoa, Kamati ya Wilaya wafanye kazi kwa *speed* kubwa ili kuokoa wananchi amba wanateseka maeneo yale. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali tunayoyataka hapa ni ya kisera ya Kitaifa; tukishaanza kuyafanya kuwa ya Jimbo, Usinge peke yake au mahali pengine peke yake, kidogo tunakosea.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kifupi.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliua kwamba, tumesikia alichokisema na tunajua namna ambavyo amekwazwa kutokana na tatizo walilolipata wananchi. Utaratibu wa kisera, kama ambavyo nimeeleza kwamba, hizi hatua lazima zifikiwe kwa hiyo, tutajiridhisha kama taarifa za Mkoa wa Tabora zimefika zinazozungumzia athari zilizopatikana kule Kaliua na mahitaji yao ni nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baadaye nimsihi, amwone Waziri wa Nchi, baada ya kipindi cha Maswali na Majibu ili amjulisho kama amepata taarifa au Mkoa wenyewe unaweza kubeba jukumu hilo la kusaidia yale maeneo kwa haraka kwa sababu suala la nyumba baada ya hapo sasa wananchi wataendelea kujenga nyumba zao, lakini kuna zile huduma muhimu kama vile, afya, elimu na vitu vingine, vile sasa Waziri wa Nchi atatoa taarifa kwake. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, Sera ya Nyumba ambayo ilianzishwa baada ya Serikali ya Awamu ya Kwanza kutaifisha nyumba hizi, lengo lake lilikuwa kuleta usawa kwa wananchi wote, Watanzania wote na wao wawefe kuishi kwenye nyumba. Mwaka 2005 kwenye Awamu ya Tatu wakati Bunge linavunjwa, Serikali ililetwa Muswada wa kuondoa lengo na nia ya kuwasaidia Watanzania wanyonge wanaoishi kwenye nyumba hizi kulipa kodi ile ya Kitanzania, badala yake shirika hili likapewa mamlaka ya kuingia na kufanya shughuli zake kibiashara na kupandisha kodi kiholela, kama inavyofanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa, wazee hawa, wengi ni wastaafu ambao wanaishi sasa hivi na wanapatwa na adha hii ya sasa hivi ya kunyanyasika, kuondolewa wakati wamelitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa sana. Kuna baadhi ya watendaji wakiingia kwenye nyumba hizi wanakagua mpaka *fridge* na vyakula wanavyokula wastaafu hawa na kuona kuwa ninyi mna uwezo wakati hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, je, lini sasa Serikali itakubali Chama hiki cha Wapangaji wa hizi nyumba za *National Housing* wakutane na Mamlaka ya *National Housing* wakae walijadili na kwa nguvu na *support* ya Serikali hawa watu wapate kunusurika? Pamoja na agizo lilitolewa na Serikali ya nyumba hizi wauziwe watu waliokaa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, Jijini Dar es Salaam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua Shirika letu la Nyumba linayo sera inayotoa mwongozo wa namna nyumba hizi zinavyotakiwa kutumika, ikiwemo na maamuzi ya wale ambao wamekaa kwa muda mrefu kwenye nyumba hizo inapofikia thamani ya nyumba kushuka iweze kurasimishwa rasmi ili wanaokaa kwenye nyumba hizo wapate fursa ya kuzinunua hata kwa kulipa kiwango kidogo kidogo ili kuwawezesha Watanzania hawa kumudu kuishi kwenye nyumba hizo. Bado sera hii pia inaendelea sasa kwa shirika letu la nyumba nchini, linaendelea kujenga nyumba za bei naafuu zinazowawezesha Watanzania kuweza kuzinunua.

Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama timu yetu ya *National Housing* wanapita kwenye nyumba kukagua mpaka kwenye *fridge* ili kuona uwezo wa huyo mtu na kufanya

maamuzi hayo. Hata hivyo, nirudi kwenye wito wa Mheshimiwa Mbunge, ni lini Serikali itafanya maamuzi ya kuwakutanisha hawa wamiliki na Chama chao cha Wapangaji ambao wako kwenye nyumba zetu za Shirika la Nyumba pamoja na shirika lenyewe.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Ardhi na Naibu Waziri wa Ardhi wako hapa ndiyo wenyе dhamana kwenye Shirika hili la Nyumba nchini. Wamelisikia hili na nataka niwaagize sasa kukutana na Chama cha Wapangaji Tanzania na hasa wale waliopo kwenye nyumba zetu za Shirika la Nyumba nchini, ili kupata changamoto wanazokabiliana nazo wakati huu na hasa wale wenyе nia ya kuuza, lakini ambao wameishi kwa muda mrefu na sasa wanaonekana wanataka kuondolewa kwa mbinu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lazima liangaliwe, ili tusiweze kuleta madhara kwa Watanzania ambao wameishi kwa muda mrefu, leo kuja kuwaondoa, unawapa kazi tena, ni wastaa fu, hawana uwezo wa kujenga nyumba mpya, jambo hili liangaliwe. Kwa agizo hili naamini Wizara sasa baada ya agizo hili watafanya utaratibu wa kukutana na Chama cha Wapangaji ili waone tatizo lao ni nini muweze kutatua.

Mheshimiwa Spika, muhimu zaidi wawape fursa ya angalau kulipia kidogo kidogo kwenye hizo nyumba kadri ya uwezo wao ili waweze kuishi kwenye nyumba hizo na familia zao ambazo wameishi miaka mingi. Jambo hili nadhani litaleta tija.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Zungu kwa swali lake zuri juu ya hili. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Sera na kauli mbiu ya Serikali ya Awamu

ya Tano ni Serikali ya Viwanda, lakini kumekuwa na sintofahamu kwa *TRA* kuendelea kufunga biashara za wafanyabiashara, kuwapelekea kodi ambazo ni kubwa ambazo wafanyabiashara hawafahamu kodi hizi zinatoka wapi. Wamepelekewa kodi zaidi ya shilingi milioni 100, milioni 200 mpaka bilioni moja wakiwa wanadaiwa hizo fedha bila kupewa maelezo ya kina ni kwa nini wanadaiwa hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tataruki kubwa sana na wengine wamepata mshtuko na kusababisha vifo vyaa wafanyabiashara hao na wengine kufunga biashara na wengine kuhamisha biashara zao kupeleka nje ya nchi na kwenda kufanya biashara huko ambako wanafikiri kutakuwa na mazingira mazuri ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili jambo linaleta athari kubwa sana kwa uwekezaji hapa nchini...

SPIKA: Sasa swali Mheshimiwa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Inasababisha athari kubwa sana kwa wafanyabiashara wetu kuendelea kuwekeza hapa nchini. Je, Serikali inatoa kauli gani kutokana na matatizo haya ambayo wafanyabiashara wameendelea kupewa na hawa watu wa *TRA?* (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili lilishawahi kuzungumzwa hapa mara kadhaa na tumelitolea maelekezo mara kadhaa kwenye Mamlaka yetu ya Mapato Tanzania. Nirudie tena kusema wafanyabiashara wote kwanza wawe na amani katika kufanya biashara zao

nchini. Wawekezaji wote waendelee kuwekeza na kuongeza mtaji zaidi ili kuwekeza zaidi kwa sababu Serikali imedhamiria kufungua milango ya uwekezaji nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba, kodi ni wajibu wa kila mmoja kulipa kodi kadri ya shughuli zake zinazomletea mapato zilivyo kwa ukubwa wake. Kwa hiyo, tumeielekeza mamlaka yetu (*TRA*) ihakikishe inapokwenda kukusanya kodi haitumii lugha ya kuudhi katika kukusanya kodi, haitumii nguvu katika kukusanya kodi.

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo sababu tulianzisha kitengo cha elimu ndani ya *TRA* kwa lengo la kumwelimisha mwananchi umuhimu wa kulipa kodi, lakini pia hata wanapopeleka bili yao au mahitaji ya ulipwaji wa kodi ni lazima pia apate elimu ya kodi hii imefikia huko kwa kiasi gani, hakuna sababu ya kumlazimisha, maelekezo haya tumeyatoa kwa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wote nchini pale ambapo kuna malalamiko, tumeunda chombo pia, ambacho kinasikiliza malalamiko ndani ya *TRA* yenye, lakini pia inapoonekana hata ndani ya *TRA* husikilizwi, Wizara ya Fedha ipo, ndiyo yenye mamlaka na *TRA*. Wana uhuru mkubwa wa kwenda kwa Kiongozi Mkuu wa eneo hilo, anaweza kuwa Mkuu wa Wilaya kwenye ngazi ya Wilaya, Mkuu wa Mkoa kwenye ngazi ya Mkoa ili kulalamikia jambo hili na hatimaye Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya watachukua hatua ya kuona kwa nini kumejitokeza tabia hiyo.

Mheshimiwa Spika, bado nirudie tena, *TRA* fanyeni kazi yenu kwa weledi. Endeleeni kuwa na mazungumzo na wafanyabiashara. Tulichogundua sasa ni kwamba kila mmoja anaona umuhimu wa kulipa kodi, muhimu zaidi ni kuendelea kuwashamasisha kulipa kodi, kuendelea kutoa elimu ya kulipa kodi, hata tathmini yake isioneshe viwango vikubwa zaidi ya mtaji ulioko pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ilipotokea pale Mkoani Lindi wananchi wote mmeona hatua kali tulizochukua dhidi ya Meneja wa Mkoa, Maafisa wenzake wote wawili ambao walikuwa wanalamisha wananchi kulipa kodi isiyokuwa na uhalisia lakini pia tuliwaondoa kazini wale ambao walikuwa wanafunga maduka bila utaratibu na bila kutoa elimu. Kwa hiyo, hatua hizi zitaendelea kuchukuliwa kwa yejote ambaye hatatumia utaratibu mzuri wa kukusanya kodi kwenye maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hii niendelee kuwasihii wafanyabiashara kuendelea kufanya biashara zao kwa amani kabisa na taratibu ambazo nimezieleza hapa zitafuatwa pindi utakapoona kuwa hutendewi haki katika ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Tunduma bado una swali la nyongeza?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninalo swali la nyongeza. Tunaelewa dhamira nzuri ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuamua kuwa Serikali ya Viwanda, tunajua dhamira yake ni kuhakikisha kwamba kunaongeza mapato kwanza ya Serikali ili kutekeleza majukumu yake kwa wananchi, lakini pia kuhakikisha kwamba inaongeza ajira kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haitachukua hatua ya lazima ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika nchi hii tafsiri yake ni kwamba, hatutaweza kufikia malengo ya Serikali. Je, Serikali inajipanga namna gani kushughulikia malalamiko haya? Kwa sababu, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba wametoa maagizo na wanachukua hatua, lakini bado watendaji walioko huko chini hawatekelezi kama ambavyo anazungumza ndani ya Bunge? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanataka kusikia Serikali inasema nini?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la awali kwamba, tunacho chombo ndani ya *TRA* cha kukatia rufaa pale ambapo mfanyakishara hajatendewa haki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, inaweza kuwa mfanyakishara akahofu kupeleka malalamiko yake ndani ya *TRA* kwa sababu ni chombo kimoja, bado anayo fursa ya kwenda kwa Viongozi Wakuu wa Serikali wanaosimamia shughuli zote za Serikali kwenye maeneo yao wakiwemo Wakuu wa Wilaya na pia, Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, pia itakapoonekana kwamba jambo hili na kama ambavyo ameemelea kwamba, bado kuna hiyo sintofahamu, Waziri wa Fedha mwenye mamlaka ya *TRA* yupo na anao wajibu wa kuitisha kikao na wana-*TRA* ili aweze kuwaambia utaratibu na mfumo na matakwa ya Serikali inayotufanya Serikali tuendelee kuwahamasisha wafanyakishara kuongeza mitaji ili kupanua biashara zao. Serikali ambayo sasa inaendelea kufungua milango kwa wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza nchini tukiwa na malengo pia ya kupata kodi na malengo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uko umuhimu sasa wa Waziri wa Fedha kukutana na *TRA* tena kuwakumbusha wajibu wao na kutoa maelekezo sahihi na kuwambia matakwa ya Serikali ili *TRA* iendelee kuwa ni sehemu ya hamasa ya wananchi kuwekeza zaidi ili tuweze kupata kodi ambayo wananchi wote sasa wanatambua umuhimu wa kulipa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namwambia Mheshimiwa Mwakajoka Mbunge, jambo hili tutaendelea kulifanyia kazi. Pia nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kuwaenzi wafanyakishara kwa sababu wanatupa tija. Hii miradi

yote inayotekelzewa sasa inatokana na kodi zetu. Nataka tuongeze miradi mingi zaidi ili tuweze kupata kodi na tuweze kutoa huduma hizi za jamii kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda wa nusu saa umeshakwisha. (*Makofi*)

Nawashukuru sana, wale ambao hamkupata nafasi basi wakati mwингine maana majina yalikuwa mengi kidogo, lakini angalau Kambi zote zimepata nafasi kidogo ya kuweza kuuliza maswali.

Nina maombi kadhaa ya watu wa Kamati ya Viwanda na Biashara kukutana kwa ajili ya suala hili ambalo bahati nzuri Mheshimiwa Lema ameliuliza na Mheshimiwa Waziri Mkuu akalijibu.

Kwa hiyo, maelekezo yangu ni kwamba hakuna sababu ya Kamati ya Viwanda na Biashara kukutana tena, maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwamba jambo hilo linafanyiwa kazi na bahati nzuri swali la mwisho la Mheshimiwa Mwakajoka lilihusu mambo haya ya *TRA* tunaamini litafanyiwa kazi vizuri.

Kwa maelezo ya mwanzo ambayo tulikuwa tumepata Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara kinachotokea ni kitu kidogo sana kama Waziri Mkuu alivyosema hebu tuipe nafasi Serikali, ni hiyo anayosema yule ya *TRA* kwa sababu anayetakiwa kufanya kazi ya ku-verify kitu hiki ni kitu gani ni Mkemia, sasa Mkemia akishasema wewe *TRA* unabisha sasa unabisha nini? La sivyo, upeleke kwa *third-party* basi achecki ajue hiki ni kitu gani halafu wewe ulipe kodi ile unayoambiwa na mkemia, vinginevyo inakuwa tabu. Kwa hiyo, hamna haja ya kukutana Kamati ya Viwanda na Biashara. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee, Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya Kawaida, tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond. Mheshimiwa Shally Raymond, tafadhali.

Na. 172

Ajira kwa Vijana Wanaohitimu Vyuo

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

(a) Je, Serikali inazo takwimu za kuaminika za vijana waliohitimu vyuo mbalimbali ambao hawajaweza kujajiri au kuajiriwa;

(b) Je, ni taaluma zipi zina fursa nyingi za zipi zina fursa chache za kujajiri au kuajiriwa baada ya kuhitimu?

(c) Je, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni ajira ngapi zilipatikana?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina takwimu sahihi na za kuaminika za vijana waliohitimu vyuo mbalimbali, lakini hawajaweza kujajiri au kuajiriwa ambazo hutumika katika kupanga na kutathmini utekelezaji wa programu zinazohusiana na masuala ya ajira. Takwimu hizo huptikana kuititia tafiti za nguvu kazi na tafiti za hali ya ajira na mapato zinazofanywa na ofisi ya Taifa ya Takwimu, pamoja na zinazofanywa na Taasisi za Elimu, kama vile *Tracer Studies*.

Kwa mujibu wa utafiti wa nguvu kazi nchini, vijana 65,614 ambaao ni wahitimu wa vyuo mbalimbali hawakuwa wamejiajiri wala kuajiriwa mwaka 2014.

(b) Mheshimiwa Spika, taaluma zenyе fursa ny ingi za kuajirika ni pamoja na fani za afya ya binadamu zikiwemo utabibu, uuguzi, ufundi sanifu wa maabara, ualimu na ufundi. Aidha, taaluma zenyе fursa chache za ajira ni pamoja na masomo ya utawala, biashara na rasilimali watu. Napenda kuchukua fursa hii kuwashauri wanafunzi kusoma masomo ya sayansi kwa kuwa yana fursa ny ingi zaidi za ajira hususani wakati huu ambaao Taifa linalekeea kuwa nchi ya viwanda.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kuanzia mwaka 2015 hadi 2017/2018, jumla ya ajira mpya 1,336,957 zillipatikana kama ifuatavyo:-

Kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Serikali ajira 593,986, sekta binafsi ajira 571,073 na Serikalini ajira 171,898. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza nimkuona.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika majibu ya msingi, Naibu Waziri ametueleza kwamba takwimu za mwaka 2014 miaka minne nyuma zinaonesha kuwa vijana 65,614 hawakupata ajira. Naamini kabisa baada ya miaka hiyo idadi hiyo imeendelea kuongezeka. Swali la kwanza; je, ni nini hasa kinawachofanya wahitimu washindwe kuajiriwa au kujiajiri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni hatua zipi mahususi zinazochukuliwa na Serikali kuwawezesha au kuwajengea wahitimu hao mazingira wezeshi ya kuajiriwa au kujiajiri. (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA

NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ameulizia kuhusu ni kwa nini sasa watu hawa wanashindwa kupata fursa ya kuajiriwa au kujajiri.

Mheshimiwa Spika, jibu lake ni kwamba katika nchi yoyote duniani suala la ajira limekuwa ni suala ambalo limekuja na changamoto nyingi sana, kutokana na kwamba nafasi za ajira zinazozalishwa na idadi ya watu ambao wana uwezo wa kufanya kazi vinakosa uwiano. Kwa hiyo, kama Taifa tunaendelea kuwa na mipango mbalimbali ya kuhakikisha kwamba tunakuja na mipango madhubuti ya kufanya nguvu kazi yetu hii kubwa iweze kupata nafasi ya kuajirika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tafiti ya mwaka 2014 ambayo wanaiita *Integrated Labour Force Survey* inasema takribani watu wa kuanzia miaka 15 na kuendelea ambayo ndio *working age population*, ambao wana uwezo wa kufanya kazi kila mwaka wanaojitokeza ni wengi zaidi kuliko nafasi za ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika kujibu swalı lake la pili, niseme tu kwamba kama Serikali tumeona kabisa suala la kwanza la kuweza kukabiliana na changamoto hii hasa kwa wahitimu wa vyuo vikuu, tumekuja na utaratibu wa kwanza wa kuzindua mpango maalum wa mafunzo ya uanagenzi na mafunzo ya vitendo ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua mwaka jana ambao unamfanya mhitimu ye yote wa Chuo Kikuu

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Ditopile, una swalı la nyongeza au una nini, maana yake Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu hapa. Endelea na majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA

NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwanza tumekuja na *framework* hiyo ambayo hivi sasa tutaanza kuwachukua wahitimu wa vyuo vikuu kwa kwenda kuwa-*attach* katika

mashirika mbalimbali, kampuni mbalimbali, waende kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu, hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, tumekuja na utaratibu wa kubadilisha *mindset* kwa mujibu wa sera ya ajira inasema ajira ni shughuli yoyote halali inayompatia mtu kipato. Kwa hiyo, tunawatoa sasa wale wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vyta elimu ya juu kutoka kwenye kufikiria kuajiriwa moja kwa moja ofisini na kubadilisha mtazamo kwenda kufanya shughuli mbalimbali zikiwemo za kilimo, ufugaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeandaa mazingira wezeshi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili vijana hao waweze kupata fursa na kupata mitaji na maeneo ya kufanya shughuli zao. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Ruth Mollel, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni kweli kama wengine walivyosema tuna tatizo kubwa la ajira. Hapa Dodoma nina hakika pia kuna tatizo la ajira. Maeneo ninayokaa mimi kule Kisasa ile mitaro ya maji ya mvua imekuwa ni madampo ya takataka, kumekuwa na nyasi nydingi, kumekuwa kama mazalia ya mbu, barabara ni chafu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukusanya hao vijana ambao hawana kazi katika makundi ili kusudi kuwapa ajira ya kufanya usafi katika mji huu. (*Makofii*)

SPIKA: Swali zuri sana linaulizwa kwa Mbunge wa Dodoma. Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma, majibu tafadhali. (*Makofii/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, nizungumze Kitaifa mpango ni nini? Kwa kutambua kwamba katika nchi yetu ya Tanzania tunao vijana wengi sana ambao wapo katika ma-group tofauti tofauti, kwa hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mpango

wa Ukuzaji wa Ujuzi kwa Vijana ambao una lengo wa kufikia vijana 4,400,000 ifikapo 2021 tumekuja na utaratibu wa kukusanya makundi haya ya vijana na kwenda kuwapa mafunzo mbalimbali ili wapate sifa ya kuajirika na kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumza sasa tunao vijana ambao walikuwa wako mtaani hawajawahi kusoma VETA, hawajawahi kusoma Don Bosco, wana ujuzi, tuna *program* ya kurasimisha ujuzi wao pasipo wao kwenda kusoma, hivi sasa tumeanza kuchukua kundi kubwa la vijana katika maeneo hayo, lakini pia tunao vijana ambao wanaendelea na mafunzo katika vyuo mbalimbali. Lengo lake ni kuwapatia ujuzi stahiki ili waje wasaidie katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nikirudi katika swali lake la kuhusu vijana waliopo hapa Dodoma. Mwaka jana ilisomwa hapa Bungeni na maelekezo yalitoka ya kuzitaka Halmashauri za Manispaa, Halmashauri za Wilaya kuhakikisha kwamba zinachukua vikundi vya vijana waliopo mitaani na kuwapa mitaani na kuwapa shughuli mbalimbali ambazo zinaweza zikafanywa na vijana kama hiyo aliyoisema Mheshimiwa Mbunge Ruth Mollel.

Mheshimiwa Spika, kama Mbunge wa Dodoma Mjini kwa sababu limenilenga hapa, niseme tu kwamba tunalichukua hilo tuone namna bora ya kuweza kuwakusanya vijana hao katika vikundi ili kuwawezesha na mitaji wafanye kazi ya kuzoa taka na kusafisha hiyo mitaro ambayo itakuwa ni sehemu ya ajira pia. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na TAMISEMI swali la Mheshimiwa John Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa John Wegesa Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini ambaye hayupo Bungeni, anamzika mdogo wake ambaye ameuawa na Polisi, naomba sasa swali lake namba 173 ijjibiwe kwa niaba ya wananchi wa Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Na. 173

**Walimu Kubebeshwa Gharama za
Vifaa vya Kufundishia**

MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y MHE. JOHN W. HECHE)
aliuliza:-

Mazingira ya ufundishaji kwa Walimu walio wengi nchini ikiwemo Wilaya ya Tarime yamekuwa siyo rafiki, ambapo Walimu wamekuwa wakibebeshwa mzigo wa gharama za vifaa vya kufundishia kama maandalio ya somo, chaki na kadhalika:-

Je, matumizi haya yatarekebishiwe katika mfumo huu wa elimu bure ulioanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara mbona unaweka maneno kwenye....

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa ruhusa yako, nimpe pole Mheshimiwa John Heche na wote ambao wamefiwa, Serikali ipo pamoja nao katika misiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa John Wegesa Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini, ambapo marekebisho yake madogo naomba yaingie katika *Hansard* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuptitia Waraka wa Elimu Na.5 wa mwaka 2015, uliota mwongozo wa Serikali kuhusu Elimu Msingi bila malipo, majukumu ya Serikali, jamii, wazazi, walezi, wakuu wa shule, Kamati au Bodi za shule, yamefafanuliwa vizuri sana kwenye Waraka huo. Mionganoni mwa majukumu ya Serikali ni kutoa ruzuku ya uendeshaji wa shule, inayogharamia chakula kwa wanafunzi wa bweni, ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada, vitambulisho, mitihani endelevi, mitihani ya Taifa, shughuli za michezo, maandalio ya somo, chaki na vifaa vingine. Hivyo siyo sahihi kwa Walimu kutumia fedha zao kugharamia maandalio ya somo na vifaa kama chaki.

Mheshimiwa Spika, nawaagiza Wakurugenzi wote wa Halmashauri, Maafisa Elimu wote wa ngazi zote na Walimu Wakuu kusimamia vizuri Mpango wa Utoaji Elimu Msingi bila malipo kama ulivyofafanuliwa katika waraka nilioutaja, kuanzia sasa Walimu wasikubali kubebeshwa mizigo ya gharama isiyowahusu.

SPIKA: Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali ningependa niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na maelezo haya bado Walimu hao wameendelea kuchangishwa michango na kwa sababu wanaowachangisha ni mabosi wao ikiwemo michango ya mwenye na Mwalimu asipokubali kuchanga michango anawajibishwa kule kwa sababu Waziri hayupo. Je, ni hatua gani zinachukuliwa kwa wakubwa wa Walimu hawa kwa maana ya Wakuu wa Idara za Elimu, Maafisa Elimu kama wataendelea kuwachangisha michango ya lazima kinyume na maelekezo ya Serikali? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa jibu hilo la Mheshimiwa Waziri ni wazi tunafahamu kwamba kuna waraka ulitembezwa ambao unatoa maelekezo, lakini baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais ilizuka sintofahamu na wananchi walikuwa wamechanga vyakula katika

mashule mbalimbali wakaanza kugawana, kuna miradi ya kuchangia madawati, madarasa na kuta mbalimbali wakaanza kukataa. Je, ni hatua gani za dharura kwa Serikali ili kutoa maelekezo kwa wananchi na wadau mbalimbali wa elimu warudi kama zamani washirikiane Walimu na walezi wa shule hizi ili shughuli za maendeleo ziendelee kuwepo kwa maana ya kuondoa kero za elimu katika maeneo mbalimbali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Kakunda tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, baadhi ya michango halali kwa mfano michango ya Mwenge inatakiwa ichangishwe kuititia Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na sio vinginevyo. Hii michango haitakiwi kuititia kwenye Kamati za Shule wala mikutano ya wazazi katika shule, hiyo hairuhusiwi. Kwa hiyo, Kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ndiyo inayoratibu masuala yote yanayohusu Mwenge michango ikiwepo michango ya mwenge.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kuhusu sintofahamu ya michango iliyosababisha baadhi ya watu kwenda kudai michango ambayo walikuwa wamechanga hapo awali. Napenda nisisitiza msimamo wa Serikali kwamba ilikuwa ni makosa hapo mwanzo tulivyokuwa tunachangisha kwa kuwahuisha Walimu kuwaondoa darasani wanafunzi kwa sababu tu wazazi wao labda kwa sababu ya umaskini wao hawakuwa wamechanga. Hilo ilikuwa ni kosa kwa sababu mtoto yule aliyekuwa anatolewa darasani hakuwa na kosa lolote.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanasi mama pale pale, isipokuwa utaratibu ambao sasa hivi tumeupitisha katika kutekeleza ule Waraka Na.5 wa Elimu

kuhusu michango ni kwamba michango yote sasa itaratibiwa na Serikali za Vijiiji na Kata chini ya usimamizi wa Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ya Kijiji, Halmashauri ya Kijiji ikikutana ikapendekeza, wanapeleka kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji, wakikubaliana wanapeleka maamuzi yao kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata ambayo ikipitisha inapeleka kwa Mkurugenzi, Mkurugenzi anatoa idhini ya mchango ule kuchangwa. Mchango ukishachangwa ukikamilika taarifa inatolewa kwa Mkurugenzi ili hatua zaidi za utekelezaji ziendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini.

Na. 174

**Watoto Waliozaliwa Njiti Kufariki Kabla ya
Kufikisha Miaka Mitano (5)**

MHE. MUSSA B. MBAROUK aliuliza:-

Tafiti zinaonesha Watoto njiti Tanzania wanapoteza maisha wakiwa chini ya miaka mitano:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani mahsusii kupambana na tatizo hili na kuhakikisha Watoto njiti walio hai wanakua bila matatizo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa Watanzania juu ya sababu zinazosababisha watoto kuzaliwa njiti?

SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk Mbunge wa Tanga, swali lako litajibowiwa na watu wa Tanga pia, Waziri wa Afya,

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, majibu tafadhalii.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa nchini Tanzania asilimia 17 ya watoto huzaliwa kabla ya muda wa mimba kukomaa. Watoto hawa huwa katika hatari zaidi ya kupoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kushindwa kupumua kutokana na kutokomaa kwa mapafu, kupoteza joto la mwili kwa haraka, kupata uambukizo wa bakteria, kushindwa kunyonya na kupata manjano, hivyo huhitaji huduma maalum.

(a) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imefanya na inaendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kuboresha huduma kwa watoto hawa na ili kuepusha vifo hivyo kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo:-

(i) Kuwapatia wajawazito dawa ya kusaidia mapafu ya mtoto kukomaa haraka iwapo mama anatarajiwa kujifungua kabla ya wakati.

(ii) Kuanzisha huduma ya Mama Kangaroo katika ngazi ya hospitali ili watoto njiti ambao hawana changamoto nyingine za kiafya watunzwe kwa utaratibu wa ngozi kwa ngozi na wazazi wao ili watunze joto mwilini. Kuanzia mwaka 2009 mpaka sasa jumla ya hospitali 63 zinatoa huduma ya Mama Kangaroo nchini.

(iii) Kununua na kusambaza vifaa vya kuwashudumia watoto njiti ambao wana matatizo ya kiafya. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za Oksijeni, mashine za kutibu manjano yaani *phototherapy machines*, mashine za

kufuatilia hali ya mtoto akiwa kwenye matibabu, mashine za kuongeza joto na vipima joto veya chumba cha kutibia watoto hawa.

(iv) Kuendelea na mafunzo ili kuwajenjea uwezo watoa huduma za afya juu ya namna ya kumhudumia mama anayetarajia kujifungua mtoto njiti kama vile mama mwenye ujauzito wa watoto pacha, mama mwenye shinikizo la damu wakati wa mimba na wenyewe upungufu wa damu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ili waweze kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya afya ya uzazi na mtoto, ikiwemo dalili za hatari wakati wa ujauzito, sababu zinazopelekea kuzaliwa kwa watoto njiti na umuhimu wa kuhuduria kliniki mapema ili jamii iweze kuhamasika na kuchukua hatua stahiki na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inaendelea kuwashamasisha wajawazito kumeza vidonge veya kuongeza damu, kumeza dawa za kuzuia malaria pamoja na kuwasisitiza wajawazito kupata muda wa kutosha wa kupumzika na kulala kwenye vyandarua vyenye dawa.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Tanga Mjini, swali.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza kwa kuwa kuna tatizo kubwa la watoto kuzaliwa na vichwa vikubwa au vichwa kucaa maji. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia tatizo hili Serikali inalishughulikia viyi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali inamudu kutoa dawa bure kwa wale watu wenyewe VVU au watu wenyewe *TB*; je, kwa nini isichukue jukumu la kuwatibu watoto hawa ambao wanaozaliwa na vichwa vikubwa ili kuondoa mateso yale ya maradhi ya vichwa vikubwa lakini pia kuondoa simanzi kwa wazazi. Kwa nini Serikali isichukue jukumu la kutoa huduma hiyo bure kwa magonjwa hao? *Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tafadhalii.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, suala la watoto wenye vichwa vikubwa Serikali imechukua hatua gani. Jambo kubwa ambalo Wizara na Serikali inaendelea kulifanya ni kuhakikisha na kuendelea kuhimiza akinamama wajawazito kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa na Daktari.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu tatizo la watoto wenye vichwa vikubwa pamoja na mgongo wazi tunaweza kulitatu endapo mama ataweza pia kuongezewa dawa kwa mfano tunasema *feo* dawa za *folic acid* ambapo nimeelekeza ziwepo katika vituo vyote vyao kutolea huduma na nafurahi kusema kwamba sasa hivi ukienda kwenye zahanati ukienda kwenye kituo cha afya utakuta dawa zote za *feo* zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuhimiza wanawake kuhudhuria kliniki. Kwa mujibu wa takwimu ni asilimia 24 tu ya wanawake Tanzania wajawazito wanahudhuria kliniki ndani ya wiki 12 baada ya kujigundua wajawazito. Kwa hiyo pale ambapo kuna matatizo yanaweza yasioneokane.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni suala la tunawasaidia vipi watoto wenye vichwa vikubwa na hili naomba nilibebe na Serikali ipo tayari kugharimia gharama zote za matibabu kwa watoto wote wenye vichwa vikubwa na tumeanza katika Taasisi yetu ya *MOI* tunafanya upasuaji bila malipo kwa watoto wote wenye vichwa vikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe rai kwa wanawake wenzangu wasiwafiche watoto wenye vichwa vikubwa, bali waende katika vituo na hospitali za Serikali ili tuweze kuwasaidia na kuwapa huduma.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru. (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda.

Na. 175

Kuwawezesha Wavuvi wa Ziwa Victoria

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA aliuliza:-

Ni Sera ya Taifa kuwawezesha Wavuvi ili wafanye shughuli zao kwa tija:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Wavuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wavuvi hususan kununua vifaa kwa bei nafuu, Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani yaani VAT kwa *engine* za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu, vifungashio na nyavu zenyewe. Pia kulingana na chapisho la Afrika Mashariki kuhusu ushuru wa pamoja la mwaka 2007 - 2012, *engine* za uvuvi, malighafi zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake vinavyonunuliwa katika Soko la Afrika Mashariki hupewa pungozo la kodi ama kufutiwa kodi kabisa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia kupungua kwa bei za zana za uvuvi ambapo wavuvi wataweza kunufaika na mpango huo hatimaye kumudu kununua zana za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanzisha Benki ya Kilimo ambayo inatoa fursa kwa wavuvi kupata mikopo kwa ajili ya kununua zana za uvuvi. Aidha, Serikali inaendelea kuwashamasisha wavuvi kuijunga kwenye Mifuko ya huduma za kijamii ikiwemo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kama vile NSSF

ambapo Mfuko wa NSSF umeanzisha utaratibu unaojulikana kama Wavuvi *Scheme* ili kuwawezesha wavuvi kupata huduma za kijamii zinazotolewa na mfuko huu kama vile huduma za afya pamoja na kupewa malipo ya uezeni.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na operesheni ya kudhibiti uvuvi haramu na biashara ya haramu ya mazao ya samaki inayokwenda kwa jina la Operesheni Sangara. Operesheni hii inalenga katika kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinalindwa ili ziweze kuwasaidia wananchi na Taifa kwa ujumla katika kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na kuongeza Pato la Taifa. Pia inalenga katika kutunza rasilimali na mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Lolesia, tafadhalii.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na jinsi ambavyo Serikali imejipanga kuwawezesha wavuvi. Vilevile wapo wavuvi ambao hawana uwemo kabisa, wanahitaji kuwezeshwa na Serikali. Ningependa kujua sasa nini mkakati wa Serikali wa kuwapatia ruzuku wavuvi hawa ili waweze kujikwamua kiuchumi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wavuvi walioko katika Mkoa wa Geita hasa katika Jimbo la Busanda katika maeneo ya Bukondo, Nyakasamwa pamoja na Nungwe wanazo changamoto nydingi. Ningependa kujua Mheshimiwa Waziri ni lini atakuja kututembelea katika Jimbo la Busanda ili kubaini changamoto hizi na kuweza kuzitafutia ufumbuzi wa kutosha?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Ulega unaalikwa Busanda, majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza linahusu ruzuku kwa wavuvi. Wizara inayo *program* maalum ya kuwawezesha wavuvi ambao wapo katika utaratibu wa vikundi ambapo tunatoa mashine za ruzuku, wao wenyewe wavuvi wanachangia asilimia 60 na Wizara tunachangia asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, hivyo, shime Mheshimiwa Mbunge aende akawahamashe wavuvi wake waweze kuwa katika vikundi, wapitishie barua zao za maombi kwa Halmashauri ya Wilaya kwa maana ya Mkurugenzi na hatimaye azilete Wizarani, tunamhakikishia Mbunge kumsaidia kuweza kupata mashine hizo kwa ajili ya vikundi vyake.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, bibi yangu huyu anaomba niende kuwatembelea babu zangu kule Busanda. Nataka nimhakikishie kwamba baada ya Bunge hili mimi na yeye mguu kwa mguu mpaka Busanda kuhakikisha nakwenda kukutana na wavuvi wa kule Busanda.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo ni la Wizara ya Maji na Umwagiliaji na linaulizwa na Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, tafadhalii.

Na.176

Mradi wa Maji katika Mji wa Itigi

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Itigi alitoa ahadi ya kusaidia mradi wa maji katika Mji wa Itigi:-

Je, Serikali imetekeleza kwa kiasi gani ahadi hiyo?

NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji katika Mji wa Itigi ambao ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Mradi huu utahusisha Vijiji saba (7) vya Itigi - Mjini, Mlowa, Zinginali, Majengo, Tambuka-reli, Kihanju na Songambele. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni utafiti wa vyanzo vya maji yaani (*hydrogeological investigation*) pamoja na uchimbaji wa visima saba.

Mheshimiwa Spika, kati ya visima saba (7) vilivyo chimbwa visima vinne (4) vilipata maji ya kutosha kwa kiasi cha mita za ujazo 3,048 kwa siku ikilinganishwa na mahitaji ya sasa ya mita za ujazo 1,248 kwa siku. Aidha, kazi ya usanifu wa miundombinu ya maji itakayojengwa umekamilika katika Vijiji sita vya Mlowa, Zinginali, Songambele, Tambukareli, Itigi Mjini na Majengo. Kwa upande wa Kijiji cha Kihanju usanifu huo unaendelea. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa kujenga miundombinu katika vijiji sita (6) zitaanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utatekelezwa kwa awamu tatu; Awamu ya kwanza inahusisha utafiti wa vyanzo vya maji na uchimbaji wa visima ambayo imekamilika. Awamu ya pili inahusisha usanifu wa msambazaji wa maji ambapo umekamilika katika vijiji sita na uandaaji wa makabrasha ya zabuni na manunuzi ya wakandarasi wa ujenzi. Awamu ya tatu itahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huu kunatarajwa kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia 47 ya sasa kufikia asilimia 85 kwa wakazi wa Mji huo, pia itawezesha kuanzishwa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Itigi.

SPIKA: Mheshimiwa Massare, swali la nyongeza tafadhalii.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ameonesha dhamira ya kweli ya Serikali ya Awamu ya Tano kuwatua ndoo kichwani akinamama, nina maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; wananchi wa Itigi kwa sasa wanununa maji ndoo moja Sh.1,000 hususani akinamama. Je, sasa Serikali, Mheshimiwa Waziri anaweza akawaambia nini wananchi wa Itigi ambao wanamsikiliza na kumwona katika TV muda huu, kwamba mradi huu utatangazwa lini, kwa kuwa kila kitu kimeshakamilika na wananchi wa Itigi tunataka kumsikia leo anasema nini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, yuko tayari sasa kwenda kuongea na wananchi wa Itigi kwamba mradi huu tunauanzisha lini katika kipindi cha mwezi huu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Maji na Umwagiliaji, tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kama majibu ya msingi ambavyo yameelezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba utekelezaji wa miradi unakwenda katika awamu tatu na awamu zote sasa zimekamilika, tunakwenda kwenye utekelezaji. Pia tuna utaratibu ambao tunachimba visima na kufunga pampu za mkono wakati tunasubiri mradi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama shida iko namna hiyo watu wanununa ndoo moja Sh.1,000 namwombaa Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane, kwa sababu bajeti yake ipo, tutachimba visima vyta haraka na kufunga pampu ili wananchi waachane na hilo la kununua maji ndoo Sh.1,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili; nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kuongozana naye kwenda Itigi tukaongee na wananchi huko baada ya bajeti yangu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Longido ni shida kubwa ya maji. Swali la nyongeza.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, wananchi wa Longido wamekuwa wakisubiri kwa hamu kukamilishwa kwa mradi mkubwa wa maji safi na salama kutoka Mlimani Kilimanjaro, Mto Simba kuja Longido. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba mradi huu kwa kasi inayoendelea sasa hivi unatarajiwu kukamilika lini?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Isack Kamwelwe, majibu tafadhali.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa jinsi anavyofuatilia utekelezaji wa miradi ya maji katika Jimbo lake na Serikali hii ya Awamu ya Tano tayari ina mkataba wa zaidi ya bilioni 16 kwa ajili ya Halmashauri yake ya Longido.

Mheshimiwa Spika, uko mradi mkubwa unaotoa maji Mlima Kilimanjaro kilomita 64. Kulikuwa na matatizo ya kupata bomba la chuma lakini Serikali, Wizara imeingilia kati Mkandarasi ameingia mkataba na kiwanda cha kuzalisha mabomba na mabomba yameanza kuingia tayari kule *site*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake kwamba kuanzia sasa tunaenda haraka ili tuhakikishe wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha tuendelee na mambo mengine.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Tuanze na wageni walioko jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Katibu Mkuu, Meja Jenerali Mstaafu Projest Rwegasira; Naibu Katibu Mkuu Balozi Simba Yahaya. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wakuu wa vyombo vilivyopo chini ya Wizara; Inspeka Jenerali wa Jeshi la Polisi Ndugu Simon Sirro. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mbona wengine hampigi makofu huku? Msiwe na ubaguzi jamani. (*Kicheko*)

Pia wapo Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza Dkt. Juma Malewa; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Thobias Andengenye; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Makakala; (*Makofi*)

Vile vile wapo Kamishna wa Jeshi la Polisi, Zanzibar, Ndugu Mohamed Hassan; Kamishna wa Uhamiaji, Zanzibar, Ndugu Johari Sururu; Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*), Ndugu Andrew Massawe; Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) Zanzibar, Ndugu Hassan Hassan; wameambatana pia na Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Wizarani. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 40 wa Mheshimiwa Kapteni George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni watumishi na wanafunzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tawi la Tabora, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline S. Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, hawa wanatoka Chuo cha Mipango, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni Watatu wa Mheshimiwa Amina Mollel ambao ni Waandishi wa Habari wa *Sunrise Radio* iliyopo Mkoani Arusha, wale pale karibuni sana *Sunrise*. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria na Mheshimiwa Zainabu Amir ambaye ni rafiki yao Ndugu Jagdish Patel, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni Wawili wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaao ni ndugu zake kutoka Pangani Mkao wa Tanga, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni wawili (2) wa Mheshimiwa Hamidu Bobali ambaao ni wapiga kura wake kutoka Mchingga Mkao wa Lindi, ahsante. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM, Wilaya ya Karagwe, Ndugu Nurubert Neckemiah, ahsante. (*Makofi*)

Wageni 17 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT, Mkao wa Dodoma, Ndugu Neema Majule, karibuni sana UWT Dodoma. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Allan Kiula ambaye ni mpiga kura wake kutoka Wilayani Mkalama, Ndugu Christine Kingu, karibu sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambaye ni mama yake mdogo, Ndugu Gonsalva Mrope, karibu mama mdogo. (*Makofi*)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Mussa Ntimizi ambaao ni wana CCM kutoka Igalula Mkao wa Tabora wakiongozwa na Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya, Ndugu Habibu Sungwa. Karibuni sana Wanyamwezi ninyi, angalieni Dodoma ni Jiji eeh, msije mkagongwa na magari huku. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba juzi tarehe Mosi mwezi wa Mei ilikuwa ni Sikukuu ya Wafanyakazi duniani na nchini kwetu na Bunge tulikuwa na wafanyakazi

ambao baada ya wafanyakazi wa Bunge kukutana wakawa wamewachagua wenzao kuwa ni wafanyakazi bora kwa utendaji kazi wao uliotukuka.

Ninao watatu (3) ambao ningependa kuwatambulisha kwenu ambao ndiyo Mshindi wa kwanza wa pili na wa tatu. Mshindi wa nafasi ya kwanza ni Mhudumu katika Ofisi ya Katibu wa Bunge Ndugu Rukia Shabani, asante sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, huyu Rukia ni mtumishi wa siku nyingi hapa Bungeni na ni mchapakazi kweli. (*Makof*)

WABUNGE FULANI: Asimame.

SPIKA: Asimame tena? Huyo hapo, ahsante sana Rukia.

Mheshimiwa Jenista alikuwepo Iringa lakini hatukupata nafasi ya kumpa mkono Mheshimiwa Rais, sijui ilikuwaje. Wafanyakazi wetu wa Bunge, kule Moshi hawakupata nafasi na Iringa pia hawakupata nafasi, basi mwakani angalau wakumbukwe kwenye venue nytingine. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Iringa natumaini mliona gari la Bunge liliyokuwa likiendelea na kikao chetu cha Bunge kilivyokuwa kinaendelea katika Uwanja wa Samora pale. Kwa hiyo Rukia yeye atapata shilingi milioni nne kama zawadi yake. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, mfanyakazi namba mbili ni Afisa Habari na Itifaki Ndugu Patson Sobha, Ahsante sana. (*Makof*)

Mfanyakazi namba tatu ni Katibu Msaidizi wa Bunge ndugu Grace Bidya. (*Makof*)

Huyu ni mmoja wa Makatibu wa Kamati na kwa kweli ni mchapakazi, aliwahi kuwa Katibu wa Kamati yangu

wakati mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naamini ni mchapakazi kabisa, nafahamu kazi zake. (*Makof*)

Hongereni sana, mmeona makofi ya Waheshimiwa Wabunge wanaridhika na kazi mnayofanya, ongezeni bidii na tija katika kazi zenu. (*Makof*)

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Haya Katibu endelea kuwataja.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mheshimiwa Anna Gidarya na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

SPIKA: Sasa kwa sababu mko wengi naomba tufanye kifupi kifupi. Mheshimiwa Mbatia ulisimama?

MHE. JAMES F. MBATIA: Hapana.

SPIKA: Okay. Tuanze na Mheshimiwa Yussuf kifupi ili tuokoe muda.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, sitaki kusoma Kanuni kwa sababu nimepewa hii karatasi asubuhi kwa hiyo lilitokea leo asubuhi humu Bungeni. Tunapochangia tunarejeshewa hizi karatasi *Uncorrected Hansard* ili kufanya masahihisho, lakini naomba mwongozo wako tu kujua Waandishi wetu wanapewa semina ya namna ya lugha au vipi. Kwa mfano, mimi nimesema ‘hujamsikia’, yeye anaandika ‘ujamsikia’. Kwa hiyo, vile anavyozungumza ndivyo anavyoandika. Je, wanapewa semina ya namna ya lugha ya kuzungumza na lugha ya kuandika?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako katika hili. (*Kicheko*)

SPIKA: Ujumbe wako umesikika na umeeleweka, nia yako ni nini tumeipokea, kwamba Katibu hebu semina ya Kiswahili iwe inafanyika kwa watumishi wetu wa Bunge.

Mheshimiwa Anatriopia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sitasoma kanuni kwa ajili ya ku-save muda, lakini wakati tupo hapa ndani, yapo mambo mengi yanajitokeza na yanaendelea kujitokeza kwenye tasnia mbalimbali na hasa vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, kumetokea Madaktari wa dharura, tumeona kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari watu wakichoma sindano/wakichanja watoto wetu wa kike hiyo chanjo ya saratani wengine wakiwemo Wabunge, Wakuu wa Wilaya na wanasiwa wa vyama vyetu vya siasa. Sasa nimepata tahaaruki na changamoto, kwamba sisi ambao hatuna taaluma ya udaktari au ya uuguzi tunachoma sindano watoto. Changamoto ya sindano tunaweza tukawasababishia maradhi ikiwa ni pamoja na kupooza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimesikia Mheshimiwa Waziri ametoa kauli, lakini kauli hiyo haitoshi kwa sababu nimesoma pia miiko ya Madaktari na taratibu wanazopaswa kupitia, nimejiridhisha kwamba hao Madaktari walioruhusu wanasiwa kuchoma sindano hawawatoto wetu wamevunja miiko. Pia wanasiwa walikubali kwenda kuchoma sindano hawa watoto ilhali wakijua hawana hiyo taaluma wamevunja pia maadili yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa mwongozo ninaouomba kwako, naomba hawa watu walichoma sindano waagizwe kuomba radhi, hao watoto wapewe fidia na vile vile tupewe taarifa; wale Madaktari walioruhusu hicho kitendo kifanyike, mabaraza husika yanachukua hatua gani dhidi ya hawa watu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Tutaiachia Serikali iendelee kulitazama jambo hilo na kufuutilia kwa ukaribu maana ni madai mengi na mazito.

Mheshimiwa Anna Gidarya.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwongozo niliokuwa nauomba ni huo ambaao umesemwa na Mheshimiwa Anatropia, hata hivyo nimwombe Waziri atoe kauli kuhusu haya mambo yanayoendelea juu ya zoezi la chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi tunaojua masuala ya kitabibu, huwezi tu kwenda kumchoma mtu chanjo; chanjo nyingi ndizo zinazoleta matatizo makubwa hasa kuondoa usikivu. Watoto wengi masikio yanaziba na wengine wamepata ulemavu wa mikono. Ukrejea chanjo ya pepopunda shulenii mwaka 1994 wanafunzi wengi walipata ulemavu kutokana na kutokuwa na taaluma ya uchomaji chanjo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukizingatia chanjo ya kifua kikuu kwa watoto, ni watoto wengi pia wamepata ulemavu wa mikono kwa sababu ya kutokuwa na taaluma ya uchomaji chanjo. Tunaomba wafuatuutilie na watuletee orodha ya watoto walioathirika kupitia chanjo hii ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi. Tumeona ni mambo mengi yanafanyaika *lobbying* nyingi, tumemwona Mbunge ameenda kumchoma mwanafunzi ameshika kama mkuki, chanjo haichomwi hivyo, sisi wengine tumeshafanya kazi huko. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, swali namba 176, nataka maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Maji ni tatizo kubwa nchi nzima hasa vijijini. Kuna miradi ya maji ya

World Bank imeanza kutekelezwa Vijijini zaidi ya miaka kumi haijakamilika na kuna miradi ina miaka mitatu haijakamilika, kwa mfano Kongwa na Mpwapwa makandarasi hawalipwi. Je, Waziri ana kauli gani wananchi wanahitaji maji vijijini. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante, hayo watakuja nayo kwenye bajeti yao wakati ukifika angalau wameshapata vionjo tayari, watajua *style* ya kuingia nayo Bungeni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Pauline Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nami naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) juu ya suala ambalo limejitokeza asubuhi wakati Mheshimiwa Shally Raymond akiuliza suala la ajira kwa vijana wetu. Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kwamba si lazima waajiriwe kwenye mfumo huu wa Serikali, wanaweza wakajajiri.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza benki washushe riba *at least* mpaka asilimia kumi ili mikopo hiyo iwasaidie vijana wetu wajajiri, lakini kauli hii haijawahi kutekelezwa na riba hizo hazijashushwa ili vijana wajajiri.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, kwa nini Serikali wasije wakatujibu sisi Wabunge maana vijana hao wamekuwa wakituuliza wamefikia hatua gani kushusha hizi riba ili vijana wachukue mikopo na wajajiri? Naomba mwongozo wako. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabla sijaomba mwongozo wangu, nikupongeze maana yake leo nilikuwa nafuatilia wakati wa maswali kwa Waziri Mkuu uliweza kutoa uwiano mzuri kabisa kulinganisha na vyama; uliweza kuwapa CCM watatu, CHADEMA wawili na CUF wakapata mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tupo kwenye Bunge la Bajeti, kipindi ambacho ni muhimu sana kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania kuweza ku-*allocate* fedha kwa maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jana wakati tunahitimisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwenye kipindi muhimu kabisa cha kushika shilingi ya Waziri ambapo tunaweza kueleza mambo ya kisera ili yaweze kupewa utatuzi mzuri, aliyekuwa kwenye kitu aliweza kusema mwanzoni kwamba atatoa majina mawili mawili akiangalia na kuzingatia muda.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo cha kushangaza wakati tumeingia anaanza kutoa aliweza kutoa nafasi tano kwa upande wa CCM ilhali akiwa anaangalia muda unaenda, akaongeza dakika 30 anacheiki muda akatoa nafasi tano. Kwa makusudi kabisa ambayo milmi nyaona, wakati wakishika shilingi akawa anatoa nafasi mpaka kumi kwenye hoja moja.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza kabisa waliishia kutoa watu watano wa CCM, watu wawili wa CHADEMA wakakosa, mtu mmoja wa NCCRMageuzi akakosa na watu wa CUF wakakosa kabisa akaingia kwenye *guillotine*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni dhana mbovu sana kabisa na haitutendei haki hasa kwenye kipindi hiki ambacho tupo kwenye bajeti, tulihuzunika sana. Hii naomba kwa kweli uweze kutoa mwongozo kwa wale ambao unakuta unawapa nafasi ya kukaa kwenye Kiti chako waweze kuzingatia uwiano. Hapa tunalijenga Taifa wote hatutaki unyanyapaa, kama ulivyofanya leo asubuhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kuna kipindi tulikaa humu ndani mpaka saa sita usiku kupitisha bajeti. Nilitarajia baada ya ile nyongeza yake ya dakika thelathini zikiisha Mheshimiwa Jenista angweza kusimama katuomba Wabunge ili tuweze kuongeza muda ukizingatia Wizara ya Elimu ni Wizara nyeti sana na elimu yetu ipo /CU sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako na uwaelekeze watendaji ambao wanakaa kwenye hicho kitu Wenye viti na hata Naibu Spika akikaa waweze kutendea haki, kipindi hiki muhimu sana cha bajeti, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mwongozo wangu naomba kutokana na swali la 173 juu ya vifaa vya kufundishia. Katika vifaa hivi vya kufundishia wapo pia Walimu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu, Toleo la mwaka 2008 unaitaka Serikali kuwapatia watumishi wenye ulemavu nyenzo muhimu za kufundishia. Kwa bahati nzuri jana tumemaliza bajeti ya Wizara ya Elimu na mambo haya yalikuwa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa katika swali la leo limezungumzia kwa ujumla Walimu, lakini katika kila jambo linalomgusa mwanadamu yoyote hapa nchini na popote pale, watu wenye ulemavu linakuwa ni *double*. Kwa maana kwamba changamoto kwa ajili ya watu wenye ulemavu inakuwa ni kubwa zaidi. Serikali imetoa mwongozo na huu mwongozo ni wa utumishi wa umma kwa watumishi wa umma wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Mwalimu ambaye haoni, anayo taaluma nzuri ya kufundisha. Umempuka katika shule humpi mashine ya *braille* na wasaidizi ambao wanatambulika kisheria waweze kumsaidia. Huyu Mwalimu atawezaje kutimiza majukumu yake katika kuwasaidia watoto na watoto wote kwa ujumla wenye mahitaji maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwongozo huu unalenga pia hata watumishi wa umma walioajiriwa, huu ni mwongozo ambao umetoka utumishi, na mwongozo huu upo kisheria.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana bahati nzuri, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, niliuliza swali na akaagiza wizara inayohusika kuhakikisha kwamba Walimu hawa wanapatiwa hizo nyenko, lakini hali ni mbaya. Tunawasaidiaje wakati huu ambapo tupo katika karne hii ya teknolojia na maendeleo kuhakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma? Walimu hawa hatuwawezeshi nyenko za kutosha, watumishi wa umma ambao tumewaaajiri kwa mfano tu katika Jiji la Dar es Salaam mpaka kufika kazini ni shida.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako juu ya watu wenye ulemavu na hawa Walimu hawa kuhakikisha kwamba vifaa hivi vinapatikana.

Mheshimiwa Spika, kuna...

(Hapa baadhi ya wabunge waliongea bila mpangilio)

SPIKA: Ahsante sana Amina Mollel, naamini umeeleweka.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Nashukuru ujumbe wangu umefika, lakini sisi wote ni watu wazima wakati mwingine hakuna haja ya kuzomeana, hata na sisi pia tunajua kuzomea.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi pia nasimama kwa kanuni ya 47(1) kwenye jambo hili ambalo Mheshimiwa Anatropia na Mheshimiwa Gidarya wamelisema, lakini nimeamua kusimamia Kanuni ya 47(1) ili kitie chako sasa kiweze kuahirisha shughuli za Bunge zilizopangwa leo kwa muda ili tuweze kujadili jambo hili la dharura.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendesha zoezi zuri sana la chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi, hili ni jambo jema; na utakumbuka saratani hii imekuwa ikipoteza maisha ya

wazazi kwa muda mrefu katika nchi hii. Kwa hiyo, Serikali imekuja na suluhisho la kuanza na hii chanjo wa mabinti wenye umri wa miaka 14 nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, matendo ambayo yameingilia kati hapa siku mbili hizi za uzinduzi yanapelekea kuwafanya wazazi kuogopa kuwaruhusu watoto wao kwenda kupata hii chanjo. Matendo yaliyojitokeza yanayoonekana sana ni haya ya Mkuu wa Wilaya ya Kibaha Bi. Asumpta Mshama ambaye naye si Daktari amekwenda kumchoma mtoto kama ishara ya uzinduzi.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Goodluck Mlinga naye ameenda kwenye uzinduzi Jimboni kwake naye akachukua sindano ya chanjo kumchoma mtoto ilhali yeye si mtaalam na hata kama angekuwa mtaalam siku hiyo hakuwa kwenye orodha ya watu ambaa walipaswa kutoa hiyo chanjo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa vitendo hivi vinawafanya wazazi kuwa na woga, kwamba nikimruhusu mwanangu aende kwenye chanjo anaweza akateuliwa kuwa ndiye awe wa kwanza akachomwe sindano na mgeni rasmi ambaye si mtaalam.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba ili tusiathiri zoezi hili zuri, uliruhusu sasa Bunge lako tuweze kujadili, pengine kuna mifano mingi kwenye kona nyiningine nchi hii ambazo nazo zinaathiri hili zoezi. Kwa hiyo, utupatie nafasi kama ambavyo Kanuni ya 47(4) inavyotaka, unipe nafasi ili niweze kutoa hoja Waheshimiwa Wabunge waweze kujadili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba ruhusa yako...

MBUNGE FULANI: Toa hoja!

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Kanuni hii haikutaki utoe hoja moja kwa moja ni mpaka uruhusiwe na Spika, naomba ruhusa yako.

SPIKA: Ahsante sana, mimi nilipomuuiliza Mheshimiwa Mlinga alisema alikuwa ana-*demonstrate* tu hakugusa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Afya kama kuna ufanuzi tafadhalii nakupa fursa.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa *ku-raise concern* kuhusu suala la utaalam katika uchomaji wa sindano. Kwanza nataka kukiri kwamba uchomaji wa sindano una taratibu zake, huwezi kujichomea sindano hovyo hovyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuwahakikishiwa Waheshimiwa Wabunge na watanzania wote kwamba Mheshimiwa Asumpta Mshama, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha na Mheshimiwa Goodluck Mlinga hawakuwachoma chanjo watoto husika ila walifanya kama vile *demonstration*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuendelea kutoa maelekezo kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuzingatia miongozo ya utoaji wa huduma za afya; kwa sababu hata kitendo cha kushika sindano kama si mtaalam si kitendo cha kitaaluma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tulishakemea na Mganga Mkuu wa Serikali leo atatoa tamko rasmi. Kwa hiyo, niendelee kuwaomba na kuwahimiza wazazi na walezi kupeleka watoto wao kupata chanjo kwa sababu chanjo hii ni kwa ajili ya maendeleo yao. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, hilo limemaliza ile miongozo mitatu; la mambo ya riba na nini tunawaachia Wizara ya Fedha na benki kuendelea kuzi-*monitor* hizi riba ili vijana waweze kupata mikopo kadri zinavyoweza kushuka.

La Mheshimiwa Esther Matiko tunalichukua, ulikuwa ni ushauri kwa kiti; huwa tuna vikao vyetu tutajaribu kukaa tuone ni namna gani tunawekana sawa. (*Makof*)

La Amina Mollel vilevile limefika, Mheshimiwa Waziri wa Elimu yupo, Profesa na Serikali kwa ujumla imesikia jinsi gani ya kuwasaidia hasa Walimu ambao wana mahitaji maalum. Nawashukuru sana. (*Makof*)

Mwisho kabisa, kuna mwongozo umewahi kuulizwa na Mheshimiwa Aida Khenan na leo amekumbusha, kwamba kuna kuvua viatu kwenye mageti yetu kwa ajili ya usalama na inaleta shida, baadhi wanapata *fungus* baadaye kwa kukanyaga chini na kadhalika.

Niseme kwamba kwa masuala ya usalama wetu sisi wote hatuwezi kushusha viwango, ikibidi uvue kiatu itabidi uvue tu kiatu, kwa sababu ndio taratibu na tunafanya hivi ili hata mkisafiri nchi za nje huko masharti yenewe ni hayo hayo. (*Makof*)

Cha kufanya ni kwamba ukikijua kiatu hiki kila ukipita pale kinapiga kelele unaacha unavaa kingine, hicho utakitumia kwenye maeneo mengine. Ukiwa na mkanda ambao kila ukipita unapiga kelele, unaacha ule mkanda unavaa mwingine, hivyo hivyo. Naamini Waheshimiwa Wabunge tunamudu kuwa na *pair/kadhaa* za viatu kwa hiyo haiwezi kuwa ni *issue* kubwa hivyo. Kwa hiyo, hapa ni kujua tu namna kiatu kilivyotengenezwa, kama kina chuma ndani lazima kitapiga kelele na kikipiga kelele hawawezi kukuruhusu kuingia bila kukivua na kukipitisha chenyewe peke yake waweze kuona kuna nini ndani yake.

Kwa hiyo nawaomba tu vitu vingine, hata kama kiatu hicho unakipenda namna gani basi mawili; ama ukubali kuwa unavua unapita kwa mguu wanakicheki, au la sivyo, kuondokana na adha hiyo unakiacha nyumbani unavaa kingine. Ahsante.

Katibu, tuendelee sasa.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

SPIKA: Ahsante sana. Sasa naomba nimwite moja kwa moja Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, karibu tafadhali kwa hotuba yako, karibu sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wale ambaao viatu vyao vinapiga kelele, watumie viatu viliwyotengenezwa na Kiwanda cha Magereza Tanzania kwa sababu havigipi kelele kama ambavyo unaona Mheshimiwa Waziri Mkuu akipita na mimi nikipita havigipi kelele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, likubali kupokea...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, dakika tu; Mheshimiwa Najma Giga anakuja kuchukua nafasi hapa.

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tuendelee.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na kuniwezesha kutoa hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo itajadiliwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza vyema Taifa letu na kuendelea kusimamia amani na utulivu na usalama wa nchi ambayo ni nguzo muhimu sana katika kuleta maendeleo ya uchumi wa viwanda na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwaletaa maendeleo wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi wengine wote wakuu wa Serikali pamoja na Bunge kwa kuendelea kusimamia shughuli mbalimbali za Taifa. Aldha, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Niwahakikishie kuwa ushauri waliotaa utasaidia sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na utazingatiwa kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangwa. Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Sh.930,396,817,000 ambapo Sh.367,706,884,000 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh.522,681,568,000 ikiwa ni mishahara na Sh.40,008,365,000 ikiwa ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2018, Wizara ilipokea jumla ya Sh.725,328,535,604, sawa na asilimia 78 ya bajeti yote. Kati ya fedha Sh.21,800,000,000 zikiwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 54 ya bajeti yote iliyokuwa imetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ilikusanya mapato ya Sh.187,075,690,000 sawa na asilimia 63 ya lengo liliokusudiwa la kukusanya Sh.293,822,132,859,000 na katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara inatarajia kukusanya Sh.297,014,614,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 umezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020, Mpango Mkakati wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2016-2021, Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti na Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto, maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyakati tofauti na Mwongozo wa Maandalizi wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka 2018/2019 na malengo ya mpango na bajeti kwa mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza na kipengele cha kwanza ambacho ni Jeshi la Polisi; amani na utulivu ni mhimili katika maendeleo ya nchi yoyote duniani kiuchumi, kijamii na kisiasa. Jeshi la Polisi limeendelea kuchukua hatua stahiki za kubaini, kuzuia na kudhibiti uhalifu wa aina zote ili kuendelea kuwa na nchi yenye utulivu utakaowezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa hali ya amani na utulivu hapa nchini, yamejitokeza matukio kadhaa ya uhalifu. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya makosa makubwa ya jinai 47,236 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 56,913 yaliyori potiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/2017. Kwa jumla makosa hayo yamepungua kwa asilimia 17. Kati ya makosa hayo, 44,866 yaliripotiwa Tanzania Bara na 2,370 yaliripotiwa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara kuititia Jeshi la Polisi itaendelea kuimarisha

mbinu za kubaini, kuzuia na kupambana na uhalifu pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa kushirkiana na Jeshi la Polisi kudhibiti hivi vitendo vya uhalifu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata silaha haramu 358 za aina mbalimbali na risasi 1,970. Watuhumiwa 333 waliopatikana na silaha hizo wamekamatwa na kufikishwa mahakamani ambapo kesi ziko katika hatua mbalimbali. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu kuhamasisha Umma kutoa taarifa za viashiria vya uhalifu pamoja na zile za watu wanaomiliki silaha kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza ajali barabarani, Wizara kwa kushirkiana na wadau imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura Na. 168 ambayo pamoja na mambo mengine inapendekeza kuzuia matumizi mabaya ya simu wakati dereva anapoendesha gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena; ili kuweza kupunguza ajali barabarani, Wizara kwa kushirkiana na wadau imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura Na. 168 ambayo pamoja na mambo mengine inapendekeza kuzuia matumizi mabaya ya simu wakati dereva anapoendesha gari; kuondoa nukta kwenye leseni za madereva watakaokiuka sheria za usalama barabarani na kufanya maboresho ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, kulifanya kuwa la kiutendaji na taasisi ya kiuongozi katika masuala ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, itaendelea kudhibiti mwendokasi kwa kutumia vifaa vya kudhibiti mwendokasi huo na kufanya operesheni na doria za mara kwa mara barabarani wakati wote. Aidha, Wizara itaendelea kufuta leseni za madereva wanaofanya makosa hatarishi barabarani mara kwa mara na kutoa elimu ya usalama

barabarani kwa umma na katika shuleni na kufanya ukaguzi wa mabasi ya abiria pamoja na magari mengine; kusimamia Mfumo wa Kielektroniki wa Udhhibit wa Mwendokasi wa Mabasi na Magari mengine kwa kushirikiana na *SUMATRA* na kupima viwango vya ulevi kwa madereva wanaofanya safari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usimamizi wa usalama barabarani, masuala yote yanayohusu vyombo vya moto, madereva, hususani katika mafunzo ya udereva na utoaji wa leseni, yatafanywa na Jeshi la Polisi kwa mujibu wa sheria. Nasisitiza kuwa vifaa vyote vinavyofungwa kwenye vyombo vya moto vinavyohusu usalama barabarani kama vile ving'ora pamoja na taa za vimulimuli, wahusika wawasiliane na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, limekamilisha ujenzi wa nyumba za kuishi familia 31 za askari Mkoani Arusha. Miradi ya nyumba hizo zilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 7 Aprili, 2018. Katika uzinduzi huo, Mheshimiwa Rais alitoa shilingi bilioni kumi kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya askari wa ngazi za chini. Jeshi la Polisi linatarajia kutumia fedha hizo kujenga nyumba 400 katika mikoa yote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kusaidia na kuboresha makazi ya askari. Aidha, napenda kutoa rai kwa wakuu wengine wa mikoa kote nchini kuzingatia agizo la Mheshimiwa Rais la kushirikisha wadau na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi kufanikisha ujenzi wa makazi ya askari na vituo vya polisi kama ilivyofanyika kwa Mkoa wa Arusha. Nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwa kuonesha mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kama huo unaendelea kwa nyumba 36 kwa upande wa Zanzibar, 24 zikiwa za Pemba na 12 zikiwa za Unguja. Nimpongeze Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kutoa shime hiyo alipotembelea katika

miradi huu. Awamu ya kwanza ya ujenzi wake imeshaanza na ujenzi unaendelea na tunatarajia nyumba 12 katika mikoa yote Kaskazini Pemba pamoja na Kusini na tunatarajia ujenzi huo uweze kukamilika mwishoni mwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa aina hiyo wa nyumba za kuishi familia 48 za askari katika eneo la Mabatini Mwanza; Musoma, Mara; zenyet uwezo wa kuishi familia 24 katika kila mkoa unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali limekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi, Wilaya ya Rungwe, ujenzi wa vituo vya polisi daraja A Mburahati, daraja B Mbweni, Dar es Salaam na Kituo cha Mbweni kimeanza kutumika. Niwapongeze wote walioshiriki katika kukamilisha zoezi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kama huo pia uko katika maeneo mengine, kwa mfano, ujenzi wa vituo vya polisi daraja C Mkoani Lindi katika maeneo ya Mtama, Rondo, Mchinga Nanjilinji na Ikokoto; ujenzi wa nyumba nane za makazi ya askari Mkoani Kigoma; ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja C Mkinga, Madebe, Handeni pamoja na nyumba tatu za makazi ya askari; ujenzi wa vituo vya polisi daraja C katika maeneo ya Kombeni na Amani, Zanzibar; ujenzi wa kituo cha polisi daraja C Kinyasini, Zanzibar; ujenzi wa nyumba mbili za makazi ya vituo vya polisi daraja C katika maeneo ya Kamogi, Kakese na Kalema Mkoani Katavi. Kazi hizo za ujenzi zinaendelea na zitakamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wote walioshiriki katika miradi hiyo kwa lengo la kuimarishe ulinzi na usalama katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Jeshi la Polisi lilikamata jumla ya kilogramu

8.4 za dawa za kulevya za viwandani. Watuhumiwa 833 wamefikishwa mahakamani ambapo kesi zipo katika hatua mbalimbali. aidha, kilogramu 37,786.8 za bangi na kilogramu 6,956 za mirungi zilikamatwa na watuhumiwa 9,005 walifikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuboresha mfumo wa upeletelezi wa kesi za jinai, mfumo wa ufuatilaji wa mienendo ya kesi za jinai umehuishwa ili kuuhakikishia upeletelezi kwamba kesi zinakamilika kwa wakati na hivyo kupunguza malalamiko kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo huo unaofahamika kama *Dossier Management System* unaimarisha ufuatilaji wa kesi kuanzia jalada linapofunguliwa kituo cha polisi hadi linapofikishwa mahakamani. Pia hutumia taarifa kutoka kwa maabara ya chunguzi za kisayansi ambapo imelmarishwa kwa kukamilisha ufunguaji wa mfumo wa uchunguzi wa vinasaba vyta binadamu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha ushirikiano wa hakijinai katika hatua mbalimbali za mashauri ya jinai; kuimarisha vitengo vyta ukaguzi kuanzia ngazi za Makao Makuu ya Polisi Mikoa, Wilaya na Vituo ili kutatua matatizo ya mlundikano wa kesi mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la kubambikwa kesi kwa wananchi, jambo hili limepungua baada ya Jeshi la Polisi kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa kusimamia mashauri ya jinai na kuyapitia kabla ya kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuimarisha ushirikiano kati ya Wapelelezi na Waendesha Mashtaka kuanzia hatua za awali za upeletelezi mpaka hatua ya mwisho ya kesi mahakamani; na ukaguzi wa mahabusu wafungwa unaofanywa na wadau wa hakijinai katika vituo vyta polisi na magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kuanzishwa kwa Mkoa Mpya wa Kipolisi Rufiji. Katika mwaka wa fedha wa

2017/2018, Serikali iliahidi kuanzisha Mkoa mpya wa Kipolisi wa Rufiji ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ahadi hiyo imetimizwa na hatua hii imeleta utulivu na udhibiti wa viashiria vya uhalifu katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, achukua nafasi hii kuvipongeza vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa juhudini na bidii kubwa waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya ya kuhakikisha kwamba eneo hili pamoja na maeneo mengine nchini yanakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba wananchi kuendelea kushirikiana na vyombo hivi kwa ajili ya kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu. Aidha, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuwa Serikali itaendelea kuwahifadhi na kuwalinda watoa taarifa za uhalifu na wahalifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi limefanya operesheni maalum na za kawaida kwa lengo la kuendelea kupambana na kudhibiti uhalifu wa aina zote ikiwemo makosa ya ndani ya nchi, ubakaji, unyang'anyi, mauaji na makosa mengine yanayovuka mipaka kama vile uingizaji wa bidhaa bandia nchini, uharamia, wizi wa vyombo vya moto, utakatishaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, operesheni maalum saba zilifanyika katika maeneo ya Kibiti, Rufiji, Mkuranga ambazo ziko Mkoani Pwani; Mapango ya Amboni Mkoani Tanga, Mwanza, Morogoro, Mtwara pamoja na Lindi; pamoja na operesheni za kawaida na misako ya doria zikiwa 3,628.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya matukio ya migogoro ya wakulima na wafugaji 86 yalijitokeza na kusababisha vifo vya watu 44. Kati ya hao wanaume walikuwa 34 na wanawake 10; majeruhi 75 na kati yao 71 walikuwa

wanaume na wanawake wanne; watuhumiwa 129 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Katika mwaka 2018/2019, Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti matukio hayo kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kuimarisha na kuboresha doria, misako na operesheni maalum na za kawaida, Jeshi la Polisi limepokea magari 172 yakiwa ni sehemu ya ununuzi wa magari kutoka nchini India. Jeshi la Polisi litaendelea kujikita kutunza vifaa hivyo na kuendelea kufanya misako na doria ili kuwahakikishia wananchi usalama mahali pao pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Magereza; hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Jeshi hili lilihifadhi jumla ya wafungwa na mahabusu 39,763. Kati ya hao 20,312 wakiwa wafungwa na mahabusu 19,451 ikilinganishwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Hali hiyo inaashiria kuendelea kuwepo kwa msongamano magerezani ambao ni kama asilimia 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili kukabiliana na hali hiyo zikiwemo kutumia utaratibu wa huduma kwa jamii, utaratibu wa *parole*, kutumia kamati za kusukuma kesi, ujenzi wa magereza mapya na ukarabati wa mabweni ya wafungwa. Rai yetu ni wananchi kupunguza utaratibu wa kufanya makosa hasa ya kukusudia na ya kupanga ili kuweza kupunguza msongamano wa mahabusu pamoja na wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa uboreshaji wa makazi ya askari wa jeshi la Magereza; ujenzi wa maghorofa 12 yenye uwezo wa kuishi familia 320 za Maafisa na Askari eneo la Gereza la Ukonga unaendelea kwa fedha za kitanzania shilingi bilioni kumi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia ujenzi wa nyumba za askari zenye uwezo wa kuishi familia 24 unaendelea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa nia yake ya dhati ya kuendelea kusaidia na kuboresha makazi ya askari wetu ili kuboresha morali ya kazi ya vijana wetu ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana ya kuhakikishia wananchi usalama wao pamoja na mali zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ujenzi wa nyumba 323 za kuishi Maafisa na Askari kwa njia ya kujitolea katika maeneno mbalimbali ya Magereza hapa nchini unaendelea. Aidha, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza limetoa shilingi milioni mia mbili arobaini na sita kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za askari katika Magereza ya Bukoba. Muleba, Biharamulo, Kigongoni, Mkuza, Kibiti, Arusha, Rombo, Karanga, Mwanga, Kisanga na Gereza Mahabusu Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Jeshi la Magereza litaendelea na ujenzi wa nyumba za kuishi askari kwenye Magereza ya Ukonga, Chato pamoja na kukamilisha ujenzi wa nyumba 223 zinazojengwa katika Magereza mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya uchumi wa viwanda jeshi la Magereza kupitia ubia na Kampuni ya Mkulazi *Holding* iliyoundwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PPF* limewekeza katika kilimo cha miwa na ufufuaji wa kiwanda cha sukari cha Gereza la Mbigili hapo Mjini Morogoro. Kiwanda hicho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka. Mpaka sasa hekta 800 zimeshalimwa na kupandwa miwa, sambamba na hilo ununuzi wa mitambo kwa ajili ya kiwanda hicho unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza limeingia ubia na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya *PPF* ili kuboresha Kiwanda cha Viatu Gereza la Karanga na ujenzi wa kiwanda kipywa katika eneo hilo. Ubia huo umeunda kampuni inayoitwa Karanga *Leather Industries* na uboreshaji wa kiwanda

unaendelea; ambapo mashine mpya zinategemea kuwasili mwishoni mwa mwaka huu. Hivyo kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha jozi za viatu 400 kwa siku badala ya 150 zinazozalishwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kipyaa kitakachojengwa kitakuwa na uwezo wa kuzalisha jozi 4,000 za viatu na kitachakata ngozi *Square feet* 12,500 na kitatengeneza soli (*shoe sole*) 3,000 kwa siku pamoja na kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi 4000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pia kwa mwaka na kwa mwaka 2018/2019 jeshi la Magereza litaimarisha viwanda vyaa katii vyaa useremala Mkoani Dodoma, Mtwara pamoja na kuanzisha kiwanda cha kuzalisha kokoto hapa Msalato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Shirika la Uzalishaji mali la Magereza limefanya kazi mbalimbali za ujenzi kwa Taasisi za Serikali na watu binafsi ikiwa ni pamoja na ukabati wa jengo la Utawala la Bunge ambalo limwekamilika na kukabidhiwa mwezi Desemba 2017, na Wabunge wote mmeona jinsi jengo ambavyo limependeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2018/2019 Shirika litaendelea na shughuli mbalimbali ikiwemo kupokea zabuni za ujenzi na kufanya kazi za ukarabati wa majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasimamia utekelezaji wa *program* ya adhabu mbadala wa kifungo Gerezani ili kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani na kupunguza gharama za kuwashudumia wafungwa na mahabusu. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya wafungwa 2,781 walinufaika na *program* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa wafungwa hawo nje ya Magereza umeisaida Serikali kuokoa jumla ya shilingi bilioni 1.3 ambazo zingetumika kuwashudumia wafungwa hawa kama wangetumikia adhabu zao magerezani

ikizingatiwa kuwa gharama za kuhudumia mfungwa mmoja kwa siku ni Sh.1,300. Serikali pia imeweza kuokoa jumla ya shilingi bilioni 4.3 ambazo zingetumika kuajiri vibarua kwenye Taasisi za Umma kwani vibarua mmoja angelipwa Sh.4,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji katika kipindi Julai mwaka 2017 hadi Machi 2018, Jeshi la Zima limekagua jumla ya maeneo 60,366 sawa na asilimia 74 ya lengo la ukaguzi kwa kipindi husika. Vile vile jeshi limeendelea kupambana na majanga ya moto pamoja na kufanya maokozi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2018 jeshi limefanikiwa kuzima moto katika matukio 1,217 hapa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika kukabiliana na majanga mengine jumla ya maokozi 335 yalifanyika katika matukio mbalimbali yakiwemo mafuriko kuangukiwa vifusi, ajali barabarani, kuzama kwa vyombo vyya usafiri, ziwani na bahaarini. Katika mwaka 2018/2019, Jeshi la Zima Moto litaendelea na ukaguzi wa tahadhali na kinga dhidi ya moto katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kuzuia na kupunguza matukio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zima Moto na Uokoaji lina magari 72 ya kuzimia moto na maokozi ikilinganishwa na mahitaji halisi ya magari 324. Hata hivyo, jitihada mbalimbali za kuimarisha hali ya vitendea kazi zinaendelea ili kuendana na kasi ya ukuaji wa miji pamoja na maeneo mbalimbali ya viwandani ikiwemo kukamilisha taratibu za kununua magari manne ya kuzimia moto kuititia bajeti ya mwaka 2017/2018 pamoja na ununuzi wa magari matano katika mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuimarisha uhusiano na nchi wahisani na wadau wa maendeleo ili kuendelea kupata misaada mbalimbali ikiwemo vitendea kazi kama ambavyo imekuwa ikifanyika katika mahusaino ya miji kwa miji ya Tanzania na majiji ya maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, Jeshi la Zima Moto na Uokoaji linaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna ya kukabiliana na majangwa mbalimbali ya moto kupitia vyombo vya habari, maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu ikiwemo shule, masoko, vivuko pamoja na vituo vya mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na matukio ya moto katika shule za mabweni hapa nchini Jeshi la Zima na Uokoaji limetoa elimu ya umma kwa kuzuia na kukabiliana na matukio ya moto katika shule za mabweni 256 katika mikoa mbalimbali. Jeshi la Zima Moto litaendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kupunguza majanga ya moto hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Uhamiaji, utekelezaji wa Mradi wa Uhamiaji Mtandao, *e-migration* ambao ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dokta John Pombe Magufuli tarehe 31 Januari, 2018 unaendelea. Hata Wabunge tayari wapo ambao walifanya maombi ya *passport* na tayari walishapata *passport* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo umeanza kutoa *passport* za kieletroniki Tanzania kwa upande wa Afrika Mashariki katika Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji Dar es Salam na Zanzibar. *Passport* mpya za kieletroniki zimetengenezwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa yenye uwezo wa kubeba taarifa mbalimbali pamoja na alama nyingi za kiusalama. Aidha, *passport* hiyo inawezesha mtumiaji kuwa na nakala yake ya *passport* kwenye simu yake ya kiganjani baada ya kupakua *up* ya *passport* yake kwenye simu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Idara ya Uhamiaji itaendelea kukamilisha ufungaji wa mifumo wa *passport* za kieletroniki katika mikoa yote hapa nchini. Vile vile tutaendelea na kufunga mifumo ya *visa* za kieletroniki, hati za ukazi za kieletroniki na kufunga mifumo ya kudhibiti watu wanaoingia kutoka nchi za nje.

Pamoja na miundombinu ya uwekaji mitandao ya mawasiliano ya mifumo katika Vituo, Ofisi, Vituo vyta Uhamiaji vya Mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka yetu yote pamoja na kuongeza udhibiti wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Nimpungeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka dira katika mradi huu na kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishwaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa misako, doria na ukaguzi Idara ya Uhamiaji inaendelea kufanya misako, doria na ukaguzi katika sehemu mbalimbali kwa lengo la kudhibiti wahamiaji haramu pamoja na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2017 Machi, 2018 jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 13,393 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikiwa ni ongezeko la asimilia 40 ya wahamiaji haramu 9,581 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ishara kwamba doria na misako na ukamataji imefanywa kikamilifu katika mwaka huu wa fedha. Vile vile jumla ya Watanzania 211 waliokwenda nje ya nchi kinyume na taratibu za uhamiaji walirudishwa nchini. Wizara kuitia Idara ya Uhamiaji itaendelea kufanya misako na doria ili kuwabaini na kuwaondoa wahamiaji haramu hapa nchini ili kuweza kuhakikisha kwamba watu wote wanaoingia na ama kutoka hapa nchini wanatumia njia zilizo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya *passport* 45,965 zilitolewa kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, ikilinganishwa na jumla ya *passport* 55,573 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, Idara ya Uhamiaji ilitoa hati za

dharua za safari 109,726 ikilinganishwa na hati za dharura za safari 8,445 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji itaendelea kufanya kazi kwa kuzingatia uadilifu, miiko na kanuni ili kuweza kuipa heshima nchi yetu na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuikumbuka Idara hii kwa kuipatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu lakini na fedha kwa ajili ya kununua nyumba kwa ajili ya makazi ya askari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wageni waliomba kupewa uraia wa Tanzania katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 ni jumla ya wageni 135. Idadi hii ni ongezeko la asilimia kumi ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2016/2017 ambapo wageni 110 walipewa uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangua kugusia Idara ya Uhamiaji imenunua nyumba 103 katika eneo la Iyumbu Mjini Dodoma kwa ajili ya makazi ya askari. Hadi sasa Idara imekabidhiwa na Shirika la Nyumba la Taifa jumla ya nyumba 63 ambazo zimekamilika na ujenzi wa nyumba 40 unaendelea. Aidha, ujenzi wa majengo ya Ofisi unaendelea katika Mikoa ya Geita, Manyara, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais kwa kutoa ahadi ya shilingi bilioni kumi kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya kisasa ya Idara ya Uhamiaji hapa katika Jiji la Dodoma ambapo utaanza katika mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, utambuzi, usajili na utoaji wa vitambulisho vya Taifa, Wizara inaendelea kutekeleza lengo la ibara ya 145(f) ya llani ua Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 kwa kuandikisha na kutoa vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania kuazia miaka 18 na zaidi, wageni, wakaazi na wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwaka 2018 Mamlaka imesajili jumla ya wananchi 14,048,493 wageni wakaazi 13,254 na wakimbizi 6,289 katika mikoa yote Tanzania Bara pamoja na Zanzibar. Zoezi la uchukuaji picha na alama za kibaolojia linaendela katika mikoa yote ili kutengeneza vitambulisho na kuvigawa kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka imeunganisha mfumo wake wa utambuzi na taasisi nyingine 35 ilii kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii na kuboresha hali ya ulinzi na usalama hapa nchini. Aidha, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa kituo cha kutunzia kumbukumbu huko Kibaha, Mkoa Pwani na kituo cha ukozi wakati wa majanga Kihonda, Mkoani Morogoro pamoja na Ofisi 13 za usajili za wilaya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile *NIDA* imeweka mtandao wa mawasiliano kati ya makao makuu na ofisi 117 za usajili wa wilaya ili kusaidia kusafirisha taarifa kutoka wilayani kwenda kituo kikuu cha kutengeneza vitambulisho na kutunza taarifa. Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kitambulisho cha Taifa na jinsi vinavyoweza kuwasaidia katika kupata huduma mbalimbali, mfano huduma za kibenki, pasi ya kusafiria, fidia kwa majanga, kubaini vitendo vya kihalifu pamoja na mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara itaendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa watu nchi nzima pamoja na kuunganisha mtandao wa mawasiliano katika ofisi za usajili wilaya 33 na makao makuu. Aidha, Wizara kuititia mkopo wa masharti na nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea inatarajia kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa katika Mkoa wa Dodoma pamoja na ujenzi wa ofisi katika wilaya 42 Tanzania Bara pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Kamati Ndogo ya Kitaifa ya Kuhoji

Waomba Hifadhi iliwahoji waomba hifadhi 1,342 kutoka nchi ya Burundi, ambapo waomba hifadhi 198 walipendekezwa kupewa hadhi ya ukimbizi hapa nchini baada ya kukidhi vigezo vya kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1968.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waomba hifadhi 1,144 walikosa sifa za kupewa hifadhi ya ukimbizi. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 50,437 kutoka Burundi walijijandikisha ili wasaidie ili kurejea kwao kwa hiari kwenye nchi yao ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuwarejesha kwa hiyari linaendelea na mpaka mwezi Machi, 2018 jumla ya wakimbizi 21,000 wamerejea Burundi. Ili kuongeza kasi ya kuwarejesha wakimbizi nchi zao Serikali ya Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa 20 wa Pande Tatu uliofanyika nchini Burundi tarehe 28 Machi, 2018 ambapo iliazimiwa kuwa ifikapo Desemba, 2018 wakimbizi zaidi ya 72,000 wawe wamerejeshwa katika nchi yao ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka kuwa katika siku za hivi karibuni kumeibuka makundi mbalimbali ya uhalifu yanayowahusisha vijana wa chini ya miaka 18 na jambo hili limejitokeza, wanaingia katika nyumba za watu wanaiba TV, wanaiba vitu vingine katika maeneo mbalimbali. Athari za kutokuwatambua vijana hawa wanapozaliwa mpaka wafike umri wa miaka 18 umeathiri upeletelezi wa kupata taarifa sahihi za kuwatambua uasili wao, wazazi pamoja na walezi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuanzisha kutekeleza jukumu la utambuzi na usajili wa watu mara wanapozaliwa na kupewa namba ya pekee ya utambuzi na usajili. Suala la utambuzi wa watoto ni muhimu katika kuimarisha hali ya usalama hapa nchini. Nielekeze mamlaka zilizopo katika maeneo husika ambayo uhalifu huu umekuwa ukijitokeza kuongeza mkazo ili watu wetu waendee kuishi wakiwa na usalama na wakiwa na uhakika wa usalama wa mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Wizara kuitia Sekretarieti ya kupambana na kuzuia na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji imewaokoa wahanga 20 Watanzania 18 na Afrika Kusini mmoja na Mrundi mmoja wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu waliokuwa wakitumikishwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kuwaunganisha na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi jumla ya kesi 24 zimefunguliwa ambapo kesi 23 zinaendelea katika mahakama zinaendelea katika mahakama mbalimbali hapa nchini na kesi moja na watuhumiwa wawili wote wanawake walihukumiwa kifungo cha miaka saba Gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti pia imetoa elimu kwa Watanzania hususan wasichana wanaoomba hati za kusafiria kwenda nje ya nchi kufanya kazi kufuatia taarifa mbalimbali zinazohusu manyanyaso kwa wasichana wanaopelekwa kwenda kufanya kazi katika nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na taarifa hizo mnamo mwezi Januari, 2018 nilitoa tamko la kuzuia utoaji wa *passport* za mafungu kwa wasichana na vijana wa kiume wanaokwenda kufanya kazi za ndani na za nje hususan katika nchi za Uarabuni mpaka pale tutakapokuwa tumehakikishiwa na Serikali husika kuhusu uhalsia wa kazi wanazokwenda kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Sekretarieti itaendelea kupambana na biashara haramu za usafirishaji wa binadamu ikiwemo kutoa elimu kwa umma pamoja na utaratibu wa mafunzo kwa wadau na vyombo vinavyosimamia Sheria za Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu. Watanzania watambue tunafanya hivyo kwa sababu tunawapenda, tunataka tuwe na uhakika wa usalama wao kule wanakokwenda kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usajili wa vyama vyatia kijamii na kidini; katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya maombi 252 ya kusajili vyama yalipokelewa ambapo maombi 178 ni vyama vyatia kijamii na maombi 74 ni vyama vyatia kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya maombi hayo, vyama 136 vilisajilliwa na maombi matano yalikataliwa tutokana na kutokutimizwa matakwa ya kisheria na sababu nyingine ni za kiusalama. Maombi 111 ya usajili wa vyama yapo katika hatua mbalimbali y akishughulikiwa. Wizara itaendelea na zoezi la usajili na uhakiki wa vyama vyatia kijamii na vyama vyatia kidini katika mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna malimbikizo mengi ya maombi ya usajili wa vyama vyatia kidini kutokana na maombi yote kutakiwa kufika Ofisi ya Msajili iliyoko Makao Makuu ya Wizara. Wakati Serikali ikiendelea kuwa na Ofisi za Msajili kwa kila Kanda, naelekeza wote wenyewe taasisi za kidini mikoaani wafike ofisi za wilaya na kuwasilisha maombi yao katika Ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote waliofikisha maombi katika wilaya husika wapate utambuzi wa awali ili taasisi hizo zifanye kazi zikiwa zinafahamika. Tunao utaratibu ambao unatumika sasa wa taasisi hizo zikiwa hazitambuliki mahali popote. Wakati taratibu za usajili wa kudumu zikiendelea, narudia, wapatiwe utambuzi wa awali wakati wanasubiri kupata usajili wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni kwa msaada wake anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Nimshukuru sana, amekuwa msaada mkubwa sana japo juzi alikesha akishangilia ushindi, kwa hiyo asubuhi tukamkosa hapa Bungeni kwa sababu ya kukesha akishangilia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niwashukuru sana kwa dhati Katibu Mkuu, Meja Jenerali Mstaafu, Projest Rwegasira; na Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Balozi Hassan Yahaya Simba kwa juhudzi zao kubwa za kusimamia utendaji wa kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawashukuru sana Inspeksi Jenerali wa Polisi, babu yangu Simon Sirro; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Dokta Juma Malewa; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Ndugu yangu Thobias Andengenye; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dokta Anna Peter Makakala; na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Shemeji yangu Andrew Massawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukurani zangu pia kwa Makamishna, Makamishna Wasaldizi, Wakuu wa Idara, Vitengo na Sehemu, askari na watumishi wote kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yao ya kila siku ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tumezingatia yale yaliyo mahitaji ya vijana wetu walioko kazini na yanafanyiwa kazi. Niwahakikishie kwamba yote kwa kiwango kikubwa tutayatekeleza ambayo tumeendelea kuongea mara kwa mara yanayohusu maslahi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile natoa shukurani zangu kwa nchi wahisani zikiwemo Australia, Botswana, Canada, China, Finland, India, Italy, Jamhuri ya Watu wa Korea, Marekani, Morocco, Uingereza, Ujerumani pamoja na Taasisi na Mashirika ya Kimataifa kama vile *DFID*, *FSDT*, *IOM*, *UNDP*, *UNHCR*, Vyombo vya Habari, Taasisi za Kijamii, Taasisi za Kidini, Zisizo za Kiserikali na wananchi kwa kuendelea kutoa misaada na taarifa mbalimbali ambazo zimeendelea kusaidia utendaji kazi hasa unaokusudia kuimarisha masuala ya usalama wa raia pamoja na mali zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naishukuru familia yangu, ndugu zangu, marafiki na wananchi wa jumboni kwangu kwa kuendelea kuniunga mkono na kunipa

ushirikiano hasa ninapokuwa naendelea kushiriki katika jukumu hili kubwa ambalo Mheshimiwa Rais alinipa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze na Mheshimiwa Spika pamoja na Wenyeviti wake na hasa hasa kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa mkifanya za kuhakikisha kwamba jahazi hili linakwenda vizuri. Salam zimfikie Mheshimiwa Spika na juzi nilimsikia alivyokuwa anasema lakini nikajua tu ni ile kiu aliyonayo kwa sababu kijana wangu ana miaka 13, hajawahi kushuhudia Simba akiwa bingwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Wizara itaendelea kudhibiti matukio ya uhalifu ili kuhakikisha usalama unakuwepo ndani ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tutashirikiana na vyombo vingine vya dola kuweza kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa nchi ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya Sh.945,555,651,000 kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo, Sh.907,269,969,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Sh.385,725,478,187 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh.521,544,490,813 ni kwa ajili ya mishahara. Fedha za miradi ya maendeleo zikiwa ni Sh.38,285,682,000 na kati ya fedha hizo, Sh.37,500,000,000 ni fedha za ndani na Sh.785,682,000 ikiwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE.
DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB.), AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA
MWAKA 2018/19 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2018/19.
2. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo itajadiliwa na Bunge hili.
3. ***Mheshimiwa Spika***, pia natumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza **Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Kwa kuongoza vema Taifa letu Na kuendelea kusimamia amani, utulivu na usalama nchini**. Ni dhahiri kuwa hali ya usalama ni nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya uchumi wa viwanda ambayo ni azma ya Serikali ya Awamu ya Tano.
4. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru Viongozi Wote Wakuu wa Serikali na Bunge kwa kuendelea kusimamia shughuli mbalimbali za Taifa. Aidha, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2018/19. Ushauri uliotolewa na Kamati utasaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.
5. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza ndugu zao kutohana

na maafa, majanga na ajali mbalimbali zilizotokea katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 mpaka sasa.

B. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA KWA MWAKA 2017/18 NA MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/19

Mapato na Matumizi

6. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18 Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopangwa. Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi 930,396,817,000 ambapo Shilingi 367,706,884,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Shilingi 522,681,568,000 ni Mishahara na Shilingi 40,008,365,000 ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

7. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2018 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 725,328,535,604 sawa na asilimia 78 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, Shilingi 21,800,000,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 54 ya bajeti ya maendeleo, Shilingi 367,055,054,909 zilikuwa ni Mishahara na Shilingi 336,473,480,695 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Pia, Wizara ilikusanya mapato ya Shilingi 187,075,690,821 sawa na asilimia 63 ya lengo la kukusanya Shilingi 293,822,132,859. Katika mwaka 2018/19 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi 297,014,614,300.

Mafanikio ya Wizara

8. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu na shughuli za Wizara kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwa ni pamoa na: kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za kuishi familia 32 za askari wa Jeshi la Polisi Mkoani Arusha; kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Rungwe; kukamilika kwa asilimia 97 kwa ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja A Mbura hati na Daraja B Mbweni – Dar es Salaam; kuhuishwa kwa mfumo wa ufuatiliaji wa mienendo ya kesi za jinai ili

kuharakisha upelelezi wa kesi; na kuanzishwa kwa Mkoa Mpya wa Kipolisi Rufiji.

9. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengine ni pamoja na kuzinduliwa kwa Mradi wa Uhamiaji Mtandao (*e-immigration*) mwezi Januari, 2018 kwa kuanza na utoaji wa pasipoti za Tanzania za kielektroni za Afrika Mashariki; kukamilika kwa Kituo cha Kutunzia Kumbukumbu (*Data Centre*) na Kituo cha Uokozi wakati wa Majanga (*Data Recovery Centre*) kwa ajili ya utambuzi na usajili wa watu; na kukamilika kwa ofisi 13 za usajili za wilaya Tanzania Bara na Zanzibar.

10. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2018/19 umezingatia: Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 –2020/21; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020; Mpango Mkakati wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi 2016/17 – 2020/21; Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti na Kuzuia Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/18 – 2021/22; Maagizo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wa Juu wa Taifa yaliyotolewa kwa nyakati tofauti; na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2018/19. Utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2017/18 na Malengo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19 ni kama ifuatavyo:

JESHI LA POLISI

Hali ya Usalama Nchini

11. ***Mheshimiwa Spika***, amani na utulivu ni muhimu katika maendeleo ya nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa. Jeshi la Polisi limeendelea kuchukua hatua stahiki za kubaini, kuzuia na kudhibiti uhalifu wa aina zote ili kuendelea kuwa na nchi yenye utulivu utakaowezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika kwa ufanisi.

12. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini yamejitokeza matukio kadhaa ya uhalifu. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla

ya makosa makubwa ya jinai 47,236 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 56,913 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Kwa jumla makosa hayo yamepungua kwa asilimia 17. Kati ya makosa hayo, 44,866 yaliripotiwa Tanzania Bara na 2,370 Tanzania Zanzibar ambapo makosa 9,252 yalikuwa dhidi ya binadamu, 23,278 ya kuwania mali na 14,706 ya maadili ya jamii. Kutokana na matukio hayo ya uhalifu jumla ya watuhumiwa 42,702 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Katika mwaka 2018/19 Wizara kuititia Jeshi la Polisi itaendelea kuimarisha mbinu za kubaini, kuzuia na kupambana na uhalifu pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kushirkiana na Jeshi la Polisi kudhibiti vitendo vya uhalifu nchini.

13. ***Mheshimiwa Spika***, kati ya mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata silaha haramu 358 na risasi 1,970 kwa mchanganuo ufuatao: gobore 224 na risasi 127; *shortgun* 43 na risasi 654; bastola 36 na risasi 208; SMG 19 na risasi 423; SAR mbili (2); *Mark iv* mbili (2) na risasi 85, *Riffle* 23 na risasi 410; Uzi Gun tano (5) na risasi moja (1); AK 47 nne (4) na risasi 55; na risasi saba (7) za *G3*. Watuhumiwa 333 waliopatikana na silaha hizo wamekamatwa na kufikishwa mahakamani ambapo kesi zipo katika hatua mbalimbali. Katika mwaka 2018/19 Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu ya kuhamasisha umma kutoa taarifa za viashiria vya uhalifu pamoja na zile za watu wanaomiliki silaha kinyume cha sheria.

Hali ya Usalama Barabarani

14. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya usalama barabarani imeendelea kuimarika kutokana na hatua za kisheria zinazoendelea kuchukuliwa kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya moto. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya ajali 4,180 za barabarani ziliripotiwa. Aidha, ajali 1,613 zilisababisha vifo vya watu 1,985 na watu 4,447 kujueruhiwa. Takwimu zinaonyesha kupungua kwa ajali hizo kwa asilimia 35.7 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2016/17.

Ajali nyingi kati ya hizo zimesababishwa na madereva kutozingatia Sheria za Usalama Barabarani na ubovu wa miundombinu katika baadhi ya maeneo. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya madereva 5,185 walikamatwa kwa makosa mbalimbali ya usalama barabarani kwa kukiuka Sheria na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria. Kati ya hao madereva wa magari walikuwa 4,102 na waendesha pikipiki 1,083.

15. ***Mheshimiwa Spika***, ili kupunguza ajali za barabarani, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura, 168, ambayo pamoja na mambo mengine inapendekeza kuzuia matumizi mabaya ya simu wakati dereva anapoendesha gari, kuondoa nukta kwenye leseni za madereva wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani na kufanya maboresho ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani kulifanya kuwa tendaji na taasisi kiongozi (*Leading Agency*) katika masuala ya usalama barabarani.
16. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kuitia Jeshi la Polisi (Kikosi cha Usalama Barabarani) itaendelea kudhibiti mwendokasi kwa kutumia vifaa vya kudhibiti mwendo huo (*Speed Radar*) na kufanya operesheni na doria za magari barabarani wakati wote. Aidha, Wizara itaendelea kufuta leseni za madereva wanaofanya makosa hatarishi barabarani, kutoa elimu ya Usalama Barabarani kwa umma na mashulenii, kufanya ukaguzi wa mabasi ya abiria kabla hayajaanza safari, kusimamia mfumo wa kielektroniki wa udhibiti mwenendo wa mabasi barabarani (*Vehicle Tracking System – VTS*) kwa kushirikiana na SUMATRA na kupima kiwango cha ulevi wa madereva.
17. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi wa usalama barabarani, masuala yote yanayohusu vyombo vya moto na madereva, hususan katika mafunzo ya udereva na utoaji wa leseni yatafanywa na Jeshi la Polisi kwa mujibu wa Sheria. Aidha, nasisitiza kuwa vifaa vyote vinavyofungwa kwenye vyombo vya moto, vinavyohusu usalama barabarani

(kama vile ving'ora na taa za vimulimuli) wahusika wawasiliane na Jeshi la Polisi.

18. **Mheshimiwa Spika**, natoa rai kwa mamlaka zote zinazofanya operesheni na kazi mbalimbali zinazohusu shughuli zote za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na ukamataji wa vyombo vya moto, ufungaji wa minyororo kwenye matairi hasa kwenye maeneo ya maegesho, kugeuza maeneo ya pembezoni mwa barabara kuwa maegesho ya magari na kutoza fedha za maegesho, kutoza fedha kwa magari yanayofika katika maeneo ya huduma za kijamii, hususan hospitali ni vyema mamlaka husika ziwasiliane na Jeshi la Polisi ili kuondoa kero na malalamiko yanayotokana na operesheni hizo.

Miradi ya Ujenzi wa Makazi na Vituo vya Polisi

19. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na sekta binafsi limekamilisha ujenzi wa nyumba za kuishi familia 31 za askari Mkoani Arusha. **Mradi wa nyumba hizo ulizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 07 Aprili, 2018.** Katika uzinduzi huo Mhe. Rais alitoa ahadi ya **Shilingi bilioni 10** kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya askari wa ngazi za chini.

Jeshi la Polisi linatarajia kutumia fedha hizo kujenga nyumba 400 katika mikoa yote nchini. **Nachukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Rais kwa kusaidia kuboresha makazi ya askari.** Aidha, napenda kutoa rai kwa Wakuu wa Mikoa wote nchini kutekeleza agizo la Mhe. Rais la kushirikiana na mashirika ya Umma na sekta binafsi katika kufanikisha ujenzi wa makazi ya askari na vituo vya Polisi katika mikoa yote nchini.

20. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Jeshi la Polisi limekamilisha ukarabati wa iliyokuwa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya Ofisi ya Makao Makuu ya muda ya Jeshi la Polisi. Aidha, ujenzi wa ofisi mpya ya Jeshi la Polisi katika eneo hilo umefikia asilimia 40. Vilevile,

ujenzi wa nyumba za kuishi familia 48 za askari katika eneo la Mabatini – Mwanza na Musoma – Mara zenye uwezo wa kuishi familia 24 kwa kila mkoa unatarajiwaka kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2018.

21. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali limekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Rungwe. Aidha, ujenzi wa Vituo vya Polisi Daraja A Mburahati na Daraja B Mbweni – Dar es Salaam umefikia asilimia 97 na Kituo cha Polisi Mbweni kimeanza kutumika.

22. ***Mheshimiwa Spika***, hatua za ujenzi katika maeneo mengine ni kama ifuatavyo: ujenzi wa Vituo vya Polisi daraja C Mkoani Lindi katika maeneo ya Mtama, Londo, Mchinga, Nanjilinji na Ikokoto vyote vimefikia wastani wa asilimia 50; ujenzi wa nyumba nane (8) za makazi ya askari Mkoani Kigoma umefikia asilimia 40; ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja C Mkinga Madebe - Handeni pamoja na nyumba tatu (3) za makazi ya askari zinazofadhiliwa na Kampuni ya Tanga Cement zote zimefikia asilimia 55; ujenzi wa Vituo vya Polisi daraja C katika maeneo ya Kombeni na Amani Zanzibar umefikia asilimia 40; ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja C Kinyasini Zanzibar umefikia asilimia 10; ujenzi wa nyumba mbili (2) za makazi na Vituo vya Polisi daraja C katika maeneo ya Kamogi, Kakese na Karema Mkoani Katawi umefikia asilimia 55. Kazi hizo za ujenzi zitaendelea na kukamilika katika mwaka 2018/19.

23. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wote waliochangia katika miradi hiyo kwa lengo la kuimarisha ulinzi katika maeneo yao. Hiki ni kielelezo kuwa tukiamua tunaweza, hivyo natoa wito kwa wananchi kuendeleza jitihada hizi katika maeneo mengine nchini.

24. ***Mheshimiwa Spika***, kazi ya upanuzi wa Chuo cha Polisi Moshi kwa ufadhilli wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China inaendelea. Ujenzi wa mabweni yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 662 na madarasa ya wanafunzi 320

umefikia asilimia 50. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2018/19.

Udhibiti wa Dawa za Kulevyva Nchini

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Jeshi la Polisi lilikamata jumla ya kilogramu 8.44 za dawa za viwandani. Watuhumiwa 833 wamefikishwa mahakamani, ambapo kesi zipo katika hatua mbalimbali. Aidha, kilogramu 37,786.8 za bhangi na kilogramu 6,956.6 za mirungi zilikamatwa na watuhumiwa 9,005 walifikishwa mahakamani. Vilevile, mashamba ya bhangi 59 yenye takribani ekari 206.6 yaliteketezwa na watuhumiwa 39 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Kuboresha Mfumo wa Upelelezi wa Kesi za Jinai

26. ***Mheshimiwa Spika***, mfumo wa ufuatiliaji wa mienendo ya kesi za jinai umehuishwa ili kuhakikisha upelelezi wa kesi unakamilika kwa wakati na hivyo kupunguza malalamiko kwa wananchi. Mfumo huo unaofahamika kama *Dossier Management System* unaimarisha ufuatiliaji wa kesi kuanzia jalada linapofunguliwa Kituo cha Polisi hadi linapofikishwa mahakamani. Mfumo huo pia hutumia taarifa kutoka Maabara ya Uchunguzi wa Kisayansi ambayo imeimarishwa kwa kukamilisha ufungaji wa mfumo wa uchunguzi wa vinasaba vya binadamu.

27. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi linaendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa Haki Jinai katika hatua mbalimbali za mashauri ya jinai na kuimarisha vitengo vya ukaguzi kuanzia ngazi ya Makao Makuu ya Polisi, Mikoa, Wilaya na Vituo ili kutatua mlundikano wa kesi.

Hatua za Utatuzi kwa Wananchi Kubambikiwa Kesi

28. ***Mheshimiwa Spika***, tatizo la kubambikiwa kesi kwa wananchi limepungua baada ya Jeshi la Polisi kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuimarisha mfumo wa kusimamia mashauri ya jinai na kuyapitia kabla ya

kupelekwa kwa Mwanasheria wa Serikali; kuimarisha ushirikiano kati ya wapelelezi na waendesha mashtaka kuanzia hatua za awali za upeletezi mpaka hatua ya mwisho wa kesi mahakamani; na ukaguzi wa mahabusu/wafungwa unaofanywa na wadau wa Haki Jinai katika Vituo vya Polisi na magerezani.

Usalama wa Makundi Maalum

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya watu 117 (wazee/vikongwe) waliuawa, kati ya hao wanawake 26 na wanaume 91. Matukio hayo yalitokea katika Mikoa ya Arusha 6, Dodoma 1, Geita 9, Iringa 1, Kagera 10, Katavi 3, Kigoma 1, Mara 2, Mbeya 7, Morogoro 2, Mwanza 9, Njombe 5, Rukwa 10, Shinyanga 3, Simiyu 5, Singida 6, Songwe 12 na Tabora 25. Aidha, katika kipindi hicho matukio mawili (2) ya kujeruhwa kwa watu wenye ulemavu wa ngozi yaliripotiwa katika Mikoa ya Morogoro na Tabora.

30. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia matukio hayo jumla ya watuhumiwa 100 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. **Natoa rai kwa wananchi kuacha kujihusisha na vitendo hivyo viovu vinavyoikiuka haki za binadamu.** Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti na kuzuia mauaji ikiwemo ya makundi maalum na kuendelea kushirikiana na wadau katika kutoa elimu kwa umma ili kuacha mila na imani potofu kama ilivyoelekezwa katika **Ibara ya 146 (v) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020.**

Kuanzishwa kwa Mkoa Mpya wa Kipolisi Rufiji

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Serikali iliahidi kuanzisha Mkoa Mpya wa Kipolisi wa Rufiji ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. **Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ahadi hiyo imetimizwa na hatua hii imeleta utulivu na udhibiti wa viashiria vya uhalifu katika eneo hilo.** Nachukua nafasi hii kuvipongeza vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa juhudini bidii kubwa waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya ya kuhakikisha eneo hilo na

maeneo mengine nchini yanakuwa salama. Pia, naomba na kuwasitiza wananchi kuendelea kushirikiana na vyombo hivi kwa ajili ya kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu. Aidha, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuwa Serikali itaendelea kuwahifadhi na kuwalinda wanaotoa taarifa za wahalifu na uhalifu.

Udhibiti wa Uhalifu Nchini

32. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi limefanya operesheni maalum na za kawaida (misako na doria) kwa lengo la kuendelea kupambana na kudhibiti uhalifu wa aina zote ikiwemo makosa ya ndani ya nchi (kama vile mauaji, ubakaji na unyang'anyi) na makosa yanayovuka mipaka (kama vile uingizaji wa bidhaa bandia nchini, uharamia, wizi wa vyombo vya moto na utakatishaji wa fedha).

Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 operesheni maalumu saba (7) zilifanyika katika maeneo ya Kibiti, Rufiji, Mkuranga – mkoani Pwani, mapango ya Amboni mkoani Tanga, Mwanza, Morogoro, Mtwara na Lindi pamoja na operesheni za kawaida ikiwa ni misako na doria zilikuwa 3,628. Kwa sasa hali ya usalama katika maeneo hayo na kwingineko nchini ni tulivu.

Kushiriki katika Kuimarisha Amani na Usalama katika Nchi Mbalimbali

33. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 jumla ya askari 74 wa Jeshi la Polisi walipelekwa kushiriki kulinda amani na usalama katika nchi mbalimbali. Kati ya askari hao 48 walipelekwa katika jimbo la Darfur-Sudan (UNAMID), 10 Abyei - Sudan (UNISFA), 15 Sudani Kusini (UNMISS) na mmoja nchini Marekani – New York (DPKO). Lengo ni kuendelea kupata uzoefu na mbinu mpya za kiutendaji, kama ilivyoelekezwa katika **Ibara ya 146 (iv) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020**.

Kushiriki katika Operesheni za Kimataifa na Kikanda

34. ***Mheshimiwa Spika***, kuanzia tarehe 4 hadi 5 Oktoba, 2017 Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Ofisi za INTERPOL Kanda

ya Kusini mwa Afrika limefanya operesheni za pamoja katika Jumuia ya SARPCCO na EAPCCO. Kufuatia operesheni hizo, magari 2 kutoka Uingereza na Malaysia yalikamatwa pamoja na dawa za kulevya kwa mchanganuo ufuatao: Heroine gramu 51.41; Cocaine gramu 20.87; bhangi kilogramu 870.16 na mirungi kilogramu 13. Pia, silaha 8 (SMG 1 na Gobore 7) na risasi 31 zilikamatwa.

Jumla ya watuhumiwa 265 walikamatwa kwa makosa hayo na kufikishwa mahakamani. Vilevile, wahamiaji haramu 31 kutoka katika nchi za Burundi (12), China watano (5), India mmoja (1), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) watano (5), Kenya mmoja (1), Malawi wawili (2), Pakistan mmoja (1), Uganda mmoja (1), Yemen mmoja (1) na Zambia wawili (2) walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Jeshi la Polisi litaendelea kufanya operesheni kwa kuzingatia **Ibara ya 146 (vi) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020**.

Kudhibiti Uvunjifu wa Amani unaotokana na Migogoro ya Wakulima na Wafugaji

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya matukio ya migogoro ya wakulima na wafugaji 86 yalitokea na kusababisha vifo vya watu 44 (wanaume 34 na wanawake 10) na majeruhi 75 (wanaume 71 na wanawake 4). Watuhumiwa 129 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Katika mwaka 2018/19, Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti matukio hayo kwa kushirikisha mamlaka husika.

Upandishwaji Vyeo na Ajira Mpya kwa Askari

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Jeshi la Polisi limeomba kibali cha kupandisha vyeo maafisa 300 na askari 3,071 wa vyeo mbalimbali. Aidha, katika kutekeleza agizo la Mhe. Rais, Jeshi la Polisi limepata kibali cha kuajiri vijana 1,500 waliopo katika Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU). Nafasi hizo zimeshatangazwa

kupitia vyombo vya habari ikiwemo radio, televisheni na magazeti.

Kuboresha Maslahi ya Askari

37. *Mheshimiwa Spika*, kati ya mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Serikali imelipa madeni ya askari na watumishi jumla ya **Shilingi bilioni 17.94** ikiwa ni utekelezaji wa **Ibara ya 146 (ii) ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 – 2020**. Madeni hayo yalitokana na madai ya posho za likizo na stahili mbalimbali kwa mwaka 2014/15 na 2015/16. Vilevile, Serikali imelipa madeni ya wazabuni na watoa huduma ya jumla ya **Shilingi bilioni 5.69**. Aidha, katika kipindi hicho askari 347 walioumia/kufariki wakiwa kazini wamelipwa fidia ya jumla ya **Shilingi bilioni 2.09**.

Ununuzi wa Sare za Jeshi la Polisi

38. *Mheshimiwa Spika*, taratibu za ununuzi wa sare na vifaa vingine vya kijeshi kwa kutumia viwanda vya ndani zinaendelea baada ya Kiwanda cha 21st Century kilichopo Mkoani Morogoro kuthibithisha uwezo wa kutengeneza vitambaa bora vya kushona sare zinazotakiwa na majeshi yetu. Aidha, Jeshi la Polisi linakamilisha mkataba wa ununuzi wa jozi 15,000 za viatu (*buti jozi 10,000, viatu vya kawaida (staffshoes) jozi 5,000*) kutoka Kiwanda cha Viatu cha Jeshi la Magereza Karanga - Moshi.

Upatikanaji wa Vitendea Kazi

39. *Mheshimiwa Spika*, ili kuendelea kuimarisha na kuboresha doria, misako na operesheni maalum na za kawaida Jeshi la Polisi limepokea magari 172 aina ya Ashok Leyland yakiwa ni sehemu ya ununuzi wa magari 777 kutoka Kampuni ya Ashok Leyland ya nchini India. Magari hayo yatagawiwa katika Mikoa, Vikosi na Wilaya za Kipolisi. Pia, Jeshi la Polisi limepokea pikipiki 10 aina ya Tongba kutoka kwa wadau wa usalama wa mkoa wa Dar es Salaam. Pikipiki hizo zimesambazwa katika Vituo vya Polisi katika kanda maalumu ya Dar es Salaam kwa kazi za doria za kuzuia makosa ya usalama barabarani.

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19 Jeshi la Polisi la Polisi litaendeleza juhudi za kupata vitendea muhimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha hali ya ulinzi na usalama nchini.

Mafunzo kwa Askari/Watumishi wa Jeshi la Polisi

41. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji maafisa 736, wakaguzi 395, askari wa vyeo mbalimbali 4,943 na watumishi raia 10 yamefanyika. Katika mwaka 2018/19 Jeshi la Polisi litaendelea kutoa mafunzo kwa maafisa, wakaguzi, askari wa vyeo mbalimbali pamoja na watumishi raia ili kukabiliana na mbinu mpya za kiuhalifu pamoja na kuongeza ufanisi.

JESHI LA MAGEREZA

Uhifadhi wa Wafungwa na Program za Urekebishaji Magereza

42. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Jeshi la Magereza lilihifadhi jumla ya wafungwa na mahabusu 39,763 (wafungwa ni 20,312 na mahabusu ni 19,451) ikilingwanishwa na uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Hali hiyo inaashiria kuendelea kuwepo msongamano magerezani kwa asilimia 33. Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ili kukabiliana na hali hiyo zikiwemo: kutumia utaratibu wa huduma kwa jamii; utaratibu wa Parole; kutumia Kamati za Kusukuma Kesi; ujenzi wa magereza mapya; na ukarabati wa mabweni ya wafungwa.

Aidha, Jeshi la Magereza liliendelea kutekeleza jukumu la kuwasindikiza mahabusu kwenda mahakamani na kurudi Gerezani katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Wilaya ya Arusha mjini na Wilaya ya Dodoma mjini.

Uboreshaji wa Makazi ya Askari wa Jeshi la Magereza

43. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa maghorofa 12 yenye uwezo wa kuishi familia 320 za maafisa na askari eneo la

Gereza Ukonga unaendelea kwa fedha **Shilingi billion 10** zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Pia, ujenzi wa nyumba za askari zenyne uwezo wa kuishi familia 24 unaendelea katika Gereza Chato. **Nachukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais kwa nia yake ya dhati ya kuendelea kusaidia kuboresha makazi ya askari.**

44. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ujenzi wa nyumba 323 za kuishi maafisa na askari kwa njia ya kujitolea katika maeneo mbalimbali ya magereza nchini unaendelea. Ujenzi huo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza limetoa **Shilingi milioni 246** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za askari katika Magereza ya Bukoba, Muleba, Biharamulo, Kigongoni, Mkuza, Kibiti, Arusha, Rombo, Karanga, Mwanga, Isanga na Gereza Mahabusu Morogoro.

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Jeshi la Magereza litaendelea na ujenzi wa nyumba za kuishi askari kwenye Magereza ya Ukonga na Chato pamoja na kukamilisha ujenzi wa nyumba 323 zinazojengwa katika magereza mbalimbali nchini.

Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Viwanda

46. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Uchumi wa Viwanda, Jeshi la Magereza kwa ubia na Kampuni ya Mkulazi Holding Ltd inayoundwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii NSSF na PPF limewekeza katika kilimo cha miwa na ufufuaji wa Kiwanda cha Sukari Gereza Mbigiri - Morogoro. Kiwanda hicho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka. Mpaka sasa hekta 800 zimeshalimwa na kupandwa miwa, sambamba na hilo ununuzi wa mitambo kwa ajili ya kiwanda unaendelea.

47. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Jeshi la Magereza limeingia ubia na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PPF ili kuboresha Kiwanda cha Viatu Gereza Karanga na ujenzi wa

kiwanda kipyta katika eneo hilo. Ubia huo umeunda kampuni inayoitwa *Karanga Leather Industries*. Uboreshaji wa kiwanda unaendelea, ambapo mashine mpya zinategemea kuwasili katika mwaka 2018. Hivyo, kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha jozi za viatu 400 kwa siku badala ya 150 zinazozalishwa sasa.

Kiwanda kipyta kitakachojengwa kitakuwa na uwezo wa kuzalisha jozi 4,000 za viatu, kuchakata ngozi sq. ft 12,500 na kutengeneza soli jozi 3,000 kwa siku pamoja na kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi (mikanda, mikoba na pochi) 4,000 kwa mwaka. Katika mwaka 2018/19 Jeshi la Magereza litaimarisha viwanda vya kati vya Useremala Mkoani Dodoma na Mtwara pamoja na mradi wa kuzalisha kokoto Msalato.

Programu za Urekebishaji wa Wafungwa

48. *Mheshimiwa Spika*, programu za urekebishaji wa wafungwa zinaendelea kuititia shughuli za kilimo na mifugo. Jumla ya hekari 7,000 za mazao kama vile mahindi, mpunga, maharage, alizeti, chai, pamba, migazi/michikichi na mikorosho zimelimwa. Aidha, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (Agricultural Seed Agency - ASA) limeendelea kuzalisha mbegu bora katika Magereza ya: Wami Kuu, Mbigiri, Idete (Morogoro), Isupilo (Iringa), Songwe (Mbeya), Mollo (Rukwa), Kitai (Ruvuma) na Karanga (Kilimanjaro).

49. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Jeshi la Magereza linaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika uzalishaji wa vipando vya mihogo yenye ukinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato kali (*cassava mosaic - Uganda variant*). Jumla ya hekta 170 zillimwa katika Magereza 23 yaliyopo katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Lindi, Mara, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

50. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Jeshi la Magereza linatarajia kulima jumla ya hekta 349 za mbegu bora za alizeti, mpunga, mahindi na nyanya katika Magereza

ya Wami, Mbigiri na Idete (Morogoro), Isupilo (Iringa), Songwe (Mbeya), Mollo (Rukwa), Kitai (Ruvuma) na Karanga (Kilimanjaro) na kuuzwa kwa wadau mbalimbali. Jeshi pia, litalima ekari 7,000 za mazao ya chakula ikiwemo mahindi, maharage, mtama na mpunga.

51. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 urekebishaji wa wafungwa kuititia ufugaji uliendelea, ambapo jumla ya mifugo 18,588 ya aina mbalimbali ilihudumiwa kama ifuatavyo: ng'ombe wa maziwa (691), Ng'ombe wa nyama (5,497) Mbuzi (2,405), Kondoo (134), Nguruwe (60), Sungura (175), Kuku na Bata (9,626). Jeshi la Magereza litaendelea kuhudumia mifugo 26,632 ya aina mbalimbali katika mwaka 2018/19.

Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza

52. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza limefanya kazi mbalimbali za ujenzi kwa Taasisi za Serikali na watu binafsi ikiwa ni pamoja na ukarabati wa jengo la Utawala la Bunge ambalo limekamilika na kukabidhiwa mwezi Disemba, 2017. Katika mwaka 2018/19 Shirika litaendelea na shughuli mbalimbali ikiwemo kupokea zabuni za ujenzi na kufanya ukarabati wa majengo.

Upimaji wa Maeneo ya Magereza

53. ***Mheshimiwa Spika***, upimaji wa maeneo mbalimbali ya Magereza nchini unaendelea kwa lengo la kupunguza migogoro iliyopo katika maeneo yanayomilikiwa na Jeshi la Magereza. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Jeshi limeweza kupima na kupata Hati za umiliki wa maeneo ya Gereza Karanga, Hati tatu (3) za mashamba ya Mbigiri na eneo la Gereza Isupilo.

Utunzaji na Hifadhi ya Mazingira

54. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Magereza limeendelea na juhudzi za utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti, kuendeleza misitu ya asili na ufugaji wa nyuki kwenye eneo

la hekta 14,698.5. Aidha, kwa sasa miti ya aina mbalimbali inaendelea kutunzwa kwenye magereza kote nchini kwa ufadhili wa Mfuko wa Misitu (Tanzania Forest Fund - TFF). Aidha, Gereza Isupilo – Iringa limeanzisha kitalu cha miti kwa ajili ya kuendeleza juhudzi za utunzaji wa mazingira.

Ajira na Maslahi kwa Askari Magereza

55. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Magereza litaajiri askari wapya 2,750 kati ya hao askari 750 wataajiriwa katika mwaka 2017/18 na askari 2,000 katika mwaka 2018/19. Aidha, katika kuimarisha uongozi wa ngazi za juu wa Jeshi la Magereza jumla ya maafisa 29 wamepandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali.

56. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya Watumishi kwa kuwalipa posho ya chakula kwa wakati na fedha za msamaha wa kodi ya bidhaa kwa maafisa na askari nchini. Serikali pia imelipa baadhi ya madeni ya askari na watumishi ya **Shilingi bilioni 5.55** katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba, 2017.

Mafunzo kwa Askari wa Jeshi la Magereza

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Jeshi la Magereza limeendelea kuwawezesha watumishi kupata mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Jumla ya watumishi 306 wanaendelea na mafunzo ya kitaaluma katika vyo mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao: Astashahada 98, Stashahada 86, shahada 85, Stashahada ya Uzamili 08, Shahada ya Uzamili 26 na Shahada za uzamivu 02. Jeshi pia limeendelea kutoa mafunzo ndani ya Jeshi ambapo askari 37 walihitimu mafunzo ya Astashahada ya ufundi bomba na useremala na askari 24 walipata cheti cha Sayansi ya Urekebishaji wa Wafungwa. Aidha, askari 17 wanaendelea na mafunzo ya cheti cha urekebishaji katika Chuo cha Taaluma ya Urekebishaji Ukonga.

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19 Jeshi la Magereza linatarajia kutoa mafunzo ya ndani katika fani na

ngazi mbalimbali kwa maafisa na askari 3,270. Vilevile, litaendelea kutoa vibali kwa maafisa na askari kusoma vyuo vya nje ya Jeshi kwa kuzingatia mahitaji kwa taaluma zenyenye upungufu Jeshini. Aidha, mafunzo ya ufundi katika Chuo cha Ruanda kwa askari, pamoja na wafungwa kama sehemu ya urekebishaji yataendelea kutolewa.

PROGARAMU YA ADHABU MBADALA YA KIFUNGO CHA GEREZANI

59. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inasimamia utekelezaji wa Programu ya Adhabu Mbadala wa Kifungo Gerezani ili kupunguza msongamano magerezani na gharama za kuhudumia wafungwa na mahabusu. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya wafungwa 2,781 walinufaika na Programu hiyo. Uwepo wa wafungwa hao nje ya magereza umesaldla Serikali kuokoa jumla ya **Shilingi bilioni 1.31** ambazo zingetumika kuwashudumia wafungwa hawa kama wangetumikia adhabu zao magerezani ikizingatiwa kuwa gharama za kumhudumia mfungwa mmoja kwa siku ni Shilingi 1,300. Serikali pia imeweza kuokoa jumla ya **Shilingi billion 4.03** ambazo zingetumika kuajiri vibarua kwenye Taasisi za Umma kwani kibarua mmoja hulipwa wastani wa Shilingi 4,000 kwa siku.

60. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18 Wizara imefanikiwa kupanuwa wigo wa utekelezaji wa adhabu mbadala kwa kuongeza Mikoa ya Kigoma na Simiyu na hivyo kufanya jumla ya mikoa 23 ya Tanzania Bara inayotekeleza programu hiyo. Katika mwaka, 2018/19 Wizara inatarajia kuongeza Mikoa ya Katavi, Rukwa na Lindi kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo.

JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

Ukaguzi wa Tahadhari na Kinga Dhidi ya Moto na Majanga

61. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Jeshi limekagua jumla ya maeneo 60,366 sawa na asilimia 74 ya lengo la ukaguzi kwa kipindi husika.

Katika mwaka 2018/19 Jeshi litaendelea na ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto katika maeneo mbalimbali nchini ili kuzuia na kupunguza matukio ya moto.

Matukio ya Moto na Majanga Mengine

62. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kupambana na majanga ya moto pamoja na kufanya maokozi katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Jeshi limefanikiwa kuzima moto katika matukio 1,217 Tanzania Bara ikiwemo tukio la moto katika soko la SIDO, mkoani Mbeya, moto katika nyumba za makazi ya Polisi mkoani Arusha, kuungua kwa kiwanda cha Superdoll, kupasuka kwa bomba la gesi Buguruni – Mnyamani na moto katika Kituo cha Utangazaji cha Clouds Media. Aidha, katika kukabiliana na majanga mengine, jumla ya maokozi 335 yalifanyika katika matukio mbalimbali ikiwemo mafuriko, kuangukiwa vifusi, ajali za barabarani, kutumbukia chooni na kuzama kwa vyombo vyaya usafiri ziwani/baharini.

Hali ya Vituo vya Zimamoto Nchini na Vitendea Kazi

63. ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina jumla ya vituo vya zimamoto 82 Tanzania Bara wakati mahitaji halisi ya vituo ni 162. Jeshi pia lina magari 72 ya kuzimia moto na maokozi, ikilinganishwa na mahitaji halisi ya magari 324.

Hata hivyo, Jeshi linaendelea na jitihada mbalimbali za kuimarisha hali ya vitendea kazi ili kuendana na kasi ya ukuaji wa miji pamoja na maendeleo ya viwanda nchini ikiwemo kukamilisha taratibu husika ili kununua magari manne (4) ya kuzimia moto kupitia bajeti ya mwaka 2017/18; kuimarisha uhusiano na nchi wahisani na wadau wa maendeleo ili kuendelea kupata misaada mbalimbali ikiwemo vitendea kazi na mafunzo; na kuendelea kutafuta mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa wadau wa maendeleo. Katika mwaka wa 2018/19 Jeshi limepanga kununua magari matano (5) ya kuzimia moto pamoja na vifaa vya kuzimia moto.

64. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Jeshi limepata msaada wa magari matano (5) ambapo matatu (3) ni ya kuzimia moto na maokozi, moja la kubebbea wagonjwa na moja la utawala kutoka nchi za Ujeruman na Italia. Pia, Jeshi limepata msaada wa vifaa mbalimbali nya kuzimia moto na maokozi zikiwemo mashine za kujazia mitungi ya kusaidia hewa ya ziada wakati wa maokozi ambayo imepelekwa katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Lindi.

Elimu kwa Umma kuhusu namna ya Kukabiliana na Majanga ya Moto

65. *Mheshimiwa Spika*, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali ya moto kupitia vyombo nya habari ikiwemo vipindi nya luninga 37, vipindi nya redio 754 na makala za magazeti 20 na katika maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu ikiwemo shule, masoko, vivuko na vituo nya mabasi.

Katika kukabiliana na matukio ya moto katika shule za bweni nchini, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetoea elimu ya namna ya kuzuia na kukabiliana na matukio ya moto katika shule za bweni 256 katika mikoa mbalimbali. Jeshi la Zimamoto litaendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kupunguza majanga ya moto nchini.

Mafunzo kwa Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

66. *Mheshimiwa Spika*, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kuwapatia maafisa na askari wake mafunzo kwa lengo la kuboresha utendaji katika majukumu yake. Katika mwaka 2017/18 askari 64 walipatiwa mafunzo mbalimbali ndani ya nchi ikiwemo mafunzo ya kuzima moto na maokozi. Aidha, maafisa na askari 10 wamehitimu mafunzo ya kuzima moto na maokozi nchini Morocco na maafisa 11 wamepatiwa mafunzo ya kukabiliana na majanga mbalimbali nchini China. Katika mwaka 2018/19 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa askari na watumishi ili kuwaongezea ujuzi.

IDARA YA UHAMIAJI

Kuanzishwa kwa Mfumo wa Uhamiaji Mtandao

67. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa Mradi wa Uhamiaji Mtandao (*e-immigration*) ambao ulizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 31 Januari, 2018 unaendelea. Mradi huo umeanza kwa kutoa pasipoti za kielektroniki za Tanzania na Afrika Mashariki katika Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji Dar es Salaam na Zanzibar. Pasipoti mpya za kielektroniki zimetengenezwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa yenye uwezo wa kubebea taarifa mbalimbali pamoja na alama nyingi za kiusalama. Aidha, pasipoti hiyo inamwezesha mtumiaji kuwa na nakala yake ya pasipoti kwenye simu yake ya kiganjani baada ya kupakua ‘app’ ya pasipoti yake kwenye simu.

68. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Idara ya Uhamiaji itaendelea kukamilisha ufungaji wa mfumo wa pasipoti za kielektroniki katika mikoa yote hapa nchini. Vilevile, itaendelea kufunga mifumo ya viza za kielektroniki (*e-visa*), Hati za Ukaazi za kielektroniki (*e-permit*) na kufunga mifumo ya kudhibiti watu wanaoingia na kutoka nchini (*e-border management Control System*) pamoja na miundombinu ya uwekaji wa mtandao wa mawasiliano ya mifumo (*wide area network*) katika ofisi na vituo vya uhamiaji vya mipakani. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka yetu pamoja na kuongeza udhibiti wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Hali ya Ulinzi na Usalama Mipakani

69. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya wageni 1,021,071 waliingia nchini kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Machi, 2018 ikilinganishwa na wageni 1,032,978 waliongia katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2016/17. Aidha, jumla ya wageni 954,926 walitoka nchini ikilinganishwa wageni 881,478 walitoka kwa mwaka 2016/17. Katika mwaka 2018/19 Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa huduma kwa kufuata Sheria

na Kanuni za Uhamiaji kwenye mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini.

Misako, Doria na Ukaguzi

70. ***Mheshimiwa Spika***, Idara ya Uhamiaji iliendelea kufanya misako, doria na ukaguzi katika sehemu mbalimbali kama vile mipakani, migodini, viwandani, mahotelini na kwenye mashamba makubwa kwa lengo la kudhibiti wahamiaji haramu pamoja na biashara haramu ya usafirishaji binadamu nchini.

Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 13,393 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria, ikiwa ni ongezeko la asilimia 40 ya wahamiaji haramu 9,581 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka 2016/17. Vilevile, jumla ya Watanzania 211 waliokwenda nje ya nchi kinyume na taratibu za uhamiaji walirudishwa nchini. Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji itaendelea kufanya misako na doria ili kuwabaini na kuwaondoa wahamiaji haramu nchini na kuhakikisha watu wote wanaoingia na kutoka nchini wanatumia njia zilizo rasmi.

Vibali Vilivyotolewa kwa Wageni Wakaazi

71. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya vibali vyaa ukaazi 13,151 (daraja "A" 1,407; daraja "B" 8,551; na daraja "C" 3,193) vilivyotolewa kwa wageni walioingia nchini kwa madhumuni mbalimbali kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kiuhamiaji ikilinganishwa na vibali 11,259 (daraja A 2,474, daraja B 6,736, daraja C 2,049) vilivyotolewa kwa mwaka 2016/17. Aidha, katika kipindi husika jumla ya Hati za Mfuasi 1,335 zilitolewa ikilinganishwa na Hati 650 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2016/17. Vilevile, Hati za Msamaha 2,393 zilitolewa ikilinganishwa na Hati 1,427 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2016/17.

Pasipoti na Hati Nyingine za Safari

72. **Mheshimiwa Spika**, jumla Pasipoti 45,965 zilitolewa kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 kwa mchanganuo ufuatao: Pasipoti za Kawaida ni 45,697; Pasipoti za Kibalozi ni 220; Pasipoti za Kiutumishi ni 48. Katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2016/17 jumla ya Pasipoti 55,573 zilitolewa kama ifuatavyo: Pasipoti za Kawaida ni 54,503, Pasipoti za Kibalozi 229, Pasipoti za Kiutumishi 56, Pasipoti za Afrika Mashariki 785.

Aidha, Idara ya Uhamiaji ilitoa Hati za Dharura za safari 109,726 ikilinganishwa na Hati za Dharura za Safari 80, 445 zilitolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2016/17.

73. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 Idara ya Uhamiaji itaendelea kuboresha na kukamilisha huduma za kiuhamilaji kwa kutumila mfumo wa Uhamiaji Mtandao (*e-passport, e-visa, e-permit na e-border management control*).

Wageni Walioomba na Kupewa Uraia wa Tanzania

74. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya wageni 135 walipewa uraia, idadi hii ni ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2016/17 ambapo wageni 110 walipewa uraia. Wageni wallopewa uraia kwa kipindi hiki ni kutoka Burundi (4), Cameroon (2), China (1), Greece (1), India (83), Jordan (1), Kenya (1), Korea (1), Lebanon (2), Rwanda (2), Sierra Leone (1), Somalia (4), Uganda (2), Umoja wa nchi za Falme za Kiarabu (6), Yemen (23) na Zambia (1).

Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine

75. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Watanzania 60 waliukana uraia baada ya kujipatia Uraia wa mataifa mengine kama ifuatavyo: Australia (2), Botswana (4), Canada (3), India (4), Kenya (4), Lesotho (1), Norway (9), Sweden (1), Uganda (2), Uingereza (1), Ujerumani (19) na Zimbabwe (3) hivyo kupoteza hadhi ya

kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Sura ya 357 Rejeo la 2002. Katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2016/17 Watanzania 35 waliukana uraia wa Tanzania.

76. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Tanzania ya Uraia, Tangazo la Serikali Na. 427/2017 imetoa punguzo la ada ya uraia kutoka Dola za Marekani 5,000 hadi Shilingi 2,000,000. Punguzo hilo la ada linawahusu watu waliozaliwa Tanganyika kabla na baada ya uhuru ambao wazazi wao hawakutambulika kuwa raia wa Tanganyika kwa mujibu wa Sheria ya uraia ya Tanganyika Sura Na. 512 ya mwaka 1961. Vilevile, Kanuni imejumuisha watu waliongia nchini Tanganyika kabla na baada ya uhuru na kuendelea kuishi nchini kwa kipindi chote pamoja na watu waliozaliwa nje ya Tanzania kwa wazazi ambao ni raia kwa Tanzania kwa kuridhi. **Hivyo, natoa rai kwa watu hao kurekebisha hadhi yao ya urala ili kukidhi matakwa ya Sheria.**

Mafunzo katika Idara ya Uhamiaji

77. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18 askari wapatao 23 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini China na wawili (2) nchini Botswana kwa ufadhilli wa Serikali hizo. Aidha, askari 47 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ndani ya nchi.

Vitendea Kazi, Majengo ya Ofisi na Makazi ya Askari wa Uhamiaji

78. *Mheshimiwa Spika*, Idara ya Uhamiaji imenunua nyumba 103 katika eneo la Iyumbu mjini Dodoma kwa ajili ya makazi ya askari. Hadi sasa Idara imekabidhiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) jumla ya nyumba 63 na ujenzi wa nyumba 40 unaendelea. Aidha, ujenzi wa majengo ya ofisi unaendelea katika Mikoa ya Geita (asilimia 50), Manyara (asilimia 40), Mtwara (asilimia 11) na Lindi (asilimia 53). Ujenzi wa nyumba ya makazi ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji umefikia asilimia 65.

Namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutoa ahadi ya Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji Mjini Dodoma ambao utaanza mwaka 2018/19.

MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

Utambuzi, Usajili na Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa

79. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza lengo la **Ibara 145 (f) ya Ilani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020** kwa kuandikisha na kutoa Vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania kuanzia miaka 18 na zaidi, wageni wakaazi na wakimbizi. Hadi kufikia Machi, 2018 Mamlaka imesajili jumla ya wananchi 14,048,493, wageni wakazi 13,254 na wakimbizi 6,289 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Zoezi la uchukua jipicha na alama za kibaioloja linaendelea katika mikoa yote ili kutengeneza vitambulisho na kuvigawa kwa walengwa.

80. ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka imeunganisha (*interface*) mfumo wake wa utambuzi na taasisi nyingine 35 ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii na kuboresha hali ya ulinzi na usalama nchini. Aidha, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa kituo cha kutunzia kumbukumbu (*Data Centre*) huko Kibaha Mkao wa Pwani na kituo cha uokozi wakati wa majanga (*Data Recovery Centre*) Kihonda Mkao wa Morogoro pamoja na ofisi 13 za usajili za Wilaya Tanzania Bara na Zanzibar.

Vilevile, NIDA imeweka mtandao wa mawasiliano (*fibre optic*) kati ya Makao Makuu na ofisi 117 za usajili za wilaya ili kusaidia kusafirisha taarifa kutoka wilayani kwenda kituo kikuu cha kutengeneza vitambulisho na kutunza taarifa.

81. ***Mheshimiwa Spika***, uelewa kuhusu umuhimu wa Kitambulisho cha Taifa umeongezeka miongoni mwa wananchi na kusababisha ongezeko kubwa la wananchi wanaojitokeza kusajiliwa kwa ajili ya Vitambulisho vya Taifa.

Hali hii imetokana na juhudzi za Serikali kupitia vyombo mbalimbali vya habari kutoa elimu ya umuhimu wa Vitambulisho vya Taifa kwa uchumi na maendeleo ya mwananchi na nchi yetu kwa ujumla. Mamlaka inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa Kitambulisho cha Taifa na jinsi kinavyoweza kuwasaidia katika kupata huduma mbalimbali mfano huduma za kibenki, pasi ya kusafiria, fidia wakati wa majanga na kubaini vitendo vya kihalifu.

82. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa watu nchi nzima pamoja na kuunganisha mtandao wa mawasiliano kati ya ofisi za usajili za wilaya 33 na Makao Makuu.

Aidha, Wizara kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea inatarajia kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika Mkoa wa Dodoma pamoja na ujenzi wa ofisi katika wilaya 42 Tanzania Bara na Zanzibar. Mamlaka pia itaendelea na ukarabati kwa baadhi ya ofisi za usajili za wilaya na kuungunisha mfumo wa utambuzi na mifumo ya taasisi nydingine ili iweze kusomana na hatimaye kubadilishana taarifa.

83. *Mheshimiwa Spika*, katika utekelezaji wa lengo la utambuzi na usajili imebainika kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuanza kutekeleza jukumu la utambuzi na usajili mara tu mtoto anapozaliwa na kupewa namba ya pekee ya utambuzi na usajili. Suala la utambuzi wa watoto ni muhimu katika kuimarisha hali ya usalama katika nchi yetu. Mtakumbuka kuwa katika siku za hivi karibuni kumeibuka makundi mbalimbali ya kihalifu yanayowahusisha vijana chini ya miaka 18.

Tumeshuhudia makundi kama *Panya Road na Wakorea weusi* wakijihuisha na vitendo vya kihalifu katika Jiji la Dar es Salaam na Mbeya. Athari za kutokuwatambua vijana hawa wanapozaliwa mpaka wafikie umri wa miaka 18 umeathiri upeletelezi wa kupata taarifa sahihi za

kuwatambua uasili wao, wazazi au walezi na makazi ili kuwadhibiti kutojihusisha katika vitendo nya uhalifu.

HUDUMA KWA WAKIMBIZI

84. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imeendelea kutekeleza jukumu lake la kimataifa la kuhifadhi wakimbizi na waomba hifadhi kutoka nchi mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, Tanzania imeshuhudia kwa mara nyingine ongezeko la waomba hifadhi wanaopokelewa, hususan kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Tanzania ilikuwa na jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 356,548. Kati ya hao 276,047 kutoka Burundi, 79,950 Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, 150 Somalia na 401 kutoka mataifa mengine.

85. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Kamati ndogo ya Kitaifa ya Kuhoji Waomba Hifadhi (*Ad hoc Committee*), iliwahoji waomba hifadhi 1,342 kutoka nchi ya Burundi ambapo waomba hifadhi 198 walipendekezwa kupewa hadhi ya ukimbizi nchini baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998 na waomba hifadhi 1,144 walikosa sifa za kupewa hadhi ya ukimbizi.

86. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kati ya Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 50,437 kutoka Burundi walijandikisha ili wasaidiwe kurejea kwa hiari kwenye nchi yao ya asili. Zoezi la kuwarejesha kwa hiari linaendelea na mpaka kufikia mwezi Machi, 2018 jumla ya wakimbizi 21,008 wamerejea Burundi.

Ili kuongeza kasi ya kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao, Serikali ya Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa ishirini (20) wa Pande Tatu uliofanyika nchini Burundi tarehe 28 Machi, 2018 ambapo iliazimwiwa kuwa ifikapo mwezi Desemba, 2018 zaidi ya wakimbizi 72,000 wawe wamerejeshwa katika nchi ya asili. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2019, wakimbizi wote wa Burundi waliopo kwenye makambi ya Kigoma wawe wamerejea nchini kwao.

87. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) inatekeleza mpango wa kuwapeleka wakimbizi katika nchi ya tatu ikiwa ni moja ya suluhisho la kudumu linalotolewa kwa wakimbizi. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya wakimbizi 926 walihamishiwa nchi ya tatu katika mataifa ya Australia 25, Canada 137, Finland 4, Marekani 756 na Uingereza 4.

88. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora ilifanya zoezi la uhakiki na usajili wa wakimbizi wa Burundi walioingia nchini mwaka 1972. Katika zoezi hilo kwenye Mikoa ya Tabora na Katavi wakimbizi 19,187 walihakikiwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Oktoba, 2017. Katika Mkoa wa Kigoma, zoezi la uhakiki lilifanyika mwezi Januari na Februari, 2018 ambapo jumla ya wakimbizi 15,791 walihakikiwa. Lengo la zoezi hili ni kuiwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za wakimbizi wote wa kundi hilo.

89. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na UNHCR imeendelea kuhamasisha na kusimamia shughuli za hifadhi ya mazingira kwenye kambi za wakimbizi na vijiji jirani. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, shughuli za mazingira zilizotekelawa ni pamoja na: Upandaji wa miti 1,988,028; ujenzi wa majiko banifu 84,590; na nyumba za tofali na bati 2,274.

Aidha, mradi wa matumizi ya gesi umeendelea kutekelezwa ambapo jumla ya mitungi 26,450 ya gesi imegawiwa kwa wakimbizi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na UNHCR inaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya athari za mazingira kutoptana na shughuli za wakimbizi ndani ya kambi na maeneo ya vijiji jirani ili kuwa na mikakati endelevu ya kukabiliana na athari hizo.

90. *Mheshimiwa Spika*, kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama imeendelea kuwa shwari ndani na nje ya kambi za wakimbizi. Wizara kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama katika mikoa inayohifadhi wakimbizi, imeendelea

kuimarisha ulinzi na usalama kwa kufanya doria za mara kwa mara. Aidha, wakimbizi wanaobainika kujihusisha na vitendo vyatia kihalifu wamekuwa wakichukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za nchi.

VITA DHIDI YA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU

91. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 Wizara kupitia Sekretarieti ya Kupambana na Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) imewaokoa wahanga 20 (Watanzania 18, Afrika Kusini (1) na Mrundi (1)) wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu waliokuwa wakitumikishwa katika maeneo mbalimbali nchini na kuwaunganisha na familia zao. Katika kipindi hicho jumla ya kesi 24 zimefunguliwa ambapo kesi 23 zinaendelea katika mahakama mbalimbali nchini na kesi moja (1) watuhumiwa wawili (2) wote Wanawake walihukumiwa kifungo cha miaka saba (7) gerezani.

92. ***Mheshimiwa Spika***, Sekretariati ilifanya ukaguzi katika maeneo hatarishi ya utumikishwaji wa wahanga wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu katika wilaya zote Jijini Dar es Salaam. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na viwanda, *massage parlor*, gereji za Wachina, kampuni kubwa na klubu za usiku. Lengo la ukaguzi huo ni kujiridhisha kuwa watumishi wanajua haki zao za msingi na kuwaelimisha juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

93. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Sekretarieti kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la *Lawyers Without Borders* imetoa elimu juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kwa wadau muhimu katika mikoa saba ambayo ni Arusha, Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga na Simiyu. Wadau hao ni pamoja na Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Askari wa Jeshi la Polisi, Maafisa Uhamiaji, Maafisa Ustawi wa Jamii, Viongozi wa Serikali za Mitaa na wawakilishi kutoka mashirika mbalimbali yasiyo ya Serikali.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa namna ya kupeleleza, kuchunguza na kuendesha mashtaka na kusikiliza kesi dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji binadamu. Sekretarieti pia imetoa elimu kwa Watanzania hususan wasichana wanaoomba hati za kusafiria kwenda nje ya nchi kufanya kazi kufuatia taarifa mbalimbali zinazohusu manyanyaso kwa wasichana wanaopelekwa kwenda kufanya kazi nje ya nchi. Aidha, **kutokana na taarifa hizo, mnamo mwezi Januari, 2018 nilitoa tamko la kuzuia utoaji wa pasipoti za mafungu kwa wasichana wanaoenda kufanya kazi za ndani nchi za nje, hususan nchi za Uarabuni.**

94. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2018/19 Sekretarietiitaendelea kupambana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu ikiwemo kutoa elimu kwa umma pamoa na kuratibu mafunzo kwa wadau/vyombo vnavyosimamila sheria ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu.

UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

95. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya Malalamiko 175 kutoka kwa wananchi dhidi ya utendaji wa Wizara yalipokelewa katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018. Kati ya malalamiko hayo 121 yalihusu Jeshi la Polisi, 26 Jeshi la Magereza, 19 Uhamiaji, matatu (3) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, matatu (3) Idara ya Huduma kwa Wakimbizi, mawili (2) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa na moja (1) Idara ya Huduma ya Sheria.

Aidha, malalamiko 100 yalishughulikiwa na kukamilika na mengine 75 yanaendelea kushughulikiwa yakiwa kwenye hatua mbalimbali. Wizara itaendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi katika mwaka 2018/19 ili kuimarisha utoaji wa huduma.

USAJILI WA VYAMA VYA KIJAMII NA KIDINI

96. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018 jumla ya maombi 252 ya kusajili vyama

yalipokelewa ambapo maombi 178 ni vyama vya kijamii na 74 ni vyama vya kidini. Kati ya maombi hayo vyama 136 vilisajiliwa na maombi 5 yalikataliwa kutokana na kutotimiza matakwa ya kisheria na sababu nyingine za kiusalama na maombi 111 ya usajili wa vyama yapo katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa. Wizara itaendelea na zoezi la usajili na uhakiki wa vyama vya kijamii na kidini katika mwaka 2018/19.

97. *Mheshimiwa Spika*, hata hivyo kuna malimbikizo mengi ya maombi ya usajili ya vyama vya kidini kutokana na maombi yote kutakiwa kufikia ofisi ya Msajili Makao Makuu ya Wizara. Wakati Serikali inaelekeea kuwa na ofisi za msajili kwa kila kanda, naelekeza wote wenyewe Taasisi za Kidini mikoani wafike ofisi za wilaya na kuwasilisha maombi yao kwa Katibu Tawala wa Wilaya. Na wote waliofikisha maombi katika wilaya husika, wapate utambuzi wa awali ili taasisi hizo zifanye kazi zikifahamika wakati taratibu za kupata usajili wa kudumu ukiendelea. Narudia wapatiwe utambuzi wa awali wakati wanasubiri usajili wa kudumu.

Maendeleo ya Rasilimali Watu na Ajira Makao Makuu ya Wizara

98. *Mheshimiwa Spika*, Makao Makuu ya Wizara imepanga kuajiri watumishi 74 ili kuziba nafasi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufariki, kustaafu na kuacha kazi. Wizara pia itawapandisha vyeo watumishi 106 wa kada mbalimbali na nafasi 11 za watumshi watabadilishwa vyeo.

Mapambano Dhidi ya Maambukizi ya VVU/UKIMWI

99. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia miongozo husika Wizara iliedelea kuwapatia fedha za kila mwezi watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa ajili ya kuimarissha afya zao dhidi ya magonjwa nyemelezi. Aidha, Wizara ilitoa elimu ya jinsi ya kujikinga na magonjwa sugu yasiyoambukizwa kwa watumishi 200. Katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea kutoa elimu ili kuwahamasisha

watumishi kufuata taratibu za afya ili kujikinga na maambukizi dhidi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI pamoja na magonjwa sugu yasiyoambukizwa.

C. SHUKRANI

100. *Mheshimiwa Spika*, natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Mhandisi Hamad Masauni kwa msaada wake anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu Meja Jeneral (Mstaafu) Projest A. Rwegasira na Naibu Katibu Mkuu Balozi Hassan S. Yahya kwa juhudzi zao kubwa za kusimamia utendaji kazi wa Wizara.

101. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, nawashukuru Inspeksa Jenerali wa Jeshi la Polisi, Bw. Simon N. Sirro; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Dkt. Juma A. Malewa; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Bw. Thobias E. Andengenye; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala; na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Bw. Andrew W. Massawe. Natoa shukrani zangu pia kwa Makamishna; Makamishna Wasaidizi; Wakuu wa Idara, Vitengo na Sehemu; askari na watumishi wote kwa kuendelea kutekeleza vema kazi na majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

102. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, ninatoa shukrani zangu kwa nchi wahisani zikiwemo Astarlia, Botswana, Canada, China, Finland, India, Italia, Jamhuri ya Watu wa Korea, Marekani, Morocco, Uingereza na Ujeruman pamoja na Taasisi na Mashirika ya Kimataifa ya DFID, FSDT, IOM, UNDP, UNHCR, Vyombo vya Habari, Taasisi za kijamii, kidini na zisizo za Serikali na wananchi kwa kuendelea kutoa misaada na taarifa mbalimbali ambazo zimesaidia utendaji kazi wa Wizara.

103. *Mheshimiwa Spika*, kipekee naishukuru familia yangu, ndugu, marafiki na wananchi, hususan wa Jimbo langu la Iramba Magharibi kwa ushirikiano wao katika kuchangia maendeleo ya jimbo letu.

D. HITIMISHO

104. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kudhibiti matukio ya uhalifu ili kuhakikisha amani na usalama unaendelea kuwepo nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itashirikiana na vyombo vingine vya dola nchini pamoja na wadau mbalimbali.

105. ***Mheshimiwa Spika***, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 945,555,651,000** kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2018/19. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 907,269,969,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 385,725,478,187** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 521,544,490,813** ni Mishahara. Fedha za Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 38,285,682,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 37,500,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 785,682,000** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa Namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili aweze kuwasilisha. Karibu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Rehani.

MHE. SALUM MWINYI REHANI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kabla ya kuanza ningeomba taarifa yangu hii iingizwe yote kama ilivyo pengine kama sitaweza kuimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 , naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka

wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa 2018/2019 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa na kuikubali na hatimaye kuidhinisha bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeipa Kamati hii jukumu la kusimamia Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa mamlaka kwa Kamati zote za kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 27 na 28 Machi, 2018 na kuchambua bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa bajeti ulitekelezwa sanjari na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaokwisha ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Nafurahia kusema kwamba, kwa upande wa Kamati, Bunge letu ilikutana tarehe 16 hadi 20 Machi, 2018, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelzwa na Wizara hii. Miradi iliyokaguliwa kwa makadirio yaliyochambuliwa yalihu mafungu matano ya kibajeti yafuatayo:-

- (1) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
- (2) Fungu 28 Jeshi la Polisi;
- (3) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;
- (4) Fungu 51 - Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*); na
- (5) Fungu 93 -Idara ya Uhaniaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni:-

Sehemu ya kwanza, Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; Sehemu ya pili, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; Sehemu ya tatu, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na Sehemu ya nne, Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangilio huu unakusudia kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kulinganisha na makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja ili Bunge liweze kuamua kuhusu maombi ya fedha ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Maeleo Kuhusu Miradi ya Maendeleo Iliyokaguliwa; ili kutekeleza masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo ilitengewa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, Kamati ilikagua miradi iliyotengewa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na fedha hizo kutolewa na kutumika katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi hiyo ulitekelezwa kuanzia tarehe 16 hadi 20 Machi, 2018, katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Miradi iliyokaguliwa ni ifuatayo:-

(a) Fungu 29-Jeshi la Magereza; mradi namba 6308, kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa Gereza la Ruangwa.

(b) Fungu 93-Idara ya Uhamiaji; mradi namba 6301 kuhusu Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika ziara hiyo, Kamati ilikagua nyumba za Jeshi la Polisi na Magereza katika Mkoa wa Lindi baada

ya kupokea taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo iliyobainisha kuwa Nyumba hizo zipo katika hali mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Ukaguzi; baada ya kueleza kuhusu miradi ya maendeleo na maeneo yaliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze taarifa hii kwa kueleza kuwa, ucheleweshwaji au kutokutolewa kabisa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina ni changamoto kubwa na ya muda mrefu ilioathiri utekelezaji wa miradi hiyo chini ya Wizara hii. Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi umegawanyika katika makundi mawili yafuatayo:-

(a) Miradi ya muda mrefu ambayo utekelezaji wake umesimama. Mfano wa miradi hii ni mradi namba 6301 kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji katika Mkoa wa Lindi.

(b) Miradi ambayo utekelezaji wake umechelewa kuanza licha ya kuanzishwa muda mrefu. Mfano wa miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa Gereza la Wilaya la Ruangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu miradi hii yanapatikana katika ukurasa wa nne hadi ukurasa wa sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ukaguzi wa nyumba za Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, Kamati ilikagua nyumba za askari katika Kambi ya FFU-Mitwero, Kambi ya Polisi-Lindi Mjini pamoja na nyumba za Gereza la Wilaya ya Lindi. Katika ziara zote hizo, Kamati ilibaini kuwepo kwa uhaba wa nyumba za askari na nyumba chache zilizopo nydingi ni ndogo na baadhi yake ni chakavu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limesababisha askari wengi kuishi nje ya Kambi, jambo ambalo si tu linaathiri morali ya kazi ya askari wetu, bali pia linaweza kusababisha athari kubwa katika masuala ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni kuhusu Miradi ya Maendeleo. Kutohana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara hizo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kutohukutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa ukamilifu kunaathiri ratiba ya utekelezaji wake.

(ii) Mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unahitaji kuboreshwa zaidi.

(iii) Kutohukamilisha miradi ya zamani na kuanzisha miradi mingine mipyä kunaingizia Serikali hasara kwa kutumia fedha nyingi kuanzisha miradi ambayo haikamilishwi.

(iv) Kutohufuatilia kwa ukaribu miradi inayotekelizwa katika mikoa ya pembezoni ya nchi kama vile Mikoa ya Lindi na Mtwara, kunasabisha baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

(v) Kutumia fedha za Matumizi Mengineyo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kunaathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika mpango kazi wa wizara za Serikali.

(vi) Upo umuhimu wa Serikali kuwa na miradi mingi inayotekelizwa kwa ubia kati ya Serikali na wawekezaji ili kuwa na miradi ambayo utekelezaji wake ni wa uhakika zaidi.

(vii) Ni vyema Serikali ikayatumia mashirika yake ya nyumba na Mifuko ya Jamii kutekeleza miradi yake ya ujenzi kwa mikopo yenye riba nafuu.

(viii) Manufaa ya miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Wizara hii yatatokana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzingatiaji wa maoni ya Kamati na mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilihusu maeneo makuu mawili. Maeneo hayo ni uzingatiaji wa maoni ya ushauri wa Kamati na mapitio ya utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa, katika masuala 21 yalitolewa ushauri 10 yamezingatiwa kikamilifu, masuala matano yanaendelea kuzingatiwa na masuala saba hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na ufinyu wa bajeti. Maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa maoni ya Kamati yanapatikana katika ukurasa wa nane hadi wa 10 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2017/2018. Kamati ilichambua taarifa ya makusanyo kwa kulinganisha lengo na makusanyo hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kama ilivyowasilishwa. Njia ya jedwali na grafu ilitumika kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kati ya lengo na makusanyo. Uchambuzi huo unaonekana katika Jedwali Na.01 na Grafu Na. 01 na Na.02 katika ukurasa wa 13 wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto; Jeshi hili lilitengenya kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia kumi na mbili (12), lakini taarifa ya makusanyo ilionesha kuwa Fungu hili limechangia kwa asilimia tatu tu ya kiasi kilichokusanywa.

(ii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi, lilitengenya kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 25, lakini taarifa ya makusanyo ilionesha kuwa Fungu hili lilitengenya kwa asilimia 27 ya kiasi kilichokusanywa.

(iii) Fungu 29 - Jeshi la Magereza, lililenga kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia moja lakini taarifa ya makusanyo ilionesha kuwa Fungu hili lilichangia kwa asilimia 0.6 ya kiasi kilichokusanya.

(iv) Fungu 51 - Wizara, lililenga kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.4 na taarifa ya makusanyo ilionesha Fungu hilo lilichangia kwa asilimia 0.2 ya kiasi kilichokusanya.

(v) Makusanyo ya Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 61.5 lakini taarifa ya makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo lilichangia asilimia 69.5 ya kiasi kilichokusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila Fungu ikillinganishwa na mapato halisi ya kila Fungu, imeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mafungu 28, 29, 51 na 93 ni wa kuridhisha. Jambo hili ni la kupongezwa kwani pamoja na changamoto ya kupungua kwa makusanyo ya Jeshi la Zimamoto kama ilivyoanishwa hapo juu bado Wizara imeweza kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya lengo liliowekwa katika robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya Wizara umeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu. kwa kuzingatia jambo hilo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2018. Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 66 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara hii.

(ii) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2018, asilimia 98 ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia mbili tu kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(iii) Hadi kufikia mwezi Februari 2018, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 76 ya bajeti ya matumizi mengineyo iliyoidhinishwa na asilimia 28 ya bajeti ya maendeleo.

(iv) Hadi kufikia mwezi Februari 2018, Mafungu mawili tu ya Jeshi la Polisi (Fungu 28) na Wizara (Fungu 51) yalikuwa yamepokea fedha za maendeleo, ambapo Fungu 28 lilipokea asilimia 25 na Fungu 51 lilipokea asilimia 50 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa kila Fungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili matumizi ya kawaida kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na taasisi zake ni wa kuridhisha. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo hauridhishi hususani kwa Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji. Kwa miaka mitatu mfululizo, Kamati imekuwa ikishauri kuhusu Mafungu haya kupewa kipaumbele katika kupelekewa fedha za maendeleo lakini ushauri huo haujazingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo unaathiri mpango na ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mafungu hayo ambayo baadhi yake imesimama kwa muda mrefu. Mfano wa miradi hiyo ni: Mradi wa Ujenzi wa Jiko na Mabweni katika Gereza la Segerea uliosimama tangu mwaka 1991 na Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa katika Gereza la Segerea uliosimama tangu mwaka 1994.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Uchambuzi wa Kamati

umeonesha kuwa utekelezaji wa kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji majukumu yake utaimarishwa endapo tu Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ukamillifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2018/2019. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya Sh.297,014,614,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati kuhusu makadirio ya mapato unaonesha yafuatayo:-

(i) Makadirio ya makusanyo kwa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 yanaongezeka kwa asilimia moja ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha ulioisha.

(ii) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linategemewa kukusanya asilimia 3.1 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 12, kiasi ambacho kiuwiano ni pungufu kwa asilimia 8.9.

(iii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi lilitegemewa kukusanya asilimia 28.5 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 25.1 kiasi ambacho ni ongezeko kiuwiano kwa asilimia 3.4.

(iv) Fungu 29 - Jeshi la Magereza linategemewa kukusanya asilimia 0.6 ya makusanyo ikiwa ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.3 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya kwa asilimia 0.9.

(v) Fungu 51 - Wizara inategemewa kukusanya asilimia 0.3 ya makadirio ya makusanyo ukilinganishwa na

mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo ilitegemewa kukusanya asilimia 0.4. Kiasi hiki ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.1.

(vi) Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji linategemewa kukusanya asilimia 67.5 ya makadirio ya makusanyo ikiwa ni ongezeko katika uwiano kwa asilimia sita ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo ilitegemewa kukusanya asilimia 61.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufanuzi huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii. Kamati imebaini kuwa wakati wa makadirio ya makusanyo ya Mafungu ya Zimamoto, Magereza na Wizara yamepungua, makadirio ya makusanyo ya Polisi na Idara ya Uhamiaji yanatarajiwa kuwa mazuri hivyo kuongeza Makadirio ya Mapato ya Wizara nzima kwa asilimia moja ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka unaoisha. Kamati inapongeza Mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika makusanyo ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio na matumizi. Kamati imefanya uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara kama yalivyowasilishwa na Waziri mwenye dhamana kwa kupitia kasma, vifungu na mafungu yote yaliyoidhinishwa na bajeti iliyoidhinishwa na utekelezaji katika mwaka wa fedha wa 2017/2018. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imeongezeka kwa Sh.15,158,834,000 sawa na ongezeko la asilimia moja ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hili linachangiwa na ongezeko la bajeti ya matumizi mengineyo ambapo kiasi cha Sh.18,018,594,000 kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka unaoishia.

(ii) Bajeti inayoombwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, imepungua kwa asilimia 0.3 kwa bajeti ya maendeleo, mishahara imepungua kwa asilimia 1.2 na imeongezeka kwa asilimia 1.5 katika matumizi mengineyo ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa 2017/2018.

(iii) Asilimia nne ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, asilimia 55 ni kwa ajili ya mishahara na asilimia 41 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

(iv) Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, asilimia 40 ni kwa ajili ya *NIDA*, asilimia 27 kwa ajili ya Idara ya Uhamiaji, asilimia 13 ni kwa ajili ya Jeshi la Magereza, asilimia 12 kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na asilimia nane ni kwa ajili ya Jeshi la Polisi.

(v) Kifungu namba 1201 kuhusu *enhancement of Prisons Industries* kimetengewa kiasi cha Sh.2,000,000,000 kwa ajili ya kuanzisha viwanda viwili vya useremala. Jambo hili ni la kupongeza kwani kwa miaka miwili mfululizo kifungu hiki hakikuwa kimetengewa fedha yoyote.

(vi) Pamoja na Kamati kusitiza kuhusu Serikali kutenga Shillingi bilioni mbili kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilitopo eneo la Mchicha, TAZARA, katika Wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam kwa miaka miwili mfululizo; mwaka 2016/2017 na 2017/2018, Serikali haijatenga kasma yoyote kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo hilo katika mwaka wa fedha 2017/2018. (*Makof*)

(vii) Hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali katika Gereza la Segerea licha ya Kamati kusitiza kwa muda wa miaka miwili mfululizo; 2016/2017 na 2017/2018 kuhusu kutengwa kwa fedha hizo hasa kwa kuzingatia umuhimu wa hospitali hiyo kwa Gereza la Segerea.

(viii) Hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha majengo ya Ofisi za Uhamiaji Mikoani licha ya kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Shilingi bilioni 10 zilizombwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Ofisi ya Uhamiaji, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri. Kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa mapendelekezo na ushauri wa jumla kwa mafungu yote na ushauri mahsusini kwa kila Fungu kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itoe fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha miradi ya muda mrefu iliyosimama hususani Miradi ya Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Idara ya Uhamiaji. Hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha unaoishia, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 28 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo za Mafungu mawili tu ya Fungu 28 - Jeshi la Polisi na 51 – Wizara na Mafungu mengine matatu kutopelekewa fedha zozote za maendeleo.

(ii) Serikali isimamie utaratibu wa kutoanzisha miradi mipya kabla ya kukamilisha miradi ambayo haijakamilika. Katika mwaka 2018/2019 kipaumbele kitolewe katika utekelezaji wa miradi ya muda mrefu iliyosimama kabla ya kuanza kutekeleza miradi mingine mipya. Hii itaiwezesha Serikali kuwa na miradi michache iliyokamilika na yenye tija kwa Serikali na Taifa kwa jumla.

(iii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa pamoja na nia njema ya Serikali kuhamia Dodoma, itekeleze miradi yote iliyokuwa imeanza kutekelezwa katika Jiji la Dar

es Salaam, hususani ukamilishaji wa Jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliopo eneo la Mchicha-TAZARA, Dar es Salaam. (*Makof*)

(iv) Serikali ishirikiane na mashirika yake ya nyumba na mifuko ya kijamii kutekeleza miradi ya ujenzi kwa mikopo yenye riba nafuu katika kujenga nyumba za askari wa Majeshi ya Polisi, Magereza, Zimamoto na Idara ya Uhamiaji. Hii itasaidia kupunguza tatizo la makazi kwa askari ambaao wengi wanaishi nje ya kambi zao jambo ambalo linaweza kuwa na athari kubwa katika masuala ya ulinzi na usalama.

(v) Serikali iweke mkakati wa muda mrefu kuhusu namna ya kutekeleza miradi yake iliyosimama ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika. Mkakati huo uainishe miradi na kipindi ambacho inatarajiwa kukamilishwa kwa miradi hiyo.

(vi) Kamati inatambua nia njema ya Serikali katika kuondoa suala la *retention* kwa Wizara zake zote. Hata hivyo, kutokana na unyeti wa vyombo vya Ulinzi na Usalama, Kamati inashauri Serikali iweke utaratibu maalum wa kuyaruhusu Majeshi ya Polisi, Magereza, Zimamoto na Idara ya Uhamiaji kubaki na angalau asilimia 40 ya makusanyo yao ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yao ya msingi kama kutengeneza magari ya doria, ununuzi wa mafuta na vilainishi na kugharamia miradi yao ya maendeleo ikiwemo nyumba za askari. (*Makof*)

(vii) Serikali ilipe madeni ya Majeshi ya Polisi na Magereza ambayo hadi kufikia mwezi Machi, 2018 Jeshi la Polisi lilikuwa linadaiwa shilingi bilioni nane kwa ajili ya gharama za umeme na shilingi bilioni saba kwa ajili ya gharama za maji. Vilevile, Jeshi la Magereza lilikuwa linadaiwa gharama za umeme shilingi bilioni nne na gharama za maji shilingi bilioni mbili. Madeni haya yamepelekea huduma hizo kusitishwa katika baadhi ya...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makamu, naomba umalizie.

MHE. SALUM MWINYI REHANI - MAKAMU MWENYEKITI, KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba dakika tano. Baadhi ya Magereza jambo ambalo limeweza kusababisha...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, malizia kwa dakika moja tu.

MHE. SALUM MWINYI REHANI - MAKAMU MWENYEKITI, KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa umakini na ufuatiliaji lakini na uwezo wao wa kuweza kuchambua mambo mbalimbali wakati wa ziara za miradi mbalimbali katika maeneo yao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati hii, napenda vilevile kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba; Naibu wake, Mheshimiwa Injinia Masauni; Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa umakini na ukaribu na Kamati na kuweza kushirikiana kwa pamoja ili kuweza kutimiza lengo lilitokuwa limekusudiwa la kusimamia Wizara hii na uandaaji wa bajeti ambayo imeweza kuwasilishwa hii leo na Waziri husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Rehani. (*Makof*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA
NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (FNGU 14, 28, 29,
51 NA 93) KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA
MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/
2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokea Taarifa hii na kuikubali, na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeipa Kamati hii jukumu la kusimamia Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia Bajeti za Wizara inazosimamia. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 27 na 28 Machi, 2018 na kuchambua Bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa bajeti ulitekelezwa sanjari na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyo tengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Nafurahi kiliarifu Bunge hili kuwa tarehe 16 hadi 20 Machi, 2018, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelze wa na Wizara hii. Miradi

iliyokaguliwa na mkadirio yaliyochambuliwa yalihusu Mafungu matano (5) ya kibajeti yafuatayo:-

- i) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,
- ii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi,
- iii) Fungu 29 - Jeshi la Magereza,
- iv) Fungu 51 - Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa- NIDA; na
- v) Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Ili kulisaidia Bunge lako tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu hizo ni :-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- ii) Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiajji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, mpangilio huu unakusudia kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kulinganisha na makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja ili Bunge liweze kuamua kuhusu maombi ya fedha ya Wizara hii.

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo ilijo chini ya Wizara ya

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo ilitengewa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Aidha, Kamati ilikagua miradi iliyotengewa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na fedha hizo kutolewa na kutumika katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Ukaguzi wa miradi hiyo ulitekelezwa kuanzia tarehe 16 hadi 20 Machi, 2018, katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Miradi iliyokaguliwa ni ifuatavyo:-

a) Fungu 29- Jeshi la Magereza

Mradi Na. 6308 kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa Gereza la Ruangwa

b) Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

Mradi Na. 6301 kuhusu Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika ziara hiyo, Kamati ilikagua nyumba za Jeshi la Polisi na Magereza katika Mkoa wa Lindi baada ya kupokea Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo iliyobainisha kuwa Nyumba hizo zipo katika hali mbaya.

2.2 Matokeo ya Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kuhusu Miradi ya Maendeleo na maeneo yaliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya utekelezaji katika Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze taarifa hiyo kwa kueleza kuwa, ucheleweshwaji au kutoikutolewa kabisa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina ni changamoto kubwa na ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi ilio chini ya Wizara hii. Kutohana na changamoto hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Miradi umegawanyika katika makundi mawili kama yanavyoiezwa hapa chini.

Mheshimiwa Spika, kundi la kwanza ni Miradi ya muda mrefu ambayo utekelezaji wake umesimama. Maeleo ya Serikali yalionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo zimekuwa hazitolewi kwa

ukamilifu kwa baadhi ya miaka ya fedha na wakati mwiningine hazitolewi kabisa. Mfano wa Miradi hii ni Mradi Na. 6301 kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ilitengewa jumla ya Shilingi **1,603,593,810.00** katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 ambapo ulianza kutekelezwa tarehe 02 Januari, 2014 na ultarajiwu ukamiliwe tarehe 07 Aprili, 2016. Hata hivyo, fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wake zimekuwa hazitolewi kwa ukamilifu. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia mwezi Mei, 2016, kiasi ambacho kilikuwa kimetolewa ni Shilingi **856,512,424.39** sawa na asilimia 53.3. Fedha zilizobaki, Shilingi **747,081,385.61** sawa na asilimia 46.7 zimekuwa zikitengwa katika miaka miwili mfululizo, 2016/2017 na 2017/2018, lakini hazijawahi kutolewa.

Mheshimiwa Spika, kundi la pili ni Miradi ambayo utekelezaji wake umechelewa kuanza licha ya kuidhinishwa muda mrefu. Maeleo ya Serikali yalionesha kuwa, kutokutolewa fedha kwa wakati kulisababisha utekelezaji wa miradi uanze kwa kuchelewa. Mfano wa miradi hiyo ni Mradi wa Ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Ruangwa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilionesa kuwa, eneo la Gereza hili lilipatikana Mwaka 2008/2009 na Wananchi waliokuwapo katika eneo hilo, walilipwa fidia jumla ya **Shilingi 21,093,907.50**, ili kupisha eneo litumike kwa ujenzi wa Gereza hilo. Utekelezaji ulipangwa ufanyike kwa miaka minne tangu kupatikana kwa eneo hilo. Hata hivyo, fedha kwa ajili ya ujenzi wa Gereza hilo hazikutengwa kwa takribani miaka mitano (5) mfululizo tangu Wananchi walipolipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, ujenzi wa Gereza hili uliidihiishiwa **Shilingi 1,590,324,000.00** kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi. Hata hivyo, **Shilingi 100,324,000.00** sawa na asilimia 6 ya fedha zilizoidhinishwa ndizo zilizotolewa katika mwaka huo wa fedha, na **Shilingi 1,490,000,000.00** sawa na asilimia 94 zilitolewa Mwezi Septemba, 2017 ikiwa ni Mwaka wa Fedha

2017/2018. Aidha, kati ya fedha zilizotolewa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, **Shilingi Milioni 20** zilitolewa kutoka kwenye fungu la Matumizi Mengineyo, kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya muda ya askari na wafungwa; ujenzi wa mabweni mawili ya wafungwa wanaume na ujenzi wa jiko la Gereza la Wilaya Nachingwea ambalo lilikuwa likitunza mahabusu na wafungwa wa Wilaya ya Ruangwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa ukaguzi wa nyumba za Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, Kamati ilikagua nyumba za askari katika Kambi ya FFU Mitwero, Kambi ya Polisi Lindi Mjini pamoja na nyumba za Gereza la Wilaya, Lindi. Katika ziara zote hizo, Kamati ilibaini kuwepo kwa uhaba wa nyumba za Askari, na nyumba chache zilizopo nyingi zao ni ndogo na baadhi yake ni chakavu sana.

Mheshimiwa Spika, Suala hili limesababisha Askari wengi kuishi nje ya Kambi, jambo ambalo si tu linaathiri morali ya kazi ya Askari wetu, bali pia linaweza kusababisha athari kubwa katika masuala ya ulinzi na usalama.

2.3 Maoni kuhusu Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kama ilivyobaininka wakati wa ziara hizo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

- i) Kutokutolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati na kwa ukamilifu kunaathiri ratiba ya utekelezaji wake;
- ii) Mwenendo mzima wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unahitaji kuboreshwa zaidi;
- iii) Kutokamilisha miradi ya zamani na kuanzisha miradi mingine mipyä kunaingizia Serikali hasara kwa kutumia fedha nyingi kuanzisha miradi ambayo haikamilishwi;
- iv) Kutofuartilia kwa ukaribu miradi inayotekelzwaa katika Mikoa ya pembezoni ya Nchi kama vile Mikoa ya Lindi na Mtwara, kunasabisha baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango;

v) Kutumia fedha za Matumizi Mengineyo kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kunaathiri utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika Mpango Kazi wa Wizara/Taasisi za Serikali;

vi) Upo umuhimu wa Serikali kuwa na miradi mingi inayotekelawa kwa ubia kati ya Serikali na Wawekezaji ili kuwa na miradi ambayo utekelezaji wake ni wa uhakika;

vii) Ni vema Serikali ikayatumia Mashirika yake ya Nyumba na Mifuko ya Jamii kutekeleza miradi yake ya ujenzi kwa mikopo yenye riba nafuu;na

viii) Manufaa ya Miradi ya Maendeleo inayotekelawa na Wizara hii yataonekana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa.

3.0 UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI NA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilihusu maeneo makuu mawili. Maeneo hayo ni uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati, na Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa, Kamati ilijadili na kuchambua mambo yote mawili kwa kina kama ifuatavyo:-

3.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilishauri masuala ishirini na mbili (22) yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo. Masuala hayo yalihu mambo mbalimbali ikiwemo:-

i) Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ukamilifu na kwa wakati ili kutekeleza kikamilifu miradi iliyopangwa;

- ii) Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Polisi Kibajeti ili Jeshi hilo liwe na ufanisi na mafanikio katika kuimarisha usalama wa Raia na mali zao;
- iii) Serikali iongeze kasi ya kulipa madeni yote yaliyohakikiwa ya Jeshi la Magereza yenye Jumla ya Shilingi 63,805,279,064.31;
- iv) Rangi ya hati za kusafiria za Kidiplomasia ibadilishwe kutoka nyeusi inayotumika sasa kuwa nyekundu kama ilivyo katika nchi nyingine;
- v) Serikali itoe Shilingi Bilioni 2 zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto liliopo eneo la Mchicha- TAZARA, katika Wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam;
- vi) Serikali iendelee kutekeleza programu za adhabu mbadala kwa wafungwa ili kukabiliana na changamoto ya msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani.

Mheshimiwa Spika, katika masuala yaliyotolewa ushauri, kumi (10) yamezingatiwa kikamilifu, masuala matano (5) yanaendelea kuzingatiwa na masuala saba (7) hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, moja ya ushauri uliozingatiwa kikamilifu na Wizara ni kuhusu kubadilisha Rangi ya Hati za Kusafiria za Kidiplomasia kutoka nyeusi iliyokuwa ikitumika na kuwa nyekundu kama ilivyo katika nchi nyingine. Katika utekelezaji wa mradi wa Uhamiaji mtandao (e-migration) Serikali imefanya mabadiliko ya rangi za hati hizo ambapo hati zinazotolewa kwa sasa zina rangi nyekundu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Taarifa iliyowasilishwa ilionesa kuwa Serikali imeendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kuliwezesha Jeshi la Polisi kibajeti ili kuliongezea ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Wizara, imeendelea kuliongezea Jeshi la Polisi Bajeti ya kila mwaka ambapo Mwaka 2016/2017 Jeshi lilitengewa Shilingi **535,211,306,105.00**, Mwaka 2017/2018 Shilingi **598,566,220,000.00**. Ongezeko hilo

limesaidia Jeshi la Polisi kuongeza na kuimarisha idadi ya vitendea kazi vyake.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwengine uliotolewa ulihusu Serikali kutoa Shilingi Bilioni 2 zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji uliokwama tangu Mwaka 2013. Ushauri huu haukuzingatiwa kwani hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa Jengo hilo.

3.2 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ulizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lillokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi cha Agosti na Oktoba, 2017 na Januari 2018, na mahojano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

3.3 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya **Shilingi 293,822,132,859** ikilinganishwa na **Shilingi 289,966,629,604** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Hadi kufikia mwezi Februari 2018, Kamati ilielezwa kuwa kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni **Shilingi 160,687,217,400** sawa na asilimia 55 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi husika. Makusanyo hayo yameongezeka kwa asilimia 2.64 ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambayo yalikuwa Shilingi **156,543,675,737.91**.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)


Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Makusanyo hayo yameongezeka katika Mafungu 28 - Jeshi la Polisi, 29 - Jeshi la Magereza, 51 – Wizara, na 93- Idara ya Uhamiaji ikilinganishwa na makusanyo ya Mafungu hayo kwa Mwaka uliopita. Aidha, Kamati ilibaini Makusanyo ya Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji yamepungua ambapo Jeshi hilo lilitkusanya asilimia 20 tu ya lengo la makusanyo katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kamati ilielezwa kuwa kushindwa kufikiwa kwa lengo la makusanyo ya Jeshi la Zimamoto kunachangiwa na kutopata sehemu ya Tozo inayotozwa na Mamlaka ya Mapato katika mafuta baada ya kufutwa kwa ada ya mwaka ya Leseni za Magari (Road Licence).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya makusanyo kwa kulinganisha lengo na makusanyo hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kama ilivyowasilishwa. Njia ya jedwali na grafu ilitumika kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kati ya lengo na Makusanyo. Uchambuzi huo unaonekana katika Jedwali Na. 01 na Grafu Na. 01 na Namba 02 za Taarifa hii.

Jedwali Na.01: MCHANGANUO WA MAPATO

FUNGU	MAKADIRIO	% YA JUMLA YA LENGO	MAKUSANYO	% YA JUMLA YA MAKU- SANYO
14 - Zimamoto	35,500,003,000	12.1	4,398,526,500	2.7
28 - Polisi	73,595,525,859	25	43,567,016,327	27
29 - Magereza	2,650,003,000	1	914,454,198	0.6
51- Wizara	1,226,601,000	0.4	375,076,607	0.2
93- Jeshi la Uhamiaji	180,800,000,000	61.5	111,432,143,768	69.5
JUMLA	293,822,132,859	100	160,687,217,400	100

Chanzo: Randama ya Wizara 2018/2019



Mheshimiwa Spika, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

- i) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto, lilitenga kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 12 lakini Taarifa ya makusanyo ilionesa kuwa Fungu 14 limechangia kwa asilimia 3 tu ya kiasi kilichokusanya;
- ii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi, lilitenga kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 25 na Taarifa ya makusanyo ilionesa kuwa Fungu 28 limeshachangia kwa asilimia 27 ya kiasi kilichokusanya;
- iii) Fungu 29 - Jeshi la Magereza, lilitenga kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 1 lakini Taarifa ya makusanyo ilionesa kuwa Fungu 29 limechangia kwa asilimia 0.6 ya kiasi kilichokusanya;
- iv) Fungu 51 - Wizara, lilitenga kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.4 na Taarifa ya makusanyo ilionesa Fungu hilo limechangia kwa asilimia 0.2 ya kiasi kilichokusanya;
- v) Makusanyo ya Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 61.5 lakini Taarifa ya makusanyo ilionesa kuwa Fungu hilo limeshachangia asilimia 69.5 ya kiasi kilichokusanya.

Mheshimiwa Spika, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila Fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo

wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Mafungu 28, 29, 51 na 93 ni wa kuridhisha. Jambo hili ni la kupongezwa kwani pamoja na changamoto ya kupungua kwa makusanyo ya Jeshi la Zimamoto kama ilivyoanishwa hapo juu, bado Wizara imeweza kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya lengo lillowerkwa katika robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

3.4 Upatikanaji wa Fedha kutoka hazina

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Wizara umeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu. Pamoja na ushauri ambao umekuwa ukitolewa na Kamati mara kwa mara kuhusu Serikali kupitia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge, bado mtiririko wa fedha kwa Wizara hii umekuwa si wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia jambo hilo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2018. Kupitia uchambuzi huo, Kamati illibaini yafuatayo:-

i) Hadi kufikia mwezi Februari 2018, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 66 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.


ii) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2018, asilimia 98 ilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na asilimia 2 tu kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

iii) Hadi kufikia mwezi Februari 2018, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 76 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo iliyoidhinishwa na asilimia 28 ya bajeti ya maendeleo.

iv) Hadi kufikia mwezi Februari 2018, Mafungu mawili tu ya Jeshi la Polisi (Fungu 28) na Wizara (Fungu 51) yanakuwa yamepokea fedha za maendeleo, ambapo Fungu 28 ilipokea asilimia 25 na Fungu 51 ilipokea asilimia 50, ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa kila Fungu.

Mheshimiwa Spika, ili kupata picha halisi kuhusu uwiano wa upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida, Matumizi Mengineyo na Maendeleo, Kamati ililinganisha Kasma za matumizi hayo kwa Mafungu yote matano ya Wizara hii na kuwianisha kama inavyoonekana katika Grafu Na. 3.

Grafu Na. 3 Uwiano wa Upatikanaji wa Fedha za matumizi ya Wizara kwa mwaka 2017/2018



Chanzo: Randama ya Wizara 2018/2019

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili Matumizi ya Kawaida kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake ni wa kuridhisha. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo hauridhishi hususan kwa Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Magereza na Idara ya Uhamiaji. Kwa miaka mitatu mfululizo, Kamati imekuwa ikishauri kuhusu Mafungu haya kupewa kipaumbele katika kupelekewa fedha za maendeleo, lakini ushauri huo haujazingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo unaathiri mpango na ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mafungu hayo, ambayo baadhi yake imesimama kwa muda mrefu. Mfano wa Miradi hiyo ni Mradi wa ujenzi wa Jiko na Mabweni katika Gereza la Segerea uliosimama tangu mwaka 1991; Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa katika Gereza la Segerea uliosimama tangu mwaka 1994; Mradi wa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto liilopo Mchicha, TAZARA ulioanza Mwaka 2013; na Mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi ulioanza tangu Mwaka 2013.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa Makadirio ya Mapato na Matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo. Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

- i) Kusimamia usalama wa Raia na mali zao;
- ii) Kusimamia marekebisho ya tabia kwa wafungwa ndani na nje ya magereza na katika maeneo ya Jamii;
- iii) Kutoa huduma za zimamoto na uokoaji;
- iv) Kudhibiti uingiaji na utokaji nchini kwa Raia na wagoni;
- v) Utoaji wa vitambulisho vya Taifa; na
- vi) Kutoa huduma kwa wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umeonyesha kuwa utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake utaimarishwa endapo tu Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2018/2019


Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 297,014,614,300/-**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la asilimia 1 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka 2017/2018. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 93 - Uhamiaji. Mchanganuo wa lengo la makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Na. 2 hapa chini.

Jedwali Na.02: MAKADIRIO YA MAPATO

FUNGU	MAKADIRIO	% YA JUMLA YA LENGO
Fungu 14 - Zimamoto na uokoaji	9,250,003,000	3.1
Fungu 28 - Jeshi la Polisi	84,687,904,000	28.5
Fungu 29 - Jeshi la Magereza	1,800,000,000	0.6
Fungu 51 – Wizara	926,601,000	0.3
Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji	200,350,106,300	67.5
Jumla	297,014,614,300	100

Chanzo: Randama ya Wizara 2018/2019

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo kwenye Jedwali Na. 02: zinafafanuliwa vizuri katika Grafu Na. 03 kwa lengo la kuwianisha makadirio ya mapato katika taasisi na idara zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama invyoonekana.



Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha yafuatayo:-

i) Makadirio ya makusanyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 yameongezeka kwa asilimia 1 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia;

ii) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linategemewa kukusanya asilimia 3.1 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 12, kiasi ambacho ki - uwiano ni pungufu kwa asilimia 8.9;

iii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi linategemewa kukusanya asilimia 28.5 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 25.1 kiasi ambacho ni ongezeko ki - uwiano kwa asilimia 3.4;

iv) Fungu 29 - Jeshi la Magereza linategemewa kukusanya asilimia 0.6 ya makusanyo ikiwa ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.3 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.9;

v) Fungu 51 - Wizara linategemewa kukusanya asilimia 0.3 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.4; Kiasi hiki ni ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.1;

vi) Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji linategemewa kukusanya asilimia 67.5 ya makadirio ya makusanyo ikiwa ni ongezeko katika uwiano kwa asilimia 6 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 61.5.

Mheshimiwa Spika, kwa ufanuzi huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii. Kamati imebaini kuwa wakati makadirio ya makusanyo ya Mafungu ya Zimamoto, Magereza na Wizara yamepungua, makadirio ya makusanyo ya Polisi na Idara ya Uhamiaji yanatarajiwa kuwa mazuri hivyo kuongeza Makadirio ya Mapato ya Wizara nzima kwa asilimia moja ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka unaoishia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika makusanyo ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mhesimiwa Spika, maelezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwaa kwa mafungu yote matano ni Shilingi **945,555,651,000/=**. Kati ya fedha hizo Shilingi **521,544,491,000/=** sawa na asilimia 55 ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi **385,725,478,000/=** sawa na asilimia 41 ni Matumizi Mengineyo na Shilingi **38,285,682,000/=** sawa na asilimia 4 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo shilingi **37,500,000,000/=** sawa na asilimia 98 ni fedha za ndani na shilingi **785,682,000/=**sawa na asilimia 2 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma, Vifungu na Mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imeongezeka kwa Shilingi **15,158,834,000/=** sawa na ongezeko la asilimia 1 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018. Ongezeko hili linachangiwa na ongezeko la Bajeti ya Matumizi Mengineyo ambapo kiasi cha Shilingi **18,018,594,000/=** kimeongezeka ikilinganishwa na Mwaka unaoishia;

ii) Bajeti inayoombwaa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imepungua kwa asilimia 0.3 kwa Bajeti ya maendeleo, Mishahara imepungua kwa asilimia 1.2, na imeongezeka kwa asilimia 1.5 katika Matumizi Mengineyo ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2017/2018;

iii) Asilimia 4 ya bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo,

asilimia 55 ni kwa ajili ya mishahara na asilimia 41 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo;

iv) Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, asilimia 40 ni kwa ajili ya NIDA, Asilimia 27 kwa ajili ya Idara ya Uhamiaji, Asilimia 13 ni kwa jilili ya Jeshi la Magereza, Asilimia 12 kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto, na Asilimia 8 ni kwa ajili ya Jeshi la Polisi.

v) Kifungu 1201 kuhusu *enhancement of Prisons Industries* kimetengewa kiasi cha Shilingi 2,000,000,0000 kwa ajili ya kuanzisha viwanda viwili vya Useremala. Jambo hili ni la kupongeza kwani kwa miaka miwili mfululizo kifungu hiki hakikuwahi kutengewa fedha yoyote.

vi) Pamoja na Kamati kusisitiza kuhusu Serikali kutenga Shillingi Billioni 2 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lillipo eneo la Mchicha, TAZARA, Dar es Salaam kwa miaka miwili mfululizo 2016/2017 na 2017/2018, Serikali haijatenga Kasma yoyote kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Jengo hilo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018;

vii) Hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali katika Gereza la Segerea licha ya Kamati kusisitiza kwa muda wa miaka miwili mfululizo 2016/2017 na 2017/2018 kuhusu kutengwa kwa fedha hizo hasa kwa kuzingatia umuhimu wa Hospitali hiyo kwa Gereza la Segerea; na

viii) Hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha majengo ya Ofisi za Uhamiaji Mikoani licha ya kuwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli hiyo. Shilingi Billioni 10 zinazoombwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Ofisi ya Uhamiaji, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia na

kujadili Randama za mafungu matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa mapendekezo na ushauri wa jumla kwa Mafungu yote na ushauri mahsusini kwa kila Fungu kama ifuatavyo:-

5.1 Ushauri wa Jumla

5.1.1 Upatikanaji wa fedha za Maendeleo kwa Wizara na Mafungu yake

i) Serikali itoe fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha miradi ya muda mrefu iliyosimama hususan miradi ya Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Idara ya Uhamiaji. Hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha unaoishia, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 28 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo za Mafungu mawili tu ya Fungu 28 - Jeshi la Polisi na 51 – Wizara, na Mafungu mengine matatu kutopelekewa fedha zozote za maendeleo.

ii) Serikali isimamie utaratibu wa kutoanzisha miradi mipyä kabla ya kukamilisha miradi ambayo haijakamilika. Katika Mwaka 2018/2019 kipaumbele kitolewe katika kutekeleza miradi ya muda mrefu iliyosimama kabla ya kuanza kutekeleza miradi mingine mipyä. Hii itaiwesha Serikali kuwa na miradi michache iliyokamilika na yenye tija kwa Serikali na Taifa kwa ujumla.

iii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa pamoja na nia njema ya Serikali kuhamia Dodoma, itekeleze miradi yote illyokuwa imeanza kutekelezwa katika jiji la Dar es Salaam, hususan ukamilishaji wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliopo eneo la Mchicha-TAZARA, Dar es Salaam.

iv) Serikali ishirikiane na Mashirika yake ya Nyumba na Mifuko ya Jamii kutekeleza miradi ya ujenzi kwa mikopo yenye riba nafuu katika kujenga nyumba za Askari wa Majeshi ya Polisi, Magereza, Zimamoto na Idara ya Uhamiaji. Hii itasaidia kupunguza tatizo la makazi kwa askari ambao wengi wanaishi nje ya Kambi¹ jambo ambalo linaweza kuwa na athari kubwa katika masuala ya ulinzi na usalama;

v) Serikali iweke mkakati wa muda mrefu kuhusu namna ya kutekeleza miradi yake illyosimama ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika. Mkakati huo uanishe miradi na kipindi ambacho kinatarajiwaa kukamilisha miradi hiyo.

vi) Kamati inatambua nia njema ya Serikali katika kuondoa suala la *retention* kwa Wizara zake zote. Hata hivyo, kutokana na unyeti wa vyombo vya Ulinzi na Usalama, Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu maalum wa kuyaruhusu Majeshi ya Polisi, Magereza, Zimamoto na Idara ya Uhamiaji kubaki na angalau asilimia 40 ya makusanyo yao ili yawawezesha katika kutekeleza majukumu yao ya msingi kama vile kutengeneza magari ya doria, ununuzi wa mafuta na vilainishi, na kugharamia miradi yao ya maendeleo ikiwemo nyumba za Askari.

vii) Serikali ilipe madeni ya Majeshi ya Polisi na Magereza ambayo hadi kufikia Mwezi Machi, 2018 Jeshi la Polisi lilikuwa likidaiwa Shilingi Bilioni nane (8) kwa ajili ya għarama za umeme na Shilingi Bilioni saba (7) kwa ajili ya għarama za maji. Vilevile, Jeshi la Magereza lilikuwa likidaiwa għarama za umeme Shilingi Bilioni nne (4) na għarama za

¹Mahitaji halisi ya nyumba za Jeshi la Magereza peke yake ni 14,740, zilizopo ni 4226 na upungufu ni 10,514 sawa na asilimia 71.3

maji Shilingi Bilioni mbili (2). Madeni haya yamepelekea huduma hizo kusitishwa katika baadhi ya Magereza² jambo ambalo linaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa makambini na magerezani kwa kukosekana maji, na kuhatarisha usalama hususan katika maghala ya silaha pale ambapo huduma ya umeme inasitishwa.

5.2 Ushauri Mahsusni

5.2.1 Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

i) Serikali itoe **Shilingi 3,500,000,000/=** za maendeleo kwa ajili ya ununuzi wa magari manne ya Zimamoto na vifaa vya kuzimia moto na maokozi kabla ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 haujaisha. Hii italisaidia Jeshi hilo ambalo kwa sasa lina uhaba wa magari na dawa za kuzimia moto, kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

ii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga na kutoa **Shilingi Bilioni 2** ambazo hazikutolewa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilitopo eneo la Mchicha Dar es Salaam uliokwama tangu Mwaka 2013. Jengo hilo likikamilika linaweza kutumika kama kitega uchumi cha Serikali baada ya Makao Makuu ya Jeshi hilo kuhamia Dodoma.

iii) Serikali ione umuhimu wa kutoa mgao wa kutosha wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC) kwa Jeshi la Zimamoto ambalo limekuwa likipata mgao pungufu tofauti na mpango kazi na mtiririko wa fedha uliopitishwa. Jambo hili linaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Jeshi hilo ikiwemo ununuzi wa mafuta na utengenezaji wa magari ya kuzimia moto.

5.2.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Jeshi la Polisi katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, Kamati inashauri yafuatayo:-

²Magereza ya Wanawake Morogoro, Wami Kuu, Mkono wa Mara, Ngara, Biharamulo Kitengule, Kayanga, Iwamrumba, Butimba, Magu na Geita

i) Serikali iendelee kutekeleza Mpango wake wa ununuzi wa magari 777 kwa ajili ya kuyasambaza katika vituo mbalimbali ambavyo vina uhaba mkubwa wa magari. Aidha, kwa kuwa kati ya magari 397 yaliyonunuliwa chini ya Mpango huo tangu mwaka 2015 hadi 2018, ni magari 234 tu yameshatolewa bandarini, Serikali ione umuhimu wa kuyatoa bandarini haraka magari 163 yaliyobaki ili yasambazwe nchini kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi hilo kuendelea kutekeleza kwa ufanisi shughuli zake za kioperesheni.

ii) Kwa kuwa Jeshi la Polisi lina uhaba mkubwa wa nyumba za kuishi Askari (Barracks) Kamati inaishauri Serikali kutenga na kutoa fedha za ujenzi wa nyumba za Askari Polisi au kubuni utaratibu mwingine wowote utakaowezesha nyumba hizo kujengwa ili kuepusha Askari hao kuishi nje ya Kambi jambo ambalo linaweza kuathiri maadili ya kijeshi ya Askari hao.

iii) Kwa kuwa ongezeko la vyombo vyamini moto kama vile pipipiki na magari vinachangia ongezeko la makosa ya usalama barabarani, na kwa kuwa ni dhahiri kuwa lipo ongezeko la vyombo hivyo nchini ikilinganishwa na miaka ya nyuma, Kamati inaishauri Serikali, pamoja na kuendelea kuisimamia ipasavyo Sheria ya Usalama Barabarani iliyopo, ikamilishe haraka mchakato wa kurekebisha Sheria hiyo ili kudhibiti na kupunguza makosa ya barabarani ambayo mengi yao yanababisha ajali na hatimaye vifo au ulemavu.

5.2.3 Fungu 29- Jeshi la Magereza

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jeshi la Magereza limekuwa likipewa ukomo mdogo wa bajeti usiozingatia mahitaji halisi pamoja na kupelekewa fedha pungufu katika migao ya kila mwezi, na wakati mwingine kutopelekewa kabisa fedha za maendeleo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

i) Serikali iweke mpango Mkakati wa kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na vyanzo vyamini mapato vyamini uhakika kupitia kazi zao za Kilimo na Ufugaji. Hii ni pamoja na Serikali kuliwezesha Jeshi hilo katika kuwekeza kwenye

kilimo kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua zana za Kilimo bora na za kisasa. Mkakati huo uanze kwa kulenga magereza yaliyo katika Mikoa rafiki kwa kilimo kama vile Mbeya, Morogoro, Katavi, Manyara, Rukwa, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Njombe, Songwe, Lindi na Mtwara. Kwa kufanya hivyo, Jeshi hili litaongeza mapato yake na hatimaye kuijendesha lenyewe hususan katika eneo la chakula cha mahabusu na wafungwa.

ii) Serikali ihakikishe Jeshi la Magereza linapatiwa mkopo wa Matrektta 50 kutoka Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kabla ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 kukamilika;

iii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuziwezesha Kamati za kusukuma kesi (Case Flow Management Committee) kukutana mara kwa mara kushughulkia Kesi za muda mrefu na muda mfupi ili kupunguza tatizo la mahabusu kukaa muda mrefu bila kesi zao kusikilizwa. Ucheleweshaji wa kusikiliza kesi si tu unachangia msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani bali pia unachelewesha haki za mahabusu kusikiliziwa kesi zao kwa mujibu wa taratibu. Ushauri huu umekuwa ukitolewa mara kwa mara lakini haujazingatiwa kikamilifu.

iv) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali, Mabweni ya Wafungwa na Jiko katika Gereza la Segerea ambao ulianza tangu miaka ya 1990.

v) Serikali itoe Shilingi 2,200,000,000/- zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya kuendeleza viwanda katika Magereza, kabla ya mwaka huu wa fedha kukamilika.

vi) Serikali iliwezeshe Jeshi la Magereza kupata magari kwa ajili ya usafirishaji wa mahabusu na ya shughuli za utawala. Kwa sasa Jeshi linahitaji magari 1,247, na magari yaliyopo ni 424 ambapo kati ya hayo 143 ni chakavu na yapo kwenye utaratibu wa kufutwa na Hazina. Kupatikana kwa

usafiri wa uhakika kutawezesha mahabusu kufika mahakamani kwa mujibu wa tarehe wanazopangiwa na hivyo kutoathiri mwenendo wa kesi zao;

vii) Shirika la Magereza liweke Mkakati mahsuswa kukusanya madeni yake kutoka katika Taasisi mbalimbali za Umma ambayo hadi kufikia Mwezi Machi, 2018 yalikuwa Shilingi 5,775,842,815.64. Madeni hayo yakikusanywa yataliwezesha Shirika hilo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

5.2.4 Fungu 51- Wizara

Serikali itoe shilingi bilioni 10 ambazo bado hazijatolewa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa utoaji wa vitambulisho vya Taifa kwa mujibu wa Kalenda iliyowekwa kwa kuzingatia umuhimu wa utambuzi na usajili wa wananchi katika masuala ya ulinzi na usalama wa nchi yetu.

5.2.5 Fungu 93- Idara ya Uhamiaji

i) Serikali itoe fedha za maendeleo Shilingi 5,791,630,000/= zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa, Wilaya na Vituo hususan kwa majengo ambayo ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu, kabla ya Mwaka huu wa fedha kuisha.

ii) Serikali iongeze ukomo wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo na kutoa fedha hizo kwa mtiririko unaotakiwa ili, pamoja na mambo mengine, kuwezesha huduma za uhamiaji za doria na misako ambazo hazifanyiki kwa ufanisi kutokana na ubovu wa magari ya kufanya kazi hizo.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- 1.Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, **Mwenyekiti**
- 2.Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/Mwenyekiti**
- 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
- 4.Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
- 5.Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
- 6.Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
- 7.Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
- 8.Mhe. Cosato David Chumi, Mb
- 9.Mhe. Bonnah Mosses Kaluwa, Mb
- 10.Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb
- 11.Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
- 12.Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
- 13.Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
- 14.Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
- 15.Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
- 16.Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
- 17.Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
- 18.Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
- 19.Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
- 20.Mhe. Sebastian Kapufi, Mb
- 21.Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
- 22.Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
- 23.Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
- 24.Mhe. Augostino Manyanda Masele, Mb
- 25.Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Eng. Hamad Masauni (Mb), Katibu Mkuu Meja Jenerali Mstaafu Projest Rwegasira, Naibu Katibu Mkuu Balozi Yahya Simba pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge

Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, **Mb**
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,
ULINZI NA USALAMA
03 Mei, 2018

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza na uchangiaji na tutaanza na Mheshimiwa Peter Lijualikali.

MHE. PETER A.P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kuna mambo ambayo yanafanyika kwenye nchi yetu mimi natafsiri ni kama vile yanaleta fedheha kwa Jeshi la Polisi. Mambo haya yanafanya jeshi letu lionekane kama vile halina weledi, sijui ni kwa nini. Kwa mfano, utaona kuna bwana mmoja alimtishia Nape bastola, Waziri akasema huyu mtu tutamshughulikia, huyu mtu atafutwe, lile suala jinsi lilivyoenda mpaka leo kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yule anaonekana mtaani, yupo na hata juzi amefanya kazi mbele ya kamera. Sasa sielewi matamko haya huwa yanatoka kwa nia gani, ina maana Polisi hawaoni kwamba haya mambo yanachafua Jeshi letu la Polisi? (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwininge Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibondo amekamatwa akiwa ofisini kwake mpaka leo amepotea, haifahamiki yuko wapi. Taarifa zinasema aliyemkamata ni *DSO*, Mzee Mkuchika hapa anasema siyo wao, anasema hii ni kazi ya Polisi, Polisi wako kimya hawasemi chochote. Hii inafanya Jeshi letu lione kane kama vile halina taaluma hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RPC* wa Iringa anasema Nondo alikwenda mwenyewe Polisi kwenda kusema kwamba ye ye hakutekwa wakati Kanda Maalum ya Dar es Salaam inasema Nondo amekamatwa. Haya mambo yanaonesha hili Jeshi letu linafanya kazi siyo kwa taaluma. Niwaombe sana Polisi wetu, kama wanapewa mashinikizo kwenye kazi yao, wajue kabisa kwamba wao ndiyo wanakuwa *answerable* mambo yanapoharibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwininge ni Roma Mkatoliki. Roma ametekwa, akasema ameteswa na akasema anashindwa kuongea kwa sababu anaogopa maisha yake yako hatarini, Polisi wanasiliza tu hawasemi chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni huyu Ndugu yangu Musiba. Musiba anaongea maneno hapa mabaya kabisa, Polisi wanasema wanachukua hatua. Mheshimiwa Lissu alisema maisha yake yapo hatarini, yapo kwenye shida, Polisi wanasema kama Mheshimiwa Lissu hakwenda Polisi kushtaki wenyewe hawana mpango lakini Musiba anaongea mambo ya hovyo kabisa, Polisi wanasema wao wanafanya kazi, *this is so unprofessional* na hii inasababisha Jeshi letu kuonekana halina weledi. Watu wamekaa juu hapo wamesoma, wana uwezo mkubwa, kwa nini wanafanya vitu ambavyo vinaonesha kwamba hawana uwezo, kwa nini wasioneshe uwezo wao ambao sisi tunaamini wanao? Kwa nini wanafanya hivi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo *yana-brand* Taifa letu kuwa ni Taifa ambalo lina taasisi ambazo hazijielewi. Taifa letu lilikuwa linaheshimika duniani

kwamba ni sehemu ya amani, ni sehemu nzuri ya kuishi. Leo Taifa letu linakuwa *branded* ni sehemu moja ya hovyo kwa sababu watu ambao mmepewa kazi za kufanya mnashindwa *ku-act professionally* mnafuata maagizo ambayo ni *politically*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili likienda sehemu mbaya, juzi hapa Mkuu wa Polisi wa Arusha alipata ajali watu wana-comment bora afe tu, *no, no, no!* Wazee huko juu msifurahie mambo haya. Mheshimiwa Waziri asifurahie mambo haya, ni lazima wajilize kuna shida wapi? Kwa nini mtu afurahie kifo chako? Wanakosea wapi? Kama Taifa tunakosea wapi? Haya mambo lazima wajilize! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema maneno yafuatayo. Diwani wangu Luena alifariki, taarifa zinasema treni ama kipisi kilipiga honi mara tatu kwenye eneo la tukio. Hii inaleta picha kwangu inawezekana ile treni ilikuwa imewachukua watu ambao walimuua Diwani wangu kwa sababu ni kwa mara ya kwanza tangu kipisi kimeanza kazi ndio imepiga honi mara tatu nusu saa baada ya tukio, haiwezekani! Naomba hili walifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nimwombe Mheshimiwa Waziri amwambie /GP wetu aje Ifakara aongee na Polisi wangu Ifakara, asikie na wao wana shida gani, asiende tu sehemu zingine anaongea nao, kule kuna shida nyingi sana, kituo kibovu. Aje, akae na sisi hata kama ni kuchanga, tuchange, kama ni kusaidia tusaidie, kama ameshindwa kujenga, sisi hela zipo, wananchi watatoa. Kwa hiyo niwaombe hilo, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lijualikali. Tunaendelea na Mheshimiwa Kahigi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tafadhalini, sasa mnaanza vurugu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa mnakwenda nje ya mipaka.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kahigi, naomba uendelee.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniamsha siku ya leo nikiwa mzima wa afya na kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea. Namshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu wake kwa hotuba nzuri ambayo ametusomea hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitachangia mambo machache katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tusikilizane tafadhali, naomba mpunguze sauti.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii nimeona kuna changamoto ambazo napaswa kuziongelea kama mbili/tatu hivi. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, kuna tatizo la upotevu wa watu wazima na watoto wadogo katika nchi yetu. Nchi yetu ilikuwa kweli ni ya amani na utulivu lakini hili janga ambalo limejitokeza kwa sasa hivi linatutia simanzi kubwa sana, linatuaibisha, sijui ni watu gani ambaao wanataka kutuchafulia amani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Jeshi lake la Polisi suala hili walifanyie kazi

kwa hali ya juu sana maana sasa hivi watu hatuna amani, tuna watoto wakienda shulenii tunakuwa na wasiwasi watatekwa, watauawa kwa sababu ya watu waovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana Serikali yangu maana ndiyo mnaobeba huu msalaba. Kuna watu wengine wanajipenyeza wenye nia mbaya ya kuchafua jina la nchi yetu ili mwonekane ni wabaya kumbe wakati mwingine Serikali haina ubaya wowote. Naomba Waziri alifanyie kazi kweli kweli suala hili. Sina ubaya wowote na Serikali yangu, sina ubaya wowote na maaskari lakini inasikitisha, walifanyie kazi. Hiyo ni namba moja kwa sababu dakika ni kidogo nitaongea kidogo kidogo kusudi niweze kueleweka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la Polisi. Maaskari sina ugomvi nao, nawapenda sana na wao wanipende sana lakini maaskari jamani wajirekebishe. Kuna matrafiki, huko njiani wanasumbua sana hasa hawa wa *PT*. Kuna makosa mengine ni madogo madogo mnaweza mkaongea, lakini wanakupiga faini, wanatusumbua yaani sasa vyombo vya moto inaonekana kama hatuna amani navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na lenyewe hilo waliangalie, wawaambie hao maaskari waache kusumbua watu, hasa wa bodaboda wanawasumbua sana na wakati mwingine na kuwapiga wanawapiga. Kwa kweli haki za binadamu zinavunjwa na maaskari wakorofi ambao wanafanya vitu ambavyo hawakuagizwa kuvifanya waache. Waheshimiwa Wabunge, wanaviona vitu vingine sisemi kwamba ni mimi hapa mama Kahigi, hapana, wanafanya mambo ya namna hiyo, yanatuudhi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja upande wa nyumba za maaskari. Nyumba za maaskari zinasikitisha sana kwani zimepitwa na wakati. Nyumba za mabati utadhani maaskari wetu ni bata au kuku kulala kwenye nyumba mbovu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumeambiwa wanajengewa nyumba 400 ni kidogo sana, naomba wakaze buti, wawajengee nyumba, wakae katika nyumba nzuri na wawe na maisha mazuri na familia zao wajisikie kama vile ambavyo sisi tunavyojisikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka katika hilo, nafikiri wamenisikia, watawashughulikia, nakuja kwenye maslahi yao. Maaskari wengine wanaongezwa vyeo lakini mshahara hawaongezwi. Naomba na lenyewe hilo waliangalie, wawaongeze mshahara ili wafanye kazi zao wakiwa na miyo safi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka hapo nakuja kwenye suala la *passport*. Kwa kweli *passport* ni kitu kizuri sana lakini kiasi ambacho wameweka kwa wananchi wetu wa vijijini nina wasiwasi hawataweza kulipia hizo *passport*. Kulipia Sh.150,000 ni labda kwa Wabunge na watu wenye vyeo vya hali ya juu ndiyo watakaoweza. Naomba wapunguze gharama hiyo ili watu wetu waweze kuwa na *passport*. Mtu mwingine anapata safari ya kwenda nchi za nje lakini *passport* inamkwamisha anashindwa kwenda kwa sababu hana hela ya kuweza kulipia hiyo *passport*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nako natoka, la mwisho ni kuhusu kesi kukaa muda mrefu. Naomba upelelezi uwе unafanyika haraka sana, wasifanye kukawa na mrundikano wa kesi, wafanye haraka haraka, kesi ziende mahakamani watu waweze kuhukumiwa, mambo yaende sawasawa sio watu kuwazungushazungusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kahigi. Tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia Shomar baadaye Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwanza sina budi kuwasifu

Wizara, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wao wote kwa kazi nzuri na hasa Kamishna wangu Bwana Mohamed Hassan ambaye anafanya kazi nzuri na uteuzi wake ameupata hivi karibuni na tunamwona jinsi anavyojitahidi kwa utendaji wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi tumelipa majukumu makubwa, majukumu ya kutulinda sisi raia na mali zetu lakini kwa kweli utendaji wao wa kazi na vitendea kazi walivyokuwa navyo siyo rafiki. Kwanza anapokuwa anaenda kazini, baadhi ya sehemu anazofanya kazi yake siyo nzuri, anaporudi kazini kachoka, sehemu anapoishi au anapokaa sio rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sisi Kamati yetu tulikwenda kutembelea Mtwara, Lindi pamoja na Kilwa, jamani nyumba tumezikuta huwezi kuamini kwamba kweli nyumba hizi wanaweza kukaa binadamu na wakafanya kazi na wakaweza kutulinda na kuwa wako kwenye nafasi ya kufanya kazi kwa weledi ambao tunauona hivi sasa majeshi kwa kazi zake nzuri wanazotufanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli utasikitika na utawaona hawa watu wana shida katika utendaji kazi wao lakini wanajitahidi kuweza kutufanya kazi na kuweza kuridhisha. Wanapokuwa katika doria wana matatizo ya mafuta, bajeti yake inakuwa ndogo. Wao wenye kimaafao pia malimbikizo yao wanakuwa hawayapati kwa wakati. Sasa haya yote yanakuwa ni mtihani kwao ina maana lazima Mheshimiwa Waziri awatazame hawa watendaji wetu kwa jicho la ziada ili waendelee kufanya kazi zao nzuri wanazotufanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea majengo ya Uhamiaji yaliyokuwepo Lindi na Mtwara. Majengo hayo kwa kweli yanositisha na kama ulifika kule, maana kipindi kile ulikuwa kwenye majukumu mengine hatukuwa na wewe lakini sisi Kamati tumeona na hatukupendezwa nayo na kwa sababu tumekuta kikwazo ni pesa za maendeleo haziendi kwa wakati na badala ya kupata kitu kizuri mtapata hasara.

Maana yake majumba yanavyopata mvua na miti ishaiza ina maana itafika wakati patabakia kiwanja badala ya kumalizia zile nyumba. Mheshimiwa Waziri aliangalia suala hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ajira za Jeshi la Polisi ambapo tayari hivi sasa zimeshatangazwa na tayari vijana wetu wameshaanza kuomba kwa mujibu wa utaratibu. Kwa upande wa Zanzibar hizi nafasi hatujui zitagawiwa vipi lakini najua utaratibu wanao na wakija hapa watatueleza jinsi wenyewe taratibu zao walivyozipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasisitiza vijana walioko JKU Zanzibar tayari ni wakakamavu, wameshakaa chuoni kule, washasomeshwa na baadhi yao elimu zao zinafika *degree*, vijana hawa wasiwasahau waweze kuwachukua. Wengine wamewekwa kama wakufunzi ili wawepo pale JKU waweze kujitolea pia waweze kuwasaidia waweze kupata kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumza ni malipo ya askari wastaafu. Kwa kweli askari wastaafu wanapata shida Zanzibar na shida wanazozipata kwamba kule Zanzibar hakuna ofisi inayoshughulikia mambo ya pensheni, inabidi waende Tanzania Bara. Mtu unapokuwa tayari umeshaastafu hata ile haiba yako kwa wenzio inapungua, sasa wanahangaika kupata pesa kwa wakati hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba ofisi kama hiyo iwepo na Zanzibar kwa wale wanaomaliza Zanzibar walau waweze kuhangaikiwa palepale na mambo yao yaweze kuwa pale pale. Kwa kipindi hiki wanakuwa hata pesa za kupanda boti kwenda na kurudi hawana tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu Makao Makuu ya Polisi Ziwani, wazee wetu walikuwa wanaita bomani. Mimi nimefunua macho boma lile nimeliona liko vilevile na hadi hivi sasa ni bovu, ukiangalia senyenje

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

iliyozunguka boma ni mbovu, ukiangalia majumba yenewe ni mabovu ambayo yapo kabla ya 1964 toka ukoloni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar pana historia na maboma yale na kuna nyimbo inaimbwaa tarehe 12 bomanii tuliiingia. Sasa kwa nini hatulipi hadhi yake ya boma hilo tuliloingia ili likaweza kuonekana? Kwa sababu kila anayekuja historia pale anaiona. Ukiingia ndani majengo mabovu, njia za kupitia usafiri wa ndani mbovu, unachokiangalia hata kama mtu anataka kwenda *toilet* pia atafute vipi apenye aingie ili akajisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuelezee katika bajeti yake ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar na boma lile lillilokuwepo Ziwanii watalisaidia vipi ili historia iweze kuijendeleza? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nashauri kwamba hawa wastaafu wetu ambaao niliowazungumzia jamani wanateseka, wazidi kuwaangalia. Kama hawatowaangalia baadaye watakuja kujuta waje kuwasifu au wasikie wamefanya vitu vingine havistahili kumbe njaa mtu imemkibili mtu na njaa kwa kweli ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia Shomar. Tunaendelea na Mheshimiwa Almas Maige na baadaye Mheshimiwa Mattar ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa maana ya Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Masauni, pia Katibu Mkuu wao na viongozi wote wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Vilevile

niwapongeze Wakuu wa Idara wote, Jeshi la Polisi, Uhamiaji, Magereza na Zimamoto. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na matatizo madogo madogo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto ambazo hatuwezi kunya maza tuiseme. Changamoto hizo nimezipanga kwa idara, nianze na Jeshi la Polisi, huu ndiyo mhimili mkuu unaotegemewa na raia hapa kwa sababu wao ndiyo wamepewa kazi ya ndani ya ulinzi wa raia na mali zao, lakini Jeshi hili la Polisi halitoshi, kwani askari ni wachache kuliko raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi nyine kampuni za sekta binafsi za ulinzi zinafanya kazi pamoja na Jeshi la Polisi kuendeleza ulinzi wa raia na mali zao. Hapa kwetu tuna makampuni mengi sana ya ulinzi, lakini kwa bahati mbaya sana makampuni haya hayana sharia. Nimekuwa nasimama mara kwa mara nikidai sheria, lakini kumekuwa na dalili ya kupindisha hiyo sheria kama ilivyo katika nchi nyine, nchi nyine kote kuna sekta za ulinzi binafsi na kuna sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sielewi kwa nini tatizo limetokea hapa la kutoleta sheria hiyo hapa Bungeni. Naambiwa sheria hiyo inaweza ikapinda ikawa ni uendelezaji wa maboresho ya Sheria ya Polisi. Mimi nasema kote duniani yalikotoka makampuni haya ya ulinzi au *idea* ya sekta ya ulinzi binafsi kuna sheria yake ya kuyaongoza makampuni haya na Tanzania hatuwezi tukawa na kisiwa. Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi ni lazima ije ili makampuni haya yanayoajiri mara tano, mara sita wingi wa Jeshi la Polisi yatusaidie kulinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikiongelea sasa hali halisi ya utendaji wa Jeshi la Polisi. Kumekuwepo na suala linalosemekana watu wasiojulikana na wenzetu wa upande wa Upinzani kule wamekuwa wanadai kwamba huenda watu wasiojulikana wanafanya matukio upande wa Upinzani tu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina orodha ya maafisa na viongozi wa CCM waliofanyiwa matukio na watu wasiojulikana. Badala ya kulaumu kwamba watu wasiojulikana wanakuja upande wenu, nikiandika orodha ya watu waliofanyiwa matukio upande wa Upinzani hawafiki hata robo ya watu waliofanyiwa matukio upande wa CCM. Nikichukua tu watu wa CCM...

T A A R I F A

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukua tu watu wa CCM waliofanyiwa matukio upande wa Rufiji kule lakini hata jana Katibu Mwenezi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige subiri taarifa, Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji mzee wangu Mheshimiwa Maige kwamba idadi ya watu waliohujumiwa na Jeshi la Polisi haiwezi kulinganishwa na kuhalalisha uovu unaofanyika katika nchi hii. Hata kama ni mtu mmoja ameumizwa au kumi lakini hoja ni kwamba kuna utekaji wa watu, mauaji ya kiholela, uonevu na uvunjifu wa sheria, hii ndiyo hoja.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza taarifa hiyo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige subiri kidogo, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nirekebishe kauli ya babu yangu Mwita pale, Jeshi la Polisi halijateka watu.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maige anaongelea mambo ya watu wasiojulikana.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndiyo tatizo la watu...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tusikilizane.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndiyo tatizo la watu kuwa na mawazo kichwani badala ya kusikiliza anachosema mtu. Mimi siongelei Jeshi la Polisi kukamata watu au kuua watu, naongelea watu wasiojulikana kufanya matukio. Mimi siongelei Jeshi la Polisi kufanya lolote, naongelea matukio yanayofanywa na watu wasiojulikana kwamba matukio hayo ni machache kwa upande wa Upinzani kuliko yaliyofanywa upande wa CCM.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, iko haja sasa ya Serikali kuiongezea nguvu na uwezo Idara ya Upenelezi.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige subiri kidogo, Mheshimiwa Mbatia.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uhalifu haliangaliwi au halililinganishwi kwa vyama vyaa siasa. Sisi sote ni Watanzania na hili ni Jeshi letu la Polisi linalinda usalama wa raia wa Tanzania na hatuangalii vyama vyaa siasa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo pia potofu...

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijaongelea uraia wa mtu, wala chama naongelea watu wasiojulikana kufanya matukio. Watu wanaofanya matukio na hawakamatwi ndiyo ninachoongelea. Nasema Serikali ifanye juhudini kubwa ya kuiongezea nguvu Idara ya Upelelezi ili watu hawa wanaofanya matukio kwa pande zote mbili wawze kukamatwa. (*Makof*)

T A A R I F A

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige, taarifa hiyo.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuzungumza, suala la kusema kwamba matukio yaliyofanyika ya utekaji nyara upande wa Chama cha Upinzani na ya kwao hayafanani, kwamba CCM ni wengi CHADEMA ni wachache inakwenda kudhihirisha kwamba Chama cha Mapinduzi na Serikali yake imebariki tukio hili ama mfumo huu wa kwenda kufanya matukio hayo ili waje waseme kwamba CHADEMA ni wachache CCM ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiki kitu si sawa kama wameamua kulidhihirisha hivyo tunashukuru

Mheshimiwa Maige ameweza kutupa taarifa kwamba limebarikiwa na Serikali. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naomba tumsikilize ili tumwelewe.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mary subiri kidogo apokee taarifa moja kwanza.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa kwa nini upande ule wanakurupuka.

(Hapa baadhi ya Wabunge wallongea bila mpangilio)

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaongelea lolote, mimi ninachotaka kusema sasa...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tumsikilize ili tumwelewe. Kama kuna la ziada tutamwambia lakini tumwelewe bado hamumuelewi.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naongelea ombi langu kwa Serikali kuiboresha Idara ya Upenelezi ya Polisi ili iweze kuwakamata watu wasiojulikana wanaofanya matukio. Hiyo ndio *message* yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie upande wa magereza. Sisi tumetembelea magereza na mambo makubwa yanayotokea kule yanahitaji msaada wa Serikali. Changamoto kubwa tulioikuta kule kwanza ni makazi yao na vilevile wafungwa wengi wamerundikana katika magereza. Kwa hiyo, programu hii ya adhabu mbadala ni muhimu sana ikachukuliwa umuhimu wake ili kupunguza mrundikano magereza. Vilevile ni bora magereza wawe na kiwanda chao cha kutengeneza sare ili waweze kuwa na sare za wafungwa na sare zao wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekuta upungufu wa chakula na yako madeni makubwa sana ya wazabuni wa chakula kwenye magereza yetu ambayo hayajalipwa na mbadala wake ingefaa kama magereza ingerudia mfumo wa zamani wakati sisi wadogo magereza walikuwa wakilima mashamba makubwa wakijilisha wao na kuuza chakula kwenye idara nyingine za Serikali. Kwa hiyo, napendekeza magereza wapewe uwezo wa matrekti ili waweze kufungua mashamba makubwa waweze kujilisha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la zima moto. Zima Moto wana kazi kubwa kabisa ya kuokoa maisha ya raia na malii zao lakini hali ya jeshi hilo kwa sasa ni mbaya. Kwanza hawana vifaa vya kufanya kazi lakini pia madawa ya kuzima moto hawana. Kwa hiyo, ningependa Serikali inapopanga bajeti yake liangalie idara hii kwa macho mawili ili waweze kupewa kile ambacho kimepangwa katika bajeti ya kila mwaka. Kwa kufanya hivyo itasaidia kupunguza ukali wa upungufu wa Idara ya Zima Moto ili waweze kutusaidia yanapotokea majanga ya moto hasa mijini na maeneo ambayo ni *sensitive* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la Idara ya Uhamiaji. Hivi karibuni kumekuwa na matukio mengi ya kukamatwa wahamiaji haramu hapa nchini lakini wahamiaji hawa wanapita katika nchi jirani. Mimi sielewi huko nchi jirani wanawaruhusu waje kwetu hapa kwa sababu sisi tunapata gharama kubwa sana kuwatunza hawa wahamiaji kwa maelfu halafu kuwasafirisha walikotoka na tukiwafunga magereza yetu yanafurika, lakini wanapita katika nchi jirani kule bila kusimamishwa. Inawezekana ni mkakati waende Tanzania kama ngao tu, ni gharama kubwa sana, kwa nini nchi jirani hawawazuii hawa wahamiaji mpaka waje wakamatwe hapa kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza sasa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wa Mambo ya Ndani wa nchi jirani wakutane wajadiliane suala hili la wahamiaji. Haiwezekani kila mwaka tukamate maelfu ya watu

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wanaopita katika nchi jirani wanakuja kukamatwa hapa kwetu, ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia Idara ya Uhamiaji wanatumia hela nyngi sana kuwatanza lakini mahakama pia inachukua muda mrefu kujadili kesi ambazo sio za lazima. Kama kuna uwezekano wa kuongea na nchi jirani kwamba wazuwe kule wanapoingia mpakani badala ya kuvuka nchi tatu waje wakamatwe hapa, ikiwa na sisi tutawaruhusu wapite itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa kuwa wanasema hawaji Tanzania wanaenda nchi fulani, wanapita *transit* hapa, kama hatusaidiani ujirani huu mwema basi na sisi tufunge mikono piteni, si wanapita tu bwana ila watakaobaki hapa tuwakamate. Kama wanapita waachenii wapite waende zao huko wanakotaka kwenda maana hakuna ushirikiano kati ya nchi na nchi. Hili ni tatizo kubwa sana na ni lazima Idara ya Uhamiaji isaidiwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Idara ya Uhamiaji pia kwa hizi *passport* ambazo tulikuwa tunaziona kama ndoto ziko mikononi mwa wananchi wa Tanzania. Hili ni jambo zuri sana, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii moja kwa moja, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maige. Tunaendelea na Mheshimiwa Mattar Ali Salum na Mheshimiwa Justin Monko ajiandae.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia leo. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa mzima wa afya na kuweza kusimama katika hili Bunge kuweza kuchangia siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutoa *passport* mpya. Vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru Rais kwa kuhakikisha Watanzania waliotimia umri wanapata vitambulisho vya Utanzania ili viweze kuwasaidia katika mahitaji yao ya kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Kamishna wa Jeshi la Polisi wa Zanzibar kwa kuteuliwa kuwa Kamishna wa Jeshi la Polisi wa Zanzibar. Nimpongeze sana na nimtakie kazi njema kwa upande wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze Wizara inafanya kazi nzuri ya kuhakikisha wanasmamia utoaji wa *passport* mpya. Vilevile niwapongeze sana Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuhakikisha Watanzania waliotimia miaka ya kupata vitambulisho vya Utanzania wanapata vitambulisho vya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar tuna vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya kazi kubwa sana kwa kutumia kodi za Wazanzibari kuhakikisha wanapata vitambulisho hivi ili viweze kuwasaidia katika majukumu yao ya kukuza uchumi. Kazi ya kwanza ambayo ni muhimu sana Serikali ya Zanzibar ilifanya ni kutoa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ili kuhakikisha Wazanzibari wanapata *passport* ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kushangaza sana vitambulisho vya Mzanzibari kwa sasa huwezi kupatia *passport* ya Mtanzania. Ili upate *passport* ya Mtanzania unatakiwa lazima uwe na kitambulisho cha Mtanzania. Kinyume na miezi mitatu iliyopita kitambulisho hiki cha Mzanzibari unaweza kupata *passport* ya Mtanzania. Hii leo huwezi kupata *passport* ya Mtanzania kwa kutumia kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *system* ya Uhamiaji, kitambulisho cha Mtanzania na kitambulisho cha Mzanzibari kimoja hapo ukikitumia unawenza kupata *passport*

ya Mtanzania. Jambo la kushangaza sana Mheshimiwa Waziri na nimwombe sana hivi sasa anapokwenda na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kinaambiwa hakifahamiki na huwezi *ku-issue passport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni la kushangaza sana, hiki kitambulisho cha Mzanzibari ikiwa Serikali ya Zanzibar imetumia gharama na kodi za Wazanzibari kuhakikisha wanapata kitambulisho hiki ili kujikwamua na maisha yao, leo unawaambia haiwezekani kupata *passport* mpaka mtu awe na kitambulisho cha Mtanzania. Niombe sana Wizara kama kitambulisho hiki cha Mzanzibari Mkaazi kina tatizo, basi waweze kutuambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara kama Serikali kama kitambulisho hiki kama kina tatizo wana uwezo wa kulitatua tatizo basi litatuliwe ili waliokuwa nacho kitambulisho hiki waweze kupata *passport* kwa kutumia kitambulisho hiki cha Mzanzibari. Wazanzibari wengi wamehamasika na wamechukua vitambulisho hivi vyा Mzanzibari kwa nia nzuri ili waweze kupata *passport* ya Mtanzania na waweze kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana kwa nini kitambulisho hiki kwa sasa huwezi kupata *passport* na ni kipindi kifupi ndiyo limeanza hili suala kwamba kwa kitambulisho hiki huwezi kupata *passport*. Vilevile ukitaka kitambulisho cha Mtanzania kwa upande wa Zanzibar zaidi ya siku 30 ndiyo unapata kitambulisho hiki cha Mtanzania. Kama hakuna uwezekano wa kuhakikisha kitambulisho chetu cha Mzanzibari unaweza kupata *passport* wapunguze muda ili Wazanzibari waweze kupata kitambulisho hiki cha Mtanzania kwa haraka zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie jambo la pili kuhusu vituo vyा polisi. Wakuu wetu wa vituo vyा polisi wanapata shida sana. Mkuu wa Kituo cha Polisi anapewa mahabusu zaidi ya 40 ambao wanahitaji kula, lazima mkuu wa kituo kufanya maarifa wale mahabusu au watuhumiwa waweze kula kwa kutumia pesa zake mfukoni. Mkuu huyu wa kituo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

cha polisi atakuwa na uwezo gani wa kuwalisha mahabusu kila siku? Pesa za kula ndani ya vituo vyetu vya polisi haziendi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine unakwenda kituoni kushtaki, unaambiwa gari lipo lakini mafuta hakuna. Inabidi Mkuu wa Kituo atoe pesa za mafuta au Mkuu wa Kituo yule aweze kupata gari na aweze kwenda au Mkuu wa Kituo hana wewe uliyekwenda kushtaki kesi unatakiwa utee pesa zako mfukoni kutia gari mafuta ili kesi yako iweze kushughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la umeme. Hata na mimi mwenyewe nimeshawahi kuchangia umeme ndani ya kituo cha polisi, hawana pesa za umeme....

(Hapa baadhi ya Wabunge walliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, utanipa dakika tatu?

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Justin Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu hii ya Mambo ya Ndani. Nianze kwa kuipongeza Serikali kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Ndani kutookana na hali ya usalama wa nchi na wananchi pamoja na mali zao. Jeshi la Polisi pamoja na majeshi mengine ambayo yako chini ya Wizara hii yamefanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo machache ambayo napenda kushauri. Wenzangu waliotangulia

wameshaanza kusema, nianzie na Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi pamoja na kwamba wanafanya kazi nzuri, lakini kwa kweli askari wetu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya watumishi wa Jeshi la Polisi ni magumu sana kwa sababu hawana vitendea kazi, usafiri, majengo yao wanayofanya kazi katika ofisi ni mabovu sana lakini na makazi yao ni duni kabisa na kuwafanya wale watumishi kuwa kama wamekata tamaa. Wakati mwingsi inakuwa kama vile wamesahaulika labda kutokana na wingi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda sana nishauri katika bajeti hii ambayo tunaendelea wajaribu kuliangalia. Sasa hivi kama Mheshimiwa Waziri alivyosema tayari kuna ujenzi umeshaanza kwa mfano kule Arusha tukishirikisha wadau. Yako maeneo ambapo wadau wa maendeleo hawa hawana michango mikubwa sana hasa katika sekta hizi za ulinzi na usalama kutokana na mapato yao au jiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukitegemea sana wadau wa maendeleo na Serikali tukakaa pembeni tu kwa kweli yako maeneo ambayo wanajeshi wataendelea wetu kupata matatizo makubwa ya vitendea kazi lakini kuendelea kuishi katika maisha duni na hivyo kutoa huduma zilizo duni kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule jimboni kwangu kwa kweli, nilishamwomba hata Mheshimiwa Waziri aweze kufika, vituo vyetu vya polisi vinatia kinyaa. Yako maeneo kwa mfano ukienda katika Kata moja ya Ngimu, kituo cha polisi wamekwenda kukodisha eneo la Serikali ya Kijiji, wamekwenda kukodisha kwenye majengo ya zamani ya Chama cha Mapinduzi na wanashindwa hata kuyakarabati majengo hayo kwa sababu kwa upande mmoja wanaona majengo sio yao na kwa upande mwingsine Jeshi letu la Polisi halina fedha za kutosha kuweza kufanya ukarabati wa majengo haya. Matokeo yake ni nini sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wale watumishi wanakaa kwenye nyumba za kupanga. Wakati mwingine ni mbali kabisa na maeneo wanakotakiwa kufanya kazi. Jambo hili linaludisha nyuma sana utendaji wa Jeshi letu la Polisi kwa sababu pale ambapo wananchi wanawahitaji kwenye vituo hawawezi kupatikana kwa urahisi. Ukizingatia bado tunalo tatizo la miundombinu ya mawasiliano hata kuwapata askari imekuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Wizara ifanye mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba tunaboresha sana mazingira ya kufanya kazi kwa askari wetu ili hizi huduma ambazo tunaziomba za kutoka Jeshi la Polisi za ulinzi na usalama ziweze kupatikana kwa urahisi, lakini tuweze kuwatia moyo askari wetu kufanya kazi ya kuilinda vizuri nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa. Wamezungumza waliotangulia, hatuna fedha za kupeleka hata mahabusu wetu kwenye mahakama zetu, kwenye Mahakama za Kata wakati mwingine hata kwenye Mahakama za Wilaya na hivyo tunajikuta kwamba haki za wananchi zinacheleweshwa ama hata wakati mwingine zinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vingine havina hata sehemu ya kutunzia mahabusu, tunao ushahidi kabisa kuna maeneo wananchi wamelazimika kwenda kuvamia sehemu hizo na kuwatorosha wahalifu wale amba walikuwa wanakusudiwa kupelekwa katika vyombo vya kutolea haki. Sasa ni vizuri sana Serikali ikaangalia suala hili na kuona kwamba tunahitaji kwa kweli kuwa na mazingira mazuri ya kufanya kazi katika vituo vyetu vya polisi kuanzia kwenye kata hata ngazi ya wilaya ili kusudi wananchi waweze kupata haki zao kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara kuna zoezi la vitambulisho linaendelea na hata kule jimboni kwangu naona sasa wanakwenda na wananchi wanaendelea kupata vitambulisho hivyo. Niombe kasi hii

iongezeke na wananchi wapewe taarifa ili katika zile siku ambazo zimepangwa, tuweze kuhakikisha kwamba tunatoa huduma hii kwa haraka na kuhakikisha kwamba wananchi walio wengi wanaostahili kupata vitambulisho wanaweza wakapata vitambulisho kabla wale watendaji wetu hawajahama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo pia suala la namna ya kuwahudumia mahabusu wetu hasa kwenye masuala ya chakula. Tunawategemea sana wananchi wale ambao wapendwa wao wanakuwa wamechukuliwa na bado wako chini ya polisi hawajafikishwa mahakamani kutoa *support* ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine kwenye jimbo kama la kwangu vituo vya polisi hivi viko vichache mno na unakuta wananchi wale ambao wanatakiwa kuwahudumia ndugu zao wako mbali. Wananchi wanapata tatizo kubwa la kuweza kuwahudumia wale ndugu na wakati mwingine wasipopata nafasi ya kufika pale, askari wetu wanapata shida kubwa sana ya kuhakikisha kwamba mahabusu hawa wanaweza wakapata angalau huduma zile za msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Jeshi letu la Polisi na Wizara tuangalie namna ya kuweza kusaidia katika maeneo haya. Kwa sababu hawa wananchi hawajahukumiwa kwamba wametenda makosa, wana haki ya kuendelea kupata chakula, wana haki ya kusikilizwa, zipo haki za kimsingi ambazo wanastahili kuzipata ili kusudi tusianze kuwahukumu kabla hata hawajafika mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni la muhimu sana kwa sababu kesho na keshokutwa na sisi pia, tutakuwa huko, vituo vyetu hali zake ndiyo hizi hakuna hata mahali pazuri pa kuwaweka wananchi. Kwa hiyo, niombe sana Wizara waangalie namna ya kuweza kuboresha miundombinu hii lakini huduma za chakula, mafuta kwa ajili ya askari wetu na vitendea kazi. Hata wale ambao tumewapa pikipiki, tusiwape tu pikipiki tukashindwa kuwapa mafuta na fedha

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

za matengenezo ili waweze kuendelea kufanya *patrol* maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la usalama barabarani. Nilipongeze sana Jeshi la Polisi, sasa hivi utii wa sheria bila shuruti umeongezeka kwa kiasi kikubwa. Hili ni jambo jema na la kujivunia sana. Pamoja na kwamba yako maeneo mengine bado askari wanafanya kazi za kuvizia ni kutokana na tabia ya sisi madereva ambao wakati mwingine tunalazimika kuanza kuviziwa katika maeneo hayo. Niombe sana Wizara tufanye kazi kubwa na hasa Jeshi la Polisi ya kuendelea kuwaelimisha wenzetu hawa madereva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ya kutoa elimu kwa madereva ni muhimu sana kuliko kutoza *fine*. Pamoja na kwamba nimesikia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri inawezekana kwamba tukakimbilia sana kwenye *fine* ili kuongeza mapato, njia hii haiwezi ikatufanya tukawa na utii wa sheria bila shuruti. Wako wengine wenyewe fedha wanavunja sheria kwa makusudi ili kusudi waweze kupigwa *fine* na wanalipa lakini wanaendelea na uvunjaji wa sheria na maisha ya wananchi wetu yanaendelea kupotea kwa sababu ya madereva wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Jeshi la Polisi litoe sana elimu kwa madereva hawa kila siku maana ni lazima kukazia maarifa. Madereva hao wanafanya makosa wakati mwingine sio tu kwa sababu wana fedha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunamalizia wachangiaji wetu wawili kwa dakika tano tano. Tunaanza na Mheshimiwa Susan Kiwanga na Mheshimiwa Goodluck Mlinga atamalizia.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachangia bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na kuwa tutaipitisha lakini matumizi ya hizo pesa mpaka leo mimi sijajua. Kwa sababu hali ya utendaji kazi wa Jeshi la Polisi baadhi yao, sijui wanasema wanapata maagizo, kwa hiyo, hawafuati misingi yao, maelekezo na kanuni na maadili ya kazi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmojawapo nimeathirika na utendaji wa Jeshi la Polisi, baadhi yao. Utakuta mkubwa kabisa eti anakuita, unasalimu amri unaenda kituo cha polisi, ukifika pale umesimama tena askari mwanaume anakupiga bonge la bao, yaani sijui wakoje mimi hata sielewi.

MBUNGE FULANI: Ukatili.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Hivi ukatili huu hawa watoto waliozaliwa na mwanamke kama mimi wanautoa wapi hawa *mashetan?* [Neno hili siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huoni kama wanachafua Jeshi la Polisi? Halafu leo tunapitisha bajeti, huyo askari anayefanya unyama kwa watu wanaokamatwa na watu wanaojisalimisha wenyewe, tunampitishia bajeti ya kwenda kununulia...

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan, naona unajumuisha askari wote, kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista kuhusu utaratibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa Mheshimiwa Susan ana *feelings* na anataka kueleza jambo na amesema kwamba jambo hilo limemgusa. Nimwombe tu Mheshimiwa Susan wakati mwingine azingatie tu kanuni, kwa mfano, tuna Kanuni ya 64(1)(g) ambayo inasema kwamba Mbunge hatatumia lugha za kuudhi na kudhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika kama ndani ya Jeshi letu la Polisi kuna Polisi ambao ni mashetani. Kwa hiyo, nadhani kuna umuhimu Waheshimiwa Wabunge wachangie lakini kwa kweli lugha nyingine siyo lugha njema kuzisema, zinadhalilisha utu wa watu bila sababu ya msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kweli Mheshimiwa Susan hilo neno la ushetani alifute aendelee na mchango wake.

MWENYEKITI: Sawa Mheshimiwa Jenista. Mheshimiwa Susan hilo neno siyo stahiki kumwita binadamu, naomba ulifute na liondolewe kwenye *Hansard*. Mheshimiwa Susan naomba uendeleee.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo neno la shetani nalitoa lakini hiyo *message* imeshafika. Kwa sababu kazi ya shetani ni kufanya mambo kinyume na binadamu na Mwenyezi Mungu anavyoamuru, nalitoa hilo neno la shetani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uharamia huu unaofanywa na baadhi ya maaskari wanaochafua Jeshi la Polisi lazima tuuzungumze, hatuwezi kufumba macho. Kwa sababu tusipozungumza hata ukimwendea Mheshimiwa

Mwigulu ukamwambia bwana kule kuna mambo haya anasema mambo mengine wanafanya kule mimi sijui. Huyu hapa anasema kwa sababu tunamwendea na tunampigia simu tunamwambia. Sasa leo nimepata nafasi kwa sababu imekuja bajeti lazima niseme. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Sema.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mimi kama kiongozi, Mwenyekiti wa Chama, Mbunge wa Jimbo la Mlimba unataka kuongea na wananchi unawekewa barua pamoja na maelekezo sema hivi, sema hivi, ndiyo kazi ya Jeshi la Polisi? Siyo kazi ya Jeshi la Polisi, acha niseme, kama unaona nimekosa, kamata, weka ndani, nipeleke mahakamani, siyo kazi yako kunizuwia kusema mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuhitaji kupewa maelekezo kwa sababu sheria, kanuni na taratibu zipo. Tunahitaji kutoa taarifa siyo kuomba kibali, hivyo vibali, vibali ndiyo vinatupeleka huko tunakofika, watu wanajiona wana nguvu sana kuliko Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kazi ya Jeshi la Polisi kwenda kuvamia kwenye *lodge* za watu ambao wanalipa kodi na kila kitu, usiku wa manane, eti kwa kisingizio hapa kulikuwa na watu mchana wamekaa wanataka kufanya maandamano ya tarehe 26, kimetokea Morogoro. Wanatoa wateja ndani wanawapiga, wanawaweka chini ya ulinzi, wanawalundika ndani, kuwaingiza hasara wafanyabiashara, huo ni uharamia, haukulaliki. Jeshi la Polisi fanyeni kazi zenu kwa weledi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya, ukiuliza wanakwambia tumeagizwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano hazijakwisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa tumekuelewa.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Ni dakika tatu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa...

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Nyle Makatibu acheni mambo haya.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan umeshaeleweka, muda wako umemalizika.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan umeeleweka muda wako umemalizika.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia saa, ametumia dakika tatu, mmemkata dakika mbili, kuweni *fair*. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, kwa mujibu wa saa ambayo tunatumia hapa tuko sawa, kwa hiyo, tunaomba tuendelee.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naomba tumalizie muda umemalizika.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanya vibaya.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tutulie muda umemalizika, tumalizie na msemaji wetu wa mwisho.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unaharibu Bunge, tunaangalia saa.

MWENYEKITI: Naomba ukae Mheshimiwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Goodluck naomba umalizie.

MHE. GOODLUCK A. MILINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda uliobaki mbona ni mchache sana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Goodluck naomba umalizie.

MHE. GOODLUCK A. MILINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa muda huu mchache ulionipa ngoja nifafanue masuala machache. Kwanza nilipongeze Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini kuna upungufu mchache ambao unasababisha Jeshi la Polisi kupata madoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni rushwa. Kwa *research* ambayo nimeifanya 85% ya wanaopata huduma ya Jeshi la Polisi wanaipata kwa rushwa. Hawawezi kupata huduma hiyo mpaka watoe rushwa. Mfano mlalamikaji akifika kituo cha polisi hawezu kupata huduma yoyote atatengenezewa mazingira mpaka atoe hela ndiyo ahudumiwe, wataambiwa karatasi hakuna, gari halina mafuta au askari wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili mlalamikiwa, huyu ndiyo balaa kabisa. Ukiwa mlalamikiwa yule askari mpelelezi inatakiwa umuheshimu kama baba mkwe wako, atakuita muda wowote, mahali popote anapotaka. Anaweza akakuita baa akakwambia lipia vinywaji, anaweza akakuita wapi akakwambia toa hela hii hapa. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu dhamana. Dhamana haipatikani bila ya kutoa rushwa. Hilo ni suala la kwanza nililotaka kuchangia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni ubambikiaji wa kesi. Ubambikiwaji wa kesi ni pale Polisi anapo-*exaggerate*, yaani anapoikuza ile kesi tofauti na ilivyokuwa. Kwa mfano, kesi ya madai inageuka kuwa ya jinai, Polisi anafanya hivyo ili kutengeneza mazingira ya kupata pesa. Pili, kesi ya uzururaji inakuwa ya ukabaji. Tatu kesi ya kuku inakuwa ya ng'ombe. Nne kesi ya matusi inageuka kesi ya kuua kwa maneno. Niwapongeze askari wanawake kwenye hili hawapo. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine *traffic*. *Traffic* ni janga lingine la Taifa. Kwa Dar-es-Salaam wanawaita wazee wa *Max Malipo* na mikoani wanawaita *TRA* ndogo. *Traffic* wameacha kazi yao ya kuangalia usalama barabarani sasa hivi wanakusanya mapato na nimethibitisha mmewawekea malengo. Makosa ambayo wanatoza *fine* ni ya uonevu. Unaenda kumtoza bodaboda Sh.200,000/= *fine* na ndiyo maana sasa hivi bodaboda zimejaa kwenye vituo vyote vya Polisi. Kwa hiyo, tunaomba waliangalie hilo. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni makosa ya mitandaoni. Makosa ya mitandaoni saa hizi imekuwa *too much*. Kwenye mtandao hajulikani kiongozi au mtu wa kawaida, wanatukanwa wananchi, wanatukanwa Wabunge wetu, Mawaziri hadi Rais anatukanwa. Mheshimiwa *IGPyupo* hapa tumemweke nyota mabegani hizo ni nguvu, atumie nguvu zake wasimchezee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, natoa *account* ambazo kwenye mitandao ya kijamii zinamtukana Rais. Kuna Kwinyala, Malisa *GJ, CHADEMA in Blood*, Yeriko Nyerere na dada yao Mange Kimambi, wamekuwa wakimtukana Rais. Jamani hakuna nchi ambayo Rais anachezewa, nitolee mfano Kagame, umeshawahi kusikia mtu anamtukana Kagame? Polisi tumieni nguvu zenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni hayo tu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa michango yenu, naamini Mheshimiwa Waziri amewaelewa.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwataje wachangiaji ambao tutaendelea nao jioni ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Katani, Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Mwantumu Dau.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge, kuna tangazo dogo tu la Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, tuna kikao cha chama pale *White House* mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Kwa hiyo, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi mnatakiwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa Khatib na baadaye Mheshimiwa Katani ajiandae.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo jioni ya leo. Naomba Mwenyezi Mungu aniongoze niseme yale yenye busara kwa nia njema ya kuimarisha amani na usalama wa nchi yetu. (*Makofj*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka nizungumzie kwenye ukurasa 46 wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri inayozungumzla usajili wa vyama vya kijamii na vyama vya kidini. Tunajua kwamba vyama na taasisi zote vinavyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya nchi hii vinakuwa ni vyama ambavyo vinatakiwa kufuata sheria ambazo zinawekwa chini ya usajili wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo hapa niseme kwamba Serikali iwe makini sana hususan na taasisi za kidini, nimeona Mheshimiwa Waziri ameleeza kama kuna baadhi ya taasisi ambazo hawakuzipa usajili na naamini kwamba waliangalia sababu na wakajiridhisha kwamba hazifai kupewa usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba, usajili wa taasisi za kidini lazima uendane na masharti kwa sababu nchi yetu haina dini; lakini Watanzania wana dini zao. Nasema hili nikirejea hoja yangu wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu Mheshimiwa maneno ya mwanzo ambalo ni suala linanipa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Si kwamba Mbunge anaposimama hapa anakuwa na yake tu, *sometime* anakuwa na mawazo yake lakini wakati mwingine anawakilisha. Mimi ni Muislam na

naelewa tatizo lililopo sasa hivi. Tatizo ambalo nataka kulisemea ni kwamba taasisi za kidini zote zinapopata usajili wa aina moja lazima isiwepo taasisi ikajiona leo taasisi hiyo ni kubwa kuliko nytingine. Hilo kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa kutambua, kwa mfano sisi Waislam tuna taasisi nydingi na narudia kusema hivyo. Siku ya mwanzo niliyosema nashukuru Mheshimiwa Waziri alinijibu moja kati ya mawili la kusema kwamba hakuna tatizo kwa taasisi zozote kutumia ukumbi wa Bunge. Limeondoa masuala katika jamii kwa sababu lile jambo lilitendeka baadhi ya wananchi wengi walidhani ni jambo geni sana kwa Bakwata kufanya mukutano humu ndani, lakini baada ya ufanuzi ule wananchi wametulia na wameridhika kwamba taasisi yoyote inaweza kuja na kufuata masharti na ikafanya vikao ndani ya Bunge, hakuna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la kuifanya BAKWATA kuendelea kuwa ni wasemaji wakuu wa Waislam Tanzania, hili kosa! Kwa sababu Bakwata haina usajili wa aina yake. Leo tumemsikia, niliuliza swali kwa Serikali, nilitegemea majibu nipate kwa Serikali, lakini bahati mbaya sana nasema kwamba wametokea Masheikh huko wamenijibu na mimi sjaisema BAKWATA kwa ubaya. Nataka sheria na haki iwepo sawa kwa taasisi zote isitokee moja ikajiona kwamba wao ni juu ya wengine, hilo ni kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna hivi leo usajili wa vilabu hivi vyta michezo hata Simba akiwa bingwa mara 10 hana mamlaka juu ya vilabu vingine. Hiyo ni *club* iliyo sajiliwa kwa sheria sawa na vilabu vingine hali kadhalika *NGO's* na vitu vingine. Kwa hiyo, naiomba Serikali bado itoe majibu ni sheria gani wanayoitumia kuitambua BAKWATA kama ndiyo chombo kikuu cha Waislam Tanzania? Nitashukuru nikipata hilo majibu na sitarudia tena kulizungumza hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninalotaka kuzungumzia ni hali ya usalama ndani ya nchi. Kwa masikitiko makubwa sana, Taifa hili ndiyo lilitokuwa nchi ya mstari wa mbele katika ukombozi wa Bara la Afrika. Kitovu na ndiyo

tuliowapa makambi wapigania uhuru wa nchi mbalimbali kupigania amani za nchi zao, kwa sababu hawakuridhika na mateso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Mwalimu Nyerere hakuridhika na unyama wa Makaburu uliokuwa unafanyika Afrika Kusini. Alikuwa anaumia sana kwa matendo wanayotendewa Waafrika ndani ya Afrika Kusini. Leo tuliwapigania sisi tunarudi kule ambako tulikuwa tukiwapigania wenzetu. Mauaji ya kiholela, utesaji usio na tija, utekaji wa hovyo hovyo ndani ya nchi, tayari umeshamiri na unashika kasi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vitu vya kusikitisha sana. Ukipikia leo tumelala tumeamka salama hatujasikia sehemu kumetokea tukio ni jambo la kumwomba Mungu. Juzi wiki tatu zillzopita Pemba wameenda kuchukuliwa vijana sita na watu na magari yao na taarifa imetolewa kwa Kamanda wa Polisi kwamba gari zilizokuja kuchukua watu hawa ni namba hizi na zikafuatiliwa mpaka mamlaka wa usajili wa vyombo vya moto na kuonekana gari zile ni za watu fulani. Sasa hebu niambieni mpaka leo hakuna hata gari moja wala mtu mmoja aliyekamatwa kuhusishwa na tukio lile, tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu! Pale Dar es Salaam lipo tukio lilitokea, mtu mmoja alienda akatekwa nyara, bahati wananchi pale Buguruni wakavamia gari wakalikamata, wakalipeleka kituo cha Polisi Buguruni na washtakiwa, lakini mpaka leo kesi hiyo haikwenda mahakamani na gari lile hatimaye liliachiwa, kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayalea matukio haya, lakini madhara yake yatakuwa makubwa sana baadaye. Kwa sababu uvumilivu wa watu unaweza ukawaishia. Leo kuna watu wanao majina wakipatwa na tatizo nchi nzima inaelewa, lakini kuna watu hawana majina. Mfano, miezi miwili iliopita pale Zanzibar ameenda kuchukuliwa Mzee wa watu anaitwa Ali Juma Suleiman. Mzee wa watu

amechukuliwa na vyombo, magari yanayojulika na watu wanaojulika, wakaenda wakamchukua nyumbani kwake mbele ya watoto wake, wameenda kumpiga siku ya pili kufa hospitali, hakuna anayezungumza, hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa limekaa kimya kwa sababu aliyekufa pale ni mtu hana jina. Hapa akifa mwanasiasa au watu mwингine ndiyo kidogo unasilia. Sasa matukio kama yale yanaleta hasira ndani ya jamii, taasisi iliopewa dhamana ya kusimamia usalama wetu, badala ya jeshi la polisi kuwa usalama wa raia leo unajeuka kuwa uhasama wa raia? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana suala la utekekaji wa kiholela unaoendelea, suala la matukito haya ya kuumiza watu kwa kweli sio masuala ya kibinadamu hayo ni masuala wanayofanya wanyama tena wale wanyama wanapokuwa na njaa ndio wanapokula mnyama mwensiwe. Sio katika hali ya kawaida, hawezi kufanya tukio kama hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi suala lingine niongelee suala la waendesha mashtaka. Juzi tumepata taarifa kama ndugu yetu Aquilina faili lake limefungwa kwamba limeishia limefungwa, kwa nini hatujui! Hata hivyo, upelelezi huu uliotumika haraka kufikia kufunga shauri la Aquilina kwa nini hauendi upelelezi huo katika mashtaka mengine mengi yaliyomo ndani ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wametumia si zaidi ya miezi miwili kujiridhisha kama ushahidi haupo na wameamua kufunga lile jalada, hebu waniambie ni kwa nini leo miaka mitano, Masheikh wa Uamsho kutoka Zanzibar wameshindwa kufunga faili hilo wakati wameshindwa kupata ushahidi. Hebu watuambie lilioko nyuma ya pazia. Kwa sababu ubinadamu hisia za utu lazima zitujie sana, sote ni wazazi, sote tuna baba tuna mama, tuna watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna yejote kati yetu humu kama ni baba yake wala ni mama yake au ni ndugu

yake angeridhika kuona watu wale miaka mitano wameshikiliwa pasipo mashtaka yao kufafanuliwa wakahukumiwa kwa ajili ya kesi zao, hakuna! Kati yetu mmojawapo angekuwa mtu yule anamhusu hakuna, hisia za ubinadamu na utanzania ziturudie. Tuangalieni mateso wanayopata familia za wale, wake wawili wa Wazee wale waliko gerezani tayari wameshafariki. Hawakuonana tena na wapendwa zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaswali kila asubuhi kumwomba Mungu atupe baraka, sisi tuliopewa madaraka kuongoza Watanzania je, tunatenda haki kwa tunaowaongoza ili tupate baraka ya Mwenyezi Mungu? Huwezi kumwomba Mungu akujalie baraka wakati wewe umepewa mamlaka lakini hutendi kwa baraka kwa watu unaowaongoza. Vipi Mwenyezi Mungu atalihurumia Taifa hili. Tuongoze kwa dhahabu Afrika, kwa mifugo, kwa maklinikla na mengine lakini kama hatutendi haki kwa tunaowaongoza Mungu hatatujalia baraka katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, suala la kesi ya Masheikh ya Uamsho ni suala ambalo linatukera sana Watanzania na wapenda haki wote na naamini kwa ukimya huu hata Bunge hili hawafurahii tena kuona suala hili la Masheikh wale wanaendelea kushikiliwa katika kipindi kirefu namna hii haiwezekani. Leo ikiwa tukio la kufa mtu Aquilina limechukua miezi miwili, tukio la Masheikh wale waliodaiwa magaidi hajakufa hata kuku ndugu zangu Wabunge. Hata kuku hakuuliwa katika tukio lile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mifano ya nchi zinazotokewa na matukio haya. Ubelgiji pale palitokea tukio la kutisha *airport* na wapo watu walishikwa ndani ya miezi mitatu vyombo vyaya upeletelezi vilijiridhisha kama watu wale hawakuhusika na waliachiwa huru mara moja. Leo tumefikwa na nini Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kuwasemea ndugu zangu hawa wa Jeshi la Polisi, jambo la kuwapandisha

vyeo hawa na wakashindwa kuwalipa stahili zao zinazolingana na vyeo vyao ni jambo linaloumiza sana. Leo askari anapanda miaka minne lakini bado marekebisho ya mishahara yake hayatekelezwi kwa nini? Miaka minne kwa nini? Wengine mpaka wafikia kustaa fu na nyota begani lakini mshahara hauongezeki, *what is this? (Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khatib. Tunaendelea na Mheshimiwa Katani.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru, nikiendelea kwa yale aliyoachia ndugu yangu Khatib, ninalo jambo la kuzungumza juu ya Jeshi la Polisi. *Page* ya 12 wamezungumzia suala la kuboresha Mfumo wa Upelelezi wa suala la kesi za jinai. Hili jambo ni jambo jema sana kama mfumo utafanya kazi inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yanaleta mkanganyiko sana. Tarehe 8 Agosti, 2015 Jimboni kwangu Tandahimba wamechukuliwa watu takriban tisa. Watu wenyewe wengi wao ni Masheikh. Bahati mbaya wamepelekwa Dar es Salaam wameingizwa kwenye kesi ya mauaji tena kesi yenyewe Polisi wanafika pale *Oysterbay* wanauliza watu hawa tuwape kesi gani. Ndiyo maana mpaka leo kesi ipo mahakamani ushahidi mpaka leo haujakamilika. Haujakamilika kwa sababu yaliyofanyika ni uonevu unaotokana na jeshi la polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano yupo mtu anaitwa Mbaraka, Mbaraka tarehe ambayo amebambikiwa kwenye kesi ile ya mauaji ya Ikwiriri, hatupendi kuona Polisi wakiuliwa, Mbaraka alikuwa kwenye kikao cha TANEKU Newala, siku ya pili ameshiriki kikao cha kamati ya shule, amelala kwenye msiba, lakini unamkamata mtu unamwambia kwamba amehusika kwenye kesi ya mauaji ya Ikwiriri. Huu ni uonevu wa Jeshi la Polisi ambaa hauna mfano kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ya ajabu kwa jeshi tunalolitegemea. Naamini /GP Kamanda Sirro anafanya kazi nzuri kwenye kudhibiti uhalifu. Kwenye kuonea watu hawa ambao hawana hatia ni mambo ya ajabu sana, wanajidhalilisha Jeshi letu la Polisi bila sababu za msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu leo wana miaka takribani mitatu au minne na kesi zao zilishawahi kwenda kwa Waziri aliyekuwa wa Sheria kipindi hicho akasema anashughulikia, lakini mpaka leo watu hawa wanakwenda mahakamani wanarudi, ushahidi bado haujakamilika. Ni lini ushahidi utakamilika? Wanawapaje vifungo Watanzania ambao hawana hatia kwa sababu ushahidi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana, Jeshi la Polisi tunalolitegemea, wanapoamua kufanya kazi zao wafanye kwa weledi. Nami naamini kabisa Jeshi la Polisi wapo watu wana uzoefu, wana uzoefu na upeletelezi. Hizi tamaa za fedha, maana matukio haya kwa Mtwara yamekuwa yanafanyika kwa ajili ya tamaa ya fedha. Wapo watu wameuawa, wapo watu wakitoa fedha milioni mbili, milioni tatu wanaachiwa, kama kweli wangekuwa wauaji wasingewaachia basi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi, leo wiki ya pili wamekamatwa watu wangu Tandahimba kule, Kijiji cha Mihamwe. Tandahimba mpaka wetu wa Tandahimba na Msumbiji ni Mto Ruvuma. Tandahimba hakuna tembo, Tandahimba hakuna mali hizo zinazosemwa watu wale wamepelekwa polisi inasemekana kwamba wanauza meno ya tembo. Meno ya tembo Tandahimba yanatoka wapi? Maana siyo Liwale Tandahimba, mwisho wa siku wanatoa 2,500,000 hawana kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo Jeshi la Polisi wanajidhalilisha bila sababu za msingi. Hata hivyo, inawezekana haya mambo yanafanyika kwa sababu ya vipato vidogo vya Jeshi letu la Polisi. Kama wangekuwa

wanawapa mafao yanayofanana, nadhani wasingekuwa na tamaa na fedha hizi ndogo ndogo hizi. Kwa hiyo, niwaombe sana kwenye kuboresha maslahi ya jeshi la Polisi labda watafanya kazi kwa weledi, basi waone namna gani wanapata maslahi yaliyo bora ili watu wetu waweze kufanyiwa mambo yao kwa utu na kwa kutumia haki za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la udhibiti wa uhalifu nchini; nimpongeze /GPna jeshi lake kwa sasa suala la uhalifu limepungua kwa asilimia 90. Mimi nilipongeze sana Jeshi la Polisi nchini. Hata hivyo, kwenye matukio haya wapo wezi ambao wanaiba pikipiki Dar es Salaam, wanapeleka Mtwara, wanapeleka maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile pikipiki wanatengeneza kadi feki unapotoa pikipiki Dar es Salaam ina kadi feki ukapeleka Ngara, mtu wa Ngara hawezi kubaini kadi feki. Anauziwa pikipiki yenye kadi feki ambayo ukiangalia *document* zinaonesha zinafanana na mwisho wa siku anakamatwa mtu wa Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *operation* yao wanayofanya kwa ajili ya wezi hawa, naamini kabisa kwamba /GP Sirro wanaweza wakawabaini watu hawa ambao wengi wao wanatoka Dar es Salaam na wizi mkubwa wa pikipiki unafanyika Dar es Salaam. Badala ya kwenda kukamata watu wetu ambao wanateswa mwishoni japo wanasema na waliowauzia pikipiki akina nani? Hata hivyo, wanashindwa kuwakamata waliouza pikipiki wanakwenda kwa watu wa hali ya chini wale, badala ya kuchukua pikipiki *wazi-hold*, wale watu na wenyewe wanaendelea kuwaresa bila sababu za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala la mipaka, kwenye Idara za Mheshimiwa Waziri kwa maana ya Wizara yake ya Mambo ya Ndani afadhali Jeshi la Polisi wana vitendea kazi vya kutosha, japo havitoshii kwa kiwango hicho kinachoridhisha, lakini wapo watu wanafanya kazi kubwa ndugu zetu wa uhamiaji. , maeneo ya mipakani ambapo

watu wa uhamiaji wapo hawana vitendea kazi, hawana magari, lakini hata *OC* zao hawazipeleki, watafanyaje kazi watu hawa wa Idara hii ya Uhamiaji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara wanajua tunapakana na Mto Ruvuma pale. Watu wa Uhamiaji ni watu ambao wanapaswa wawe na magari kwa ajili doria na vitu vingine kule, lakini leo hawana magari; lakini *OC* hizi za milioni moja moja tunazosema wakienda kuangalia Uhamiaji wamepeleka lini wataona aibu wenyewe. Waende wakaangalie wataona aibu wenyewe! Wawapelekee *OC* hizi waweze kufanya kazi kwa ufasaha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye kuboresha maslahi ya ndugu zetu hawa wa Uhamiaji ambao wanafanya kazi kubwa sana. Wanafanya kazi kweli kweli, amepata kuzungumza Mzee Ally Keissy pale kwamba zamani kulikuwa na *passport* zinapatikana kwa raia ambao hata sio Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wanatoka Burundi wanafanya ujanja ujanja wanapita Tanzania wanapata *documents*, wanaenda *South Africa* ndio wanauza madawa ya kulevyaa kikamatwa kwa sababu ana *document* ya Tanzania, anaonekana ni Mtanzania. Uhalifu huu umefanywa katika maeneo mengi wakitajwa Watanzania kumbe sio Watanzania ni Wanyarwanda wengine ni Warundi, wanafanya matukio haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuimarisha mifumo hii, Idara yetu ya Uhamiaji ni lazima waipe nguvu ya kutosha, waweze kufanya kazi zao vizuri ili tuweze kuimarisha mazingira haya na kuondoa maneno yanayotajwa Tanzania kumbe sio Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kumwambia tatizo la Askari wetu wa Usalama Barabarani hususan Tandahimba, lakini hata alipokwenda Waziri Mkuu wananchi wameweza kuonesha mabango pale. Jeshi la Polisi Usalama wa

Barabarani kuna tatizo gan? Kwa nini askari wa usalama barabarani apige mtu viboko ndio sheria inavyotaka, ndiyo *PGO* ilivyoandikwa ndani humo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa yametokea matukio ya Tandahimba zaidi ya matatu au manne hata akisema Mheshimiwa Waziri tuondoke au */GPTwende* atakuta vijana wamepata ajili kwa sababu *DTO* anachomeka gari yake anamchomekea bodaboda na sio mara moja au mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yametokea matukio zaidi ya mara tatu, mara nne, kwa ajili ya ustahimilivu ya watu kuheshimu Serikali, vinginevyo wangeamua kuchukua sheria mkononi, wao kwa sababu wana silaha za moto wanasesma wananchi ndio wenyewe matatizo, kumbe matatizo mengine yanazalishwa na Jeshi la Polisi lenyewe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tandahimba tatizo kubwa ni *DTO* peke yake, askari wengine wa usalama barabarani wanafanya kazi kwa weledi, yeye ndiyo anafanya matukio haya ya oyo na siyo mara moja au mara mbili, Mheshimiwa Mwigulu nimeshamwambia zaidi ya mara tatu jambo hili. Waziri Mkuu amekwenda kwenye ziara Tandahimba amekutana na mabango, bahati mbaya mimi sikuwepo nilikuwa Ubelgiji huko, amekutana na mabango watu wakilalamikia hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wanampenda sana *DTO* wambadilishe hata kituo wachukue Mheshimiwa Mwigulu wapeleke kwake pale, akawafanyie watu wake aone uchungu atakaoupata. Atajua wapiga kura wake wakipigwa, mtu amekosa kuvala *helmetkweli* amefanya kosa ni sahihi apigwe viboko na *DTO*? Ni sahihi achomekewe gari na *DTO*? Kwa nini *DTO* wa Tandahimba avunje sheria na Jeshi la Polisi lipo, Waziri anajua bado tunaendelea kukaa naye. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bwana ni wanadamu kweli kweli na tuna utu kweli kweli, wakati mwingine ukionewa

sana utakapoamua kunyanya u mguu, aliyenya nyua mguu ataonekana mkorofi. Hatutaki watu wa Tandahimba tufike huko. Najua wana busara za kutosha, *IGP* yupo anasikia, Waziri nimemweleza jambo hili zaidi ya mara tatu, lakini wameendelea kumwacha yule bwana, aidha kuna jambo wanalitengeneza Tandahimba, aidha utokee ugomvi baina ya polisi na raia kwa sababu wana bunduki wapige watu wa Tandahimba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana mtu mmoja asisababishe amani ya watu wa Tandahimba wote. Miaka miwili mfululizo Tandahimba hatufanyi biashara kwa uhuru pale. Watu wanakwenda Newala ambako kuna unaifu *Traffic* hawatumii nguvu kubwa wanakwenda kununua bidhaa kule, tunaiacha Tandahimba ikididimia pale kwa ajili ya mtu mmoja ambaye anafanya watu washindwe kuingia Tandahimba kwa kutofuata sheria. (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Katani. Tunaendelea na Mheshimiwa Godbless Lema baadaye Mheshimiwa Ali Hassan King ajiandae.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge ile biashara ya miongozo, miongozo wakati wangu bora muipunguze kwa sababu nataka niongee mambo *serious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo humu ndani wako viongozi wote wa vyombo vyaya ulinzi na usalama. Unapokuwa na viongozi ambao mshahara na cheo kwao ni msingi kuliko utu na thawabu, lawama wanazozipokea kutoka kwetu lazima zitaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Upinzani na Wabunge ilikuwa ni kutetea ustawi na maslahi ya Jeshi la Polisi, badala yake Wabunge ndani ya Bunge wanaliongea Jeshi la Polisi kama ni kikosi cha mauaji. Kama hawawezi

kuiona hii sense kwamba Taifa limepotea kwamba Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi na *opposition* wakiongea wanalaumu Jeshi la Polisi na Jeshi la Polisi linalaumiwa kwa sababu tumeli-*politicize*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo shughuli za siasa zimekuwa ngumu, mimi leo niko upinzani, kama lengo la demokrasia ni Mbewe, Lema na Mwambe na Mbatia na walioko huku, hawa watu wanaweza wakaamua kurudi kwenye biashara zao. Yeyote anayefikiria kuua demokrasia kwa sababu ya ushindi wa chama chake hampendi mjukuu wake. Wakijua msingi wa demokrasia hawawezi kutengeneza mkakati wa kisiasa wa kuua demokrasia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi siyo maadui, leo hatufanyi mikutano ya hadhara, leo vikao vya ndani vimezuiwa, Polisi wamepewa amri na kwa sababu wao wameapa kutekeleza amri leo kazi ya siasa imekuwa ngumu. Tukimalizwa sisi, tukaondoka sisi, hiyo vita itahamia ndani yenu, na nawaambia mwaka 2020 kwenye uchaguzi unaokuja kama sisi tutakuwa tumesafukiwa, nyie hamtakuwa na kura ya maoni, mtakuwa na kura ya vidole, imeonekana Songea na sehemu nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulinda demokrasia haisaidii chama tawala inasaidia *the next generation of this country*. Leo wewe ni Mwenyekiti hapa alikuwepo *IGP* Mangu leo hayupo leo yupo Sirro na kwa utawala huu Mwigulu kesho anaweza ye ye akajikuta amekuwa *DC* kama ambavyo *Deputy DG/S* leo ni *RAS* anaenda kukaa kwenye kikao ambacho *RCO* anakuwa *boss* wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajifunze kwamba tunavyotaka kuhimiza demokrasia maana yake ni kwamba ni kwa ajili ya ustawi wetu. Mimi ni mchaga naweza nikaamua kuuza sumu ya panya, naweza nikaamua kuwa na hardware nikaachana na siasa. Siachani na siasa kwa sababu sifikiria uchaguzi unaokuja, nafikiria *next generation*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, linda muda wangu, Katibu nakuomba linda muda wangu. Nyie mliopewa zawadi ya kurekodi naomba hii video yangu niipate baadaye kwa sababu siku hizi hamnipi video zangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema endelea.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nasema hivi Waheshimiwa Wabunge nyie mko wengi, nyie mna kura, nyie mna maamuzi, kuna Mawaziri huko wa nyanja zote saidieni hili Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila mtu analia, tuna Mashehe Gereza la Arusha, tuna Mashehe Dar es Salaam, tuna Mashehe Songea, unapoweka viongozi wa dini kwa miaka minne bila kumaliza mashauri yao unajenga *enemity* ya kidini. Hawa watoto wao na wajukuu wao waliokaa kimya hawana maana kwamba wamekuwa wajinga, kuna siku wataamka na siku wakiamka itakuwa ni hatari sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kibiti nauliza lini tumeona Jeshi la Polisi limeita *Press Conference* ya kusema mambo ya Kibiti, watu wamekuwa, watu wanapotea. Hawa watu walitakiwa wapelekwe Mahakamani, wasomewe mashtaka wahukumiwe, leo hakuna. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mkristo naogopa uadui unaojengwa kati ya Waislam na Wakristo wako Mashehe 85 karibu kule Arusha mwaka wa nne watu wamekatwa miguu, upelelezi haujakamilika. Huu uadui unaojengwa Waheshimiwa nyie mnaweza mkasaidia nchi hii, nyie mko wengi, kuna Mawaziri huku Maprofesa na namna ya kusaidia nchi hii ni kupuuza vyeo na mshahara *against dignity*. *Dignity* ni thawabu kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kesi ya kubambikizwa, mimi najua Mboge alikuwa anapewa kesi ya mauaji, Halima anapewa kesi ya uhaini, kwa sababu gani! Hakuna Mbunge huku ambaye ana kesi. Kila siku unaona Jeshi la Polisi linapambana na vijana wadogo wa *cyber-crime*, kijana wa

miaka 25 amemkosoa Rais mnakwenda mnamkamata. Mnawapa polisi mzigo ambao ni *unnecessary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina matatizo mengi bahaarini, matatizo ya madawa ya kulevyaa, Sirro anaanza kukimbizana na mtu ame-*twitt* kwamba Rais Magufuli hafanyi vizuri. Msipomfundisha Rais kukosolewa hamuwezi kupata, "*Mungu anakosolewa ndio maana kuna Uislamu na Ukristo itakuwa mtu? Mungu anakosolewa, mjifunze kukosoana, kukosoana ni tiba siyo balaa*". [*Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge*]

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema tafadhali naomba ufute kauli Mungu anakosolewa, Mwenyezi Mungu hakosolewi.

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, pamoja na kwamba kanuni ya 64(1) haizungumzi jina, haizungumzii suala la imani la kumkosoa Mungu ama kutokumkosoa, nakushukuru umeliweka vizuri, lakini narudi pia kumkumbusha katika mijadala wake azingatie kanuni ya 64(1)(d)(e) kwa sababu anapoendelea kuzungumza na kuchangia *as if* kwamba haya yote yanayofanyika yanafanyika kwa sababu Mheshimiwa Rais hashauriwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge kwa mujibu wa kanuni hizo nilizozisema aendelee kuchangia kwa kuhestimu kanuni hizo ambazo zinaleza vizuri mamlaka ya Rais kikatiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana utaratibu huo ufuatwe.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtukufu Rais wetu asiyekuwa na makosa kabisa, niseme hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakristo wenyewe wanabishana kuhusu imani; *Catholic* kunywa bia siyo dhambi, Pentekoste kunywa bia ni dhambi, huku ni kumkosoa Mungu. Unavyo-*challenge faith* maana yake Mungu anakosolewa. Waislamu wanamuita Issa na Issa sisi tunamwita Yesu.

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema taarifa subiri, Mheshimiwa Katani.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Lema kwamba Mungu anakosolewa wapo wanaume wanajigeuza kuwa wanawake na tunawaita mashoga, kwa hiyo, ni kumkosoa Mungu. (*Kicheko/Makof*)

MBUNGE FULANI: Na kuna wanawake wanajibadili ngozi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema naomba unavyotafsiri wewe isiwe kwa jumla jamala, iwe ni wewe peke yako imani yako.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Katani napokea taarifa yako. Kwa vile tafsiri ya imani ni pana hata Jenista anatakiwa akiona tafsiri hiyo akae chini kwa sababu ni pana sana. Nyie mniamuita Yesu Nabii Issa, sisi tunamwita Mwana wa Mungu na ni mgogoro, hiyo ni kumkosoa Mungu.

KUHUSU UTARATIBU

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti,

naomba sana Mheshimiwa Lema atusaidie kwa mujibu wa katiba sisi wote tuna uhuru wa kuabudu na kuwa na imani zetu. Mheshimiwa Lema asitufikishe katika misingi ya upotoshaji kwenye imani zetu, kila mtu humu ndani kwa mujibu wa Katiba ana imani yake na ana uhuru wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kumzungumza Mungu kwa mtazamo wake anaweza kuyafanya mahali ambapo anaruhusiwa kuyafanya huko anakoona inawezekana, lakini hapa ndani kwa sababu Katiba yetu hairuhusu mambo hayo anayotaka kuyazungumza kwa sababu imani zetu zinasimamiwa na katiba. Tunamwomba Lema achangie hoja zake lakini attuache na imani zetu asitupeleke huko anakotaka kutupeleka. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema ni sahihi kidogo hata na mimi naamini kwamba kumkosoa Mungu kwangu mimi ni dhambi. Kwa hiyo, atakayefanya hivyo, naona anafanya madhambi, kwa hiyo kama unaweza kuchangia zaidi naomba uendelee hivyo.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jenista namshukuru kwa sababu pia amekuwa mtetezi wa Mwenyezi Mungu. Mungu akubariki sana, basi nahama kabisa. Sasa dakika 3 .6 nimetumia, Katibu usije ukalera mambo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ya kwamba kuna matatizo makubwa katika Jeshi la Polisi. Nimesema wabunge wote hapa asilimia karibu 60 wana kesi, wote wana kesi, wote wapinzani wana kesi, sasa haya mambo yanaongewa na Wabunge lawama kwa Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi likiwa imara siyo kwa faida ya CHADEMA wala CCM ni kwa faida ya *generation* ya nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa Mbunge ni thamani kubwa. Mbunge maana yake unawakilisha wananchi, unatunga sheria kuhusu nchi. Nilisema Bunge lililopita Wabunge wote mlioko hapa asilimia 70 hatukuwa wote *term* iliyopita. Tunapotunga, tunaposimamia maadili na *integrity*

ya Jeshi la Polisi tushikamane pamoja kujenga jeshi imara ambalo hata kama wewe siyo Mbunge litakupa nidhamu, hata kama wewe siyo Rais litakupa nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Jeshi la Polisi leo lina lawama nyingi, mimi nimekaa magereza miezi minne na siku 16 nimeona mambo ya kutisha. Nimeona watu wanaishia magereza, leo polisi kupata dhamana ni mpaka uka-*apply habeas corpus* Mahakamani. Leo polisi *bail*/haipo, sasa kuna chuki inajengwa kati ya polisi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu leo Mheshimiwa Spika alisema mbona Sirro alivyotajwa makofi hayakupigwa upande huu? Siyo upande huu huko nje hawapigi makofi wakimuona polisi, kwa sababu gani, Marekani ukimuona polisi unaomba kupiga naye picha, hapa ukimuona polisi unakimbia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ninachosema ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema naomba uendeleet tu.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi nawaomba sana hakuna kazi muhimu tutakayofanya kama ya kujenga *integrity* ya Jeshi la Polisi. Ukiangalia undani kabisa Jeshi la Polisi wao wenyewe wanaharibiwa na sisi wanasiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna uadui kati ya raia wa kawaida na Jeshi la Polisi. Unasikia mtu ameuawa Mbeya, mdogo wake Heche amepigwa kisu akiwa na pingu kwenye gari ya polisi, wanaenda kutupa mwili bodaboda ikaona. Boda boda imeona, watu wakasema, wakapiga kelele.

MWENYEKITI: Malizia ya mwisho hiyo Mheshimiwa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado dakika tano, mimi zangu dakika 10 bado naangalia saa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda umekwenda naomba umalizie sentensi yako.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko hapa *IGP*. *IGP* ushauri wangu ni huu mimi nimekuwepo Bunge hili nimeona Bunge hili likisema *Sethi Harbinder* zile pesa za *IPTL* zilikuwa ni mali binafsi. Nimeona Bunge hili hili wakisema asulubiwe, kabla jogoo halijawika mara tatu hawa watu hawa wanaokutuma kazi leo kuna siku watakuning'iniza, ushauri wangu ni huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia *IGP*, sio kila maelekezo ya kuumiza watu mnayachukua Mheshimiwa Lissu kapigwa risasi hapa, Naibu Waziri Kalamani anang'oa *CCTV Camera* kwake, kuondoa ushahidi. Ben Sanane kapotea, Azory kapotea, maiti zinaokotwa mchangani Mwigulu Waziri anasema hizi maiti zimeuawa na watu wasiojulikana. Kama wewe ni Waziri wa Mambo ya Ndani, kama kuna *IGP* maiti zinaokotwa zaidi ya elfu moja, huwezi kujua aliyeuwa unakaa ofisini kufanya nini, nenda kauze maandazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *integrity* ya Jeshi la Polisi ni ya msingi kuliko chochote. Waheshimiwa Wabunge nawaambia...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lema, nimeshakuongeza. Tunaendelea na Mheshimiwa Ali Hassan King, ajiandae Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Mwantumu Dau.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Mimi la kwanza kabla sijamshukuru Mungu niseme *Subhanallah min-dhalika*.

Mwenyezi Mungu ametakasika na yote ambayo yamesemwa na mtu ambaye hajielewi, ametakasika. Mungu hakosolewi kwenye imani yoyote ile. Sasa waone Watanzania jinsi gani kwamba mtu kama huyu ndio awe wanamwamini kwamba kumfuata maneno yake ikiwa kwamba kauli zake ndiyo hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu na naomba Mwenyezi Mungu aniongoze, anitoe kile kitanzi wanachotiwa wenzetu wanapojikakamua sauti kali na halafu haitoki, kile kitanzi Mungu mimi aniondoshee nizungumze hivi taratibu ili *message* yangu ifike vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanazungumza matukio lakini wanashindwa kusema sababu. Wanataja kulaumu lakini wanashindwa kutaja sababu zilizowapelekea au zilizowafikisha watu pale wao wanapolaumu. Wanalilaumu Jeshi la Polisi lakini wanashahau kwamba kuna mambo yalifanyika Kibiti wakidhibitiwa, mambo yalifanyika Tanga wakidhibitiwa, mambo yanayohamasisha maandamano, mambo ya watu wanaozungumza tofauti, ni sawasawa na kusema kwamba lawama sasa zinahama kwa mjambaji zinakwenda kwa mtema mate. Hivi ndivyo walivyo wenzetu, lawama zinahama kwa mjambaji sasa zinaenda kwa mtema mate, kwa sababu wahamasishaji wa ubaya ni wao. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niongee ya kwangu kwa Jeshi la Polisi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tutulizane tumsikilize.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa masikitiko makubwa sana kusikitikia Wizara hii ya Mambo ya Ndani na huzuni kubwa sana, mwaka wa tatu huu haya ninayoyasema leo nayasema

tena. Hakuna hata moja ambalo limefanyika kwangu na mimi sasa nazungumza masikitiko yangu Jeshi la Polisi kwangu mimi natokea Jimbo la Jang'ombe, kuna Ziwani Polisi...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tusikilizane, mwachenii na yeye achangie. Waheshimiwa tutulizane tafadhali.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Jamani hebu tulieni kidogo, taratibu. Jeshi la Polisi kwangu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tujifunze kuvumiliana, wenzeni wamevumilia na nyie mvumilie.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kwangu ni sawasawa na *double edged sword*, upanga wenye ncha mbili. Ncha ya kwanza ni sehemu ambayo tunapata ulinzi na usalama kwa Tanzania nzima na hiyo tunanufaika katika Jimbo letu, lakini ncha ya pili kwa Jeshi la Polisi kwangu mimi ni wapiga kura wangu Mkoa mzima wa Mjini Magharibi Unguja askari wake wanakaa Ziwani Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya ziara tarehe 7 Januari, 2018 kwenda Ziwani Polisi nikakuta pale kuna zile nyumba ambazo za *single* wanakaa mtu mmoja mmoja kutokana na ukosefu wa nyumba, zile nyumba zinakaa familia, zile nyumba zipo 15 kila nyumba moja ina familia nane kuna familia 120, kule kwetu sisi mashallah watu wanazaa. Tukimpa kila mmoja watoto wanne wanakaa watu wanne ndani basi watu 480 wanakaa, lakini wanatumia choo kimoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nimeshalisema na lilianza kusemwa na Mbunge aliyejita mwaka 2011 halijafanyiwa kazi. Pale kuna choo kimoja kiliwahi kujengwa na Mheshimiwa Nyanga aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe. Nampa tena Mheshimiwa Waziri hii taarifa tena, je, likitokea la kutokea choo kimoja watu 480 wanatumia vipi

askari hawa. Masafa ya kufuata choo ni mita 100 mpaka mita 200; kila mmoja anatoka na kopo la maji na ndoo, ukitokea ubakaji pale tutasemaje? Yakitokea maradhi ya mlipuko katika choo kile kimoja tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hili naomba nitekelezewe na nimepeleka kwa *DCP* Malika, Kamishna wa Ujenzi wa Polisi Makao Makuu nimepeleka mwenyewe kwa mkono. Tunahitaji milioni 50 kujenga vyoo pale vya askari, kama kuna dharura basi tuje tusubiri dharura ya kupata maradhi watu wakafa...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Jambo la pili...

MWENYEKITI: Mheshimiwa King naomba uendelee tu.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa endelea.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Yule mimi akinipa taarifa nitamjibu hapa hapa tu, unayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa King, endelea tu usitoe ruhusa.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nyumba ya Kilimanjaro Ziwani Polisi, hii nyumba imejengwa tokea kwenye miaka hiyo ya 1980, hii nyumba inatakiwa kukarabatiwa, nyumba inakaa 12, tukimpa kila mmoja watoto wanne, nyumba inavuja na inakaribia kuanguka. Hivi leo ndio tunataka mpaka nyumba ianguke askari wafe tulete mfuko wa maafa. Tunahitaji milioni 68 kukarabati kuweka paa ili kudhibiti vitu ambavyo vinatokea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi mvua za juzi, familia mbili zinazokaa juu kwenye jengo la Kilimanjaro Ziwani Polisi zimehama kwa sababu jengo linavuja, je, tunasubiri lianguke? Kama hiki sio kipaumbele, kipaumbele ni kuzika askari wetu? Kipaumbele ni kwenda kuzika familia askari wetu kama hiki sio kipaumbele. Kwa hiyo, nazungumza leo kwa uchungu kabisa katika Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika *Vote 28 subvote* 2005 ya Zanzibar nimeona kuna fedha pale za *maintenance and repair of building* kwamba imewekwa ni milioni 22. Fedha hizi haziwezi kutosha kwa kufanya hili jambo. Kwa hiyo, naomba Waziri atakapokuja hapa aje anipe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetajwa katika ukurasa wa tisa wa hotuba ya Waziri miradi ya ujenzi mpya wa nyumba za polisi. Tuliahidiwa tutajengewa nyumba 423 mwaka juzi kukawekwa na bajeti, mwaka jana hakukuwekwa bajeti, mwaka jana kuliwekwa milioni 200 kukarabati kituo cha Mkokotoni, mwaka huu nimeangalia kwenye *development* hakuna lakini tunaambiya kuna bilioni 10 ya Mheshimiwa Rais itatokea kwenye bajeti gani, kwanza nataka niambiwe hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zitajengwa nyumba 400, tulikuwa tunataka tuambiwe kwa Mjini zitakuja ngapi, kila siku unatajwa ujenzi lakini haziji fedha. Sasa na hili vipi tunataka Mheshimiwa Waziri waje watuambie ukweli wanaposema hapa tunayapeleka majimboni kwetu na mimi naishi na askari kule au hawataki nirudi mwenzao hapa. Hakuna jambo hata moja nililotekelzewa tokea mwaka wa kwanza nakuja hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Ziwani Polisi kuna hospitali, kwa nini tusiipelekee *ambulance* kama inavyokuwa kwa majeshi, ikitokea dharura ya kuhamisha mgonjwa pale tunafanya nini? Ziwani Polisi wamejenga kituo cha afya kipo kinaendelea kama hospitali nyingine katika kambi lakini

katika kituo hiki cha afya wamejenga *maternity* pale mradi ule haujaisha. Kwa hiyo, je, hapa tunafanya nini katika kuwa-*support* kwenye hii? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie jambo ambalo amelizingumzia Mheshimiwa Khatib, kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya (*The Society Ordinance*) ya mwaka 1954, Wizara ya Mambo ya Ndani ndiyo ambayo inatakiwa kuwa na usimamizi wa jumuiya hizi za kidini. Sasa hapa kifungu kinataka kuteuliwa kwa Msajili wa Jumuiya, msajili huyu hajateuliwa, watu sasa hivi wanafanya hayo mambo chini ya kitengo cha sheria cha polisi, kwa hiyo kifanyike hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara inao uwezo wa kupendekeza hilo jina la Msajili likateuliwa lakini pamoja na kuanzisha Ofisi ya Msajili. Kwa hiyo, hili linatakiwa pia nalo lifanyike. Mheshimiwa Waziri amshauri Mheshimiwa Rais amchague Msajili wa mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu umeme, askari wanalipa wenyewe umeme. Bajeti iliyopita ya mwaka 2016/2017, ilikuwa *actual* milioni 74 zilizoenda Zanzibar zimeshushwa sasa hivi milioni 24, je, matumizi ya umeme yamepungua? Mwaka jana zimebekwa milioni 24, mwaka huu milioni 24. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje aweke sawa katika suala hili, sisi tunapokea malalamiko ya askari polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan King. Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo, baadaye Mwantumu Dau Haji ajiandae.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kunipa nafasi nichangie katika hotuba iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ama kweli baniani mbaya kiatu chake dawa, Jeshi la Polisi wanalaumiwa lakini wanafanya kazi nzuri sana kwa sababu nasema kama polisi wasingekuwepo hali ingekuwaje? Usipomchokoza polisi hawezi kuhangaika na wewe, ukiona polisi wanashughulika na wewe ujue kwamba kuna kitu umekifanya kwamba umeenda kinyume na utaratibu na kinyume cha sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya, wote tupo salama siku zote za maisha yetu kwa sababu ya Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Njombe bado Serikali hajalitendewa haki vizuri, Jeshi la Polisi hawajatendewa haki vizuri kwa sababu Njombe ni mkoa toka mwaka 2013 lakini mpaka leo hawajajengewa jengo la polisi la mkoa, hakuna Ofisi ya *RPC*, hakuna nyumba za polisi, polisi wale wa Njombe wanafanya kazi vizuri lakini hawana makazi. Polisi 400 vijana hawana makazi, hakuna nyumba hata moja ya polisi Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki nakiona kwamba hatuwatendei haki askari wetu na wakati mwingine tunaweza tukawalaumu polisi kwamba hawatimizi wajibu wao vizuri, lakini wakati mwingine pengine wanapata na msongo kutokana na mazingira ya kazi wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kituo cha Polisi Njombe nafikiri Mheshimiwa Waziri alifika alikiona, kile kituo nadhani ni cha mkoloni nimezaliwa nimekikuta. Kile kituo kwanza kipo ndani ya mita 30 za barabara halafu ni kichakavu sana. *RPC* wa Njombe kila siku anabomoa kaukuta angalau aongeze apate chumba cha kumtosha kufanya kazi. Kwa kweli hadhi ya polisi kwa Njombe bado haijawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Jeshi la Polisi Njombe waangalie kwa namna gani wanaweza wakasaidia

kama Wizara na kama Serikali kuona kwamba Jeshi la Polisi linakuwa na jengo lake, linakuwa na ofisi nzuri na wanaweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza; kwanza kabisa katika Mkoa wa Njombe Magereza Mkoa haijafiki. Maafisa wa Magereza Njombe wakihitaji mahitaji yao ya kiofisa ni lazima waende Iringa. Sasa je tukubaliane hapa kimsingi kwamba Magereza wamegoma kuja Njombe ama wanakuja? Nami kama wananiambia wamegoma nipo tayari kumwambiwa mwenye nchi kwamba magereza wamegoma kuja Njombe. Tunahitaji watu wa magereza waje Njombe ili kusudi shughuli zinazohusiana na Jeshi la Magereza ziweze kufanyika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Magereza Njombe wanafanya kazi nzuri sana, tarehe 2, nakumbuka illkuwa Jumatatu ya Pasaka nilitembelea Magereza Njombe, niliongea na wafungwa, niliangalia makazi yao, lipo tatizo moja tu la msongamano lakini wafungwa wenyewe kwa maneno yao walitamka kwamba wanalelewa vizuri na wanatunzwa vizuri. Nilitembelea vyumba vyao viro vizuri na wanasesma kwamba maisha pale, ukiacha kwamba wao ni wafungwa na mahabusu lakini maisha ni mazuri na wanatendewa haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika nikamweleza Mheshimiwa Waziri, lakini nilipata fursa ya kuuliza swali hapa na nikawa na mahabusu mmoja pale alikuwa anaumwa, namshukuru sana alichukua hatua haraka na mahabusu yule ametibiiwa. Tatizo kubwa la Magereza Njombe ni uchakavu na msongamano, lakini msongamano huu unatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa msongamano unasababishwa na kesi zisizokwisha mahakamani na upelelezi ambao haukamiliki. Kwa hiyo, ni kati ya Jeshi la Magereza na polisi kwa maana kwamba polisi hawapelelezi kesi kwa wakati na magereza wanashindwa kuwatunza wale mahabusu vizuri kwa sababu ya nafasi ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalojitokeza ni kwamba Magereza Njombe wana maeneo ya mashamba, maeneo yale hayatumiki, yamekuwa mapori kwa miaka mingi sana. Niombe sana Jeshi la Magereza hebu waone ni kwa namna gani wanaweza wakayatumia yale maeneo, vinginevyo sisi kama wananchi wa Njombe tutayavamia yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi katika matumizi ya ardhi ni kwamba sisi tukivamia ardhi ile tukiiilima wasije wakatulaumu, lakini ni wajibu wao kuhakikisha kwamba Magereza Njombe wanalima mashamba yale na wanayaafanya kazi ili kusudi tuondokane na mapori hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nillilliona pale Magereza Njombe pamoja na uzuri nilliouona ndani ya gereza, usafi na mazingira ya ndani ni kwamba yule afisa magereza anakaimu. Mheshimiwa Waziri hebu angalieni kwa nini yule anaonekana msomi na anamudu kazi vizuri, kwa nini aendelee kukaimu siku zote hizo kwa sababu inamsababisha anashidwa kutoa maamuzi kwa sababu ya kukaimu. Niombe sana walialangalie hilo kiutumishi waone namna gani wafanye. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uhamiaji haramu, nimeenda Gereza la Njombe nimekuta pale kuna watu wa Ethiopia 15 walikamatwa wakapelekwa mahakamani, wamehukumiwa wamemaliza kifungo lakini bado wapo gerezani, sababu wanasesma hawajasafirishwa. Gereza lile ni dogo wanasesababisha msongamano, halafu kesi imekwisha bado wanaendelea kuwepo gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niombe kama utaratibu wetu sisi ni kuwakamata hawa wanaoitwa wahamiaji haramu, basi tuangalie utaratibu mwengine wa kufanya, kwa sababu naamini kama tunaweza tukawakamata, kama tumewakuta kwenye lori tunamwambia dereva wa hilo lori, nyuma geuka, mbele tembea, rudi ulipotoka, kuliko anaenda kukamatwa

Njombe anakaa Magereza ya Njombe anahukumiwa, matokeo yake anasabisha msongamano katika Gereza la Njombe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya naona yapo sehemu nyingi sana katika nchi yetu kwamba Jeshi la Magereza linapata tabu kutunza hawa wahamiaji haramu. Kama ni watu wanaopita njia tu tuangalie sheria zimekaaje; kama inawezekana kuwasindikiza wakamaliza msafara wao tuwasindikize wavuke waende wanapokwenda kuliko tunaendelea kubabaika nao hapa. Kwanza wanakula sembe yetu ya bure, hawatakiwi kwenda kazini tumewapeleka mahakamani, tunatumia nguvu zetu nyingi kuwatunza bila hata sababu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliombe sana Jeshi la Uhamiaji waweze kuangalia hili jambo na Serikali iliangalie kwa umakini ili kusudi hawa waweze kurudi kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la usalama barabarani, tunashukuru sana Askari wa Usalama Barabarani wanafanya kazi vizuri lakini wapo mionganini mwao hawafanyi kazi vizuri. Askari wa usalama barabarani wamegeuza kile kitengo kwamba ni sehemu ya kipato, wananyanyasa sana vijana wa bodaboda na maaskari wa usalama barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeshatokea mahali pengine unakuta askari wa usalama barabarani amesimamisha gari katikati ya barabara halafu amefungua milango wa gari ili kusudi yule kijana asimame kwa ghafla au aingie porini ili amkamate, kuna sababu gani? Kwa sababu bodaboda zote zinajulikana ni za wapi, haiwezekani bodaboda ikawa inatoka Tabora kuja Dodoma haiwezekani. Kama ni bodaboda ya hapa Dodoma ni ya Dodoma na kama ni ya Njombe ni ya Njombe. Naomba vijana hawa waangaliwe, kama wana makosa basi wakamatwe kwa utaratibu wa ukamataji; wapo askari ambao kwa kweli ukamataji wao hauridhishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana tuwasaidie sana askari, tuwaelimishe vizuri ili kusudi ukamataji wao uweze kuwa ni ukamataji ambao unaweza ukamsaidia hata yule unayemkamata ajue ana kosa gani kuliko unapofungua milango ya gari halafu unataka mwenye bodaboda ajigonge kwenye milango ya gari au aingie porini ili umkamate, kwa hiyo ukamati huo sio ukamataji sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa muda. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwalongo. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwantumu Dau na Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pia nlmshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya kwa wakati huu na pindi hizi kusimama katika Bunge hili Tukufu ili kuichangia Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu wake kwa kazi zao nzuri wanazozifanya na kuzitekeleza katika masuala yao ya utendaji wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kuhusu suala la hali ya usalama barabarani, hali ya usalama barabarani ni nzuri na niwapongeze sana maaskari wetu wanafanya kazi nzuri, wanajitahidi kuifanya kazi hii ya barabarani lakini kuna suala la barabarani la kuhusu yale mataa. Katika vile vitengo vya mataa pale wananchi wanakuwa wanakasirika sana baadhi yao madereva. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taa zile zimebekwa pale ili kupitisha zile gari lakini askari wanatoka wanakwenda kusimama pale kuzipeleka zile gari kwa mikono na kasi, imekuwa wanaungana msururu mkubwa sana huku wa magari na muda mrefu sana watu wanapeleka wakati zile taa pale zipo zina kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Waziri kwamba lile suala walizingatie kwa kina wale askari. Hatutaki kwamba wasiwepo, wawepo maana wapo kwenye kutengeneza suala la usalama lakini wanapokuwepo pale wakae pembedi wangalie zile gari na zile taa zinazopitisha; kuna taa kijani, nyekundu lazima utajua hii nyekundu sasa hivi kule siendi lakini hii kijani ni yangu mimi lakini ndio ataposimama kuleta zaidi msongamano wa magari katika sehemu hiyo ya mataa barabarani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu mradi wa ujenzi wa majengo na vituo vya polisi. Nilizungumzia suala hili hapa katika Bunge hili Tukufu, nikalizungumzia suala la vituo vya polisi ambavyo havina hadhi na mpaka hivi sasa bado vituo havijawa na hadhi hasa katika Mkoa wa Kusini Unguja. Mkoa wa Kusini ni mkoa mama, Mkoa wa Kusini unajulikana kila kitu kwamba ule mkoa ni mkoa wa utalii lakini vituo vya polisi bado havijawa na hadhi na hili nililiomba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tena hii Wizara ya Mambo ya Ndani kwamba Mheshimiwa Waziri anasikia na Mheshimiwa Naibu Waziri nimshukuru kwamba alitembelea huu Mkoa wa Kusini lakini alikwenda akatembelea kuhusu suala la madawa ya kulevyo, vile vituo navyo pia kaviona, hali ni mbaya. Vituo vya Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini sio vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kusini kituo cha Paje bado hakijawa kituo na pale ukatarajia ni msafara mkubwa sana wa gari zinazokwenda kwenye suala la utalii. Wilaya ya Kati Jimbo la Chwaka kituo chao cha polisi wamejitatihidi, niwapongeze. Wamejenga kwa nguvu zao wenyewe, hawakusaidiwa na Serikali wala na mtu. Kituo kipo kizuri, kinang'ara na hivi sasa hivi kinafanya kazi kituo kile, hakina wasiwasi. Akamatwe mwanamke kama hivi apelekwe mahabusu basi chumba chake kawekewa maalum cha kwenda kuhifadhiwa, Kituo cha Polisi kile cha Chwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nishukuru kwamba Kituo cha Polisi cha Makunduchi tayari sasa hivi kimeweka *foundation*, nishukuru. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri kwamba vituo hivi nilivyovitaja hapa ajitahidi katika kuviedesha na katika kutekeleza huu mpango wao waliouweka wa kuhusu utengenezaji wa vituo hivi vya kwenye mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nizungumzie kuhusu uboreshaji wa maslahi ya askari, maslahi ya askari bado hayajawa moja kwa moja mazuri, yanatoka lakini kuna askari ambao wanapandishwa vyeo, mfano koplo au *sergeant*, koplo yule anayepandishwa cheo kwenda u-*sergeant* basi bado maslahi yao yanakuwa yameganda kwenye ule ukoplo, hawajapata maslahi yao mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala nililileta mpaka kwenye swalii langu la msingi, lakini bado sikuwa nimejibowi lolote mpaka sasa hivi. Naomba sasa nilizungumzie hili suala, kwamba maslahi ya polisi wale ambao walikuwa wamepandishwa vyeo, u-*sergeant* na ukoplo, wafanyiwe haraka maslahi yao wanapopandishwa vyeo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na mengi, nizungumzie hayo ambayo nimeyaweka ndani ya nafasi yangu na ndani ya moyo wangu kwamba niyatoe leo hapa katika Bunge lako Tukufu, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima na baadaye Mheshimiwa Innocent Bilakwate ajiandae.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana. Kabla sijaanza kuchangia nitoe tu ushauri wa jumla, tunapozungumza hapa kwa hisia kali kumkosoa Rais,

tunashauriwa sisi Wabunge wa CCM mwambieni Rais awe anakosolewa. Ndugu zangu, hata kwenye familia zetu kuna wakuu wa familia, hivi huwa tunawatukana wale wakuu wa koo zetu? Tukitaka kuzungumza na wale wakuu wa koo zetu au wakuu wa familia zetu, huwa tunawaijibu tunawatukana? Tunaongea nao taratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu, naomba nishauri kwa nia njema kabisa; Rais ni Rais tu, ni mamlaka ambayo amepewa kwa mujibu wa Katiba, kwa hiyo lazima tumheshimu, lazima tufahamu kwamba waligombea wengi lakini Mungu alimpanga yeye awe Rais wa Tanzania. Kwa hiyo, tunapokuwa tunasimama jazba zetu kidogo tuwe tunazishusha chini halafu tunajua huyu ndiye Rais wetu, tupende tusipende tayari Mungu ameshamtukuza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nianze kuchangia. Kwanza nimpongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya katika Wizara hii, lakini pia nimpongeze ndugu yangu *IGP* kwa kazi nzuri anazofanya, kwenye mazuri hapakosi kasoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizzungumze kasoro, hususani katika Jimbo langu la Kigoma Kusini, Idara ya Polisi, *Vote* 28, nilikuwa naangalia kwenye *Vote* hii 28 naona mikoa mingine imetengewa pesa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za maaskari wa ofisi za ma-*OCD*, lakini nimwombe sana Mheshimiwa Waziri; amekuja Kigoma ameona hali halisi ya maaskari, niombe sana kwa nini hawatotai upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Uvinza ni wilaya mpya, ina miaka sita sasa lakini *OCD* hana nyumba, *OCD* hana ofisi, hana gari, katika mazingira kama yale anafanyaje kazi? Naomba sana, nimeona wametenga magari lakini hakuna gari hata moja kwenye wilaya, gari ambalo tumepewa Halmashauri ya Uvinza ni gari lilitokuwa linatumika kwenye Ofisi ya *RPC*. Hata hivyo, tunavyoongea leo hii hata

pakitokea matukio ya ujambazi *OCD* lazima aombe gari mkoani ndiyo afanye kazi katika eneo lake la kazi. Niombe sana hebu wajaribu kumwangalia *OCD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za maaskari; maaskari wetu wanaishi uraiani, tunawatumwa waende wakakamate wahalifu; wanakamata vipi wahalifu wakati wanaishi nao uraiani? Kwa hiyo, kwenye bajeti ijayo wajaribu kuangalia watenge pesa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za maaskari jamani, wana maisha magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nichangie kuhusu Magereza, tunalo Gereza la llagala, gereza hili limechukua maeneo makubwa ya wananchi wa eneo la llagala. Mheshimiwa Waziri alikuja tukafanya kikao akatoa maelekezo tuhakiki mipaka ya wananchi na mipaka ya gereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki ule umeonesha ni dhahiri kabisa kwamba gereza wamehodhi maeneo ya wananchi. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, hebu tufikie mwisho. Wamechukua eneo kubwa karibu ekari 5,000, kwa nini wasitoe hata ekari 2,500 zirudi kwa wananchi na zile 2,500 tuwaachie wao waendeleze na masuala mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwa harakaharaka kwa sababu nataka nisimame sana kwenye Uhamiaji. Katika uhamiaji tuna kero kubwa sana na uhamiaji ndani ya Mkoa wa Kigoma. Katika Tanzania hii sio Kigoma peke yake ambayo inapakana na nchi za jirani, hata Arusha wanapakana na Kenya, ukienda Mtwara wanapakana na Msumbiji, lakini ukienda Kagera wanapakana na Rwanda. Leo wananchi wa Kigoma hatuishi na amani, kutwa kucha tunaitwa Banyamurenge, tunaitwa Wakongo, tunaitwa Warundi, roho zinatuumwa sana sisi watu wa Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, roho zinatuumwa kwa sababu unaposikia wananchi wanavamiwa saa nane za usiku, hivi

tujulize, saa nane za usiku operesheni za kwenda kuvunja milango kwenda kukamata raia. Nane usiku wote tunafahamu sisi wanawake humu ndani, mwanamke saa nane usiku ndio anatafuta namna ya kujaza nyumba. Leo saa nane usiku watu wanabomolewa milango, inauma, naongea kama mwanamke, inaniuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapigiwa simu Mheshimiwa Mbunge tunavamiwa saa tisa, sasa hawa watu wakiwavamiamia mwisho jamani wanaume wetu wale watashindwa kusimamisha mambo vizuri. Hii haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa uchungu. Operesheni zinazofanywa ndani ya Mkoa wa Kigoma sio sahihi, ile Kigoma ni Tanzania, wananchi waliopo ndani ya Wilaya za Kigoma ni Watanzania, leo tukisimama hapa tumechaguliwa kwa sababu ni Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe, najua kwamba Mkurugenzi wa Uhamiaji ni mwanamke, hali ya uhamiaji ndani ya Mkoa wa Kigoma ni mbaya ndugu zangu, lazima ifike mahali tuambiane ukweli. Abiria wa kutoka Mkoa wa Kigoma wanapanda basi saa 11.30 alfajiri, wakifika Uvinza mabasi yanasmamishwa wanateremshwa wote wanaanza kuambiwa wewe shuka tuone uraia wako, mbona maeneo mengine hawafanyi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshalalamika, nimeshaongea mpaka na Mkurugenzi wa Uhamiaji. Kwenye bajeti ya mwaka jana nilimwomba Mkurugenzi wa Uhamiaji pale nje kwamba hali ya operesheni zisizokuwa na ubinadamu hatuzitaki ndani ya Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma ni wa Tanzania, kama tunaongea lugha moja na Warundi isiwe sababu, ule ni Mkoa wa Waha, ni Mkoa wa Wamanyema lakini sio mkoa wa kusema sio wa Tanzania; nimeongea kwa jazba kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NIDA*, zoezi la vitambulisho vya uraia Tanzania linaendelea katika Mkoa wa Kigoma, lakini

cha kunisikitisha, wanaambiwa watoe pesa Sh.15,000 ndiyo waweze kuandikishwa. Hivi hili zoezi la nchi nzima mbona hatukusikia watu wanaambiwa watoe hela; kwa nini sisi kule wanaambiwa watoe hela?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mambo yanayoendelea ndani ya Mkoa wa Kigoma, kama sisi tusipowasemea hawana mtu mwingine wa kuwasemea. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, hebu ajaribu kuwasiliana na idara husika, huu uonevu unaofanyika katika Mkoa wa Kigoma hatuwezi kukubaliana nao; tunajua yeye ni mchapakazi, tunajua ni msikivu na mimi binafsi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hasna. Tunaendelea na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na baadaye Mheshimiwa Anatropia Theonest na Pascal Haonga wajilandae kwa dakika tano, tano.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara hii muhimu. Kwanza nimpongeze Waziri Mwigulu kwa kazi nzuri anayoifanya. Lakini pia nilipongeze na Jeshi la Polisi, wanafanya kazi nzuri. Naamini Taifa hili limetulia kwa sababu ya mchango mkubwa wa Jeshi la Polisi, kwa hiyo, tunawapongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria na mtu yeote anayetaka kuishi kwenye Taifa letu kwa amani, kwa furaha, lazima afuate sheria za nchi hii, vinginevyo Jeshi letu la Polisi fanyeni kazi kwa mujibu wa sheria, washughulikieni wote ambao wanaenda kinyume na sheria ya nchi hii. Katika hili haijalishi ni kiongozi wa dini, haijalishi ni kiongozi wa kisiasa, hebu washughulikieni, Taifa

hili lina amani kwa sababu wanafanya kazi nzuri na hizi kelele zinazopigwa zisije zikawatisha wakaacha kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunawaunga mkono na naamini mtu ambaye ametulia kwenye Taifa anaafuata sheria, hawesi kusumbuliwa wala kubugudhiwa kwa namna yoyote. Wewe ukiona unasumbuliwa ujue una shida, ukiona wanavamia kwako, mara unalala magereza, mara unalala ndani, ujue una shida, fuata sheria uishi kwa furaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengi ambao wanajidai kumtaja Mungu lakini maandiko yanasema katika Tito, kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu. Kama unataka Mheshimiwa Rais afanye kazi vizuri pamoja na wewe mtii kwa sababu huyo ameletwa na Mungu na maandiko yanasema hivi, hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu hata hiyo iliyopo imeamuliwa na Mungu. (*Makofi*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unataka kuishi kwa imani...

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Itii hiyo mamlaka; ujumbe umefika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Godbless Lema, naomba ukae chini.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipewa taarifa ukakubali, nataka nimsaidie.

MWENYEKITI: Hapana Mheshimiwa Lema, naomba ukae chini.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kulisemea Jeshi letu la Polisi kwa upande wa Kyerwa. Nimwombe sana Mheshimiwa Mwigulu na watendaji wote wa Mambo ya Ndani, kwa kweli Jeshi letu la Polisi Kyerwa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, hawana kituo cha polisi, wanafanya kazi kwenye ofisi ya kata ambayo ofisi yenye hali yake ni mbaya. Kwa hiyo, niombe polisi wetu hawa ambao wanafanya kazi kwenye maeneo ya mipakani wapewe vitendea kazi lakini wapewe ofisi ambayo inafanana na hadhi ya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo ambazo nimewapa polisi, upo upungufu ambao naamini kila binadamu anao upungufu; hivyo tunashauriana, tunarekebishana, tunasonga mbele. Kwa upande wa bodaboda niwaombe sana Jeshi la Polisi; mazingira, namna ambavyo wanaendesha hawa vijana wetu wa bodaboda kwa kweli haipendezi. Kwa upande wetu kule Kyerwa bodaboda wakati mwingine wanakimbizwa mpaka kwenye migomba, wakati mwingine wanapata ajali, kwa hiyo, niwaombe sana polisi hili mliangalie tusije tukaanza kusema mambo mengine makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Magereza kuna eneo ambalo Magereza walichukua pale Kyerwa na wakawaahidi wananchi kuwapa fidia. Wananchi hawa bado hawajafidiwa na wanasubiri kwa muda mrefu na maeneo yao wamezuiwa wasiyaendeleze. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Mwigulu hili aliangalie na walismamie ili wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa waweze kupewa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niongelee upande wa uandikishaji unaoendelea. Kule kwenye Jimbo langu la Kyerwa wananchi wangu wengi unakuta unapomhoji saa mbili, tatu kwa Kiswahili inakuwa ni shida. Sasa kwenye mahojiano yale unakuta wanapowahoji wananchi mwingine anaposhindwa kujibu maswali mawili matatu kwa Kiswahili wanaanza kusema huyu ni mhamiaji haramu. Kwa hiyo, niombe sana hili waliangalie ili uandikishaji huu uweze kufanyika vizuri na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilisemee, Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukipita sana eneo la Mikese na eneo lile kituo cha polisi mara nyingi tunapata ajali, tunakuwa na matatizo mbalimbali. Hebu nimwombe Mheshimiwa Mwigulu, kile kituo cha polisi kipewe vitendea kazi, wana gari moja ambalo haliwasaidii. Kwa hiyo, niombe sana kile kituo Waheshimiwa Wabunge wengi tumekuwa tukipata msaada pale, kwa hiyo na chenyewe wakikumbuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru na niendelee kusema Mheshimiwa Mwigulu asonge mbele, Rais wetu anafanya kazi nzuri, hebu wamuunge mkono na Jeshi letu la Polisi kazi kubwa waliyoifanya Kibiti imedhihirisha Jeshi la Polisi wanafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Bilakwate. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Anatropia kwa dakika tano.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitaanza mchango wangu kwa kum-quote Nelson Mandela, muda wangu ni mchache sana, amesema; *I learned that courage was not the absence of fear, but the triumph over it. The brave man is not he who does not feel afraid, but he who conquers that fear.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusemaje; tumefika hapa au tunalazimishwa kufika mnakotaka tufike sio kwa sababu hatuogopi, kwa sababu tunalazimishwa kutokuogopa tena. Humu ndani sisi Wabunge wa Upinzani nakumbuka ndio tulikuwa mstari wa mbele kuwatetea polisi, kutetea makazi yao, kutetea matatizo yao, lakini nini kimetokea; polisi wametufikisha hapa, polisi tulikuwa tunawapenda sana na tunawapenda lakini mnakokwenda baba mmepotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upolisi ni taaluma na kama walipenda kuwa wanasiasa wangekwenda kugombea kama tulivyofanya sisi. Tunaamini wao ndio wanapaswa kututetea, tunaamini watu ni lazima wajione wako salama mikononi mwa polisi, lakini leo nini kinatokea; ukikamatwa na polisi huna uhakika kama utatoka salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Saguta Heche anakufa akiwa amefungwa pingu mikononi mwa polisi, Akwilina mtoto wa watu akisafiri kwenye daladala, anashutiwa na kufa na polisi na tunakuja kuambiwa hatujaweza kumtambua nani polisi kamuua kwa hiyo faili limefungwa. Mnatiupeleka wapi ninyi watu? Tunawapa fedha kutoka kwenye kodi ya nchi hii, polisi tunawapenda lakini mlikotufikisha siko tulikokutamani. Narudia kusema tunaamua kuwa *courageous* sio kwa sababu sisi sio waoga ila kwa sababu mmetulazimisha kufika hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *case study* ya polisi mmoja ambaye alimvamia mtu wangu wa karibu na Mheshimiwa Waziri nilimpigia simu nikakwambia mume wangu amekuwa *attacked* na polisi anayenifahamu mimi, anaishi kwenye mtaa wangu, yule polisi amemwonea yule baba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa taarifa kwenye kituo kikuu cha polisi, nimekwenda mbali zaidi nimekwenda hata kwa Mnadhimu wa Polisi, bw. Matiko *Central*, barua ninazo hapa, tangu 2017 hakuna kitu kilichofanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona, uozo wa polisi wanaouona chini ni kutoka chini mpaka juu. Kama kiongozi mdogo, afisa wa polisi amekosea, unakwenda kwa bosi wake amrekebishe, unakwenda kwa Waziri, Waziri alinipa pole, lakini pole inasaidia nini kama tunawaacha wale vijana wanazidi ku-*harass* watu wasiokuwa na hatia mtaani kwa sababu tu alikuwa kwenye bodaboda na walikuwa hawajavaa *helmets*. Ni kazi ya polisi kukamata na kupiga watu kwa sababu hawajavaa *helmets?* Come on guys! Come on guys! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niambieni kama Polisi wetu hawaelewi miiko na kazi yao kutokana na maandishi yao na vitabu vyao vya PGO's naomba muwafundishe. Walipotufikisha ndio maana tunaongea haya yote, siyo kwa sababu hatuwapendi, ni kwa sababu wameondoka wenye msingi. Turudi kwenye masuala mazima ya maadili ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunajua tunapokuja hapa tunachopaswa kuongelea ni weledi wa Jeshi la Polisi, ni namna gani linafanya kazi, ni namna gani inatumia kodi tunazowapatia na ni namna gani *in-a-deal* na raia? *Those are the things you must be talking here.* Hatupaswi kuwasifia, kufanya kazi ni wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunachokitaka ni kuangalia makandokando yao na namna gani tunaweza kuwarekebisha kwenda mbele. Wamegeuka wanasiasa, wamegeuka wapiga debe wa Chama cha Mapinduzi. Nani hataki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwaambia Jeshi la Polisi, sisi tukiingia madarakani, tunawahitaji, tutawatumia wao. Hata hivyo, hatutaki watupe *favour* sisi dhidi yenu ninyi, tunaka wasimame katika kama *referee.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kusema, mmomonyoko mkubwa wa maadili ya Jeshi la Poilisi nau-*associate* na kumhujumu Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba. Naamini pengine hawamtaki Mheshimiwa Nchemba. Ni kwa nini tunaona Jeshi la Polisi wanafanya mambo ambayo hatujawahi kuyasikia katika historia ya Taifa hili? Pengine Mheshimiwa Waziri labda ukijiuzulu tunaweza tukapona. Wewe unaonaje? Pengine ukijiuzulu tutaweza kupona. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nam-*quote* Che Guevara, aliwahi kusema: "*If you tremble with indignation at every injustice then your comrade of mine.*" Kama dhamira yako

Mheshimiwa Waziri inaguswa na matendo ya Jeshi la Polisi na Maafisa wa Jeshi la Polisi, tunataka tukuone ukichua hatua dhidi ya hao maharamia wanaochafua Jeshi la Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia. Mheshimiwa Haonga, baadaye Mheshimiwa Mwita Waitara ajiandae.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, lakini kabla sijaendelea, naomba nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Sugu ambaye yuko ndani kwa sababu ya uonevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pole hiyo, pia akitoka Mheshimiwa Sugu nitakuja kumpa pongezi kwa sababu tunajua hata Mandela naye amewahi kuitia hatua kama hiyo na naamini kwamba yeze ndio atakuwa Mandela wa Tanzania huko mbeleni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya ndani na naomba nianze na kusoma Ibara ya (14) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria." (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea mauaji yanayofanywa na baadhi ya Maaskari wetu, Maaskari ambao tumewasomesha kwa kodi zetu, Maaskari ambao hatujui kitu gani, either kwa maagizo kama wanavyosema yametoka juu. Mauaji haya yanasisitisha sana na yanavunja Ibara ya (14) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu, Mheshimiwa Anatropia amezungumza vizuri sana. Ameuawa ndugu yetu Suguta Chacha Heche; amekamatwa, amepigwa pingi, anachomwa kisu na Askari. Inasikitisha sana na inatia huzuni sana. Ameuawa Aqualina, lakini kuna Maaskari walikamatwa

kama sita hivi. Hao Maaskari wako wapi? Leo anakuja DPP anasema kwamba hao Maaskari; yaani leo tunaambwa kwamba hilo shauri limeshafungwa wakati Maaskari sita walikuwa wamekamatwa tangu awali, hatujui Maaskari hao wamepelekwa wapi; na hatujui kesi imekuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Comredi Mwigulu Nchemba. Nimwambie ukweli wanaompongeza wanamharibu na wanaompongeza hawamtakii mema. Namshauri jambo moja tu, kujuzulu Uwaziri wa Mambo ya Ndani. Namshauri *pia IGP pia aweze kujuzulu*. Siyo dhambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushe kitu kimoja. Kuna watu hawakumbuki historia ya Taifa letu. Mheshimiwa Mwinyi, Rais Mstaafu amewahi kujuzulu miaka ya 70 kwa sababu ya wale wafungwa kule Shinyanga walifariki gerezani akajiuzulu na baadaye akaja kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kujuzulu haimaanishi kwamba wewe umetenda dhambi, lakini watu wa chini yako maana yake hawaendi sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mwingine inaitwa Meja Jenerali Abddallah Said Natepe, ambaye alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Alijiuzulu kwa sababu kuna watu walikuwa Magerezani, walikuwa wanatuhumiwa; walifungwa kwa kesi ya uhaini, wakatoroka. Walipotoroka, akaamua kujuzulu kulinda heshima yake, lakini pia kuchukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Comredi Mwigulu Nchemba amekaa hapo kwenye kiti hicho, sikutegemea kama angeweza kuwepo hata dakika tano hadi sasa kwa sababu kilichotokea kwenye Wizara yake ni madudu; ni takataka. Anachong'ang'ania sijajua ni kitu gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo kama kuna watu wanauawa, kuna watu leo wanatekwa, kuna watu

wamepotea kwenye nchi hii, Beni Saanane hatui yuko wapi hadi leo, ni mwaka mmoja na nusu; Azori Gwanda. Nasi hatuwatetei CHADEMA tu, tunawatetea na wengine. Azori Gwanda alikuwa ni Mwandishi wa Habari. Yule Diwani wa Kibondo kule alikuwa ni mtu wa CCM. Sisi tunawatetea wote ndugu zangu, hatuwatetei CHADEMA tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba hiyo nafasi, hicho kiatu kimempwaya. Nadhani angweza kuondoka kwa sababu nafasi haiwezi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua yeye alikuwa ni mionganoni mwa watia nia kwenye Chama chake kwa nafasi ya Urais, nadhani ndoto za Urais zitakuwa zimeshaanza kuota mbawa kwa sababu madudu aliyofanya kwenye Wizara hii hayajawahi kufanywa hata mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja nyingine. Leo Magereza zinajaa, Mahabusu wako Magerezani, wafungwa wako Magerezani, siyo kwa sababu labda uovu umeongezeka.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Hapana ni kwa sababu kulikuwa na uonevu wa hali ya juu sana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzee mwenzangu taarifa!

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wanaonewa. Mheshimiwa Sugu kawekwa ndani kwa sababu ana uhuru wa kutoa maoni, ametoa maoni yake, leo amefungwa ndani miezi mitano. Uonevu wa namna hiyo hauwezi kuvumilika hata kidogo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwitwa Waitara dakika tano na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Polisi wamefanya kazi sana, ila wamefanya kazi vibaya sana. Kazi wamefanya, lakini wanafanya mbaya, ndiyo maana watu wanalamika. Ni muda tu mfupi lakini kwa kweli Wizara hii mambo ambayo yamefanyika ni mengi sana na mengi yake ni mabaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ndugu yangu, asikilize tunachokzungumza hapa. Inawezekana watu wanaingiza siasa katika mambo ya msingi katika maisha ya watu, ni bahati mbaya sana. Tunatarajia Mheshimiwa Mwigulu Nchemba atakapokuja hapa kuhitimisha hoja, aje atueleze zile *CCTV Camera* ambazo zilikuwa kwenye nyumba ambayo ndugu yake Mheshimiwa Lissu wa Singida alikuwa anaishi, nani allziondoa? (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pia aeleze upelelezi umefika wapi? Muhimu sana. Hili jambo halihitaji siasa. Huyu mtu amelalamika kwamba anafuatiliwa na magari, akataja mpaka namba ya simu, akataja hata namba ya gari. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba hajawahi kusimama hadharani na akawaeleza Watanzania, nani alikuwa na gari ile? Wale ni akina nani mpaka leo! Sidhani hata ndugu yake Mheshimiwa Lissu kama pole alimpaa. Sina hakika kama ametoa hiyo pole kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, yako mambo yanazungumzwa hapa; tumezungumza juzi, Mheshimiwa Heche amezungumza akaomba Mwongozo hapa kwenye Bunge hili, kwamba Mbunge anasema ametishiwa maisha. Hawa watu wanapiga simu, wakati mwингine wanaandika *message*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Polisi ukiandika maneno yenye ukakasi kwenye mitandao, unafuatiliwa popote ulipo, unawekwa ndani, kizuizini. Hawa ambaa

wanatuma *message* za kwamba "nitakushughulikia;" "nitakuonyesha;" "utanikoma;" kwa nini hawashughulikiwi? Mheshimiwa Heche alilalamika hapa Bungeni, lakini bahati mbaya naona haya mambo yamebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mwigulu Nchemba aseme, yule ndugu yake John Heche, Ndgu Chacha Suguta ambaye amezikwa leo, yule bwana amekamatwa na Polisi akapigwa pingu. Hapo ndipo watu wanahoji maadili ya Polisi. Hata kama sio wote, watu wanahoji inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi aliyefundishwa, ameenda Chuo cha Mafunzo kule Moshi au *elsewhere*, anamkamata mtuhumiwa aidha ana makosa au hana makosa; wala hata hakuua; au hata kama ni muuaji, Mahakama ndiyo ina wajibu wa kusema huyu ahukumiwe kiasi fulani au apewe adhabu gani. Anapigwaje kisu? Hiyo kauli ni lazima ichukuliwe kwa uzito wake katika Taifa hili na iwe fundisho na matukio mengine ambayo yanafafana na hayo. Hayo ni mambo ambayo kwa kweli yanahitaji kuangaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alizungumza kwamba kuna watu wanaokotwa kama jambo la kawaida. Hii hali ya watu kuamka asubuhi amekatwa mapanga kama yule wa Kilombero, kama dudu la mgomba, halafu watu wanaona, watu wanaokotwa kwenye mifuko ya *sulphate* kwenye kingo za bahari kama mambo ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya mnazoeza Watanzania mauaji, itafika mahali kuanza kuona siyo jambo la ajabu ajabu sana. Mwingine anasimama hapa mtu mzima kabisa anatwambia kwamba eti kwa sababu idadi ya Wapinzani ni chache kuliko ya CCM; *so what?* Yaani unahalalisha uhalifu kwa idadi ya watu, kitu ambacho hakikubaliki. Yaani mtu sikutarajia anaweza kuongea kitu cha namna hiyo ambacho kimsingi ni jambo ambayo haliruhusiwi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema, Polisi wamefundishwa. Polisi wanalipwa kodi ya Watanzania; Polisi viatu wanavyovaa ni kodi yetu, chakula chao ni nguvu yetu; nguo wanazovaa ni sisi; wafanye kazi kwa uadilifu, wafuate maadili yao. Hiyo ndiyo hoja ya msingi hapa. Hatusemi wamfuatilie mtu yejote yule. Kamata mtu yejote ambaye ana makosa yaliyothibitishwa apelekwe Mahakamani ahukumiwe. Siyo ku-*retain* watu katika *retention* kama ilivyo kwa wale Mashehe. Ni makosa makubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, hivi sisi tunachangisha kujenga Vituo vya Polisi; pale Chanika tumejenga. Hawa Polisi tunajenga pamoja nyumba na Vituo vya Polisi, hawana magari. Kwa nini magari ya washa washa yale msiyabadiishe yawe magari ya kufanya *patrol*/kwenye vituo vyetu ambako kuna kuna raia? Ujambazi unafanyika, hawana mafuta ya kufanya *patrol*, lakini magari ya washa washa yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ndugu yangu na mjukuu wangu, nilishangaa sana. Jeshi la Polisi nchi hii, ndugu yangu Sirro, kaka yangu wa kule Musoma, anafanya maandamano ya magari kwenye mikoa nchi nzima kwa Mange Kimambi? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani *they are not serious*, yaani mtu yuko Marekani, anaandika maneno kwenye mtandao, tutaandamana tarehe 26. Wamekamata vijana wetu nchi nzima, wanawapiga. Mange Kimbambi, kweli! Haki ya Mungu mimi nisingehangaika naye. Nilikuwa nawashangaa hapa Wabunge wa CCM kuwe na maandamano kwa hoja ipi? Nani anaandamana? Sisi tulikuwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kuandamana tutakaa vikao, tutaitishana, hakuna Mbunge wa Upinzani atabaki humu ndani. Tutakwambia weka barabarani majeshi, weka maji ya kuwasha, weka bunduki, piga risasi, ua unayeua, atakayebaki ataandamana. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani mnahitaji kutumia akili sana. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Natambua kwamba leo ni Siku ya Uhuru wa Vyombo vyta Habari duniani. Napenda kutumia fursa hii kuweza kuwakumbuka wale wote ambao waliweza kupoteza maisha kwa sababu ya kazi yao ya uandishi kama ndugu Mwangosi ambaye aliuawa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ndugu yetu Azori ambaye mpaka sasa hivi amepotea hatujui yuko wapi; na wengine wote Ansbert Ngurumo sasa hivi yuko uhamishoni kwa sababu ya shughuli ya Uandishi wa Habari na wengine wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuko kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani na nafikiri tumekuwa tukishuhudia baadhi ya Maafisa ndani ya Jeshi la Polisi, tena wakubwa kabisa wakisema maneno kinyume kabisa cha weledi unavyowataka ndani ya Jeshi la Polisi na hekima kabisa hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *wengi watakuwa wameshuhudia RPC wa Dodoma anaongea kabisa, anasema atawapiga raia kama mbwa koko. Sasa utashangaa, kama RPC anasema atapiga raia kama mbwa koko, mnashangaa nini Polisi kuua raia kituoni, Afisa wa kawaida, kama RPC anatamka hayo maneno? [Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafedhehesha sana kwamba Jeshi la Polisi ambalo kazi ni kulinda raia na mali zao, wamegeuka kuwaona raia kama mbwa koko ndani ya nchi yangu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha (32) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinawataka Jeshi la Polisi kumfikisha mtuhumiwa Mahakamani ndani ya saa 24. Tumeendelea kushuhudia Jeshi la Polisi ama kwa makusudi au kwa kile wanachokiita maagizo kutoka juu; na sijui ni juu wapi siku hizi kwenye Awamu hii ya Tano, kitu kikifanyika, tunasubiri maelekezo kutoka juu. Sijui ni sheria ipi ambayo wameitunga ambayo hajjaletwa Bungeni hapa kuthibishwa kwamba kuna maelekezo yanatakiwa yatoke juu ili Jeshi la Polisi litende kazi kwa mujibu wa weledi wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa Gerezani nilikutana na binti anaitwa Salma Ramadhani ambaye alifutiwa mashtaka yake baada ya kukaa miaka minne Gerezani na Mheshimiwa Hakimu Mwijage akatoa *ruling* kwamba huyo dada asikamatwe na wenzake watatu; lakini alivyotoka tu, akakamatwa baada ya siku mbili akarudishwa Kisitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule Hakimu Mwijage akasema, "nimesema huyu mtu asikamatwe mpaka apate kibali cha Mahakama Kuu." Polisi walimkamata akaenda na wenzake wakaa Kituo cha Kawe zaidi ya miezi nane ndani ya Kituo cha Kawe. Ukaguzi ukiwa unapita, wanawachukua wanakuja wanawaweza pale Kisitu, hawawaingizi ndani ya zile *chamber*, baadaye wanawarudisha. Hawa Watanzania ndani ya miezi nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hawa Maaskari ambao kuwaweka Watanzania zaidi ya miezi nane kituoni mpaka sasa hivi bado wako nao, watueleze hizi ni sheria za wapi? Ni mambo mengi sana yanatendeka kinyume. Nina muda mchache sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Magereza kuna wastaafu ambao wamestaafu mwaka 2017, mpaka leo hawajawalipa stahiki zao hata fedha za kubeba mizigo hawajawapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kuna magari 950 mwaka 2012 ambayo yaliidhinishwa kwamba yanunuliwe na yasambazwe nchi nzima kwa ajili ya kubebaa mahabusu kwenda Mahakamani. Mpaka leo hayo magari hayajulikani yameota mbawa za wapi. Sasa kwa sababu Awamu ya Tano mna-*fight* ujisadi, tunataka mliambie Bunge hili, hayo magari yameota mbawa za wapi? Kama yamenunuliwa, yako wapi? Maana yake tunashuhudia ndugu zetu ambao wako Magereza wanabebwa kwenye makarandinga kupelekwa Mahakamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda kuzungumzia kwa haraka haraka, tunaomba waweke vifaa vyta kisasa kuweza kuwakagua wale watu ambao wanaingia Magereza. Kinachofanyika sasa hivi ni udhalilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mwana mama anakuja anataka aingie gerezani, *ana-bleed* anaambiwa kama *ana-bleed* anabidi aruke kichurachura kumchunguza kama ana kitu ameweeka ndani au wanamwingiza mkono. Huu ni udhalilishaji, haukulaliki. Nunueni vifaa vyta kisasa vyta kuweza kuwapima na kujua kama ana kitu, *vina-detect*. Naomba wanunue vifaa vyta kisasa ambavyo ni vyta bei rahisi sana, wasidhalilishe Watanzania. Wanunue vifaa vyta kisasa waweze kufunga, waweze kukaguliwa wakati wanatoka na wakati wanataka kwenda Mahakamani na wakati wanaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Magereza imepitwa na wakati, tunaomba ifanyiwe marekebisho. Leo utashuhudia Askari Magereza ana *masters* lakini analipwa kama mtu wa *Form Four*. Pia kuna mengine mengi ambayo yanatendeka kwenye Jeshi la Magereza ambayo ni kinyume. Leo wafungwa hawa *uniform*. Unakuta wakati mwingine Askari anatoa jezi yake anampa mfungwa. Ni aibu! Wao

kama wamepeleka wafungwa, wawahudumie, hawana *uniform* kabisa. Wanawapa adhabu Maaskari Magereza. Unakuta eti mfungwa ameweke kilemba kimeandika tu "mfungwa" huku hana sare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba wanatumia nguvu nyingi sana, fedha za Watanzania maskini; wakati wa Ukuta ndiyo tuliona watu wanafanya *demonstration* na Askari, wakati wa Mange Kimambi tukaona watu wanafanya *demonstration* ya Askari wajulikane kama wanafanya mazoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiharibu fedha za Watanzania maskini kwa kutembeza Maaskari na magari ya washwa washwa, hizo fedha wapeleke kwenye mahospitali, hizo fedha wangezi-*convert* zingeweza kujenga shule. Watoto wanasoma 200 kwenye darasa moja. Leo anaweza akajitokeza mtu amekaa sijui Canada akasema anaanzisha maandamano Tanzania, halafu Serikali inakuwa iko tete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *tumeshuhudia matamko ya IGP, (Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)* tumeshuhudia matamko ya Mheshimiwa Waziri pale, tukamshuhudia Rais, tukamshuhudia Mkuu wa Majeshi, *just a single lady who is sitting in the USA*, wanawatetemesha, wanatumia rasilimali zetu vibaya. Wana hofu gani Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Muda wako umemalizika Mheshimiwa Esther. Katika mchango wake Mheshimiwa Esther ametaja Maafisa wawili akiwemo *IGP* na *RPC* wa Dodoma. Naomba maelezo hayo yafutwe kwenye *Hansard* kwa vile hatuwezi kumtaja mtu ambaye hatoweza kutoa utetezi wake ndani ya Bunge.

MBUNGE FULANI: Kwa sababu gani?

MWENYEKITI: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Rukia...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, huo siyo utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther naomba ukae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: *No, no, no!*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia naomba uendelee. Dakika tano.

(Hapa Baadhi ya Wabunge wallongea bila mpangilio)

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi jioni hii ya leo nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Jeshi la Polisi. Wakati mwingine Jeshi la Polisi wanakwenda tofauti na dhana ambayo tumeizoea. Jeshi la Polisi tunasema kama ni wanaolinda usalama wa raia na mali zao, lakini inakuwa ni tofauti kabisa na mambo wanayoyafanya, kwa sababu kuna baadhi ya Vituo vya Polisi unapokwenda, kauli wanazozitumia mtu anapokwenda pale ana tatizo, siyo nzuri. Kwa hiyo, tunaomba wajirekebishe. Hili nalisema nikiwa na ushahidi kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kituo kimoja cha Polisi Zanzibar, Kituo cha Mazizini. Mheshimiwa Waziri ananisikia na namwomba hili jambo alifanyie kazi. Hili illinitokea hata mimi mwenyewe binafsi nilikwenda pale. Ilikuwa ni kesi ndogo tu ya *traffic*, lakini nilipokwenda, huyo niliyemkuta, aliniuliza: "Mama wewe unahoji neno hili;" kwanza kauli alioitumia mimi kama mtu mzima siwezi kuitaja hapa. Kwa sababu mtu

mzima unapotukanwa, unapovuliwa nguo unatakiwa uchuchumae siyo unyanyuke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno aliyoyatumia kwa kweli ni kumkashifu mtu au kuwakashifu baadhi ya watu na pia ingeleta uchochezi ndani ya nchi. Kwa sababu mimi ni mtu mzima, sikutaka maneno yale niyarudie wala niyaseme hapa. *Finally, aliniambia "wewe mama unataka nikuheshimu au nikuvunjie heshima?" nikamwambia nitafurahi sana kama ukinivunja heshima, lakini bahati nzuri sana nafikiri baada ya kujiamini kumwambia vile aliogopa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema sitaki niwataje wala sitaki niongeze la ziada hapo, ila hiki Kituo cha Polisi Kimekaa kama ni kijiwe labda cha wacheza Keram au wavutaji wa bangi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri akifatalie sana kituo hiki. Hata baadhi ya majina ya hao Polisi waliopo pale, ni ya ajabu ajabu na yanaashiria shari kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema kama Jeshi la Polisi ni usalama wa raia na mali zao, lakini wakati inapotokea *operation*, kwa nini Jeshi la Polisi linatumia nguvu kubwa? Ni sawa na kumuua labda inzi kwa kutumia bunduki jambo ambalo siyo sahihi. Inapotokea *operation* watumie nguvu za kiasi ili wananchi wetu wajenge imani na Jeshi letu la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya vituo anakamatwa mtu pengine kwa shinikizo tu la mtu fulani, anawekwa *lockup* zaidi ya siku saba, wakati Sheria inaeleza wazi kwamba mtu anaweza kukaa *lockup* kwa muda wa masaa 48. Kwa hiyo, naiomba Serikali waliangalie hili ili haki itendeke katika vituo vyetu vya Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo, nataka njielekeze kwenye Jeshi la Zimamoto. Katika Wilaya zetu, hakuna Ofisi wala vituo vya Zimamoto, viko katika Mikoa. Unapotokea moto katika Wilaya zetu inakuwa ni shida na kwa kweli inakuwa ni janga kubwa sana. Hata hapo inapopatikana hiyo gari, pengine itafika katika eneo la tukio

lakini hawana maji. Kwa hiyo, naishauri Serikali katika Wilaya zetu waweke vituo na Ofisi za Zimamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo, nitajielekeza sasa kwenye vitambulisho vya *NIDA*. Bunge limepitisha pesa nyingi sana kupeleka katika zoezi hili, lakini utendaji kazi wa *NIDA* unasuasua. Inachukua muda mrefu kupatikana kwa vitambulisho. Kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie sana jambo hili ili ituambie hasa, Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze, baada ya muda gani watu watakuwa wamepata vitambulisho? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo, nataka njielekeze katika Jeshi la Polisi vilevile. Askari wetu wanaishi katika mazingira magumu sana. Ni ushahidi, hata hapa Dodoma tunawaona wanaishi katika nyumba za mabati, nyumba zimeezekwa kwa mabati na pia hazikukandikwa, zina mabati, joto tupu. Jamani hawa ni binadamu kama sisi, wanastahili na wao wakae sehemu nzuri. Wanapopata utulivu wa mwili na akili ndiyo wataweza kufanya kazi vizuri. Leo wanaishi mle kama wanyama, ni kuwadhalilisha na kulidhalilisha jeshi letu. Kwa hiyo, naishauri Serikali tuanze na hapa Dodoma kwanza kuwarekebishia makazi yao Askari wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Vituo tunawapa mizigo mikubwa. Hakuna mgao wa fedha kwa ajili ya umeme wala maji. Unapomalizika pengine umeme katika Kituo, Mkuu wa kitengo kile cha mahabusu, kunakuwa pengine ndani kuna mahabusu chungu nzima, hawawezi kuwacha wale na giza, wanaweza wakadhuriana, kunaweza kukatokea neno lolote. Mkuu wa Kituo anajilazimisha kutoa hela yake mfukoni, mshahara wenyewe tunaujua haukidhi haja, ana watoto, ana familia; jamani wenzetu tuwaoneeni huruma na Serikali ihakikishe kila Kituo cha Polisi kinaweka fungu la fedha kwa ajili ya maji na umeme. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Rukia.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea zaidi na uchangiaji, naomba tuwatambue wageni waliopo Bungeni jioni hii.

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambaao ni wageni 179 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana pamoja na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ambaao ni washiriki wa Mkutano wa Bunge Kivuli la Vijana chini ya Umoja wa Mataifa, liliofanyika Mkoani Dodoma.

Vijana hao wametoka Mataifa ya Kenya, Uganda, Rwanda, Sudan Kusini, Sudan Kaskazini, Somalia, Ethiopia, Ghana, Nigeria, Marekani, Zimbabwe, India, Uingereza na mwenyeji Tanzania wakiongozwa na Ndugu Jackline Kamwau. Karibuni sana wageni katika Bunge letu. (*Makofi*)

Pia tuna wageni 13 wa Mheshimiwa Willy Qambalo, Mbunge ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu. (*Makofi*)

Vile vile leo jioni hii tunao wakuu wa vyombo vya usalama, Makamanda wa Mikoa jirani, Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Morogoro na Singida, yaani Makamanda wa Polisi, Magereza, Zimamoto, Uhamaaji na Vitambulisho vya Taifa pamoja na Maafisa wengine kutoka Makao Makuu. Karibuni sana Maafisa wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Lucy Mayenga ajiandae. (*Makofi*)

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa nasikiliza michango dhidi ya utendaji wa Jeshi la Polisi, ilifika hatua nikajuliza kwa hizi sifa kwa nini tunakuwa na Jeshi la Polisi? Wamepewa sifa mbaya ambazo kwa kweli hawastahili hata kuendelea kufanya kazi. Nikajuliza, kwa nini bado wanaendelea kuwepo? Pamoja na hizi sifa zinazotolewa dhidi yao, kwa nini bado wapo? Ikabidi nijipe *homework* kidogo ya kusoma na kujua kwa nini kulikuwa na Jeshi la Polisi? Kabla ya kuwa na utaratibu huu rasmi wa kuwa na vyombo vyta Ulinzi na Usalama na kuwa na Serikali yenye mihimili mitatu inayojitegemea, dunia ilikuwa inaishi kama wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa wewe ukilima shamba lako, mtu anakuja anaswaga ng'ombe zako, anaondoka nao. Mbabe akikuona mtaani, akijisikia kukuchezesha makofi ya kutosha, anakupiga makofi ya nyota nyota, utaratibu ulikuwa hivyo. Baadaye dunia ikaamua kuja na Jeshi la Polisi likiwa na kazi tatu ambazo dunia nzima kazi za Polisi ni hizo. Kazi ya kwanza ni kulinda raia na mali zao; kazi ya pili, ni kuzuia uhalifu na uvunjaji wa sheria; na kazi ya tatu, ni kusimamia utekelezaji wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kazi tatu ukiziangalia katika mtitiriko, karibu wote hapa tunaipenda sana kazi ya kwanza. Kazi ile ya kwanza ambayo ni kulinda watu na mali zao, kila mmoja hapa anapenda kulindwa; na kila mmoja hapa anapenda mali yake ilindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya pili na kazi ya tatu ni ile kazi ambayo uhuru wangu unapoisha ndipo unapoanza uhuru wa mtu mwingine. Hapo tunatofautiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajuliza, hivi hawa Askari wetu ni kweli wachache wana mambo ya hovyo, hivi kweli wote tunawapa lugha mbaya namna hii za kuwachoma, hatutambui mema yao hata kidogo? Walichofanyiwa Askari leo huku ndani kwenye mjadala ni ule msemo wa samaki mmoja akioza, wote wameoza. Ule msemo umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msemo wa siku hizi, samaki mmoja akioza, atolewe yule mmoja, waliobaki tunaweka ndimu, pili pili na chumvi tunawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Askari wote wakabebeshwa mzigo hapa ikaonekana ni watu wa ovyo kama hawafanyi kazi. Hivi leo, tukubaliane tu kimsingi hapa. Sirro aamue *traffic* wote leo Dar es Salaam ondokeni kwenye zile *traffic lights*. Kwa sababu kati ya kazi za msingi za Askari siyo ku-control/zile *robot*, kuita magari. Taa zifanye kazi yake; lakini inafika kipindi, taa zinashindwa, Askari pale wanatusaidia. Siku ikitokea wote waondoke pale, kitakachotukuta, Mungu nisaidie. Au leo ondoa Askari wa doria wote, halafu *Panya Road* waingie barabarani, tutatafutana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kawaida sana ya kuwaona Askari ni wema pale wanapofanya yanayotupendeza, lakini pale wanapofanya kazi ya pili ambayo inawezekana imemgusa jamaa yako, imemgusa jirani yako; hata inawezekana hata mimi akaguswa mtu ambaye kanigusa sana, sitaweza kufurahi. Hiyo ndiyo hulka ya mwanadamu. Siyo kila mwanadamu hufurahia pale anapopata msukosuko wa kisheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba kwa Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na *IGP* afanye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anapojitekeza Askari akaenda kinyume na maadili na utendaji wa Askari, hatua zake anazopaswa kuchukuliwa ziwe tofauti sana na raia wa kawaida. Nafahamu kuna Askari wanachukuliwa hatua za kinidhamu kwenye Kambi zao, lakini inapofika mahali Askari anafanya uhalifu *against* raia, aina za hatua ziwe tofauti na umma ujulishwe kwamba nini yule Askari mkosefu alifanyiwa. Wakiendelea kuwapa adhabu za kule ndani, jamii haitawaelewa na ndiyo maana wanakuja kuambiwa samaki mmoja akioza, wote wameoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana *RPC* wa Mara alivyo*-handle issue* ile, ni *issue* mbaya sana. Unapokutana na Askari anamuua raia aliyemkamata, ni jambo bayo, hatupaswi kulifurahia, hatupaswi kulichekeia. Ila hatua alizozifanya *RPC* akasema tumemkamata, tumemfanyia moja, mbili, tatu na kesi inaendelea hivi na tumethibitisha hili liko sahihi. Sasa Askari, *IGP* ukiwaeleza Ma-*RPC* wako wote na Ma-*OCD* wa-*handlesuala* kwa *design* hii hatutapata shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nchi yetu inapakana na nchi nane. Katika ya hizi nchi nane tunazopakana nao hakuna nchi hata moja ambayo iko salama. Tafsiri yetu, usalama wa nchi yetu ni tenge, una matege, hauna miguu iliyonyooka. Nchi zote nane zinazotuzunguka ukianzia Kenya mpaka unakuja kumalizia Mozambique, hakuna nchi ambayo iko *stable*. Nchi zote zina chokochoko, zina mambo yasiyokuwa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine zina *population* iliyoziidi kiasi kwamba ardhi haiwatashi, nyingine zina njaa kali ambazo zinahitaji chakula. Katika mazingira haya, mikoa yetu ya mipakani ina hali mbaya sana sasa hivi. Kwa taarifa nilizozipata rasmi, Idara ya Uhamiaji tafadhali, wafanye kazi sana mipakani kuhusu raia. Mara baada ya kuona nchi yetu ina ardhi ya kutosha ya kulima na chakula kiko cha kutosha, jirani zetu wengi wameingia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tulipo-*introduce* elimu bure, kuna watu wameingia kwa sababu tuna jamaa zetu; nchi zote za mipakani haya makabila, kuna Wamakonde kwa ndugu zangu akina Bobali kule wako wengine Msumbiji. Ukienda Masai kule ndugu zangu wa Tarime wanapakana kule na Migori ni ndugu, ni jamaa tu wale. Kwa hiyo watu ku-cross ni kitu cha kawaida. Naiomba Idara ya Uhamiaji, sasa hivi ifanye kazi yake ya kukagua Uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, tumeitumia demokrasia vibaya na tumeshindwa kuitafsiri demokrasia vizuri. Demokrasia kwa asili yake haikuwahi kuwa

ya Kiafrika. Demokrasia kwa asili yake haikuwahi kuwa ya Kitanzania. Demokrasia inatokana na maneno mawili ya Kigiriki na ndiyo wenye asili ya demokrasia; "Demons" inayomaanisha "people" na "Cratos" inayomaanisha "Power." Kwa tafsiri nzuri na fupi "The people holds power." (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya wanaoitazama demokrasia juu juu wameshindwa kujua vitu gani vinapima demokrasia. Kuna sehemu tunapima demokrasia inayoendana na watu ili tuthibitishe kweli hii demokrasia ni ya watu, ni pale ambapo kila Mtanzania anapochagua. Kwa hiyo, kipimo namba moja cha demokrasia na kuisema nchi hii ina demokrasia, yaani ina nguvu zinazotokana na watu, lazima kuwepo na *election*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *electionzinatofautiana*. Kuna wengine wanachangua mtu, wengine wanachagua vyama, wengine wanakwenda *winner takes it all*, wengine wanakwenda *PR System*; kuna mifumo mingi duniani kutokana na mila na desturi. Sasa ninyi ndio mnajiamulila kwamba kwa mazingira yetu mfumo huu ndio unaotufaa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kampeni za uchaguzi kupita kila kijiji ni mila na desturi za watu husika. Leo mnaweza mkauna hauwafai. Tukumbuke kwamba unapoishia uhuru wangu, ndipo unapoanza uhuru wa mtu mwingine. Demokrasia nzuri ni ile inayotetea *the right of individual*. Unaposema *the right of individual* ni pamoja na kutokunkwaza, kwa nini haki yako wewe iwe kunikwaza mimi? Wewe unakuja na m Kutano wako, mimi nasali. Kwa nini haki yako ilindwe, yangu isilindwe? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwambieni ndugu zangu, nchi yetu anayefanya *active politics* hatujafika asilimia 10. *The rest 90 percent* hawana habari na siasa zetu hizi, *active*

politics za Majimbo, hawana kabisa. Wao wanakwenda asubuhi kulima, wanakwenda kufanya kazi zao, wanarudi makwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili tukilichukua demokrasia kwa kisingizio cha upuuzi wetu na upumbavu wetu, hatupaswi kuwa watu wa namna hiyo. Tuisome demokrasia tuijue. Demokrasia nzuri ni ile inayoendana na mila na desturi za watu husika na ile inayolinda haki za mtu mmoja mmoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa mwenyekiti, la mwisho,...

*(Hapa kengele illilia kushiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Sixtus, muda wako umekwisha.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kengele bado moja, namalizia la mwisho. Muda wangu una dakika moja tu.

MWENYEKITI: Dakika moja.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: ...muda wangu nina dakika moja tu.

MBUNGE FULANI: Hamna!

MBUNGE FULANI: Kaa chini wewe.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Lema...

MBUNGE FULANI: Malizia.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Lema...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Nina dakika yangu moja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sixtus Mapunda. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Mayenga, baadaye Mheshimiwa Amina Makilagi ajiandae.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo kusimama hapa na kwa kweli kutoa mchango wangu wa mawazo kwenye Wizara hii. Kwanza kabla sijaanza, niseme ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Shinyanga Mjini kwenye Jimbo letu la pale Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Waziri naomba achukue hili suala na shida hii kubwa ambayo tunayo; tuna tatizo kubwa sana la uchakavu mkubwa wa Kituo chetu cha Polisi pale Shinyanga Mjini. Vilevile tuna tatizo kubwa sana la ubaba wa magari; kuna Wilaya mbili za Kipolisi, Ushetu pamoja na Msalala, hazina magari ya Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nianze. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa sana ambayo amekuwa akiifanya. Nalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa *IGP* na Makamanda wake, watulie wala wasiwe na wasiwasi. Waendelee kuchapa kazi. Kazi wanazozifanya zinaonekana, mambo mema wanayoyafanya yanaonekana. Hatuwezi *to compromise* kwenye suala zima la usalama. Hii nchi watu walikuwa wamezoea kudeka, kufanya mambo ya ajabu na

kuropoka maneno ya ajabu kila siku na kutukana hovyo kwenye mikutano. Lazima ifike wakati tushikishwe adabu. (*Makofî*)

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. LUCY T. MAYENGA: Vyama vyote vya Siasa, ukiwa CCM, ukiwa chama chochote lazima ufile wakati ujue kwamba nchi lazima ifike wakati itawalike. Isiwe kwamba watu wanakuwa huru kiasi ambacho mtu anakaa ana uwezo wa kuamka leo asubuhi akafanya anachotaka, ana uwezo wa kukaa mchana akafanya anachotaka, lazima ajue kwamba nikifanya jambo lolote nikiwa na azma mbaya, nitashughulikiwa. Hiyo ndio Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu mpaka wamefikia kusema kwamba Jeshi la Polisi ni wapiga debe wa CCM; watu wanashahau. Ndiyo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuzungumza hapa kwamba yanapokuwa masuala mema, pale tunapokaa tunalindiiwa mali zetu na usalama wetu, tunaona hivi vyombo vya ulinzi na usalama kwamba ni vizuri sana. Pale inapokuja sasa kwamba na sisi tunashughulikiwa kwa mambo yetu ambayo tumeyafanya mabaya, tunaanza kuona Jeshi la Polisi ni baya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi sio wote ni wabaya, sio wote wanafanya kazi zao kinyume na sheria na utaratibu, wapo watu wengine baadhi ambao tunaona na hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tusione kwamba Polisi wote hawafai, Polisi wote sijui wameoza. Kwanza hali ya usalama iliyopo sasa hivi, uhalifu ulivyopungua, sasa hivi inaonesha kabisa kwamba Jeshi letu la Polisi na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza *RPC* wa Dodoma, licha ya haya maneno ambayo watu wanasesma sijui amesema hivi, lakini mimi nampongeza. Nampongeza *RPC* wangu wa Mkoa wangu wa Shinyanga, nampongeza

pia sana *RPC* wa Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Kwa ujumla ni mfumo mzima ndani ya Jeshi la Polisi wanafanya kazi nzuri, lakini yote haya, lazima na sisi tukiwa kama Watanzania bila kujali itikadi zetu za kisiasa, tofauti zetu za kiitikadi, lazima tujiulize, kwa nini nchi yetu imekuwa na chokochoko namna hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mambo mengi sana sasa hivi yamekuwa yakisemwa na kumekuwa na chokochoko namna hii? Tena mpaka imefikia kiwango watu wa nje sasa wanaanza kuingilia uhuru wetu na mwenendo wetu wa nchi. Lazima tujiulize, yote haya yanababishwa na kazi nzuri ambayo anaifanya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ndiyo! (*Makofi*)

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambayo anaifanya, kwa namna yoyote ile hakuna mtu ambaye anaweza akakaa akafurahia. Wawekezaji kwenye Sekta ya Madini huko watu wamebanwa, wameshikwa pabaya; wakiangalia sijui watumishi hewa, wameshikwa pabaya; mafisadi, watu walikuwa wamekaa wamejiachia, wanakula pesa, wanafanya mambo ya ajabu, wameshikwa pabaya. Kwa hiyo, lazima tujue kwamba vita hii tuliokuwa nayo ni vita kubwa kuliko ambavyo tunaweza kufikiria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tu asubuhi Mheshimiwa Lema hapa amezungumza, aliuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu suala zima la matatizo ya mafuta ghafi ambayo yamezuiliwa huko bandarini. Hilo suala lina makorokoro mengi sana huko ndani. Namshukuru Mheshimiwa Lema hata kwa kuuliza lile swali. Sasa watu kama hawa ambao wamekuwa wakishughulikiwa lazima wao wenyewe kwa wenyewe watakuwa wanapiga makelele. Mwaka jana Mheshimiwa Rais alisema, wewe ukiwa kama mwanaume, unafanya biashara halali, ikifika mwezi wa Sita wewe utakuwa ni mwanaume kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anasema namna ile kwa sababu hawa watu ambao wameguswa pabaya na wengi wetu na hata hawa wengine wa upande wa pilii wanawajua na wengine wengi wao ambao wanawajua, wanajua kwamba baadhi yao wafadhili wao. Lazima ifike wakati na wao wawe wazalendo kutoka miyoni mwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiona kwamba jambo hili ni bayo, tuangalie hatima zetu za huko mbele, tusiangalie tu leo; tuangalie wajukuu na watoto wetu na ndugu zetu hao wengine wa baadaye. Tusikae tu kuangalia kwamba eti tumekaa, mara mambo yamekuwa yanaibuka ovyo, mara sijui hivi na hivi na hivi; lazima tujue kabisa kwamba hawa wafadhili wetu itafika mwisho sisi tutaondoka, lakini maisha ya Watanzania yanaendelea.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakiendelea kusema, mimi nimezoea. Waseme wee, wakichoka wananyamaza, mimi naendelea. Watulie misumari iingie. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa ambao mnafanya fujo, nawaona huko.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kwa muda mrefu wamekuwa wakizungumzia kuhusu suala zima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. LUCY T. MAYENGA: Muda umekwisha?

MBUNGE FULANI: Ni kengele ya kwanza.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Ya kwanza.

Mheshimiwa mwenyekiti, licha ya changamoto nyingi ambazo Jeshi la Polisi limekuwa linazo, lakini kazi kubwa ambayo imekuwa ikifanyika imekuwa inaonesha kabisa kwamba nchi hii, kinachotakiwa kimsingi ni dhamira ambayo iko kwa viongozi wetu.

MBUNGE FULANI: Harusi ya tano.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka nizungumzie, nataka nizungumzie Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Nailaumu Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Nampongeza sana Kamishna wa Uhamiaji, mwanamke, Kamishna Anna Makakala, anafanya kazi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamishna wa Uhamiaji anafanya kazikubwa na nzuri sana. Kamishna huyu amekuwa anashughulikia masuala ya uhamiaji haramu, lakini yako mambo na matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza. Kuna taarifa kwamba wapo wahamiaji ambao wamekuwa wakiingizwa hapa Tanzania na watu ambao hawana uzalendo na nchi yetu; wahamiaji hawa haramu wamekuwa wakifa kwenye magari; wahamiaji hawa haramu wamekuwa wakitupwa na wale watu ambao wanaingiza kinyume na sheria; wanawatupa kwenye mito, bahari na kadhalika, lakini Wizara hii ipo kimya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwigulu, matokeo yake sasa imekuwa ni kwamba Serikali na sisi ambao tupo Chama cha Mapinduzi tumekuwa tunalaumiwa kwamba watu hawa sijui wanakufa, sijui wanauawa na kadhalika. Kwa nini Serikali hamsemi? (*Makofii*)

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mnapokaa mnanyamaza kimya inafanya kwamba kile ambacho kinaendelea kufanyika sasa hivi, watu wanatumia

sana mitandao hii ya kijamii, taarifa ambazo zinapelekwa kule siyo zote ni za kweli.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy naomba subiri kidogo. Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Waitara.

MBUNGE FULANI: Kwa nini umeruhusu?

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anyeendelea kuchangia kwa mujibu wa kanuni ya 64(1)(a) inasema, mchangiaji hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

MBUNGE FULANI: Yes.

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimwia Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge wakati anaendelea kuchangia anasema, matukio haya mengi na malalamiko yaliyopo nchini yanababishwa na mambo ya kibiashara na hao watu ambao wamenyang'anya fursa mbalimbali ni wafadhili wetu, ametaja hilo neno. Sasa nikasema hizo taarifa kama hawezikuzifuta, athibitishe hao waliwafadhili ni akina nani na ushahidi alete mezani. Kwa sababu kanuni inakataza taarifa ambazo siyo za kweli. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara unatakiwa uthibitishe wewe kwamba hilo alilosema siyo kweli na ukweli ni upi. (*Kigelegele/Makofi*)

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nathibitisha kwamba hakuna mfadhili ye yeyote ambaye ametufadhili sisi juu ya mambo haya. Mambo ambayo yanaendelea katika Taifa hili ni ugandamizaji ambao unafanyika. Sasa ye ye kama ana *counterpart* yake alete hapa, tukutane mezani. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara tutaamini vipi kwa maneno hayo tu? Naomba Mheshimiwa Lucy uendelee.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya CAG, naomba Mheshimiwa Waitara akaichukue, atulie kichwa chake kiwe *sober*, aisome yote ataaelewa ninachokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia kuhusu Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Naomba kuanzia sasa hivi Wizara hii iamke. Iwe inatoa taarifa bila kumwonea mtu aibu. Matukio ambayo yanatokea, changamoto ambazo zinaendelea; ninafahamu kwamba endapo kama mtu ameuawa aidha kisiasa au hata kama siyo kisiasa, kwa sababu yapo mambo mengi ambayo yanafanyika, jinsi mwendelezo wa huo uchunguzi unavyoendelea, wawe wanatoa taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nafahamu kwamba hawawezi kusema kila kitu, lakini wawe wanasema kwamba angalau tumemkamata mtu na mambo haya yanaendelea. Kwa sababu yapo mambo ambayo yanasemwa kisiasa wakati kiuhalisia hata kwenye vyama vyetu vyaa siasa kuna mambo mabaya tunafanyiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa mwanachama wa Chama cha Mapinduzi, kuwa mwanachama wa CUF, kuwa mwanachama wa CHADEMA, kuwa mwanachama wa chama chochote haina maana ya kwamba huwezi kuwa na matatizo yako mengine ya kijamii. Haina maana kwamba wewe kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa au wewe kuwa kiongozi wa Chama cha Siasa, basi ni mtakatifu kwamba ikitokea kuna chochote ambacho kimetokea dhidi yako maana yake ni kwamba umefanywa au jambo hilo limefanywa na mpinzani wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii waamke. Wamekuwa wananyamazia sana haya matukio. Matokeo yake Serikali imekuwa ikisemwa na ikihusishwa kwa mambo mengine ambayo hata hayapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili Mheshimiwa Waziri kwa kweli endapo kama ataendelea kunyamaza namna hii

wakati anajua kabisa kwamba haya mambo yapo mengine ambayo yanafanyika kinyume na utaratibu; naomba watu watajane na watu watajwe kwamba huyu amehusika na huyu amehusika kwa moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lucy. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Makilagi, baadaye Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi ajiandae.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kipekee nianze kwa kumshukuru Mungu, muweza wa yote aliniwezesha kusimama na kutoa mchango katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kuandaa taarifa nzuri na kuiwasilisha vizuri. Kipekee, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na timu yake yote; *IGPKamanda Sirro, Kamanda wa Magereza, Kamanda wa Uhamiaji na Kamanda wa Zimamoto* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha nchi ya Tanzania tunaendelea kuishi kwa amani na usalama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashuhudia kwamba Mamlaka hii ya Mambo ya Ndani wameweza kudhibiti mauaji ya *Albino*. Ni ukweli usiopingika, wamedhibiti wezi wakiwemo na wezi wa magari; ni ukweli usiofichika, wamedhibiti mpaka na wezi wa mabenki; ni ukweli usiofichika, wamedhibiti mauaji ya raia wasiokuwa na hatia; *Albino*, vikongwe, Askari wetu waliokuwa mstari wa mbele na hata wananchi wa Kibiti ambao walikuwa wanauawa kama kuku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni, haki yake apewe. Hongera sana Kamanda Sirro, hongera sana Makamanda wote. Nataka niwaambie, akutukanaye hakuchagulii tusi; na ukiwa kwenye maji unaoga, akija

mwendawazimu usimfukuze, chutama kwenye maji. Atakayewalipa ni Mwenyezi Mungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, unaona mpaka watu wanatembea, wanaongea na wanazungumza watakavyo ni kwa sababu ya amani. Watu wamekula, wameshiba, wanalala kwa amani mpaka sasa wanavimbiwa wanatukana ovyo. Kamanda Sirro na timu yake wasikate tamaa. Mti mzuri wa maembe ndiyo unaopigwa mawe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wanawake wa Tanzania ambaao tumeachwa wajane kule Kibiti, ambaao wameachwa wajane kule Rufiji, *Albino* wasiokuwa na hatia ambaao wameachwa wajane au wameachwa yatima, sisi tunawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu na ndiye atakayewalipa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiona watu wanapiga kelele, wajea wamewashika pabaya. Maana wamedhibiti kila kona. Madawa ya kulevyo, waliokuwa wanafanya wengine wako hapa wengine wako nje, wamedhibiti. Mikutano isiyokuwa na tija, watu walikuwa muda wote maandamano, wamedhibiti, hongereni. Ndiyo maana leo unaona sasa kila anayesimama, wanawapiga kwa sababu wamewashika pabaya. (*Makofî*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatia moyo. Wasivunjike moyo, wasonge mbele, tunatambua kazi yao na Watanzania wanatambua kazi yao na ndiyo maana wanawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, Jeshi la Polisi limedhibiti ajali za barabarani.

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba tutulizane. Mheshimiwa Mwakilagi naomba uendelee.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Jeshi la Polisi limedhibiti ajali za barabarani. Nani ambaye hajui kwamba kwa miaka ya hivi karibuni kulikuwa na ajali za kupitiliza? Kuna watoto wamebaki yatima, kuna wamama wamebaki wajane; kuna familia zimeondoka zote kwa sababu ya mwendokasi. Nani alikuwa hajui?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi wamedhibiti, wameweka mwendo wa taratibu, ajali zimepungua kwa kiwango cha asilimia 35. Nawapongeza, waendelee kuchapa kazi na wakaze buti. Wakiona tunapiga kelele wametushika pabaya, tukiwemo na sisi Wabunge tulikuwa ni mionganini mwa watu tulikuwa tunakwenda mwendo kasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshamtangazia dereva wangu, tukikamatwa hiyo kesi ni ya kwako. Endeleeni kudhibiti ili kuokoa Watanzania wanaofariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa sababu wamedhibiti wahamiaji haramu. Nchi yetu ilikuwa inaelekea kubaya kwa sababu Tanzania ni barabara. Nampongeza Kamishna wa Uhamiaji, Mama Anna, kwa kazi nzuri anayoifanya. Wamewadhibiti, wametushika pabaya, kwa sababu baadhi ya wasioitakia mema nchi yetu, walikuwa wanawatumia wahamiaji haramu kuvuruga amani ya nchi yetu. Hongera sana, wapige kazi wala wasiwe na wasiwasi. Sisi tulio wengi tuko nyuma yao na Mwenyezi Mungu atawapa baraka zaidi. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Amina.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mara bada ya utangulizi huo, nimemsikia mtoto wangu Lema akieleza hapa. Mimi nimeita mwanangu, analeta *propaganda* mwanangu. Hivi watu 1,000 wafariki katika nchi hii ya Tanzania; familia za watu 1,000 zipoteze, watu 1,000,

tuendelee kuwa hivi mwanangu! Jamani hebu semen i ukweli, msipotoshe umma. Jamani hata kama tunatafuta *kick* siyo kwa namna hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani Mheshimiwa Lema aje na ushahidi atuoneshe. Kweli familia 1,000 watu wapotee halafu nchi ibaki kuwa hivi? Jamani, hebu waseme ukweli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya utangulizi huo, njielekeze kwenye michango yangu. (*Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naomba nizungumzie bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Tumeona kwamba kuna fedha zimepelekwa zaidi ya asilimia 78. Ninachokiomba ili Taasisi za Mambo ya Ndani ziweze kutekeleza wajibu wao sawasawa, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama yuko hapa anisikie. Hebu wapeleke fedha kwenye haya Majeshi waweze kununua vipuli kwa ajili ya magari, waweze kupata fedha kwa ajili ya kununua mafuta, waweze kupata fedha kwa ajili ya kulipa madeni. Taasisi zinafanya kazi kwa hali ngumu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi ni sawasawa na hospitali. Shida haina hodi wala nini. Unapotoka uhalifu, Kamanda wa Mkoa hana mafuta, *OCD* hana mafuta, Mkuu wa Kituo hana mafuta, wote wanakuwa ombaraombwa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake na Serikali iko hapa na Waziri Mkuu yuko hapa. Hebu waipe kipaumbele kinachostahili Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Zimamoto. Mfano tu ni Dodoma, wana magari mawili tu, moja liko uwanja wa ndege, moja liko hapa; na hapa ni Makao Makuu. Hivi gari mbili zinatosha kwa Dodoma? Vile vile bajeti ya kwenda kujenga nyumba za Askari hakuna. Naomba hebu Serikali ione Wizara hii ya Mambo ya Ndani ipewe heshima inayostahili ipelekewe fedha kwa ajili ya maendeleo yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie nyumba za Askari. Naomba niungane na wenzangu kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali, lakini ni ukweli usiopingika, hali siyo nzuri katika nyumba za Askari wetu. Askari wetu wanaishi katika nyumba mbaya. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kujenga nyumba za Askari; na kwa mujibu wa taarifa, zitajengwa nyumba 400. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, Jeshi la Polisi linalo Kitengo cha Ujenzi, Jeshi la Magereza linalo Kitengo cha Ujenzi; hebu imarisheni vitengo hivi. Sasa hivi vile vitengo vimekuwa, matokeo yake sasa tunahitaji kutumia fedha nydingi zaidi tofauti na ilivyokuwa zamani. Na-*declare interest* kabisa, nami ni mtoto wa Askari na ndiyo maana nikiona mtu anamkejeli Askari huwa naingia na uchungu sana kwa sababu Askari ni mtu aliyemtariki wa mbele kupambana usalama wa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba, waimarishe hiki kitengo wakipatie fedha. Bahati nzuri kinao Watendaji wazuri, kinao mainjinjina. Kwa sababu sasa hawana kazi, wengine sasa ndio ma- *OCD*. Mfano *OCD* wa lleje, ni injinia yule lakini leo ni *OCD*; na watu wengine. Hebu waimarishe hiki kitengo kiweze kujenga kwa gharama nafuu ili kwa kutumia na nguvu ya wale wafungwa, tunaweza kuokoa fedha nydingi za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie maslahi ya Askari wetu. Askari wetu wanafanya kazi ngumu sana katika mazingira magumu tena ya hatari. Wanaishi na raia na raia wengine wako humu ndani, wanaona jinsi wanavyozungumza. Hivi akikutana na Askari kwenye kona, itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Askari hawa tuimarishe ulinzi wao, tuwajengee nyumba za kutosha, tuhakikishe maslahi yao yote wanapata, tuhakikishe wanapokwenda likizo wanapata haki zao, wanapopanda madaraja tunawapa fedha zao. Wapo Askari wamepanda

madaraja, hawaongezewi mishahara, mpaka wanastaafu matokeo yake hata *pension* yao inakuwa ni kidogo. Askari huyu ambaye anatufanya kazi nzuri, tunamlipa nini? Naomba sana, hebu waangalie kwa macho ya huruma katika jeshi hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala zima la upandishaji wa vyeo kwa Askari wetu. Nashukuru sana Serikali hii na majeshi yote yameweka utaratibu. Kuna kanuni ya namna ya kuajiri na namna ya kuwapandisha madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kabisa, hebu angalieni na wale Askari waliofanya kazi kwa muda mrefu. Wamefanya kwa weledi, kwa uaminifu lakini hawana elimu ya juu. Hawa wanasuasua katika kupanda vyetu, utakuta ni *Constable* tangu ameanza; akisuasua mara amekuwa *Corporal*, mara amekuwa *Sergeant* mara amekuwa *Major* kwa muda mrefu sana. Hivi kwa nini hawa wasipewe heshima kama ambavyo wengine wanavyopata? Kwa sababu wamefanya miaka 25, miaka 30 anabaki kuwa *Constable*. Hebu naomba hii kanuni iangaliwe tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la posho za chakula cha Askari. Naishukuru Serikali, angalau wamewaongezea Sh.300,000/=. Namshukuru na Mheshimiwa Rais wetu amewapa Sh.100,000/= kwa ajili ya vinywaji. Askari wanashukuru. Nami nazungumza nao, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba, hebu Serikali ijaribu kuona uwezekano hata kuwaongezea tena laki moja moja hata zikawa shilingi laki nne, kwa sababu wanafanya kazi nzuri sana, kazi ambayo ni ya kutukuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Askari wetu wanaishi uraiani, kwenye nyumba za kupanga; walikuwa wanalipwa posho asilimia 15 kwa ajili ya kulipa kodi ya nyumba, iliondolewa kwa maelezo kwamba wanahakiki. Nataka njue, huu uhakiki utakwisha lini? Vile vile Askari wa Zimamoto

hawana nyumba kabisa; Askari wa Uhamiaji hawana nyumba kabisa, wa Magereza ndiyo usiseme, wengi wanaishi uraiani. Hivi hawa hii posho yao ya nyumba asilimia 15 ni lini wataipata? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na mafunzo ya Askari. Naipongeza Serikali inafanya kazi nzuri sana ya kuwajengea uwezo Askari wetu. Ombi langu, naomba sasa wajifunze namna ambavyo hasa wale *CID* wanaoweza kukabiliana na hii mitandao, kwa sababu sasa hivi wizi ulio mwingu ni wa kwenye mitandao. Hawa Askari wetu *CID* wanajengewaje uwezo ili waweze kukabiliana na changamoto za sasa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ambalo nataka njue, nimepata habari kwamba sasa hivi Askari wanaokwenda kusoma *CID*, *traffic* na kozi nyingine wameambiwa sasa wanatakiwa kuchangia kila siku shilingi 7,000/=. Nataka kujua, huo utaratibu umeanza lini? Kwa nini wachangie? Hivi anapoondoka ameiacha familia yake, itakula nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Amina Makilagi. Tunaendelea na Mheshimiwa Maufi, baadaye Mheshimiwa Omary Kigua ajiandae.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami kuzungumza na Bunge lako Tukufu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya ya kuweza kusimama leo hii katika kuzungumzia suala zima la Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyojitokeza mbele kabisa kuhakikisha ya kwamba anaboresha na kuweka maisha bora kwa askari wetu Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mnyonge mnyongeni na haki yake mpeni. Wizara ya Mambo ya Ndani inafanya kazi kwa hali ngumu sana, lakini inafanya kazi kwa weledi na kuthibitishia Watanzania kuwa katika amani na utulivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao Wanajeshi, Polisi, Zimamoto, Uhamiaji na Magereza, wote hawa wako karibu na wananchi wa kawaida na wanashirikiana na wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, Mambo ya Ndani ni msingi wa amani na utulivu wa nchi yetu. Bila hawa, hii amani tunayojivunia hivi sasa tusingejivunia hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tusione kigugumizi na wala tusione aibu, ni lazima tuseme kwa ukweli kabisa kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani inafanya kazi yake vizuri na kwa weledi, iliyobakia kwetu sisi ni kuwaunga mkono ili bajeti yao hiyo wanayoipata na hiyo walioyoiunda iweze kuongezeka na waweze kufanya kazi yao vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala zima la bajeti. Bajeti ya 2017/2018 tuliweza kutenga, lakini Wizara ya Fedha imetoa kwa asilimia 28 tu kwa miradi ya maendeleo. Naomba Wizara ya Fedha, hii asilimia 28 ni ndogo sana, naomba wajitahidi kwa Jeshi la Polisi ama kwa Wizara ya Mambo ya Ndani waweze kupata bajeti yao kamilifu. Hawa watu wanafanya kazi kubwa sana. Bila usalama na amani hata hayo mengine tusingeweza kuyafanya. Mengi wameyasema wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Ndani ipatiwe kwa asilimia mia moja bajeti yao wanayoipanga na kwanza hata hii bajeti tuliyoiweka haikidhi mahitaji ya Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la makazi. Napenda *ku-declare interest* kwamba mimi ni

Mjumbe katika Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Tumetembelea Mikoa ya Lindi na Mtwara; nyumba za Wanajeshi wetu kwa kweli siyo nzuri, haziridhishi, ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe maamuzi magumu, kama ilivyotolewa maamuzi kwa Uhamiaji hapa Dodoma kuhusu kununua nyumba pale lyumbu, basi tunaomba na Wizara ya Mambo ya Ndani wachukue jukumu la kununua nyumba kwa Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyumba zilizojengwa na *National Housing* ambazo wanasema kwa bei nafuu, lakini siyo bei nafuu na wananchi wameshindwa kuzinunua. Naomba hizo nyumba zinunuliwe na Serikali kwa Wanajeshi wetu ambao hawana nyumba za kukaa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba zitolewe ramani maalum za kujenga nyumba za Wanajeshi yetu kwa sababu nyumba zile walizonazo siyo za kuishi binadamu ni nyumba za kuishi mifugo. Tunaomba nyumba za kuishi binadamu zitolewe kwa kila mkoa na kila mkoa upewe idadi maalum kwa kila mwaka wajenge nyumba ngapi; ili tuweze kutathmini baada ya hii miaka miwili na nusu ni mkoa upi utapata ushindani wa kujenga nyumba za kutosha za Wanajeshi wetu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalopenda kulizungumzia ni kuhusu kupandisha madaraja Askari. Kwa kweli inachukua muda mrefu sana kupandishwa madaraja Askari hawa na wale wanopandishwa madaraja inachukua muda kuwapatia fedha zao stahiki kwa daraja walilopandiswa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuna Askari ambao wanastaifu. Mtu anapostaifu kwa mujibu wa Jeshi wanapewa likizo ya kustaifu. Likizo ya kustaifu ni miezi minne. Kipindi hiki cha miezi minne kinatosha kabisa kumwandalia mafao yake ili akimaliza tu likizo yake, anapoanza kustaifu,

fedha yake inapatikana; lakini tangu mwaka jana, Askari wamestaafu mpaka hivi leo wanatimiza sasa ni mwaka hawajapata mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Jeshi liweze kuwapatia fedha yao. Hii ni kutokana na kwamba kile kifungu cha matumizi ya kawaida na matumizi mengineyo hakifiki kwa wakati kwa Wizara ya Mambo ya Ndani na kinafika kikiwa hakikidhi mahitaji kwa wenyewe katika kutekeleza mahitaji hayo yote. Kwa hiyo, nawaomba Wizara ya Fedha, wawape fungu hili katika ukamilifu wake ili waweze kulipa madeni ya hao Maaskari wanaolalamika; wengine wana hali duni na wanaweza wakapoteza maisha kabla hawajapata stahiki zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iweze kuhakikisha kwamba fungu hilli kwa Majeshi yote; Zimamoto, Uhamiaji, Magereza na Polisi wapelekewe katika ukamilifu ili waweze kuondoa matatizo ya Wanajeshi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu suala la kiwanda. Tunacho kiwanda Morogoro kinachotengeneza sare za Polisi na wafungwa. Tunaomba viwanda hivi viweze kuongezwa au viwezeshwé na Serikali ili viweze kuzalisha kiasi cha kutosheleza wananchi na Wanajeshi wetu katika nchi yetu. Tunawajua idadi yao. Wanajeshi hawa wakipata angalu *pair* mbili zinaweza zikawasaidia. Vile vile kiwanda cha viatu kiongezwe ili kiweze kutoa viatu kwa Wanajeshi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda Lindi na Mtwara, tumekuta baadhi ya Askari viatu vyao kwa kweli tulisikitika sana. Tulisikitika mno! Kwa hiyo, tunaomba hiki kiwanda kinachotaka kujengwa hivi sasa kitakachowea kuzalisha jozi 4,000, naomba kianzishwe mara moja ili Wanajeshi wetu waweze kupata vifaa vya kutumia katika nchi yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nashukuru na kutoa pongezi sana kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Ila naomba kwa Serikali yangu sikuvi, suala la mazingira yetu Mkoa wa Rukwa, Bonde la Rukwa, Bonde la Tanganyika, kwa kweli hali siyo nzuri kimiundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tunahitajika tupate Vituo vya Polisi. Vituo vya Polisi viro lakini havina amari. Kwa hiyo, wako Askari wanalinda bila kuwa na silaha, lakini wananchi wao wa kule wanazo silaha na ndio maana mauaji katika Bonde la Rukwa yanaendelea. Kwa sababu hakuna amari katika vituo vyetu, inaweza kuleta matatizo, Polisi wetu wanashindwa kufanya kazi iliyokuwa katika ukamilifu wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani ione umuhimu wa kuweka amari katika hivi Vituo vyetu vya Polisi viliivyo kuwa kule Bonde la Rukwa. Vinginevyo, nadhani zile silaha zao wanaweka mahali pasipokuwa salama na kwa maana hiyo inahatarisha vile vile suala zima la ulinzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba Wizara yetu ya Mambo ya Ndani iweze kupewa fedha kamilifu katika mwaka huu wa 2018/2019 ili iweze kutimiza majukumu yake katika ukamilifu wake. Kutokana na kazi ngumu wanayoifanya Polisi wetu, ndio maana maneno mengi yanazungumzwa. Daima mti ukiwa na matunda hupopolewa na mawe, mti usiokuwa na matunda mazuri hakuna mtoto hata mmoja atakayeupopoa mawe. Kwa hiyo, maneno mengi haya tunayozungumza Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani ni dhahiri kusema kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani inafanya kazi yake vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu zangu wa Zimamoto waweze kuongezewa vituo na vile vile waweze kupewa magari angalau nusu ya vituo viwepo na nusu ya magari ya vituo hivyo yaweze kupatikana, kwa sababu wananchi wetu wanaendelea kujenga majumba na hatimaye kufikisha miji yetu kuwa *scattered*, inakosekana miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, likitokea la kutokea, Zimamoto hawawezi kuingia kwa urahisi mle ndani. Kwa hiyo, tunachokiomba ni kwamba, hawa watu wa Zimamoto wapewe vituo vya kutosha angalau nusu ipatikane na hali kadhalika magari yaweze kupatikana ili waweze kutusaidia vizuri ndugu zetu hawa wa Zimamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ni kuhusu watu wa Uhamiaji. Watu wa Uhamiaji kwa kweli katika nchi yetu hii ya nchi nane zinazotuangalia wanahitaji kupewa nguvu ya ziada na nguvu ya ziada ni kuhusu na magari yao na nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachokiomba ni kwamba hawa watu wana doria, Polisi wana doria, Magereza wana doria, Zimamoto wana doria na Uhamiaji wana doria. Vile vile wana suala la kufuatilia makosa mbalimbali katika kufanya msako wa kuangalia Wahamiaji, wahalifu na kadhalika. Sasa watu hawa wana dharura mbalimbali, lakini hawana magari na wala hawana mafungu ya mafuta ya kukamilisha shughuli zao hizo na ni shughuli muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani waone umuhimu kwamba sasa umefika wakati wa kuhakikisha watu hawa wanapata magari ya kutosha, mafungu ya mafuta ya kutosha. Vile vile wanafanya kazi na baada ya saa za kazi, pamoja na kwamba ni saa 24, lakini hawa ni binadamu, tujaribu kuweka na motisha kwa watu hawa wakati wa kufanya kazi zao ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo pia naomba ndugu zangu Serikali, najua kila Wizara huwa inapewa ukomo wa bajeti, lakini kwa majeshi yetu tunaomba ukomo uangaliwe kwa Serikali. Ukomo ni mdogo na kazi wanayoifanya ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, naomba ukomo wa miradi ya maendeleo, ukomo wa shughuli za kawaida uangaliwe upya na kuwaongeza nguvu ili waweze kufanya kazi vizuri. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuunga mkono hoja na nawapongeza sana Makamishna wote, Waziri na Naibu wake na wataalam wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani, *aluta continua, big up! (Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Kigua.

MHE. OMARY M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kusema machache katika bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu wake pamoja na uongozi mzima wa Mambo ya Ndani kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa sana. Sote Wabunge hapa katika Bunge hili tunakuja humu ndani na kutembea lakini amani na usalama wetu unategemea Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, mtu mwenye akili timamu na busara ni lazima asifie Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kesi chache chache tu ambazo kwa kweli kama Wabunge ni lazima tuziseme na ni jukumu letu kama Wabunge tushauri pale ambapo pana changamoto hizo. Kwa hiyo, ni ukweli usiopingika kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumza ni kulipongeza Jeshi la Polisi hususan Kitengo cha Magereza. Magereza wanafanya kazi nzuri sana hasa katika utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Viwanda.

Tumeona namna gani ambavyo wamefanya shughuli mbalimbali, mfano ni Karanga. Karanga wao wanatengeneza viatu, lakini tumeona katika hotuba hapa kwamba watu wa Jeshi la Magereza wanataka kuingia ubia na Mifuko ya Jamii kwenye Gereza la Mbigiri Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kuonesha kwamba Jeshi letu hususan Magereza na wao wako sambamba na Serikali yao kuonesha kwamba Sera ya Uchumi na Viwanda inakwenda vizuri zaidi. Hilo napongeza vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hotuba hapa nimesoma, nimeona kwamba mfungwa kwa siku gharama yake ni Sh.1,300/=, *kum-retain* mfungwa mmoja Gerezani kwa maana gharama ya chakula. Nasema, hivi kweli Magereza hawawezi kujilisha wao wenye? Tunao wataalam Magerezani mle; wanaweza kujenga majumba. Kuna kitengo hapa cha ujenzi. Hivi kwa nini hao wasi-*compete tender* na wengine kwa ajili ya kujenga shule, hospitali na kadhalika? Hili linawezekana. Magereza wana nafasi kubwa sana ya kuchangia uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Kamanda wa Magereza, hebu tuifanye Magereza iwe ni Magereza ya kisasa, iwe na wataalam, wawe ni sehemu ya kuchangia maendeleo ya nchi hii; wasitegemee sana ruzuku ili na wao wawewe kusogeza gurudumu la maendeleo mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona hata baadhi ya Magereza, kwa mfano Ofisi za Magereza mikoani ziko katika hali mbaya sana. Nilipata fursa ya kwenda kwenye Ofisi ya Magereza Mkoa wa Tanga, nikawa najiuliza, hivi kweli hata kupiga rangi inahitaji ruzuku? Hii inachekesha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri kwamba tuiwekee utaratibu kutumia Magereza, wafungwa wetu wawewe kufanya ukarabati wa Magereza yetu na taasisi mbalimbali. Tunawapa watu binafsi lakini nadhani Magereza wana nafasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia juu ya changamoto ya ukosefu wa Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Kilindi. Mheshimiwa Waziri, nilizungumza hapa siku moja kwamba Wilaya ya Kilindi ina takriban miaka 13 toka imekuwa Wilaya. Wilaya yetu haina Kituo cha Polisi, tunatumia kama *post tu*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri na *IGP* yuko hapa, afanye ziara kuja Kilindi, aangalie ambavyo hata *OCD* hana nyumba ya kukaa; *OCCID* watumishi hawana. Hivi inawezekanaje, Polisi huyu aweze kuhudumia watu katika mazingira magumu kama haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, leo hii mahabusu pale hatuna. Leo mtu kama ana kesi pale inabidi apelekwe Handeni. Kutoka Kilindi hadi Handeni ni takriban kilometra 130. Maana yake tumewanyima haki wananchi hawa wa Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye bajeti ijayo ahakikishe kwamba Wilaya ya Kilindi inatengewa kujengewa Kituo cha Polisi kwa sababu ni haki yao wananchi hawa kuwa na Kituo cha Polisi. Vile vile ni kwamba Wilaya ya Kilindi, tuna eneo takriban heka 100 ambazo tumetenga kwa ajili ya kujenga Gereza kwa sababu hatuna Gereza Wilaya ya Kilindi. Sasa eneo lile linaweza kutumika kwa ajili ya uzalishaji, pia litatupunguzia usumbufu wa kupeleka wananchi kutoka Kilindi kwenda Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nimelizungumza mwaka 2017, nimeandika lakini namwomba Mheshimiwa Waziri, najua changamoto ziko nyingi, lakini nimeona hapa zimetengwa shilingi milioni 400 ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi. Namwomba sasa kwamba nasi mwakani kama siyo mwaka huu tuweze kutengewa kujengewa Gereza na Mahakama katika Wilaya ya Kilindi. Hilo linawezekana kwa sababu tunao mafundi, tunao wafungwa ambao wamefungwa katika Magereza yetu haya, ni mafundi wazuri

tu maana yake tunaweza kutumia pesa hizo hizo kuhakikisha kwamba tunapunguza gharama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni suala la kulinda mipaka yetu. Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumza hapa, lakini ni ukweli usiopingika kwamba haiwezekani watu wa *Home Affairs* wasifuatilie wageni wanaoingia katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni kubwa, ni pana kwa hiyo lazima watu wa *immigration* wahakikishe kwamba wanatekeleza wajibu wao kwa kuhakikisha kwamba kama wageni wanaingia lazima wafuatilie. Ni kitu cha kushangaza sana kama mtu anaweza kuhojiwa juu ya uraia wake, unasema kwamba watu wanafuatiliwa. Hilo jambo haliwezekani. Ni wajibu wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba mipaka yetu inakuwa salama na watu hawaingii ovyo nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Ntimizi.

MHE. MUSSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya, Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Vile vile nawapongeza Wakuu wa vyombo vilivyo chini ya Wizara hii. Nampongeza *IGP* kwa kazi nzuri anayofanya, Mkuu wa Magereza, Kamishna wa Zimamoto na Kamishna wa Uhamiaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa upo upungufu katika Majeshi yetu, lakini yako mambo mazuri yanayofanyika katika Majeshi yetu. Ni vizuri kueleza upungufu uliopo ili uweze

kurekebisha, lakini wakati tunaeleza upungufu huo tuisahau wajibu wetu kama viongozi pia kupongeza pale ambapo mazuri yanafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko humu ndani kushauri na tusijiondoe katika utaratibu huo. Tuna nafasi ya kuendelea kushauri pale ambapo upungufu unatokea. Sasa namna gani tunashauri, ni jambo la msingi sana sisi kama viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni zao la Polisi. Baba yangu alikuwa Polisi na mama yangu alikuwa Polisi. Najua changamoto za Polisi. Ninapozungumza hapa leo, nazungumza nikijua kabisa shida za Polisi ziko wapi, ndiyo maana nataka leo niwapongeze kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi tunaotoka vijijini, Jimbo langu ni la kijijini, Makao Makuu ya Polisi yalipo na maeneo yangu ni takriban kilometra 120, maeneo mengine kilometra 150. Wananchi tunapopata matatizo, kama Polisi hawapo katika maeneo yetu, shida tunazopipata, ndiyo maana tunajua umuhimu wa Polisi katika maeneo yetu. Usipopata Polisi katika maeneo yako huwezi kuona faida na hasara zake Polisi asipokuwepo katika maeneo yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja. Kata yangu moja ya Loya siku moja majambazi waliingia kwenye Kata yetu moja ya Loya, walivamia wakaiba pesa, wakafanya wanachotaka. Waliomba mpaka kupikiwa ugali, wakala. Tulipiga simu Polisi, walifika baada ya masaa mawili. Maeneo ambayo Polisi wapo, ujambazi au wizi hauwezi kufanyika katika maeneo hayo. Kwa hiyo, umuhimu wa Polisi katika maeneo yetu sisi tunaojua, tunapongeza kazi kubwa wanayofanya pamoja na changamoto zilizokuwepo katika maeneo yao ya utekelezaji wa kazi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka pia napongeza kazi nzuri wanayofanya Askari wetu wa kawaida.

Askari hao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, lakini hawajaacha wajibu wao wa kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie baadhi ya changamoto ambazo zipo, nami najielekeza katika Wilaya yangu ya Uyui na Jimbo langu la Igalula. Wilaya yetu ya Uyui Makao Makuu yetu yapo Isikizya, ni Makao Makuu mapya lakini mpaka sasa tuna takriban mwaka mmoja Askari wetu wamehamia pale, hakuna nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hakuna nyumba za kuishi Askari wetu, Askari wetu wamekubali kwenda kupanga nyumba mitaani, wanalipa gharama hizo wenywewe. Niombe sasa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ione umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za Askari wetu pale Isikizya Makao Makuu ya Wilaya yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali lazima iangalie sasa wale Askari wanaoishi katika nyumba za kupanga, wanaojilipia fedha kutoka katika mishahara yao, waone namna ya kuwapa posho ya kujikimu, kuweza kulipia makazi yao wanapokaa huko uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Makilagi, wanakaa katika mazingira magumu. Wale ambao sisi wahalifu tunakaa nao mitaani mle, lakini Mwenyezi Mungu anaendelea kuwalinda Askari wetu, tuone umuhimu kwa kweli kabisa wa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za Askari wetu katika maeneo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Igalula kama nilivyo sema ni kubwa sana, takriban kilometra 150 toka Makao Makuu ya Isikizya, lakini Wilaya yetu ya Uyui ina upungufu wa magari ya Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo eleza, tukio likitokea Kata moja mpaka Askari waweze kufika, kwanza

wana upungufu wa magari, lakini wakitaka kufika huko magari saa nyingine mabovu au hayana mafuta. Naomba Wizara iangalie utoaji wa magari kwa Wilaya ambazo zina changamoto ya umbali. Tukipata magari ya kutosha maana yake hata kama kuna matatizo Askari wetu wanaweza kufika katika maeneo mbalimbali kwa haraka na wananchi wetu wakaweza kupata huduma za kipolisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie kwa ujumla wake nchi nzima uhitaji wa Vituo vya Polisi katika nchi yetu yote, jje na mpango mahususi wa kujenga Vituo vya Polisi katika maeneo yetu. Tumewahamasisha wananchi wetu na maeneo mengi wamekubali kujenga Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, katika Kata yangu ya Loya ambayo iko takriban kilometra 120 toka Makao Makuu ya Isikizya, Halmashauri yetu lilitenga shillingi milioni 200, tumejenga Kituo cha Polisi pale. Wananchi wamechangia takriban shillingi milioni 50, mimi Mbunge wao nimechangia takriban shillingi milioni 10. Mpaka sasa kituo kile kimefikia asilimia zaidi ya 95, kimekwisha, lakini mpaka leo kituo kile hakijafunguliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waangalie mazingira, kilometra 150 toka Makao Makuu ya Wilaya ambako ndiyo Polisi ipo, mpaka kufika Loya, tuliamua kujenga kwa sababu ya umuhimu wake na sababu za kiusalama kutokana na maeneo yenye yaliyokuwa kule. Naomba Kituo hiki cha Polisi kiweze kukamilishwa, kifunguliwe na kiweze kupatiwa nyenzo za usafiri ili kuweza kusaidia usalama katika maeneo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kubwa ya mafuta ya kusaidia magari ya Polisi wetu kufika maeneo mbalimbali. Kama nilivyoeleza ukubwa wa Jimbo langu, saa nyingine Polisi wana magari, wanapigwa simu kwenda kwenye maeneo mbalimbali kunakuwa na shida kubwa ya mafuta. Mgao wa mafuta uangalie na jiografia ya Majimbo yetu. Jiografia ya maeneo mengine *trip* moja ya gari kwenda Kata moja mpaka nyingine ni takriban lita 150 mpaka lita

200, lakini mgao wa mafuta kwa mwezi unaweza ukakuta *OCD* anapewa lita 200 au lita 300. Naomba hili liangaliwe ili tuweze kusaidiwa. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ntimizi, muda wetu umemalizika.

MHE. MUSSA R. NTIMIZI: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku hii ya leo. Nawashukuru na kuwapongeza wote kwa kazi nzima tuliyofanya kutwa ya leo na michango yenu na naamini kwamba michango yote itakuwa na tija na maslahi kwa Taifa letu, basi Mwenyezi Mungu atajaalia Mheshimiwa Waziri wetu na Naibu wake na timu yao waichukue na kuifanyia kazi kama inavyotakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Ijumaa saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 4 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*